# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Saba – Tarehe 11 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazi ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):**

Repoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 *(The Annual General Report of the Controller and Audit General of the Financial Statement of Local Governments For the Year Ended 30$^{th}$ June, 2017).*

Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Hali ya Uharibifu wa Ardhi na Misitu *(Study on the Status of Environment With the Focus on Land Degradation, Forest Degradation and Deforestation)*

Repoti ya Ukaguzi wa Ufanisi na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki *(Performance Audit Report on Electronic Waste Management)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Repoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa za Fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 *(The Annual General Report of The Controller and Auditor General on Financial Statement of Central Government for the Year ended 30th June, 2017).*

Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mashirka ya Umma kwa Mwaka wa Fedha2016/2017 *(The Annual General Report on The Financial Statements of Public Authorities for the Financial year 2016/2017).*

Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2018 *(The General Report of The Controller and Auditor General on Performance and Specialized Audit for The Period Ended 31st March, 2018).*

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 *(The Annual General Report of The Controller and Auditor General on The Financial Statements of Development Projects for The Year ended 30th June, 2017).*

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa mwaka 2014 *(Follow up Report on The Implementation of The Controller and Auditor General's Recommendations for The Six Performance Audit Report issued and tabled to Parliament on April, 2014).*

Ripoti ya Ukaguzi ya Ufanisi ya Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Performance Audit Report on Preparedness for Implementation of Sustainable Development Goals).*

Majibu ya hoja na mpango wa kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2017 *volume I and II* (A na B).

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa ufanisi ya Utoaji wa huduma za Kusaidia Viwanda Vidogo na vya Kati Nchini *(Performance Audit Report on the Provision of Support Service for Small and Medium Enterprises)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Maji taka Maeneo ya Mijini *(Performance Audit Report on Provision of Sewage Services in Urban areas)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(Performance Audit Report on Management of Repayment and Recovery of Higher Education Student Loans?.*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Ripoti ya Ukaguzi na Usimamizi wa Viuatilifu vya Kilimo *(Performance Audit Report on The Management of Pesticides in Agriculture)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI):**

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Ugawaji wa Viwanja *(Performance Audit Report on The Management of Plots Allocation)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Performance Audit Report on Marine Protected Areas Management)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI YA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA-MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI YA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 54

### Idadi ya Watu Wenye Ulemavu Nchini.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI** aliuliza:-

Tanzania ina idadi kubwa ya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Je, Serikali inajua idadi kamili ya watu wenye ulemavu na aina ya ulemavu waliokuwa nao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2012 inaeleza kuwa, ulemavu ni hali inayotokana na

dosari ya kimwili au ya kiakili ambayo inampunguzia mtu uwezo na fursa sawa katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali katika jamii. Upungufu huo unaweza kuchochewa na mazingira na mtazamo wa jamii kuhusu ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina mbalimbali za ulemavu ambao umegawanyika katika makundi yafuatayo:-

Ulemavu wa viungo, wasioona, viziwi, wasioona, ulemavu wa akili, wenye ualbino, ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi, ulemavu wa matatizo ya afya ya akili, yaani walioupata ukubwani bada ya kuugua kwa muda mrefu pamoja na ulemavu wa ngozi yaani walioathirika na mabaka mabaka ya ngozi mwilini. Sababu za kiujumla ni pamoja na ukosefu wa chakula bora au lishe duni, magonjwa kama malaria, uti wa mgono na surua, ajali mbalimbali, urithi na hali ya mama yaani umri na hali ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maelezo hayo, naomba kujibu sasa swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wingi huo wa aina za ulemavu, Sense ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 imejumuisha vipengele mahususi kwa ajili ya kupata taarifa zinazohusu watu wenye ulemavu hivyo Tanzania inakadiriwa kuwa na takribani watu 44,928,923 ambao sasa kwa hapo mgawanyo wake uko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ualbino ni 16,477,000 ambayo ni sawa na asilimia 0.04, wasiiona ni 848,530 sawa na asilimia 1.19, ulemavu wa uziwi ni 425,322 sawa na asilimia 0.97, viungo ni 525,019 sawa na asilimia 1.9, ulemavu wa kumbukumbu ni 401,931 ambayo ni sawa na asilimia 0.9, ulemavu wa kushindwa kujihudumia ni 324,725 sawa na asilimia 0.74, na ulemavu mwingine yaani kwa ujumla wake ni 99,798 ambao ni sawa na asilimia 0.23.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Nassir una swali la nyongeza?

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa takwimu hizo zinatokana na sensa ya mwaka 2012 na Tanzania sasa inakadiriwa kuwa na watu wasiopungua milioni 50, hii inaonesha wazi kwamba Serikali haina takwimu sahihi kwa sasa.

Swali langu la kwanza, Serikali haioni kwamba kukosekana kwa takwimu sahihi kunapelekea kushindwa kuwapatia mahitaji yao ipasavyo?

Swali langu namba mbili, je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kufanya takwimu ili kuweza kupata idadi kamili ya watu wenye ulemavu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana mdogo wangu kwa ajinsi ambavyo anafuatilia masuala ya watu wenye ulemavu, lakini pia na yeye ni mdogo wetu yaani mdogo wa watu wote wenye ulemavu kwa sababu dada yake ni kiziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa takwimu kwa watu wenye ulemavu, na sambamba na hilo kama tunavyofahamu, sensa inafanyika kila bada ya miaka 10 ambapo kutokana na kwamba ilifanyika mwaka 2012 kwa hiyo tunategemea sensa nyingine ifanyike mwaka 2022; lakini kwa sababu ya umuhimu wa jambo hili yaani takwimu kwa watu wenye ulemavu tayari Serikali imeshaanza kufanya mazungumzo na kuangalia ni jinsi sasa

tunaweza kupata takwimu hizi kabla ya wakati huo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Khadija Nassir Ali kwamba hili suala Serikali imeliangalia kwa umuhimu wake kabisa kwa sababu ni makusudi na nia ya Serikali kuona kwamba inapanga bajeti zake kulingana na uhalisia wa mahitaji ya watu wenye ulemavu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiwaficha watoto ambao wamekuwa na ulemavu na hivyo kukosa haki za msingi kama afya na elimu. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu wazazi na walezi hawa ambao wanawakosesha hawa watoto? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua na imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara kuhusiana na umuhimu wa kwamba kila mtoto mwenye ulemavu anawajibika ama ana fursa sawa na watoto wengine ambao hawana ulemavu. Kwa kuliona hilo hivi ninavyozungumza tayari kuna zoezi linaendelea la kuwatambua watoto wenye ulemavu kila mahali nchini ili kuona sasa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba hawafichwi tena ndani na wanapatiwa huduma kama watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili linafanyika. Hata hivyo niendelee kutoa rai kwa wazazi wote nchini pamoja na walezi kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanawapatia fursa sawa na watoto ambao hawana ulemavu. Mtu mwenye ulemavu ni sawa na mtu

mwingine ambaye hana ulemavu, akiwezeshwa anakuwa anaweza. Kwa hiyo, nitoe rai sana na niwaombe wazazi pamoja na walezi kulizingatia hilo kuona kwamba watu wenye ulemavu wako sawa pamoja na watu ambao hawana ulemavu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Watoto wanaozaliwa na ulemavu nao wanastahili kupata elimu kulingana na ulemavu walio nao. Sisi pale Temeke tuna Shule ya Msingi Jeshi la Wokovu ambayo inatoa elimu ya msingi kwa watoto wenye ulemavu kutoka sehemu mbalimbali za nchi, lakini ukweli ni kwamba shule ile inakabiliwa na changamoto nyingi za vifaa wezeshi kwa wale walemavu, lakini pia mazingira yenyewe ya shule. Nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kuisadidia shule ile ili watoto wasome kwenye mazingira rafiki?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana kaka yangu Mtolea, Shule ya *Salvation Army* nimefika pale na nimejionea mazingira yalivyo. Kwa hiyo kama shule zingine ambavyo tumekuwa tukifanya kuhakikisha kwamba zinapata vifaa saidizi na Shule ya *Salvation Army* tutahakikisha kwamba itaendela kupata vifaa saidizi sawa na shule zingine ambazo tumekuwa tukigawa vifaa saidizi kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimia Mwenyekiti, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mtolea kwamba shule hii na yenyewe itaendelea kupata vifaa saidizi kama ambavyo shule zingine zimekuwa zikipata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamtumu.

**MHE. MWAMTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kuniona. Kwa kuwa…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mwamtumu kaa nimemtaja Mheshimiwa Waziri wa Elimu alikuwa anataka kutoa maelezo kwanza.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa pia kuongezea na kulihakikishia Bunge lako kwamba Wizara ya Elimu imekuwa ikinunua vifaa visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Katika bajeti ambayo tutakuja kuiwasilisha Bungeni tarehe 3 na 4 Mei, 2018 pia tumetenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba shule hiyo pamoja na shule nyingine ambazo zina wanafunzi na ambao wanahitaji visaidizi watapatiwa ili waweze kujifunza kwa ufanisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mwamtumu Dau.

**MHE. MWAMTUMU D. HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kuniona. Kwa kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu kwenye suala la ubakaji, je, Serikali imejipanga vipi kuhusu suala hili?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikihakikisha ulinzi kwa watu wenye ulemavu kila iitwapo leo. Kwa hiyo, niseme kwamba hata hili la ubakwaji kwa watoto wenye

ulemavu Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inawapatia ulinzi. Hata hivyo si hilo tu, mtu ambaye atabainika kwamba amefanya kitendo hicho kwa mtu mwenye ulemavu atachukuliwa hatua kali na hatua stahiki kama inavyostahili ahsante.

**MWENYEKITI**: Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Catherine Ruge, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 55

**Kodi Katika Vifaa vya Walemavu**

**MHE. CATHERINE N. RUGE** aliuliza:-

Upatikanaji wa vifaa vya walemavu ni mdogo sana lakini gharama zake ni kubwa sana hali inayofanywa walemavu kushindwa kumudu, kwa mfano mguu bandia mmoja unauzwa shilingi milioni mbili.

Je, ni lini Serikali itatoa agizo la kufutwa kodi za vifaa hivyo kama ilivyo katika nchi nyingine na kwa kuzingatia kauli mbiu ya Serikali ya kumkomboa mnyonge?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa watu wenye ulemavu ni kundi kubwa miongoni mwa Watanzania ambalo linakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya kujimudu vikiwemo miguu bandia ambayo huuzwa kwa gharama kubwa kiasi cha kuwafanya Watanzania wenye kipato kidogo kushindwa kumudu gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa vifaa hivyo vya kujimudu kwa watu wenye ulemavu, Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 inayotoa tamko juu ya upatikanaji wa nyenzo mbalimbali za kujimudu kwa watu wenye ulemavu ili kuwarahisishia utendaji wao wa kazi na katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo pamoja na kuwarahishia mawasiliano kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo bado kumekuwepo na changamoto ya upatikaji wa vifaa hivyo kwa bei kubwa ambayo inakuwa vigumu kwa wananchi wengi kuweza kumudu na pia vifaa hivyo kuagizwa nchi za nje kwa kuwa hapa nchini vinapatikana vichache. Hivyo, Serikali kwa kutambua changamoto hiyo na kwa lengo la kumkomboa mnyonge, ilifuta kodi kwa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu kama alivyoeleza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mbunge) kupitia hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2017.

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Swali langu la kwanza, natambua halmashauri zetu zote Tanzania zinatakiwa kuwapatia asilimia mbili vikundi vya ujasiriamali vya watu wenye ulemavu. Swali langu, je, ni kiasi gani cha pesa kilitolewa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa vikundi vya watu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunapoelekea kwenye uchumi wa viwanda Serikali imewaandalia mazingira gani watu wenye ulemavu ili waweze kushiriki moja kwa moja kwenye uchumi huo kwa kupata fursa ya ajira, fursa ya kujiajiri kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo na fursa ya kupata masoko kwa ajili ya bidhaa zao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Catherine Ruge kama ifuatavyo, nikianza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi na nzuri na majibu mazuri aliyoyatoa leo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiendelea na hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu jana suala hili la asilimia 10 katika mifuko ya Halmashauri za Wilaya ilijitokeza. Ninaomba nikubaliane na maelekezo ama kauli ya Serikali iliyotolewa na Waziri wa TAMISEMI jana kwamba maeneo yote yanayohusiana na asilimia 10 yatatolewa maelezo katika bajeti itakayoanza leo inayohusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI na hivyo tutaweza kuwa na maelezo fasaha.

Lakini la pili, kuhusu namna nzuri ya kuwafanya watu wenye ulemavu kuingia nao katika uchumi wa viwanda, kama tulivyotoa maelezo jana wakati tunahitimisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, suala hili ni suala la kisheria liko ndani ya sheria ya watu wenye ulemavu namba tisa ya mwaka 2010. Kwa hiyo, sisi sasa tunachokifanya ni kusimamia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kutoa rai kwa watu wote na wawekezaji wote ambao wanaanzisha viwanda katika nchi yetu ya Tanzania kuona kwamba wenye ulemavu nao wanaouwezo wa kutoa mchango katika ujenzi wa taifa kupitia auchumi wa viwanda hivyo basi wawape fursa kwa kuzingatia sheria ambayo tuko nayo na sisi kama Wizara tutaendelea kusimamia kuona jambo hili linatekelezwa.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sambamba na ufutwaji wa kodi

wa vifaa vya watu wenye ulemavu, je, ni lini Serikali itawagawia bure walemavu kwenye kaya maskini vifaa vya uhafifu hauoni kwa watu wenye ulemavu wa macho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA I. ALEX):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu kadri vinavyokuwa vinapatikana, kwa hiyo, hili ambalo ameliuliza dada yangu Sophia nimhakikishie tu kwamba Serikali itaendelea kutoa vifaa hivi. Hata hapa, muda mfupi uliopita kama wiki mbili/ tatu/mwezi mmoja uliopita tumekuwa na hilo zoezi la kugawa vifaa hivi saidizi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kufanya hivyo kupitia bajeti zake lakini pia kupitia wadau mbalimbali wanajitokeza kusaidia kundi hili la watu wenye ulemavu (*Makofi*).

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya litauliza na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda.

Na. 56

**Kujenga Majengo ya Kisasa ya Ofisi za Uhamiaji na Customs Katika Mpaka wa Tanzania na Kenya – Wilayani Rorya**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE (K.n.y MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Katika mpaka wa Tanzania na Kenya uliopo Wilayani Rorya, kuna Ofisi za Uhamiaji na *Customs* za nchi yetu zipo kwenye makontena.

Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya kisasa kwa ajili ya ofisi katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mpango inatambua uwepo wa mahitaji ya ofisi ya kisasa katika Kituo cha Forodha kilichopo mpakani mwa Tanzania na Kenya, Wilayani Rorya Mkoa wa Mara. Kwa sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania ipo katika hatua za kupata umiliki wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 22,933.5 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya ofisi. Mara hatua za umiliki wa eneo zitakapokamilika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania itaanza taratibu za ujenzi wa ofisi na tuna uhakika tunaweza kuwa pamoja na ndugu zetu wa uhamiaji mara ofisi hizi zitakapokamilika na wao wakiwa wanashughulika na ujenzi wa ofisi zao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante kwa kuwa hili tatizo la uwepo wa ofisi mmbovu na ambazo hazina hadhi katika maeneo yetu ya Tanzania na zinatutia aibu limekuwepo kwa muda mrefu sasa nini *commitment* ya Serikali kwamba sasa hizi aibu tunaziondoa lini katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mambo haya pia yanahusu mambo ya uhamiaji na kwa kuwa katika Jimbo la Rorya na Jimbo la Bunda kwenye vijiji vya Tlinati, Jabuzume na Nyaburundu kumekuwepo na hisia za kuwaita watu jamii ya Wanandi, Wakisii na Wajaruo kwamba ni wahamiaji na hasa wakati wa uchaguzi, je, ni lini sasa Serikali katika upande wa uhamiaji watamaliza hii kero ili wananchi waishi huru? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwani amekuwa mstari wa mbele sana kwenye kufuatilia mambo yanayohusu wananchi wake na mpaka kuna siku aliwahi kunipeleka kufanya mkutano saa mbili usiku, na kwa kweli wananchi wake hawakufanya makosa kumchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali hili analolisema kwamba lini Serikali itamaliza tatizo hili; sasa hivi Serikali iko kwenye uandikishaji wa Watanzania kupewa vitambulisho vya uraia na zoezi hili linaendelea mikoa yote, na Mkoa wa Mara ni moja ya mkoa ambao zoezi hilo limefanyaka vizuri sana. Pale ambapo zoezi la upatikanaji wa vitambulisho vya uraia vitakuwa vimepewa kwa kila Mtanzania tutakuwa tumemaliza tatizo la watu kuhisiana kuwa si raia kwa maslahi ya kiuchaguzi kama alivyosema ama kwa kutazamana kwenye sura ama lugha mtu anapoongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo punde ambapo kila mmoja atakuwa na kitambulisho cha uraia tutakuwa tumelimaliza tatizo hilo na wananchi wake wataendela kukaa kwa usalama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Gashaza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna kituo kidogo cha forodha katika eneo la Murusagamba Kusini mwa Wilaya ya Ngara kwenye mpaka wa Tanzania na Burundi, kituo hiki kimekuwa maarufu tangu miaka ya 1970 lakini kwa muda mrefu mpaka sasa kinahudumiwa na watumishi kutoka kituo kikubwa cha Kabanga.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kupandisha hadhi kituo hiki ili kiweze kujitegemea kwa sababu kuna ofisi nzuri ya *TRA*, kuna kituo cha Polisi ni Makao

Makuu ya Tarafa ya Murusagamba eneo ambalo ni *strategic* kwa ajili ya maendeleo. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kupandisha kituo hiki kuwa kituo cha forodha kinachojitegemea?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania inafanya tathimini ya vituo vyake vyote vya forodha na vituo vya mamlaka vilivyopo katika ofisi zetu zote ili kutambua uhitaji wa ofisi zote hizo na kwamba tutaweza kubadilisha ofisi zetu hizi. Ni dhamira ya Serikali yetu na ndio maana tumeanza kufanya tathimini na uhakiki wa nini kinachohitajika. Lakini kwa kituo alichokitaja Mheshimiwa Gashaza kuhudumiwa na watumishi kutoka kituo kingine, Serikali ndani ya mwaka huu imetoa tayari nafasi za kuajiri watumishi 52,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya watumishi 52,000 wataajiriwa watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili tuweze kuwapeleka katika ofisi zetu zote hasa ofisi zetu za forodha zilizo katika mipaka ya Taifa letu.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahasnte sana Mheshimiwa Naibu Waziri tunaendelea na wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Mpango wa Kuzalisha Vifaranga vya Samaki**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN** aliuliza:-

Je, ule mpango wa Serikali wa kuzalisha vifaranga na kuwapa wafugaji umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali wa kuzalisha na kusambaza vifaranga kwa wafugaji wa samaki unaendelea kutekelezwa kupitia bajeti ya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na mkakati wake wa kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki katika vituo vyake vya Kingolwira (Morogoro), Mwamapuli (Tabora) na Ruhila (Ruvuma) ambapo kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 mpaka mwaka 2017/2018 jumla ya vifaranga milioni 21 vilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji kwa bei ya ruzuku ya shilingi 50 kwa kifaranga aina ya sato na shilingi 100 kwa kifaranga aina ya kambale.

Mheshimiwa Mwenekiti, aidha, bei ya vifaranga kwenye mashamba ya watu na taasisi binafsi ni kati ya shilingi 150 hadi shilingi 300 kwa kifaranga kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara imekamilisha ujenzi wa *hatchery* ya kisasa ya kituo cha Kingolwira (Morogoro) yenye vitotoleshi 20 vyenye uwezo wa kuzalisha vifaranga takribani milioni 15 kwa mwaka.

Aidha, ni mkakati wa Wizara kujenga *hatchery* kama hiyo na kufunga vitotoleshi kama hivyo kwenye vituo vya Mwamapuli (Tabora) na Ruhila (Ruvuma) kwa lengo la kuzalisha takribani vifaranga milioni 45 kwa mwaka kutoka sekta ya umma ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kudhibiti ubora wa vifaranga wa samaki wa kufugwa Wizara imeendelea na mkakati wake wa kuimarisha vituo vyake kwa lengo la kuhifadhi samaki wazazi bora *(broodstock)* watakao sambaza kwenye *hatchery* za sekta binafsi zinazotambuliwa na Wizara ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga kwa mwaka

kutoka vifaranga 14,120,000 (2016/2017) hadi vifaranga 60,000,000 ifikapo mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha Halmashauri na sekta binafsi kuanzisha vituo vya kuzalisha vifaranga bora vya samaki ambapo vituo 23 vimeanzishwa na kuzalisha takribani vifaranga milioni 20 kwa mwaka na kusambazwa kwa wafugaji. Aidha, ni lengo la Wizara kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi kutekeleza mikakati wa kuongeza uzalishaji wa samaki wa kufuga kutoka tani 10,000 tulizonazo sasa hadi tani 50,000 ifikapo mwaka 2020/2021(*Makofi*).

**MWENYEKITI**: Mhesimiwa Yussuf maswali ya nyongeza halafu Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa masikitiko makubwa niiombe Serikali inapokuwa haina majibu ya maswali tunayouliza basi wasitujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili nilichangia bajeti 2015/2016 Naibu Waziri akiwa Olenasha yule pale akanijibu kwamba hivi ni vifaranga vya mfano milioni 21 ndio vimezalishwa kwa ajili ya kuwapelekea wakulima imo katika kitabu cha bajeti cha Wizara hii 2015/2016; leo Serikali inaniambia kutoka 2009/2010 mpaka 2017/2018 imezalisha vifaranga milioni 21 na kuvigawa. Tukisema Mheshimiwa Jenista anakuja juu ni uongo uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haina majibu isitujibu kwa sababu tunafuatilia haya mambo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Sasa mimi siwezi kukubali kama Serikali imezalisha ina mpango huu swali la kwanza ninalomuuliza Mheshimiwa hata siku hiyo katika mjadala wangu niliuliza hivi vifaranga miloni 21 kwa Tanzania kwa mwaka vinatosha hata mboga ya siku moja kwa Watanzania

maana hata shemeji zangu wamasahi wanakula samaki Je, Serikali iko *serious* kweli? Kwa hiyo Je, vinatosha hata hizo tani 50 mnazosema ikifika 21 zinatosha hata kwa mboga ya siku moja? Wako *serious* hawa kweli? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, katika bahari sasa kuna upungufu mkubwa wa samaki baharini na ongezeko la walaji wa samaki limeongezeka, je, kule baharini mna mpango gani wa kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania; Wizara yetu ina nia thabiti ya kuhakikisha kwamba ufugaji wa samaki na kusambaza vifaranga kwa watu ni jambo ambalo linapewa kipaumbele. Mheshimiwa Mbunge ana wasiwasi na takwimu tulizozitaja zinazohusu usambazwaji wa vifaranga milioni 21 nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba katika vituo vyetu nilivyovitaja, Kingolwira pale Morogoro ninao uhakika wa kwamba vifaranga hivyo vinazalishwa na vipo kwa ajili ya wakulima wetu na wafugaji wetu. Kama ana taarifa tofauti na hiyo sisi Wizara yetu ipo tayari kupokea taarifa yake iliyo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nimwambie kwamba katika kuhakikisha kwamba ufugaji wa samaki unapewa kipaumbele Serikali tumehakikisha katika msimu huu tunaokwenda nao wa fedha wa 2018/2019 tunaendelea na mazungumzo ya Wizara ya Fedha ili kuhakikisha tozo na kodi mbalimbali ambazo zinazuia ama kurejesha nyuma sekta hii ya ufugaji wa samaki zinaondolewa kusudi Watanzania walio wengi waweze kufuga samaki, waweze kupata kipato, waweze kupata lishe na tuache biashara ya kuagiza samaki kutoka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge katika swali lake la pili ametaka takwimu ya kwamba je, hii tani 50 niliyoitaja ndiyo inayotosheleza? Ni kwamba hivi sasa katika nchi uwezo wetu wa kuzalisha samaki ni tani 350,000 kwa mwaka, ambapo tani zaidi la 250,000 zinatoka katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitaji la samaki katika nchi ni tani 700,000 kwa hiyo tuna *gap* ya tani 350,000 na ndiyo maana ni muhimu sana katika *aquaculture* katika kipindi hiki kuliko kipindi kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameniuliza tuna mipango gani na bahari yetu. Mpango tulionao hivi sasa katika uzalishaji wa samaki kwenye bahari tuna kitu tunaita *cage farming. Cage farming* ni uzalishaji wa samaki wa kufugwa katika bahari, katika mito na katika maziwa. Mkakati huo tumeuanza na unakwenda vizuri. Tumeshaweka *cage* za kutosha pale Bagamoyo, zaidi ya *cage* 40. Tunaendelea kuweka *cage* vilevile katika Ziwa Victoria na maziwa yetu mengine ili kuhakikisha kwamba ufugaji wa samaki na kuzifikia hizi tani 50,000 unapatikana. Nawahamasisha Waheshimiwa Wabunge wote ya kwamba ufugaji wa samaki unalipa, na wewe Mheshimiwa Salim ingia katika ufugaji wa samaki uweze kunusurika pia vile vile katika kuinua kipato chako. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Dkt. Sware atafuatia Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, ningependa kupata majibu ya Serikali, kwa nini sekta hii ya uvuvi nchini iko nyuma sana au haikui kabisa ukilinganisha tu na nchi jirani zetu za Kenya na Uganda ilhali sisi tuna maeneo makubwa zaidi ya rasilimali maji nchini na wavuvi wengi wa kutosha. Sasa kwa nini tunasababisha kwamba sekta hii ya uvuvi iko chini sana kiasi ambacho tunaagiza samaki kutoka nje wakati rasilimali tunazo, wavuvi tunao, ili kukuza uchumi wa hawa wavuvi husika pamoja na uchumi wa nchi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri sana la mwalimu wangu Dkt. Semesi Sware. Anauliza ni kwa nini sekta ya *aquaculture* (ufugaji wa samaki) bado iko chini Tanzania ukilinganisha na nchi jirani za Kenya na Uganda. Ni kweli, Uganda wanazalisha tani za samaki zisizopungua 30,000 na Kenya wanazalisha tani zisizopungua 25,000, sisi tuko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waganda waliweka mkakati mzuri wa *cage farming* na uzalishaji wa kambale, lakini vilevile Wakenya waliweka mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba Serikali yao inapeleka nguvu ya kutosha katika *county* zote nchini kwao ili kuhakikisha wanajenga vizimba na mabwawa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Sware na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mkakati wa Wizara yetu ya Mifugo na uvuvi tunataka tufike mahali huko. Nataka niwahakikishie ya kwamba tayari tumeanza kazi hiyo. Idara yetu ya *Aquaculture* zipo sheria ambazo zilikuwa zinasababisha tusiende mbele kama nilivyotangulia kusema katika jibu langu la msingi; ambazo tayari tunakwenda kuzifanyia marekebisho. Ninaamini baada ya kufanya mabadiliko hayo yote, na kwa mkakati ambao tunao kama Wizara tutatoka na kwenda mbali sana katika sekta hii ya uzalishaji ya *aquaculture.* Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali hapo amezungumza kwamba upo mkakati wa kuzishirikisha Halmashauri na kuweza kuingia katika uzalishaji huu wa samaki.

Sasa kwa bahati mbaya sana mimi natokea katika Milima ya Usambara ambako huko hakuna mito, hakuna mabwawa, hakuna chochote, sisi samaki tunamuona kwenye picha na wenzangu Wapare kule Same. Sasa anatuambia nini, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hizi Halmashauri ambazo hazina mito wala maziwa zinafaidika na huu uzalishaji wa samaki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kumjibu Mheshimiwa Shangazi swali lake la nyongeza na anauliza Wizara ina mkakati gani wa kuwasaidia watu wa milimani ambao hawana maziwa, hawana mabwawa wala hawana maji yanayotiririka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mpango mzuri sana na hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Shangazi na ni ukweli kwamba samaki ni chanzo cha *protein,* lakini vilevile na madini yaliyo muhimu kabisa katika mwili wa binadamu yanayoenda kuimarisha mifumo ya mifupa na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechukua ombi lake Mheshimiwa Shangazi la kutaka watu wa kule Mlalo waweze kupata mabwawa ya samaki ili waweze kufuga samaki ili waweze kupata faida ya kupata *protein* na virutubisho vingine.

Namhakikishia ya kwamba tutampatia wataalam watakaoweza kushirikiana na halmashauri yake, watakaoweza kwenda kufanya mapinduzi haya ya ufugaji wa samaki na watapata na vifaranga pia tena si vifaranga tu, vifaranga bora.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 58

**Mradi wa Maji Katika Manispaa ya Morogoro**

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** aliuliza:-

Serikali imeahidi mradi wa maji ambao utamaliza kero ya maji katika Jimbo la Morogoro Mjini hasa maeneo ya Kihonda, Tungi, Lukobe, Mkundi katika Kata ya Mindu.

(a) Je, ni lini mradi huo wa maji utaanza ili kuondoa kero za maji katika Jimbo la Morogoro Mjini?

(b) Je, mradi huo utagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeandaa mipango madhubuti katika kuhakikisha inaboresha huduma ya maji kwa wakazi wanaoishi katika Manispaa ya Morogoro. Katika kufikia lengo hilo, Wizara inatekeleza mipango ya muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa muda mfupi, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya mradi wa kuboresha huduma ya maji kwa maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji wenye urefu wa kilometa 41.9 na kituo cha kusukuma maji eneo la Mizani. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao 17,000 wanaoishi maeneo ya Kihonda, Kilimanjaro, Mkundi, Yespa, Kiyegea na Kihonda Kaskazini. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo la *AFD* itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Manispaa ya Morogoro. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na kuongeza kina cha bwawa la Mindu, ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji, ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka Tumbaku hadi Kingolwira, upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji, ukarabati wa miundombinu ya majisafi na ukarabati wa mabwawa ya majitaka. Gharama ya utekelezaji wa mradi huo ni *Euro* milioni 70. Aidha, kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za kusaini mkataba wa kifedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul-Aziz, swali la nyongeza.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni lini Serikali itasaini mkataba huu wa *Euro* milioni 70 maana toka mwaka 2017 tunaambia itasaini. Sasa tunataka kujua ni lini Serikali itasaini mkataba huu ili wananchi wa Morogoro wapate maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Morogoro Mjini kuna mgao wa maji, mwananchi anaweza akakaa miezi mitatu hajapata maji lakini cha ajabu analetewa bili ya maji mwisho wa mwezi ili aweze kulipa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ya kipekee anavyowapigania wananchi wake, ni namna gani jinsi anavyowapenda. Mimi nataka niwahakikishie wananchi wa Morogoro hawakukosea kumpata Mbunge huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kubwa mimi kama Naibu Waziri nilifika Morogoro na niliona hali ya upatikanaji wa maji katika Mji ule wa Morogoro na namna gani wananchi wanavyolalamika kuhusu suala zima la maji. Anataka kujua ni lini sasa tutakaposaini mkataba ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana hasa katika suala zima la fedha na suala la fedha lazima lifuate taratibu zake. Sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa maji hayana mbadala, si kama wali ukikosa wali utakula makande au ugali kuna haja ya haraka kuwapatia wananchi wake maji na sisi kama Wizara ya Maji tutafanya jambo hilo haraka ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la bili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kutokana na changamoto hiyo Waziri wangu aliitisha kikao cha Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Maji nchini katika kuhakikisha wanajadili changamoto hii ya maji na akawapa maelekezo. Nataka niwaagize tena Wakurugenzi wote. Maagizo ambayo ametoa Waziri kuhusu suala zima la kutokuwababambikia wananchi bei lazima watoe bei ambazo zimeidhinisa na *EWURA* na yale maelekezo ambayo yanahusu suala zima la bei wafanye kama walivyoelekezwa.

Mheshimwia Mwenyekiti, kama kuna Mkurugenzi atakayekaidi atakavyoenda ndivyo sivyo atuharibie sisi kazi tutamharibia yeye kabla ya sisi kutuharibia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aisharose.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililoko Morogoro Mjini halina tofauti na tatizo lililopo Manyoni Magharibi. Wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwa muda mrefu wamekuwa wakihangaika na kero kubwa ya ukosaji wa maji safi na

salama na maeneo yaliyoathirika ni Itigi Mjini, Songareli, Mlowa, Tambukareli, Majengo na Zignal.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi maji safi na salama na kuwatua ndoo wanawake? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri amejiandaa na maji Morogoro; haya kama una jibu la jumla kuhusiana na Manyoni.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na si mara moja amenieleza kuhusu suala hili, mambo mazuri hayataki haraka. Kwa kuwa sisi Wizara ya Maji si Wizara ya ukame tarehe 7 Mei, 2018 tunawasilisha bajeti yetu ya Wizara ya Maji; kwa hiyo namuomba sana tuwe katika suala zima la subira na subira yavuta heri, heri itapatikana katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Ahsante sana, itatekelezeka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ishengoma, Mheshimiwa Khadija na Mheshimiwa Waitara maswali mafupi.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali fupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Morogoro licha ya mipango mizuri ya Serikali imekuwa na matatizo kweli ya maji. Je, kuna mkakati gani wa kuanzisha vyanzo vingine vya maji katika Manispaa ya Morogoro ikiwa ni mkakati wa muda mfupi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe majibu kwa ufupi kabisa kama alivyouliza swali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji halisi kwa sasa ya Mji wa Morogoro ni lita 45,000 mita za ujazo kwa siku, lakini Mamlaka

ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira *(MORUWASA)* yanatoa maji 34,000 lita za ujazo kwa siku; kwa hiyo kuna uhaba katika suala zima la maji. Serikali kwa kuona haja ya kuongeza kiwango cha maji ndiyo maana tupo katika utaratibu wa kusaini *Euro* milioni 70 katika kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo la maji katika Mji wa Morogoro.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija, swali fupi.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nina swali dogo kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha katika Halmashauri zote hawa mawakala wa maji, *pre-paid meter* ili kuepusha wananchi kubambikiziwa bili na kuepusha wananchi au taasisi kutokulipa bili za maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi. Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe majibu kwa ufupi. Hivyo ndivyo inavyotakiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Wizara ya Maji ni katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na mpango wa kisasa kuwa na *pre-paid meter.* Mpaka sasa Mheshimiwa Waziri ameshaziagiza mamlaka hizo zifungwe na mpaka sasa zipo mamlaka saba ambazo zimeshaanza kutekeleza mradi huo. Kwa zile mamlaka ambazo bado hazijatekeleza lazima watekeleze katika kuhakikisha tunaondoa tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kata ya Msongola, Chanika, Zingiziwa, Buyuni na Pugu hazina maji; na kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Maji alisema kuwa Mradi wa Kimbiji na Mpera ukikamilika ndio utaleta maji Ukonga. Ningeomba nijue mpaka sasa mradi huu umefikia katika hatua gani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyowapigania wananchi; lakini kubwa sisi tulifanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam na nimefika hadi katika maeneo yake. Jitihada kubwa ambayo Serikali inaifanya mpaka sasa ni kuchimba visima 20 kwa maeneo ya Kimbiji na Mpera katika kuhakikisha wanapeleka maji maeneo yale. Hata hivyo kikubwa sasa hivi katika utekelezaji wa mradi ule lazima tusambaze kwa kutegemea na fedha. Kwa hiyo, tupo katika jitihada ya kutafuta fedha ili tuweze kutekeleza mradi ule na kuweza kuondoa tatizo la maji katika maeneo ya Ukonga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko na Mheshimiwa Kuchauka, tunamalizia. Maswali mafupi na majibu mafupi kama anavyojibu Waziri.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina swali dogo kwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya Morogoro inafanana sana na shida iliyoko Kigoma ambapo Mkoa wa Kigoma tuna mradi wa maji wa Ubelgiji ambao fedha zake zimeshasainiwa. Katika Mji wa Kasulu vijiji vya Nyansha, Nyantale na Kibondo vina shilingi bilioni mbuili katika mradi huo. Hata hivyo tangu fedha zimesainiwa kati ya Waziri wa Fedha na Balozi wa Ubelgiji mpaka sasa hakuna kazi yoyote iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwneyekiti, ni kwa nini Wizara haifuatilii mradi huu ambao tayari una fedha zake; lakini bado haujaanza kwa sababu ya urasimu tu? Nilikuwa naomba majibu katika swali hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona swali limerukia Kigoma sasa. Kama utaweza lijibu, huwezi,jibu kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri mwenyewe yupo, haya.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Nsanzugwanko kuhusiana na shilingi bilioni 18 kutoka Ubelgiji ambazo zimeelekezwa moja kwa moja Kigoma kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo kwenye eneo lake la Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi una hatua zake. Hatua ya kwanza, kusaini mkataba wa kifedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshasaini. Hatua ya pili sasa hivi Katibu Tawala wa Mkoa anaendelea na kufanya manunuzi kwa ajili ya kupata wakandarasi. Baada ya kukamilisha hayo manunuzi basi utaratibu wa utekelezaji wa miradi utaanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kujibu kwa ufupi. Mheshimiwa Kuchauka tunamalizia, swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Liwale ni mji unaokua kwa kasi sana hasa baada ya korosho kufanya vizuri na kuna mradi wa kutafuta chanzo cha maji mbadala kwa Mji wa Liwale. Mradi ule sasa hivi una zaidi ya miaka minne umesimama. Nini kauli ya Serikali juu ya kuwapatia maji wananchi wa Mji wa Liwale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeelekeza kwamba maeneo yote ya vijijini yatapata maji kufikia asilimia 85 na mijini asilimia 95. Mheshimiwa Mbunge naomba uvute subira kidogo, tarehe 7 mpaka 9 Mei, 2018 tutawasilisha bajeti yetu kwa hiyo miradi yako yote ambayo ilikuwa imekwama utapata kidogo maelekezo kule ndani na tutahakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Maji. Tunaendelea na Wizara ya Madini sasa Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala sasa aulize swali lake.

Na. 59

## Wananchi Waliodhulumiwa na Mgodi wa *ACACIA*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Wananchi wa Msalala husUsan wakazi wa Bulyanhulu wamefanyiwa dhuluma nyingi sana na Mgodi wa *ACACIA,* Bulyanhulu ikiwemo kuondolewa kwenye maeneo yao bila fidia mwaka 1996 na kwa wale wanaopata kazi mgodini kufukuzwa kazi bila kufuata utaratibu, kupata madhara makubwa ya kiafya na hata kusababishiwa vifo; na Serikali ya Awamu ya Tano imesimama kidete kutetea wananchi na kuwaepushia dhuluma hizi.

Je, ni hatua gani imefikiwa katika mazungumzo kati ya *ACACIA* na Serikali kuhusu ulipaji fidia kutokana na dhuluma hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa madini, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Bulyanhulu unamilikiwa na Kampuni ya *ACACIA* na unaendelea shughuli zake za uchimbaji madini tangu mwaka 2000. Kabla ya kuanzishwa kwa mgodi huo fidia stahiki kwa ardhi ya wananchi iliyotwaliwa ililipwa. Kwa sasa mgodi hauna madai yoyote ya wananchi wa Bulyanhulu yatokanayo na fidia ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 wafanyakazi wapatao 1,331 wa Mgodi wa Bulyanhulu walifanya mgomo kinyume cha sheria hivyo wakaachishwa kazi. Hata hivyo wafanyakazi 643 walirudishwa kazini. Tarehe 6 Novemba, 2007 wafanyakazi 658 waliogoma kurudi kazini walifungua kesi mahakamani na kuomba kufanyiwa uchunguzi wa kiafya ili kubaini hali za afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchunguzi huo wafanyakazi 78 walionekana kuwa na matatizo ya kiafya. Kwa sasa kampuni ya *ACACIA* inajadiliana na Serikali kupitia *OSHA* na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kuhusiana na madai yao ya matibabu na fidia kulingana na sheria za nchi. Ili kupunguza magonjwa yanayohusiana na kazi za migodini Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji zinafanyika kwa kuzingatia usalama, afya mahali pa kazi, pamoja na utunzaji wa mazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezekiel swali la nyongeza.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kabla sijauliza maswali ya nyongeza naomba nioneshe tu masikitiko yangu kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri kimsingi hajaenda kwenye *thrust* ya swali langu.

Swali langu nimeuliza je, ni hatua gani imefikiwa katika mazungumzo kati ya *ACACIA* na Serikali kuhusu ulipaji wa fidia na athari nyingine ambazo wananchi wa msalala wamezipata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika majibu yake pia, amesema kwamba hakuna fidia inayodaiwa, jambo ambalo si kweli kwa sababu kwa miaka 22 Serikali inafahamu kwamba watu walioondolewa mwaka 1996 Bulyanhulu, hakuna shilingi moja iliyolipwa. Mbaya zaidi kwa hawa wagonjwa Serikali imesema wamepatikana wagonjwa 78, lakini haijasema hatua gani zinachukuliwa kuhakikisha

wanatibiwa, kwa sababu tayari kuna watu 49 wameshafariki na hawajalipwa fidia yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa sababu uharibifu au wizi uliofanywa na *ACACIA* kwa Tanzania haujafanywa kwa Tanzania peke yake, umefanywa hasa kwa wananchi wa Bulyanhulu pia; na kwenye ripoti ya Profesa Ossoro ilionesha mabilioni mengi ambayo Tanzania ilipaswa kupata na mimi nilishasema kwamba wananchi wa Msalala wanastahili kulipwa shilingi bilioni 973 kama *service levy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kujua kwa sababu *ACACIA* walisha-*concede* hivyo na tayari walishatoa kishika uchumba kwa Serikali, kile cha dola milioni 300. Nilitaka kujua kwa wananchi wa Msalala wanaodai bilioni 973, je, Serikali inaweza ikawasaidia sasa ili angalau katika hii mitambo inayotaka kuuzwa na *ACACIA* ikabidhiwe kwa Halmashauri kama sehemu ya fidia ya *service levy* ambayo haijalipwa kwa miaka yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili,...

**MWENYEKITI:** Kwa ufupi tafadhali.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Sswali la pili, katika uwasilishwaji wa taarifa ya mazungumzo Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba uchunguzi ufanyike kwenye migodi mingine kuhusu utoroshwaji wa madini, ukiacha makinikia peke yake, utoroshwaji wa vitofali vya dhahabu na Wizara iliagizwa kwamba ifanye uchunguzi kwenye migodi mingine. Nilitaka kujua uchunguzi kwenye hilo eneo umefikia hatua gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la msingi imeonesha kabisa Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusiana na masuala ya fidia. Kwa taarifa tulizonazo katika Wizara yetu ni kwamba Mgodi ule wa Bulyanhulu ulivyokuwa unaanzishwa na kuanza kufanya kazi zake mwaka 2000 hakukuwa na madeni yoyote ambayo mgodi unadaiwa. Isipokuwa kama Mbunge ana hao watu ambao anawafahamu wanadai fidia katika yale maeneo kwa sababu yale maeneo ya Mgodi wa Bulyanhulu waliyapata kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli kuna watu ambao wanadai fidia zao, basi tunamuomba Mheshimiwa Mbunge awalete hao watu na madai yao, sisi kama Wizara tuko tayari kuwasimamia na kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi yeyote anayedhulumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ni kwamba ile taarifa ya *ACACIA* ambayo waliji-*committ* kutoa kishika uchumba, Serikali inaendelea na mazungumzo na uchunguzi ambao uliweza kutolewa, kama vile yalivyoweza kutolewa yale maoni na zile kamati mbili teule za Mheshimiwa; Rais ni kwamba yale mashauriano au ushauri uliotolewa wa uchunguzi, uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itaonekana katika vile vitofali kuna wizi wa dhahabu ulitokea kwa sababu, kulikuwa kuna *under declaration.* Kama kweli ilitokea ni kwamba wale wa *ACACIA* wako tayari kuweza kutoa au kulipa fidia zote ambazo wameji-*committ* na walitoa kishika uchumba cha dola milioni 300, kwa maana ya kwamba waliji-*committ* kwamba kama kutakuwa na pesa nyingine za kutoa basi wataendelea kufidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni kwamba maongezi yanaendelea na uchunguzi unaendelea na kama kuna upungufu wowote au kama kuna fedha yoyote ambayo inatakiwa ilipwe katika Halmashauri, kama *service levy,* na wewe mwenyewe umetaja kwamba

kuna bilioni 973 kama kweli ni haki ya Halmashauri haki hiyo italetwa katika halmashauri hiyo. Uchunguzi unaendelea na maongezi yanaendelea. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Upendo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii ya madini kwa wachimbaji wadogo wakiwemo wachimbaji wa Jimbo la Mbulu Mjini, ni kwamba wanakosa mitaji, lakini pia uchimbaji wao ni wa kubahatisha. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia fursa za uwezeshaji, lakini pia na vifaa vya kubaini madini yako wapi na njia rahisi ya uchimbaji?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kwamba, wachimbaji wadogo wanakumbana na tatizo kubwa la kuwa na mitaji midogo. Sisi kama Serikali tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba, wachimbaji wadogo tunakwenda kuwasaidia, ili waweze kupata mitaji ya kuweza kuchimba na waweze kuchimba kwa kupata faida, na sisi kama Serikali tuweze kupata maduhuli na kodi kutokana na uchimbaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wachimbaji wadogo wengi wanachimba kwa kubahatisha. Sisi kama Wizara kwa kushirikiana na *Geological Survey of Tanzania* taasisi ambayo chini ya Wizara ya Madini, tuna mkakati kabambe wa kuhakikisha tunafanya tafiti mbalimbali. Tafiti ambazo zitaonesha ni wapi kuna madini ya kutosha na kuweza kuwapa ushauri wachimbaji wadogo kuchimba maeneo ambayo yana madini ili kuepukana na tatizo la kuchimba kwa kubahatisha. Wanatumia fedha zao

za mfukoni, wengine wanauza hadi mali zao, ili waende wakachimbe maeneo ambayo hayajafanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumejipanga vizuri, tunafanya tafiti za kutosha na tutaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo, ili waweze kuchimba maeneo ambayo yana madini na waweze kuchimba kwa teknolojia nzuri ya kisasa na nyepesi, ili waweze kupata tija na waweze kuendesha maisha yao vizuri zaidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Upendo swali fupi kabisa.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutokana na swali la kwanza la msingi mazingira hayo pia yanafanana na kule kwetu Geita ambako wananchi wa Geita wamekuwa wakiathirika kwa kiasi kikubwa na shughuli za Mgodi wa *Geita Gold.* Serikali kipindi cha Waziri Muhongo na Naibu Waziri Kalemani waliunda tume kwenda kuchunguza matatizo hayo kule Geita na kubaini nyumba ambazo zimeathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa suala hili litaisha? Kwa sababu, wananchi wanaishi katika maeneo yenye mitetemo, wanaathirika na vumbi, wanapata hata madhara ya kiafya. Ni lini sasa Serikali itasimamia huo Mgodi wa *Geita Gold Mine* kuhakikisha ya kwamba, inawaondoa wananchi katika maeneo ya *Compound* na maeneo ya Katoma ili kupisha shughuli za mgodi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kuna watu ambao wanaishi ndani ya maeneo ambayo ni *square kilometer* 290,000 ambazo zinamilikiwa na *GGM.* Kwa mujibu wa sheria ilivyo ni kwamba kuna watu ambao bado wanamiliki zile *surface area,* yaani kwa maana ya eneo la

juu la ardhi, na maeneo ambayo ni ya chini yanamilikiwa na mgodi wa *GGM,* kwa hiyo, kuna wananchi ambao bado wanaishi maeneo ambayo yako ndani ya leseni ya *GGM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kufika pale mwezi wa pili na nilitoa tamko kwamba kuna Kamati ziliundwa na Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia na ilionesha kabisa kwamba kuna watu ambao wameathirika katika maeneo yale. Nikatoa tamko kwamba wale ambao wako ndani ya maeneo ya *GGM, GGM* kama kampuni ikae nao iwalipe fidia iwaondoe yale maeneo ambayo wale wananchi wanaathirika na mgodi huo.

Vilevile kuna watu ambao wako maeneo ya Katoma, wameathirika na matetemeko kutokana na milipuko inayofanywa na *GGM.* Kulikuwa kuna taarifa mbili ambazo zilikuwa zimetolewa moja ikiwa ya *GST* kuangalia ni namna gani yale matetemeko yalikuwa yanaathiri zile nyumba. Majibu yaliyokuwa yanatoka yalikuwa yanakizanzana kwamba kuna wengine walisema milipuko ilisababisha nyufa katika nyumba zile na kuna taarifa nyingine inasema kwamba ile mitetemeko haikusababisha zile nyufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeamua kwa pamoja kwamba wakae waangalie tena upya na vile vile wafanye tathmini ya kutosha kwenye zile nyumba zilizoathirika wawalipe wale wananchi. Ikiwezekana wale wananchi walimo ndani ya hiyo leseni ya *GGM* waondolewe, wawalipe fidia, ikiwemo na watu wa Nyakabare, walipwe fidia waondoke yale maeneo ya uchimbaji. Kwa hiyo, hiyo tumeshawapa *GGM* na tunaendelea na maongezi na tunaendele na mikakati kuangalia namna gani ya kuweza kuwalipa fidia wananchi hawa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Musukuma, swali fupi kabisa la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Halmashauri ya Geita inaudai mgodi wa *GGM* zaidi ya dola milioni 12; tumekaa tukakubaliana

watulipe kwa awamu. Awamu ya kwanza ilikuwa itekelezwe mwezi wa pili, lakini utekelezaji huo haujafanyika na Halmashauri haina nguvu tena ya kuudai Mgodi wa *GGM.* Je, Wizara inaisaidiaje Halmashauri ya Geita ili tuweze kulipwa pesa hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Geita inaudai *GGM service levy.* Tulitoa ushauri kama Wizara kwamba wakae kwa pamoja na waangalie ni namna gani Kampuni ya *GGM* inaweza ikawalipa wale Halmashauri ya Geita, yaani wakae kwa pamoja waelewane ili wangalie namna bora ya kuweza kulipa kidogo kidogo deni hilo na wameshakaa na nilipokwenda mara ya mwisho mwezi wa pili walisema kwamba wanakwenda kukaa na Halmashauri, ili waweze kusaini *memorandum of understanding,* namna ya kuweza kulipa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hawajalipwa mpaka sasahivi, naomba nishirikiane na Mbunge kwamba nifuatilie. Sisi kama Wizara tuko pamoja tutahakikisha kwamba haki ya Halmashauri ya Geita italipwa kama inavyostahili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Tatizo la Walimu wa Sayansi**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sasa Serikali imekuwa na mipango mahsusi ya kuhakikisha kwamba tatizo la walimu wa sayansi linapungua au kumalizika kabisa.

(a) Je, ni kwa kiwango gani mipango hii imesaidia kupunguza tatizo husika?

(b) Katika utekelezaji wa mpango tajwa hapo juu, Jimbo la Bunda Mjini na Halmashauri ya Mji wa Bunda imenufaika vipi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati kama ifuatavyo:-

(i) Imetenga Vyuo vya Ualimu 10 mahsusi kwa ajili ya kuandaa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati.

(ii) Kuongeza udahili wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati katika vyuo vikuu vya Serikali ambavyo hapo awali vilikuwa havitoi kozi za ualimu, kama Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA)* na Chuo Kikuu Mzumbe.

(iii) Kutoa kipaumbele cha udahili katika mafunzo ya ualimu wa stashahada na shahada kwa wahitimu wa kidato cha sita wa masomo ya sayansi na hisabati.

(iv) Kutoa kipaumbele cha ajira kwa wahitimu wa mafunzo ya ualimu, sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha pia kozi maalum ya stashahada ya ualimu kwa masomo ya sayansi na hisabati ambapo wahitimu wa kundi la kwanza wapatao 1,799 watamaliza mafunzo yao ifikapo Mei, 2018 na kundi la pili la wahitimu wapatao 5,441 watamaliza Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha ufundishaji na kuvutia wanafunzi wengi kusoma masomo ya sayansi na hisabati na hatimaye kupata wahitimu wengi wa masomo hayo, Serikali imeendelea kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi ikiwa ni pamoja na kusambaza vifaa vya maabara na kemikali katika shule za sekondari na kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa sayansi na hisabati. Mkakati huo unalenga kupata wahitimu wengi zaidi watakaojiunga na mafunzo ya ualimu wa sayansi na fani nyingine zinazohitaji masomo hayo na hivyo kuendelea kukabiliana na upungufu wa wataalam wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Bunda ilianzishwa mwaka 2015/2016 baada ya kugawanywa iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Kabla ya kugawanywa Wilaya hii ilikuwa na jumla ya walimu 144 wa masomo ya sayansi na hisabati. Katika taratibu za kugawana rasilimaliwatu katika Wilaya hiyo, Halmashauri ya Mji wa Bunda ilipewa walimu 69 wa masomo ya sayansi na hisabati.

Aidha, walimu wa sayansi na hisabati walioajiriwa mwaka 2016/2017 waliopangwa katika Halmashauri ya Bunda Mji ni wanane ambao wamepangwa katika shule za sekondari za Kunzugu, Rubana, Bunda, Wariku, Sazira, Sizaki, Nyendo na Daktari Nchimbi. Serikali itaendelea kuajiri na kupanga walimu wa masomo ya sayansi na hisabati katika Halmashauri hiyo, kadiri watakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza ninachoweza kusema Mheshimiwa Waziri katika mgawanyo takwimu wamekuongopea, Halmashauri yangu imepata walimu ambao hawafiki hata 60; ni 58 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kusema, hao wanane Bunda sisi hawatutoshi. Hisabati mahitaji ni 55 waliopo 20 peke yake, fizikia mahitaji 27 waliopo 10 peke yake, *biology* mahitaji 32 waliopo 15 *chemistry* kidogo

ndio mmejitahidi mahitaji 29 waliopo 21 bado wanane. Ukiangalia yaani hao tuliogawanywa na mahitaji kwa ujumla wake ni 68. Ni lini Serikali mtatupa Bunda walimu wa sayansi? Tumechoka Bunda kuwa miongoni mwa Wilaya zinazofanya vibaya katika masomo, swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunajia *TEA* ina-*deal* na masuala ya *infrastructure.* Hivi kwa nini Serikali msitenge fedha za kutosha, mkawapa *TEA* wakajenga pia na nyumba za walimu mbali na kwamba kuna changamoto kwenye shule za walimu ili pia walimu wawepo shuleni kuepuka usumbufu ambao unajitokeza na kusababisha watoto kufeli halafu hatimaye tunalaumiana mnaanza kuwafukuza wao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa walimu uliopo katika shule za Jimbo lake; ni kweli kwamba kuna upungufu wa walimu wa sayansi nchi nzima na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimeeleza mikakati iliyopo ya kuhakikisha kwamba, tunaondokana na upungufu huo.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba tunafahamu kwamba kuna upungufu na si kwake tu. Kwa hiyo tutaendelea kuhakikisha kwamba, upungufu huo unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)* kujiingiza zaidi katika kujenga shule za walimu, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kutegemeana na bajeti ambayo *TEA* wanatengewa ambayo kimsingi kwa miaka mitatu sasa mfululizo wanatengewa shilingi bilioni 10, itaendelea kujenga nyumba za walimu, lakini ikumbukwe kwamba jukumu hasa la *TEA* ni suala la kuongeza ubora, lakini vilevile kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji wa elimu na suala la usawa yaani *access, equity* na *quality.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *TEA* haikuundwa ili ichukue majukumu yote ya miundombinu za shule katika Halmashauri zetu. Jukumu la kujenga miundombinu katika shule ambazo ziko chini ya Serikali za Mitaa litabakia kuwa jukumu la Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, nimuombe Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu sisi wenyewe ni Madiwani tuendelee kuwahamasisha wananchi washirikiane na Serikali kujenga miundombinu kwa ajili ya shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *TEA* vilevile na hasa nyie Waheshimiwa Wabunge mkiwaongezea bajeti kwa sababu nyie ndiyo hasa mnaongeza bajeti itaendelea kufanya hayo kuhakikisha kwamba kunakuwa na usawa, ubora lakini yale maeneo ambayo yatakuwa na upungufu yaweze kupatiwa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze utaratibu kwamba ukiacha mbali la Halmashauri yenyewe kuomba *TEA* waweze kupatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi lakini vilevile Wizara kwa kushirikia na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunakusanya takwimu, kwa hiyo, tunajenga miundombinu kulingana na takwimu ambazo tumepata za nchi nzima. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamalizia maswali yaliyobaki, naomba nitambue wageni wa Mheshimiwa Spika ambao wanatakiwa kuondoka saa 4.30 ambao ni Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Mheshimiwa Balozi Richard Tumisiime Kabonero, karibu sana Mheshimiwa Balozi wa Uganda nchini Tanzania ambaye ameambatana na Ndugu Freda ambaye ni Afisa wa Ubalozi wa Uganda nchini Tanzania. Karibuni sana Mheshimiwa Balozi na Afisa wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Munira Mustafa Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 61

## Mpango Maalum wa Kujiendeleza Kimasomo Wasichana Wanaokatiza Masomo kwa Ujauzito

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU** aliuza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuratibu na kuwatambua wasichana wanaokatiza masomo kwa sababu ya ujauzito na wale walionyimwa fursa ya kuendelea na masomo na kuwaandalia mpango maalum wa kujiendeleza kimasomo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inao utaratibu wa kuwatambua wanafunzi wanaoacha shule kwa sababu mbalimbali. Takwimu hutolewa kupitia kijitabu kinachojulikana kwa jina la *National Basic Education Statistics in Tanzania (BEST).* Kijitabu hicho hutoa takwimu za kielimu ikiwa ni pamoja na idadi ya wanafunzi, walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima hutoa fursa za kielimu kwa makundi tofauti ya walengwa wakiwemo waliokosa nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari kwa sababu mbalimbali kama ujauzito, utoro na utovu wa nidhamu. Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima huendesha Mpango wa Elimu ya Sekondari kwa ujifunzaji huria katika vituo vilivyopo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika mwaka 2017, walengwa 10,420 wamesajiliwa kati yao 7,074 ni wanawake na 4,346 ni

wanaume. Aidha, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima huandaa na kuendesha Programu ya Elimu Mbadala kwa Vijana na Watu Wazima kulingana na mahitaji yao ambapo hutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kama vile ujasiriamali, stadi za maisha, ufundi wa awali na Programu za Kisomo cha Kujiendeleza kwa Watu Wazima ili waweze kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanaoacha shule za msingi, hupata fursa ya kuendelea na masomo kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Pia Serikali ina mpango wa kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* ili viweze kuongeza wigo wa kudahili wanafunzi kwa nyanja mbalimbali za mafunzo na hivyo kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wanaoacha masomo kwenye mfumo rasmi wa elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Elimu ya Watu Wazima imekuwa ni elimu dhaifu ndani ya mikoa yetu, ndani ya mikoa yetu iko chini yaani mikoa mingine hata haitambuliki kama kuna Elimu ya Watu Wazima. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia na kuboresha elimu hii ya watu wazima ili waweze kukabiliana na majukumu yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali ina mpango wa kuimarisha Vyuo vya Maendeleo *(FDCs).* Je, ni lini sasa Serikali itaimarisha Vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi ili vijana waweze kupata elimu katika vyuo hivi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake kwamba Elimu ya Watu Wazima imedhoofika katika baadhi ya maeneo, ni

suala la mtizamo lakini kama tulivyosema rekodi tulizonazo ni kwamba karibia katika mikoa yote kuna vituo kwa ajili ya kutoa Elimu ya Watu Wazima. Mheshimiwa Mbunge labda kama atakutana na mimi ataniletea orodha ya mikoa ambayo anafikiri haifanyi kazi lakini nimhakikishie kwamba Elimu ya Watu Wazima bado ipo pale. Ni ukweli vilevile kwamba kadri tunavyozidi kuimarisha na kuboresha elimu ya mfumo rasmi mahitaji ya Elimu ya Watu Wazima kwa baadhi ya watu yanaanza kuonekana kwamba yamepungua lakini ukweli wa mambo ni kwamba bado kuna watu wengi ambao wanajifunza na kupata elimu kwa kupitia Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile swali lake kuhusiana na namna Serikali inavyoboresha Vituo vya Maendeleo vya Wananchi *(FDCs),* nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango unaoitwa *ESPJ* ambao pamoja na mambo mengine utajenga na kukarabati miundombinu ya Vyuo vya Wananchi 55 na baadae tutahakikisha watakuwa na rasilimali watu wa kutosha. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kupata fursa ili vijana wengi waweze kujifunza stadi za kazi na ufundi na hasa kwa sasa hivi ambapo tunakazania kuhakikisha kwamba tunaingia kwenye uchumi wa kati ambapo rasilimali watu wa aina hiyo inahitajika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rehema Migilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali sikivu sana kwa wananchi wake hali iliyopelekea mpaka imewarudisha kazini watumishi wa darasa la saba. Swali langu, je, ni lini sasa Serikali itatoa tamko la kuwarudisha masomoni wasichana wote waliopata ujauzito na kuthibitishwa na Mahakama kuwa walibakwa kwani kwa kutowarudisha ni kuwanyima haki yao ya kupata elimu lakini vilevile ni kuwapotezea ndoto zao? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri waliobakwa tu siyo wote.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hata sisi Serikali kwa kweli hatupendi na hatutaki kusikia vitendo vya uonevu dhidi watoto wa kike, kwa sasa mfumo wetu wa elimu umepangwa katika namna ya kuhakikisha kwamba wanafunzi ambao wanapata ujauzito wanapata fursa ya kusoma lakini nje ya mfumo rasmi.

Kwa hiyo, kuna fursa nyingine nyingi za kusoma kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwa kupitia Elimu ya Watu Wazima na Vyuo vya Ufundi. Serikali haitarajii na naomba niweke wazi kuwarudisha wanafunzi ambao wamepata ujauzito kwa njia yoyote ile. Ni kwa sababu tukifanya hivyo maana yake tunahalalisha na kuhamasisha ngono shuleni wakati mila na sheria zetu haziruhusu ngono katika ngazi hizo maana yake shule za msingi na shule za sekondari.

**WABUNGE FULANI:** Wamebakwa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kubakwa, tunaposema kwamba hawaruhusiwi kuendelea na elimu katika mfumo rasmi siyo kwamba ni adhabu kwa kujifungua, tunachochukulia ni kwamba tayari ana mtoto na hivyo tukifanya hivyo tunakuwa tumefungulia milango ya vitendo kama hivyo kuendelea.

**WABUNGE FULANI:** Wamebakwa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kuna fursa zingine ambazo watoto wale wanaweza kutumia kupata elimu, zipo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunamalizia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini aulize swali lake.

Na. 62

**Mkakati wa Kuinua Soka la Tanzania**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Tunatambua kuwa michezo duniani kote imekuwa chanzo cha mapato na kuinua uchumi wa Taifa husika, lakini nchini Tanzania michezo hususan soka imebaki kuwa burudani tu.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuinua Soka la Tanzania?

(b) Je, kuna mahusiano gani kati ya Serikali na *TFF* katika kuimarisha soka la Tanzania kuanzia ngazi ya Wilaya?

(c) Je, Shirikisho la Mpira wa Tanzania *(TFF)* linapata fedha za ruzuku kiasi gani toka *FIFA* na Wadhamini kama *TBL* na *Serengeti Breweries?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuhakikisha kuwa michezo ikiwepo soka inaimarika nchini, imeendelea kuendesha mashindano mbalimbali ya michezo mashuleni kitaifa ikiwepo UMISETA pamoja na UMITASHUMTA ili kuibua vipaji mapema na imeteua shule 56, mbili kwa kila mkoa hadi tatu kwa kila mkoa ili ziwe shule za michezo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo ikiwepo mchezo wa soka.

Aidha, Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mafunzo ya muda mrefu kwa wakufunzi wa michezo mbalimbali ukiwepo mchezo wa mpira wa miguu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFF*, vyama vya michezo pamoja na mashirikisho mengine ya michezo vimesajiliwa na kufanya kazi chini ya Sheria ya Baraza la Michezo (BMT) Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake ya mwaka 1971. Aidha, *TFF* inaendelea na uboreshaji wa viwanja vya soka nchini, mfano ni viwanja vya Kaitaba na Nyamagana mkoani Mwanza. Vilevile *TFF* inatoa msaada wa kiufundi katika viwanja mbalimbali ili kuhakikisha kwamba viwanja vinakuwa katika ubora unaotakiwa. Wizara yangu inaunga mkono programu mbalimbai za *TFF* katika kukuza mchezo wa mpira wa miguu wilayani na mikoani zikiwemo programu mpya kabisa za *grass root* pamoja na programu ya *live your goals* kwa wanawake ambazo zilizinduliwa Mkoani Kigoma Februari, 2018. BMT nayo inaendelea kusimamia utekelezaji wa Katiba, Kanuni na Sheria zinazosimamia michezo mbalimbali nchini.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato ya *TFF;* kwanza *TFF* ina udhamini wa miaka minne (2015-2018) kutoka *FIFA* kwenye programu ya *FIFA Forward* ambayo hutoa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 1.25 kwa mwaka ambapo kati ya hizo dola za Kimarekani 750,000 hutumika kwa ajili miradi ya maendeleo na dola za Kimarekani 500,000 hutumika kwa ajili ya gharama za kuendeshea ofisi, timu za Taifa pamoja na ligi. Fedha hizi za maendeleo hazikuwahi kutolewa na *FIFA* tangu mwaka 2015, hivyo, *TFF* wanatarajia kupokea kiasi fedha cha dola za Kimarekani milioni tatu kwa ajili ya kutekeleza miradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TFF* iliingia mkataba na Kampuni ya Bia ya *TBL* mwaka 2013-2017 kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 10 kwa ajili ya Timu ya Taifa ambap kwa sasa mkataba huo umeshamalizika. Hivyo, *TFF* imeingia mkataba wa ufadhili na Kampuni ya Bia ya Serengeti wa miaka mitatu (2017-2019) wenye thamani ya shilingi milioni

700 kwa ajili ya timu ya Taifa ya wanaume na shilingi milioni 450 kwa ajili ya ligi kuu ya wanawake nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na niipongeze Serikali kuwa wazi kwenye swali hili. Pia ni-*declare interest,* mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Na. 12 ya mwaka 1967 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 1971 na Kanuni za Usajili wa Vyama vya Michezo, Namba 442 ya mwaka 1999, kifungu cha 7(2)(c)(ii), inatambua mamlaka ya Waziri na Waziri ndiyo mwenye maamuzi ya mwisho ya vyama vya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini viko baadhi ya vyama katiba zao hazitambui mamlaka ya Waziri na vyenyewe ndiyo vyenye mamlaka ya mwisho ikiwemo *TFF*. Mheshimiwa Waziri, nikuombe sana, ikikupendeza kama utakuwa tayari kulinda, kuheshimu na kusimamia sheria hii iliyotungwa na Bunge na kuhakikisha vyama hivi kwenye katiba zao zinatambua *role* ama wajibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, Serikali imekiri wazi katika ruzuku ambayo inatolewa *TFF* ni zaidi ya bilioni 10 na ile dola milioni tatu tunazungumzia karibu bilioni saba, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, kama utakuwa tayari uiombe *TFF* ilete mpango kazi kwenye mikoa yetu ili tuweze kujua fedha hizi zinatumikaje. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Sima kwa sababu amekuwa ni

mwanamichezo mahiri na vilevile ni mdau mkubwa sana wa michezo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na kujibu swali lake la kwanza ambalo ametaka kujua kama kuna vyama vya mpira ambavyo havitambui mamlaka ya Waziri. Mimi niseme kwamba tunatambua kabisa kwamba *TFF* pamoja na viongozi wake wote wanapaswa, wanalazimika na hivyo wanatambua mamlaka ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Ukisoma Katiba ya *TFF,* Ibara ya 1(2) inasema kwamba *TFF* ni chombo cha mpira ambacho kimesajiliwa chini ya Sheria ya Baraza la Michezo ya mwaka 1967 kama ambavyo umesema na marekebisho yake ya mwaka 1971. Kwa maana hiyo sasa, kimsingi kwa sababu Baraza la Michezo ambalo ndiyo ambalo linasajili *TFF* liko chini ya Wizara ya Habari, kwa maana lipo chini ya Waziri husika mwenye dhamana ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu *TFF* iko chini ya Baraza la Michezo, kwa hiyo, kimsingi ni kwamba *TFF* inapaswa kutambua mamlaka ambayo Waziri kwa maana ya Serikali inayo. Naamini kabisa kwamba *TFF* inatambua mamlaka ya Waziri kwa sababu ni takwa la kikanuni na kikatiba na wanapaswa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija kwenye swali lako la pili ambapo unataka kujua hizi fedha za *FIFA Forward* ambazo zimetolewa, unaiomba Serikali iweze kuishauri *TFF* iweze kutoa mchanganuo wa fedha hizo mapema. Mheshimiwa Sima natambua kabisa kwamba wewe ni Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu katika Mkoa wa Singida na kwa jinsi mimi ninavyotambua ni kwamba humu ndani tuna Wabunge wengi ambao ni viongozi wa vyama vya mipira. Kwa hiyo, najua kabisa kwamba ninyi kama Wenyeviti pamoja na Makatibu ndiyo mhimili mkubwa kabisa wa *TFF* lakini kimsingi ninyi ndio washauri wakubwa wa *TFF*. Kwa hiyo, kwa sababu *TFF* ina taratibu zake, ina mikutano yake ambayo huwa mnakaa na kila mwaka huwa

mnakutana, mna mkutano wa robo mwaka, nusu mwaka pamoja na wa mwaka, naamini mtakapokutana ninyi mna nafasi kubwa kabisa ya kuweza kuishauri *TFF* ili kuweza kuandaa huo mchanganuo wa fedha.

Niseme kabisa sisi kama Serikali tumelipokea wazo lako na tunakubaliana kabisa na wazo lako kwa sababu tunajua kwa namna moja au nyingine litasaidia kuweka uwazi wa mapato na matumizi na kuondoa sintofahamu ambazo zilikuwepo siku za nyuma. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umemalizika, kwa hivyo tuna matangazo hapa machache.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Kaimu Mkurugenzi Utawala na Rasilimali Watu, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaohitaji viwanja katika Manispaa ya Dodoma, waweze kuorodhesha majina yao katika eneo la mapokezi lililopo Ukumbi wa Bunge. Zoezi hili lilikwisha fanyika na orodha iliwasilishwa kwa iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* lakini baada ya Mamlaka hiyo kuvunjwa na shughuli zake kuhamishiwa Manispaa ya Dodoma, upimaji wa viwanja umekamilika na wanatarajia kuanza uuzaji wa viwanja hivyo kuanzia tarehe 11 Aprili, 2018 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma wameomba kupatiwa upya orodha ya Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji au watakaohitaji viwanja hivyo kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo. Hiyo ni fursa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tangazo la pili ni leo Jumatano tarehe 11 Aprili, 2018 kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristo wa Madhehebu ya Katoliki, mara baada wya kuahirishwa Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa Ghorofa ya Pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kushiriki ibada hiyo mnakaribishwa.

Tangazo la tatu, kuna uteuzi wa Wasemaji wa *Bunge Sports Club*. Kwa kuwa *Bunge Sports Club* ni klabu ya michezo iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi kama ilivyosajiliwa Klabu za Yanga, Simba na Azam na kadhalika; na kwa kuwa mfumo wa kisasa wa uendeshaji wa vilabu vya michezo duniani ni pamoja na kuwa na wasemaji maalum ambao ni viungo muhimu kati ya klabu na umma kwa ujumla; Kamati ya Utendaji ya *Bunge Sports Club* imewateua Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini na Mheshimiwa Amina Mollel, Mbunge wa Viti Maalum kuwa wasemaji rasmi wa *Bunge Sports Club* kuanzia tarehe ya Tangazo hili yaani leo tarehe 11 Aprili, 2018. *(Makofi)*

Bunge na umma kwa ujumla unaarifiwa kwamba hadhi ya wasemaji hao wa *Bunge Sports Club* ni sawa na hadhi ya wasemaji wa vilabu vya *Simba Sports Club*, Yanga na *Mtibwa Sugar.* Kwa upande mwingine, Kamati ya Utendaji ya *Bunge Sports Club* imeunda Kamati Ndogo ya Uratibu wa Michezo na Burudani, Wajumbe wa Kamati hiyo ni wafuatao; Mwenyekiti ni Mheshimiwa Cosato Chumi; Makamu Mwenyekiti ni Mheshimiwa Joseph Haule (Profesa Jay) na Wajumbe ni Mheshimiwa Neema Mgaya; Mheshimiwa Godfrey Mgimwa; Mheshimiwa Zubeda Sakuru; Mheshimiwa Khadija Nassir; Mheshimiwa Stanslaus Mabula; Mheshimiwa Sixtus Mapunda; Mheshimiwa Mussa Ntimizi; Ndugu Waziri Kizingiti na Ndugu Frank Mbilinyi, hawa wawili ni Makatibu. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, tuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni 24, wageni wa Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Dkt. Laurean Ndumbaro - Katibu Mkuu Utumishi, Ndugu Dorothy Mwaluko - Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Charles Mwankupuli - Kaimu Katibu Mkuu Ikulu, Mheshimiwa Jaji Mstaafu Harold Nsekela – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ndugu Waziri Kipacha – Kamishna wa Maadili, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ndugu Valentino Mlowola – Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU. *(Makofi)*

Wageni hawa wameambatana na Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hiyo. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Mkuchika. *(Makofi)*

Wageni 66 wa Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao ni viongozi wa Wizara hiyo pamoja na familia yake wakiongozwa na *Engineer* Mussa Iyombe - Katibu Mkuu, Dkt. Zainabu Chaula - Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Tixon Nzunda – Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Binilith Mahenge – Mkuu wa Mkoa Dodoma, Ndugu Rehema Madenge – Katibu Tawala, Mkoa Dodoma na Ndugu Mariam Mvano – Kamishna Tume ya Utumishi wa Walimu. Pia hawa wameambatana na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na Idara zilizo chini ya Wizara hiyo. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Jafo. *(Makofi)*

Wageni wengine ni familia yake wakiongozwa na mkewe Bi. Asha Shame Vuai, karibu sana familia hii ya Mheshimiwa Jafo. *(Makofi)*

Wageni 26 kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambao ni Profesa Mussa Assad – Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameambatana na Manaibu Wakaguzi Wakuu watano, pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 25 wa Mheshimiwa Stephen Ngonyani ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hamidu Bobali ambaye pia ni mpiga kura wake kutoka Mchinga Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambao ni Wanakwaya wa Kwaya ya Vijana wa Parokia ya Ukonga wa Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Katibu tuendelee.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Miongozo, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Jaku, Mheshimiwa Nkamia, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Kubenea, wote mnataka! Haya Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Haonga, haya tuanze.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Maige.

**MWENYEKITI:** Nani?

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Maige.

**MWENYEKITI:** Yuko wapi?

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mbele yako hapa.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Maige. Haya tunaanza na Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwongozo wangu ulikuwa unahitaji ufafanuzi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wangu unatokana na jambo ambalo Mheshimiwa Spika alizungumza jana jioni na ambalo linaendelea sasa hivi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi kinachofanyika Dar es Salaam kila mmoja wetu anakipenda, *idea* anaipenda, ila njia inayotumika ni ya kubomoa siyo ya kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba majibu kutoka Serikali, kwa kuwa moja, Katiba ya Jamhuri ya

Muungano, Ibara ya 16 inatakiwa kila mwananchi alindwe faragha yake, nafsi yake na maisha yake binafsi. Utakubaliana na mimi kinachofanyika Dar es Salaam tunaya-*expose* maisha binafsi ya watu kwa mambo ambayo chanzo chake ni cha siri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, Sheria ya Kumlinda Mtoto ya mwaka 2009 inazuia kuweka hadharani picha za mtoto kwa madhumuni ambayo hayafai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi, kwa maisha yetu ya kimitandao, kwa mfano mimi utakuta nina watoto wangu tumepiga picha mtandao, lakini watu wanazichukua zile picha wanasema kuwa huyu ametelekeza mtoto na wakiangalia kweli wanafanana. Kwa mfano, kuna rafiki yangu mmoja kule wameweka picha za mtoto wake tena kafanana naye kweli pale hachomoki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, linabomoa na linajenga uadui wa kudumu baina ya familia hizo. Mtakubaliana na mimi, sidhani kama kuna baba atakayethubutu kumsogelea mama au mtoto ambaye amemu-*expose* kwenye vyombo vya habari, kwa hiyo, inajenga uadui wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa sisi wale waislamu, mtoto wa nje ya ndoa tunaita haramu siyo mtoto wa baba. Sasa kitendo cha kuendelea ku-*expose* mambo hayo hadharani inaingilia masuala yetu ya dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge suala la mtoto siyo kubwa vile kama linavyowekwa. Kwa sisi kwa mfano Wapogolo ukishakula wali ni sekunde moja tu mtoto anapatikana. Kwa hiyo, siyo suala kubwa kama wanavyolifikiria. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba majibu ya Serikali, *idea* ni nzuri lakini njia ambayo inatumika ni mbaya. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Nilikuwa naomba Mwongozo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini wakati akijibu swali namba 59 lililoulizwa na Mheshimiwa Maige na mimi nikapewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Niliuliza kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Geita inaudai mgodi dola milioni 12 na baada ya mgogoro kati ya Halmashauri na mgodi ilipelekea Katibu Mkuu, TAMISEMI kuita pande zote mbili na kututaka twende tukakae tukubaliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoenda kukubaliana wakatupa masharti ya kutaka kama kutuhonga dola laki nane halafu tusidai pesa zingine. Katibu Mkuu Madini akaandika barua ya kuwaelekeza mgodi watulipe pesa zetu bila masharti mwisho wa mwezi Februari, lakini mpaka leo bado kuna danadana na tumeshapeleka *demand notes* zaidi ya mara mbili, ndiyo maana nikaomba msaada kwenye Wizara. Sasa Waziri alipokuwa akijibu hili swali langu amejibu tena kama tunaanza mchakato wa mwezi Februari. Mwongozo wangu nataka kujua ni nini msaada wa Wizara ya Nishati na Madini kwenye hela zetu tunazodai Mgodi wa *GGM?* Ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa dhati kabisa na nitakuwa mtovu wa adabu kama sikukushukuru. Tokea Jumatatu na Jumanne hatimaye leo Jumatano nimekuwa nikifanya mazoezi ya kusimama na kukaa lakini leo nimefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo unasema anayehangaika hachoki akishapata ndiyo anachoka. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), leo hii nilikuwa na taarifa kuwa swali langu linakuja Bungeni. Nimejiandaa na majirani zangu hapa wamenisaidia hawaoni jina langu katika *Order*

*Paper* na swali hili limeandikwa kiswahili wala si kizungu, kijapani wala kifaransa na swali hili nimelileta inakaribia miezi miwili. Je, kuna utata gani Serikali kushindwa kujibu swali langu hili? Swali kama lina matatizo kwamba halijakaa sawa Mwalimu wangu Mheshimiwa Jenista nimshukuru sana aliniongoza vizuri lakini sijapata taarifa. Kuna ugumu gani wa swali hili kutopata maelezo na mimi nishajiandaa leo kuja kusikiliza swali langu.

**MWENYEKITI:** Swali lipi hilo Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Sijui ni lipi katika maswali yangu, ni Mahakama ya Kadhi, nimeshalikumbuka maana nina maswali matatu. Suala hili limepata kigugumizi na chombo hiki kimeahidiwa humu ndani kwamba wanakwenda kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wa Kiti chako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 68(7), naomba mwongozo wako kutokana na mambo ambayo yametokea hapa Bungeni. Leo Naibu Waziri wa Elimu kaka yangu Mheshimiwa Olenasha wakati anajibu swali la Ester Bulaya alizungumzia juu ya ajira za walimu na juhudi ambazo zinafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mwongozo wangu uko hivi, sasa hivi *NIDA* wanaandikisha Vitambulisho vya Taifa karibu Wilaya zote Tanzania, lakini wanawatumia walimu wa shule za sekondari kuandikisha vitambulisho hivi na walimu hawa hawafundishi madarasani. Kinachofuatia ni watoto wakishindwa kufaulu vizuri tunalalamika kwamba walimu hawatoshi. Pia *NIDA* badala ya kutumia bajeti zinazopitishwa na Bunge hili wanakwenda kwenye Halmashauri kuzitaka ndiyo ziwalipie gharama za kufanya zoezi la Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali na bahati nzuri Waziri wa Mambo ya Ndani yuko hapa, hivi hawa *NIDA* hakuna bajeti maalum kwa ajili ya zoezi la Vitambulisho vya Taifa? Matokeo yake sasa Halmashauri ambazo hazina uwezo wanazitaka ndiyo ziwalipie posho hawa watumishi wanaofanya zoezi la Vitambulisho vya Taifa.

Kwa hiyo, naomba kauli ya Serikali, je, ni kwamba Serikali imeshindwa kuwahudumia hawa watu au wanadanganya wanachukua hela mara mbili? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nasimama kwa Kanuni ya 68(7). Jana wakati nilipouliza swali langu kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani, swali namba 50, swali la pili lilihusiana na ucheleweshwaji wa ushahidi kupelekwa Mahakamani jambo linalochangia kwa kiasi kikubwa Mahakama kushindwa kumaliza kesi zilizopo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilishindwa kusimama kuomba Mwongozo kwa sababu nilitaka nijiridhishe vizuri kupitia Kumbukumbu za Bunge majibu halisi aliyonijibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Nimejiridhisha pasipo na shaka kwamba jibu lake lilikuwa kwamba hatupaswi kuzungumzia masuala yaliyoko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipitia tena Kumbukumbu za Bunge nikagundua *ruling* aliyotoa Mwenyekiti Chenge katika jambo linalohusiana na hilo akisema kwamba Bunge au Mbunge hazuiwi kuongelea juu ya mwenendo wa mashtaka kwa masuala yaliyoko Mahakamani. Kinachozuiwa ni kuingilia mwenendo wa Mahakama au kuingilia kazi ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni nyeti sana kwani washtakiwa na mahabusu walioko Mahakamani kwa sasa ndani ya nchi yetu wamezidi kipimo. Tunapouliza suala hili

juu ya ucheleweshwaji wa kesi jambo ambalo si jukumu la Mahakama ni jukumu la Waendesha mashtaka na Ofisi ya *DPP*, hiki ndio kiini cha swali langu.

Je, inafaa Mheshimiwa Naibu Waziri kuendelea kukwepa kujibu suala la msingi na badala yake kuisingizia Mahakama kana kwamba Bunge hatuna haki ya kuhoji juu ya chombo hiki cha *DPP* na Waendesha Mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 68(7) kwa mambo ambayo yametokea humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati wa kupitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilisimama kuzuia shilingi nikitaka maelezo ya Waziri kuhusiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba Serikali ilete Muswada wa Mabadiliko ya Sheria yatakayoifanya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa chombo huru na kinachoaminika miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisimama akasema kuna kesi iko Mahakamani inayojadili Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kwa msingi huo jambo hilo haliwezi kujadiliwa Bungeni. Hata hivyo, tayari Mheshimiwa Khatibu amesaidia hapa kutoa uamuzi *(ruling)* iliyotolewa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelipotosha Bunge, ameingilia kazi za Bunge na amempotosha Mheshimiwa Spika. Kesi iliyopo Mahakamani...

**MWENYEKITI:** Hebu rudia hapo nani kampotosha Mheshimiwa Spika?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi iliyopo Mahakamani ni kesi Na. 6 ya mwaka 2018 inayoomba tafsiri ya ushiriki wa makada wa Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi, ndiyo kesi ya msingi. Jana nilitoa mfano kwamba ilikuwepo kesi ya Kikatiba ya ku-*challenge* Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na Serikali ilileta Muswada Bungeni wakati kesi iko Mahakamani ya kuunda Sheria mpya ya Magazeti na Sheria mpya ya Kupata Habari na sheria hizo zimejadiliwa ndani ya Bunge hili na zimepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini orodha ya kesi ambazo zilikuwepo Mahakamani na Serikali ikaendelea na kazi zake za kutunga sheria ni pamoja na kesi ya Bunge Maalum la Katiba ambayo ilikuwa inaomba tafsiri na kesi ya viongozi wa Chama cha Wananchi *(CUF)*. Bunge halikuzuiwa kupokea Wabunge wengine walioletwa na upande mwingine pamoja na kwamba kuna kesi iko Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kauli ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itachukuliwa ndio msingi katika Bunge hili…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea, naomba umalize haraka.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MBUNGE FULANI:** Anapotosha Bunge, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Kaa wewe.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza. Ibara ya 97(5)…

**MBUNGE FULANI:** Anapotosha Bunge huyu.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Inaeleza masharti ya utungaji wa sheria ndani ya Bunge. Suala la kesi kuwepo Mahakamani siyo sehemu ya hayo mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kitendo kilichofanywa jana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni halali ndani ya Bunge letu? Je, Bunge linamchukulia hatua gani Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzuia Wabunge wasifanye kazi yao kwa kusingizia Mahakama? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni la bajeti na jana tulianza kupitisha bajeti ya Waziri Mkuu lakini mpaka navyoongea ni ajabu sana, tunatakiwa tuwe na *Volume IV* kwa maana ya *Volume I* ile ya mapato, tuweze kupata *reflection* ya mapato ya Serikali, lakini tuna *Volume II* ambayo ni *estimate of public expenditure consolidated funds and supply vote* kwa maana ya *ministerial,* tuna *Volume III* ambayo ni *estimates of public expenditure supply vote* ya mikoa na tuna *Volume IV* ambayo ni *public expenditure estimates development vote* (ya maendeleo). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumepitisha bajeti ya Waziri Mkuu bila kuwa *Volume I* ya mapato na hii imekuwa ni mazoea, tunavyokuwa tunapitisha bajeti lazima tuweze ku-*compare* mapato na matumizi. Sasa sijui Serikali inaficha nini kwa kutuletea hiyo *Volume I.* Napenda kabisa tunavyoenda kuanza Wizara ya TAMISEMI tuweze kuletewa hicho kitabu cha *Volume I* ili tuweze kufanya *reference. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wangu ni kwamba naomba utuhakikishie kwamba tunavyorudi

mchana tukute vitabu vya *Volume I* ili tuweze kuendelea vizuri katika kutimiza wajibu wetu wa kupitisha bajeti. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na kwa sababu ya muda sitapenda kuisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara nyingi sasa tumeona wakati mwingi viti vya mbele hivyo ambavyo anatakiwa kuwepo mwakilishi wa Serikali vimekuwa wazi mara kadhaa. Leo hata unamuona Mheshimiwa Jenista yupo hapo amekuja muda sio mrefu lakini muda mwingi niliona muda mrefu pako wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, je, inaruhusiwa vile viti vinne vya mbele kubaki wazi kwa muda mrefu?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mbona Mbowe hayupo, mbona Mbowe hayupo?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Maige atamalizia Mheshimiwa Amina Makilagi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu Waheshimiwa Wabunge, endelea Mheshimiwa Maige.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Ndanda Kosovo hayupo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), nilitaka kuzungumzia kuhusu Kanuni ya 46 ya swali kujibiwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza swali namba 59 na kabla ya kuuliza maswali ya nyongeza nili-*register* masikitiko yangu kwamba swali halikuwa limejibiwa kwa ufasaha na mbaya zaidi likawa limesema vitu ambavyo sio vya kweli. Hivi tunavyozungumza simu yangu hapa ina *video clips* za wananchi wanalia kule Kakola wakisikitika kwamba kwa miaka 20 Serikali imekuwa ikijua kwamba hawajalipwa fidia, leo Serikali inakuja kusema kwamba wamelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lilikuwa zito, nilitaka kujua mazungumzo kuhusu suala zima la makinikia kwa sababu wananchi wa Kakola Bulyanhulu ndiyo wadau wakubwa, yapo mambo yao yanawahusu ambapo wanadai *service levy* shilingi bilioni 973. Nimependekeza kutokana na hali ilivyo kwa sasa hivi Mgodi wa Buzwagi wanauza mitambo yao, angalau ile mitambo itolewe kwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kama sehemu ya fidia ya hiyo shilingi bilioni 973, yote hayo hayajajibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuomba mwongozo wako, katika mazingira kama haya ni kwa nini Mheshimiwa Waziri ama asiende kulijenga jibu lake vizuri zaidi na lije lijibiwe upya au ikiwezekana sisi wenyewe na Serikali tupate tume kamili inayojitegemea itakayoenda kuangalia hali ya Kakola na kuweza kujua kwa mfano hata hilo suala la wagonjwa amesema kuna wagonjwa 78 lakini mimi navyojua wagonjwa 78 ni wale wanaoumwa sasa hivi lakini wapo 49 ambao wameshakufa kutokana na madhara wanayoyapata mgodini lakini Serikali haijasaidia lolote kwa wagonjwa hao kutibiwa, hata sasa hivi hawatibiwi.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mwongozo wako katika mazingira haya

ni namna gani Serikali inaweza ikarekebisha jibu lake na kujibu kwa usahihi kama ambavyo wananchi wanataka kusikia. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka, ahsante. Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kuna jambo ambalo limetokea jana lakini linaendelea mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Spika wakati akifunga Bunge alitujulisha kwamba wapo vijana wetu mahiri, ambao ni askari wetu na akawa amemtaja kijana wetu Rashid Kapongo kwa niaba ya mwenzake yule Milton Malumbe kwamba walifanya kazi nzuri sana ya kuzima moto tena baadhi ya wale vijana waliondoa *power bank* ndani kwa mkono.

Kwa kweli mimi kama mama na hata baadhi ya Wabunge tuliwiwa kwamba kumbe tuna vijana shupavu ambao walituokoa sisi kuathirika kama Wabunge, lakini vilevile kuteketea kwa Bunge maana siyo tuseme mabaya tu ya askari wetu, tuseme hata haya mazuri. Kwa kweli mimi naomba niungane na Wabunge wenzangu kupongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwashawishi Wabunge wenzangu na naomba wote mniunge mkono, kama ambavyo tumekuwa tukisaidiana kwenye maafa, harusi, kwa raha na shida na hawa vijana wetu kila mmoja achangie shilingi 40,000.

**MBUNGE FULANI:** Wapandishwe vyeo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kila Mbunge achangie shilingi 40,000.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Apandishwe cheo hela haitamsaidia kitu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kila mtu atoe kwa hiyari yake…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu tumsikilize amalize.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Wapandishwe vyeo hali ngumu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchangie…

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Cheo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Sisi Wabunge tuchangie kama motisha na kuwashika mkono.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Wapandishwe cheo

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Lakini vilevile wafikiriwe…

**MBUNGE FULANI:** Wapewe *promotion.*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Katika kuongezewa madaraka katika nafasi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mniunge mkono katika jambo hili na leo tuanze na kama tutachanga vizuri tutapata...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Jeshini hakuna mchango kuna cheo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Tutapata zaidi ya shilingi milioni 20 na hawa vijana kila mtu atapata shilingi milioni 10 kama mkono wetu wa kuwapa hongera. *(Makofi)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Jeshini hakuna mchango, kuna cheo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa yamemalizika hayo, tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mwongozo alioomba Mheshimiwa Mlinga kuhusiana na suala lililozungumzwa na Mheshimiwa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Naomba tusikilizane Waheshimiwa au hamtaki kusikiliza miongozo niache?

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na mwongozo wa Mheshimiwa Mlinga kuhusu suala lililotokea jana ambalo Mheshimiwa Spika alizungumzia lile la zoezi linaloendelea Dar es Salaam. Amezungumzia zaidi kisheria, ameifafanua vizuri sina haja ya kurejea, kila mtu anastahili kulindwa faragha yake kwa mujibu wa Ibara ya 16.

Kuhusu Mwongozo huu nasema kwa vile jambo hili lipo kisheria zaidi lakini pia hakuna ambaye anapinga suala la utelekezwaji wa watoto kuwa ni baya hasa sisi wanawake na kwa vile linaendelea kwa maana ya kwamba ni endelevu, hatuna uthibitisho kamili wa kwamba hao Waheshimiwa Wabunge wetu waliotajwa ndiyo wenyewe wanaohusika na suala hilo na wala hatuna uhakika kwamba ndiyo, kwa hiyo, kama ni ndiyo ama siyo hatuna uhakika na jambo hilo mpaka sasa hivi. Pia Bunge siyo kazi yake kujadili suala ambalo limezungumzwa mitaani ama kwenye mitandao ingawa suala hili linatugusa.

Kwa hiyo, tusubiri utakapomalizika huo mchakato unaofanywa na uhalisia ukapatikana na ukweli ukadhihirika,

kila mmoja atabeba kwa mujibu wa sheria. Ikiwa imebainika kwamba kweli Mbunge amefanya kitendo hicho atakamatwa kwa sheria yake ...

**MBUNGE FULANI:** Umechemka.

**MWENYEKITI:** Na ikiwa hakufanya na yeye ataweza kutoa namna nyingine kwa sheria yako.

Huo ndiyo Mwongozo hili jambo bado linaendelea haliwezi kutolewa maamuzi kwa sasa hivi.

Tunaenda na suala la ...

**MBUNGE FULANI:** Mpe Waziri wa Afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, naomba tusikilizane au hamtaki majibu ya miongozo?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Kuna udhalilishaji wa watoto hapo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaeleze muelewe, nimeshasema Mwongozo wangu ni huo kwamba suala hili ni la kisheria na litafuatiliwa kwa mujibu wa sheria.

**MBUNGE FULANI:** Kuna udhalilishaji wa watoto hapo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Hatuna ushahidi wa Mbunge yeyote, Waheshimiwa tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Kuna udhalilishaji wa watoto hapo. Tunazungumzia watoto siyo Wabunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nimeshasema, suala lote hilo la watoto na Waheshimiwa Wabunge ni moja, naomba tafadhali...

**MBUNGE FULANI:** Asimamishwe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Tunaomba Waziri wa Afya atujibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Milinga...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hoja ya kuvunja Katiba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlinga ameshanielewa ndiye aliyeomba Mwongozo, naomba mtulie.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hoja ya uvunjaji wa Katiba.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sitaki fujo.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hoja ya uvunjaji wa Katiba.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mlinga keshaelewa kaniambia.

**MBUNGE FULANI:** Hajaelewa huyu kasimama.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Musukuma kuhusu Naibu Waziri wa Madini alivyomjibu, suala hili tutalipitia kwenye *Hansard* na kuangalia usahihi wake na baadaye tutatolea majibu.

Suala la Mheshimiwa Jaku kuhusiana na swali lake aliloleta la Mahakama ya Kadhi tunawaachia Kamati ya Bunge yenyewe itatuambia au itatujibu kwa nini swali hili halijaletwa au kuna tatizo gani, inabidi yeye mwenyewe aweze kufuatilia na kujua zaidi.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati gani?

**MWENYEKITI:** Uongozi wa Bunge kwa maana ya Katibu wa Bunge, naomba uonane naye ili ujue swali lako lina tatizo gani.

Mheshimiwa Nkamia kuhusu mambo yaliyotokea Bungeni kwenye swali la Mheshimiwa Ester Bulaya kuhusu ajira za walimu na vitambulisho vya taifa, nalo hilo litafanyiwa kazi na kutolewa majibu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Khatib kuhusu swali la jana la Mambo ya Ndani, hali kadhalika suala hilo litafuatiliwa na kuonekana kama limejibiwa kisahihi ama halikujibiwa, kwa hiyo, litaletwa. Ikiwa kama kweli Waziri amekwepa tutaona majibu hayo.

Mheshimiwa Kubenea, anasema wakati wa kupitisha bajeti kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi alizungumzia kuhusu Serikali kuleta Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili iwe huru. Lakini mimi kwa maoni yangu na navyoona mpaka sasa hivi hii ni Tume huru mpa sasa hivi. Kwa hiyo, tuendelee na mengine yaliyo ya muhimu na hilo la kuwa Tume huru tayari hiyo ni Tume huru.

Kuhusu suala la kwamba Mwanasheria Mkuu kuwa amempotosha Spika sio la kweli, suala alilozungumza ni kwamba hatustahili kuzungumzia masuala ambayo yapo Mahakamani. Suala hilo lipo kikanuni kwa maana Kanuni zetu zinatukataza na lazima tutii Kanuni zetu.

Suala lingine ameuliza Mheshimiwa Matiko kuhusu *volume* za vitabu hilo suala siwezi kulijibu kwa sasa hivi nitalijibu hapo baadae. Kwanza hutakiwi kusema kwamba vitabu vipatikane mchana, hutakiwi kuiagiza Serikali kwa namna hiyo yaani hutakiwi kutumia lugha uliyotumia lakini naambiwa vitabu hivyo vipo tayari na mchana vitakuwepo.

Mheshimiwa Haonga anasema wawakilishi wa Serikali hawapo, siyo kweli. Siku zote katika Bunge hili lazima wawakilishi wa Serikali wawepo na Mawaziri na Naibu Mawaziri wanakuwepo na wao ndiyo wawakilishi wa Serikali ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maige naye alisema swali lake namba 59 halijajibiwa, tutaangalia kwenye *Hansard* tuone kama kweli halijajibiwa ipasavyo tutaweza kulileta baadae.

Mheshimiwa Amina Makilagi huo siyo mwongozo, ameomba tu Wabunge kwa hiyo mna hiyari ya kukubaliana naye.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hiyo ndiyo majibu ya miongozo kwa leo, Katibu tuendelee.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hoja ya kuvunja Katiba, hoja ya kuvunja Katiba.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo tu.

**MWENYEKITI:** Taarifa unampa nani?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hoja ya kuvunja Katiba.

**MHE. JUMA S. NKAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe ruhusa niseme kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu wa Kanuni zinazoongoza Bunge...

**MWENYEKITI:** Nani anayezungumza huyo ambaye hajapewa ruhusa? Katibu naomba tuendelee. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tunaanza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, karibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha hotuba yangu hapa, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama tulivyoi-*table* hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa

kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Kwa heshima na taadhima, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza nchi yetu kwa falsafa ya uchumi wa viwanda na utekelezaji makini wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Vilevile nawapongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kwa uongozi wao mahiri na miongozo ambayo imetoa dira katika utekelezaji wa utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, lakini nimpongeze Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge hapa Bungeni. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya njema na hekima katika kuongoza mhimili huu muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo Novemba, 2017 Bunge lako tukufu liliondokewa na Mheshimiwa Leonidas Gama aliyekuwa Mbunge wa Songea Mjini. Kwa masikitiko makubwa napenda kutumia fursa hii kukupa pole wewe Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge pamoja na Wabunge wote wa Bunge hili tukufu kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu mahiri. Aidha, natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wote waliofiwa na wapendwa wao katika ajali za magari, pikipiki na nyinginezo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kwa kuchaguliwa tena kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati na

Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa tena kwa mara nyingine ya pili kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Kuchaguliwa kwao kwa mara nyingine kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kunadhihirisha wazi kwamba kwa uongozi na umahiri wao katika kuiongoza Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati kwa kupoea na kuchambua kwa kina na hatimaye kupitisha makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, naomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Fungu 56; Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu namba 02 pamoja na mafungu mengine 26 ya Mikoa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 6.57 kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.27 ni mishahara, shilingi bilioni 519.45 ni matumizi mengineyo na shilingi trilioni 1.78 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.31 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 467.67 ni fedha za nje. Hadi Februari, 2018 fedha zilizopokelewa ni shilingi trilioni 3.33 sawa na asilimia 50.68 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maduhuli, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mikoa, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa kukusanya

maduhuli ya shilingi milioni 14. Hadi Februari, 2018, makusanyo halisi yalikuwa shilingi milioni 10.3 sawa na asilimia 74 ya lengo. Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI zimekusanya maduhuli ya shilingi bilioni 9 kati ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 22.8 sawa na asilimia 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maduhuli yaliyokusanywa na mikoa yalikuwa shilingi bilioni 3.3 sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 3.51 katika kipindi hicho. Kuimarika kwa makusanyo ya maduhuli ya mikoa kumetokana na ufanisi wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa *GoT-HOMIS* unaotumika katika Hospitali za Mikoa, matumizi ya kadi katika kufanya malipo na kuimarika kwa usimamizi wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani ya halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 687.30 kutoka vyanzo vya mapato ya ndani. Hadi Februari, 2018 shilingi bilioni 343.82 zimekusanywa, sawa na asilimia 50 ya makadirio. Kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la shilingi bilioni 90.68 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 253.12 zilizokusanywa hadi Februari, 2017. Ongezeko la makusanyo limechangiwa na kuimarishwa kwa usimamizi, elimu na uhamasishaji kwa walipa kodi, ushuru mbalimbali pamoja na matumizi ya mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama *Local Government Revenue Collection Information System* ambao umefungwa katika Halmashauri zote 185.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, hadi kufikia Februari 2018, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na taasisi zake imepokea jumla ya shilingi bilioni 245.17, sawa na asilimia 53 ya bajeti ya shilingi bilioni 459.41 iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu katika mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa upande wa mikoa, fedha zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 285.13 ambapo kiasi kilichopokelewa ni shilingi bilioni 156.18, sawa na asilimia 55. Aidha, Halmashauri zimeidhinishiwa shilingi trilioni 5.81 ambapo tayari jumla ya shilingi trilioni 3.17 zimepokelewa hadi Februari, 2018, ikiwa ni sawa na asilimia 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utawala bora, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa walipata fursa ya kushiriki vikao mbalimbali ambavyo viliwasaidia sana kutimiza majukumu yao. Aidha, mafunzo ya kujenga uwezo yalitolewa kwa Wakuu wa Wilaya 139, Wakurugenzi wa halmashauri 185, Maafisa Utumishi 185 na Maafisa Mipango 185. Aidha, viongozi na watendaji hao wamekumbushwa wajibu wa kusimamia maendeleo na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika maeneo yao ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi za halmashauri za wilaya mpya pamoja na nyumba za viongozi zikiwemo nyumba za Wakuu wa Wilaya. Ujenzi huo umeendelea katika halmashauri mbalimbali hapa nchini zikiwemo Halmashauri za Wilaya za Gairo, Kiteto, Mkarama, Ikungi, Busega na Halmashauri za Wilaya nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeendelea kuimarika. Kwa mujibu wa Hati ya Ukaguzi iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kati ya Halmashauri 185 zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri 166, sawa na asilimia 90, zimepata hati safi; Halmashauri 16 zimepata hati zenye mashaka na Halmashauri tatu tu zimepata hati chafu ikilinganishwa na ukaguzi uliofanyika mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo kati ya halmashauri 171 zilizokaguliwa, halmashauri 138, sawa na asilimia 81, zilipata hati safi, Halmashauri 32 zilipata hati zenye mashaka na Halmashauri moja ilipata hati chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hatua mbalimbali za kudhibiti ubadhirifu na ukiukwaji wa sheria zimechukuliwa kwa watumishi walioshindwa kutimiza wajibu wao ambapo watumishi 434 waliobainika kwa ubadhirifu na ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi na Utumishi wa Umma wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na wengine 28 michakato ya

nidhamu inaendelea ili waweze kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti kupitia Mfumo wa *EPICOR* ambapo halmashauri zilizounganishwa katika mfumo huo zimeongezeka kutoka halmashauri 168 katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi halmashauri 185 katika mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, Serikali imeanzisha Mfumo wa *Tanzania Interbank Settlement System – TISS* ambapo malipo yote ya Serikali yanafanyika kutoka akaunti zilizofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania kwenda moja kwa moja kwa mlipwaji. Mfumo wa *TISS* umeunganishwa katika Mikoa 11 ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro, Lindi, Mtwara, Mwanza, Songwe, Pwani na Tanga kwa kuzifikia jumla ya Halmashauri 77. Mikoa 15 iliyobaki na Halmashauri zake itaunganishwa kwenye mfumo katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika utengaji wa maeneo ya uwekezaji, hadi Februari, 2018, Halmashauri 184 zimetenga maeneo yenye ukubwa wa hekta 196,710 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa. Aidha, katika utekelezaji wa agizo la ujenzi wa viwanda 100 kwa kila mkoa, jumla ya viwanda 1,285 vimejengwa kati ya mwezi Novemba, 2017 hadi Machi, 2018 ambapo utekelezaji huo ni sawa na asilimia 49.4 ya malengo yaliyowekwa ya kujenga viwanda 2,600 kwa mikoa yote 26. Katika mafaniko haya, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza viongozi wote wa Mikoa na Wilaya kwa usimamizi wao wa agizo hili lenye lengo la kupunguza tatizo la ajira hapa nchini na kukuza uchumi wa nchi pamoja na kupitia uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA iliyopo kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utendaji na uwajibikaji. Mifumo hiyo ambayo imesimikwa na kuimarishwa hadi sasa ni pamoja na mfumo funganishi na usimamizi wa udhibiti

wa matumizi wa fedha *(EPICOR), Facility Financial Accounting and Reporting System (FFARS),* Mfumo wa kuandaa Mipango na Bajeti za Halmashauri *(PlanRep-Web based), Basic Education Management Information System, Government of Tanzania Hospital Management Information System* pamoja na *Local Government Revenue Collection Information System.* Mifumo hii ya kielektroniki imeongeza ufanisi katika utendaji kazi, imepunguza gharama na imeongeza udhibiti wa rasilimali, uwajibikaji na upatikanaji wa taarifa, hivyo kuwawezesha viongozi kufanya maamuzi sahihi kwa wakati mwafaka. Ili kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, mafunzo ya kujenga uwezo yametolewa kwa watumishi 262 wa mikoa na watumishi 1,507 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake umetengewa jumla ya shilingi bilioni 61.6 ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya mikopo ya vikundi 18,233. Hadi Februari, 2018, kiasi cha shilingi bilioni 15.6 zimetolewa kwa vikundi 8,672 vya wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Programu ya *Local Investment Climate* hadi Februari, 2018 jumla ya shilingi bilioni 2.89 zimetumika katika kuendesha shughuli za program za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Aidha, jumla ya wananchi 1,000 wamewezeshwa kuandaa maandiko ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inahusika na uratibu pamoja na usimamizi wa hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati ili kuhakikisha zinatoa huduma bora kwa afya ya wananchi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, ujenzi wa hospitali mpya za wilaya umeendelea katika Wilaya mbalimbali zikiwemo Wilaya za Kilolo, Mvomero, Siha, Buchosa, Morogoro na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha sekta ya afya katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliamua kuweka jambo la kihistoria hapa nchini kwa kuanza zoezi kubwa la kuboresha vituo vya afya 208 ili kuviwezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji. Zoezi hili limehusisha ujenzi wa majengo ya upasuaji, wodi ya akina mama, wodi ya kujifungulia, maabara, nyumba ya daktari, majengo ya kuhifadhia maiti na ujenzi wa vichomea taka ili kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto. Hadi sasa ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 44 umekamilika na vituo vingine vilivyobaki vipo katika hatua mbalimbali ya ujenzi na maandalizi. Zoezi la ujenzi na ukarabati wa vituo hivyo, sambamba na upatikanaji wa vifaa pamoja na ukamilishaji wa zoezi la uboreshaji wa mifumo ya kupeleka fedha vituoni linagharimu jumla ya shilingi bilioni 156.7. Mpango uliopo ni kuhakikisha vituo vyote vya afya vilivyopo hapa nchini vinatoa huduma ya upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kuboresha afya ya msingi, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya shilingi bilioni 35.5 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa zahanati na kipaumbele kikiwa ni kukamilisha ujenzi wa maboma yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi ambapo kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2018. Katika upande wa madawa, Serikali imeongeza bajeti ya dawa, vifaatiba, chanjo na vitendanishi kutoka shilingi bilioni 31 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi shilingi bilioni 269 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Juhudi hii kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewezesha upatikanaji wa dawa muhimu kwa sasa kufikia asilimia 92 ikilinganishwa na asilimia 81 katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa huduma za ustawi wa jamii unatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Katika kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo, kwa mwaka 2017 Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilitoa waraka kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa

kuwakumbusha na kuwataka Wakuu wote wa Mikoa katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza maelekezo hayo ili kuimarisha ustawi wa makundi yote ya jamii, hususan watu wenye ulemavu. Kutokana na juhudi kubwa iliyofanywa, kwa sasa watu wenye ulemavu wapatao 221,090 wametambuliwa na kupatiwa huduma zikiwemo vifaa vya shule, kofia za kuzuia jua na mafuta ya ngozi kwa watoto wenye ualbino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Afya ya Jamii, jumla ya wanachama 12,278,406 wamejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)* katika mwaka 2017. Hadi Machi, 2018 jumla ya shilingi bilioni 22.5 zilikuwa zimekusanywa na Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Halmashauri zimetunga Sheria Ndogo ambazo zimeweka viwango vya michango kati ya shilingi 5,000 hadi 30,000 kwa kila mwanachama. Aidha, katika kuimarisha afya ya wazee, jumla ya wazee 1,652,206 wasiokuwa na uwezo wametambuliwa katika mikoa 22 ambapo kati yao, wazee 462,513 wamepatiwa kadi za *CHF* kwa ajili ya matibabu bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa elimu ya msingi na sekondari; Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuboresha utoaji wa elimu katika ngazi zote za elimu ya awali, msingi na sekondari. Hadi Machi, 2018 shule za msingi zipatazo 16,140 ambapo kati ya hizo, shule 16,004 zina madarasa ya elimu ya awali, sawa na asilimia 99.2 ya lengo. Wanafunzi wa elimu ya awali walioandikishwa hadi Machi, 2018 ni 1,283,790 sawa na asilimia 85.7 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,498,043.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa darasa la kwanza, wanafunzi walioandikishwa hadi kufikia Machi, 2018 walifikia wanafunzi 1,751,221 ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi 1,732,303 sawa na asilimia 100.1 ya lengo. Wito unatolewa kwa wazazi na walezi na jamii kwa ujumla kwamba wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anaandikishwa na kuanza masomo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu na wananchi, imekamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 2,278 kwa shule za msingi. Ujenzi huo umeongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka 120,766 vilivyokuwepo mwaka wa fedha 2016/2017 hadi vyumba vya madarasa 123,044 kufikia Machi, 2018, sawa na ongezeko la asilimia 1.8. Aidha, nyumba za walimu zimeongezeka kutoka nyumba 43,075 zilizokuwepo mwaka 2017 hadi 43,365 sawa na ongezeko la nyumba 290 zilizojengwa hadi Machi, 2018.

Aidha, Machi, 2018, jumla ya matundu ya vyoo 6,274, ofisi za walimu 316 na maktaba 165 zimejengwa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imefanikiwa kuajiri walimu wapya wapatao 2,767. Serikali imewahamisha walimu wa ziada 8,834 wa masomo ya sanaa na lugha kutoka shule za sekondari kwenda katika shule za msingi na kufanya upungufu wa walimu kuwa 85,916 ikilinganishwa na upungufu wa walimu 97,517 kwa mwaka uliopita, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017, ufaulu wa wanafunzi wa darasa la nne umepanda hadi asilimia 97.1 ya lengo ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 93.76 kwa mwaka 2016. Kwa upande wa darasa la saba ufaulu umepanda hadi asilimia 72.75 kwa mwaka 2017 ikilinganishwana ufaulu wa asilimia 70.84 kwa mwaka 2016. Hali hii imetokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuimarika usimamizi wa shule pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa kwa walimu wa masomo mbalimbali, walimu wakuu, waratibu wa elimu kata na maafisa wa elimu wafikao zaidi ya 17,518.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu ya sekondari, katika mwaka 2018 wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza walikuwa 661,059 ikinganishwa na wanafunzi 555,291 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika mwaka 2017, sawa na ongezeko la wanafunzi 105,768 ambao ni asilimia 19.05. Hadi Machi, 2018, wanafunzi wapatao 586,830 wameripoti katika shule walizopangiwa, sawa na asilimia 88.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha elimu ya sekondari, hadi Februari, 2017, nyumba za walimu wapya 274, vyumba vya madarasa 788, matundu ya vyoo 2,071, maktaba 176 na mabweni 543, majengo ya utawala 36 na maabara 165 zimejengwa. Utekelezaji umefanyika kupitia fedha za Programu ya Elimu ya Lipa Kulingana na Matokeo *(EP4R)* pamoja na fedha za ndani za Halmashauri. Serikali inaendelea na ukarabati wa shule kongwe 89 hapa nchini ambapo shule 43 ukarabati wake umekamilika. Ukarabati unahusisha kuondoa miundombinu iliyochakaa ikiwemo paa, kupaka rangi, kuboresha mifumo ya maji safi na maji taka, umeme na kujenga miundombinu mipya kulingana na tathmini ya mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa fedha za Elimumsingi Bila Malipo kila mwezi tangu mpango huo uanze kutekelezwa Desemba, 2015. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Februari, 2018, Serikali imefanikiwa kutoa jumla ya shilingi bilioni 172.4 kugharamia Mpango wa Elimumsingi bila Malipo ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 77.2 zilitolewa kwa shule za msingi na shilingi bilioni 89.2 zilitolewa kwa shule za sekondari nchini. Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo umesaidia watoto wenye umri wa kwenda shule kupata fursa ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulidhihirishia Bunge lako tukufu kwamba ufaulu wa wanafunzi wa sekondari umeendelea kuimarika kutokana na uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali. Kwa mwaka 2017 ufaulu wa kidato cha pili umepanda hadi asilimia 89.05 na watoto hao wamefanikiwa kuendelea na kidato cha tatu.

Kwa upande wa mtihani wa taifa wa kidato cha nne, ufaulu umepanda hadi asilimia 77.09 ikilinganishwa asilimia 75.99 kwa mwaka 2016. Kwa matokeo ya kidato cha sita, ufaulu umepanda hadi asilimia 97.74 kwa mwaka 2017 matokeo hayo mazuri yamechangiwa na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali chini ya Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendelezaji wa miji. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekamilisha uandaaji wa mwongozo wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi na ukaguzi wa majengo ambapo mwongozo huo umesambazwa katika mikoa na halmashauri zote. Mwongozo huu unapunguza muda wa utoaji wa vibali vya ujenzi ambapo kibali kinatolewa kati ya siku saba hadi 30 kutegemeana na aina ya jengo ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali ambapo kibali kilikuwa kinatoka kati ya siku 60 mpaka siku 309. Mwongozo huu umesisitiza wadau wote wanaohusika na utoaji wa idhini ya vibali kuwa katika eneo moja ili kuondoa urasimu. Utekelezaji wa mwongozo huu utaiwezesha Tanzania kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na kupunguza muda wa upatikanaji wa huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo inachangia sehemu kubwa ya mapato ya uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia ushuru wa mazao ya kilimo na ushuru wa huduma katika sekta ya mifugo na uvuvi. Mikoa na Halmashauri imeitikia wito wa kusimamia kilimo cha mazao makuu matano ya biashara katika maeneo yao. Mazao hayo ni pamoja na pamba, korosho, kahawa, chai na tumbaku. Usimamizi huu umechangia kuongezeka mavuno ya mazao hayo katika msimu wa mavuno ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Maafisa Ugani ili kusimamia ipasavyo uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo mazao makuu ya biashara ili kuongeza tija katika kilimo na hivyo kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Aidha, maelekezo yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kushirikiana pamoja na vyombo vingine vya usalama kuhakikisha wanawafuatilia na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wale wote wanaochafua ubora wa mazao, iwe kwa kuweka mawe, maji, mchanga na uchafu wowote katika pamba, korosho ama zao lingine lolote linalolimwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania ni mradi unaofadhiliwa na fedha kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu unalenga kuifanya miji yetu kuwa miji ya kisasa zaidi kwa kuiboreshea miundombinu yake. Mradi huu unatekelezwa katika Majiji nane ya kimkakati ambayo ni Arusha, Mbeya, Mwanza, Tanga, Halmashauri za Manispaa za Dodoma, Kigoma Ujiji, Ilemela na Mtwara Mikindani. Mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara za lami, madampo ya kisasa, mifereji, taa za barabarani, *stand* za mabasi na ununuzi wa mitambo ya kuzolea na kuchakata taka ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Januari, 2018, jumla ya shilingi bilioni 21.17 zimetolewa kati ya shilingi bilioni 81.5 zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara. Jumla ya kilometa 12.74 za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami katika halmashauri nane zinazotekeleza mradi huu. Aidha, ujenzi wa nyongeza wa mashimo sita *(six cells)* katika madampo matano ya kisasa katika Miji mitano ya Dodoma, Arusha, Mbeya, Mtwara Mikindani na Kigoma unakamilika. Vilevile, ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 7.25 pamoja na uwekaji wa taa za barabarani katika barabara zilizojengwa nao pia umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuzijengea Uwezo Halmashauri za Miji inaendelea kutekelezwa katika miji 18 ambayo ni Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Singida, Musoma, Iringa, Bukoba, Kibaha, Mpanda na Lindi na Halmashauri za Miji ya Njombe, Babati, Geita, Korogwe na Bariadi. Kupitia programu hii, jumla ya kilometa 64.38 za barabara zimejengwa kati ya kilometa 220 za barabara zilizopangwa kujengwa. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa 67.03 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Hadi kufikia Desemba, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 91.9 zimetolewa na kutumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za lami, mifereji, uwekaji wa taa za barabarani, madampo, *stand* za magari, ununuzi wa magari ya kuzolea taka ngumu pamoja na upimaji wa miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuendeleza Jiji la Dar es Salam ni mradi unaolenga kubadilisha kabisa sura ya Jiji la Dar es Salaam wakazi wa Dar es Salaam wanafanyiwa uboreshaji mkubwa wa barabara za kisasa, masoko ya kisasa, mifereji ya maji, maeneo ya kupumzikia, pamoja na upangaji upya wa maeneo yaliyojengwa kiholela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa miaka mitano kwa gharama ya shilingi bilioni 660**.** Serikali inaendelea kutekeleza malengo ya Programu ya Kuendeleza Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 15 zimejengwa likiwemo tuta la kilometa 1.5 lenye daraja la meta 16 na makalvati kwenye bonde la Mto Mzinga linalounganisha maeneo ya Kijichi na Tuangoma. Aidha, usanifu wa miradi ya barabara zenye urefu wa kilometa 110 umekamilika. Jumla ya shilingi bilioni 17.7 zimetumika kutekeleza miradi hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, Serikali inaendelea na usanifu wa mradi wa Bonde la Mto Msimbazi unaofanywa na Kampuni mbili za *COWI Tanzania Ltd.* na *ECORYS* ya nchini Netherland ili kumpata mkandarasi wa kujenga na kuboresha miundombinu ya bonde hilo. Hii ni safari ya kihistoria ya kubadilisha kabisa Bonde la Mto Msimbazi, Jijini Dar es Salam, kazi ya usanifu imepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2018. Mradi huu utatekelezwa kwa mkopo wa dola za Kimarekani milioni 20 kutoka *Department for International Development (DfID)* ikiwa ni mkakati wa kupunguza athari za mazingira na mafuriko katika Bonde la Mto Msimbazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/18, mradi wa kuondoa vikwazo uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 10.95 kwa ajili ya matengenezo maalum ya kilometa 122.2 kwenye Halmashauri tisa ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Kyerwa, Kishapu, Babati, Kondoa, Magu, Mpwapwa, Bariadi, Kibiti na Songwe. Hadi Februari,

2018 jumla ya shilingi bilioni 4.36 zilitumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 24. Aidha, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DfID),* imetumia shilingi bilioni 15.74 kujenga kilometa 11.45 za barabara na kilometa 78 zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu inayoendelea Sekta ya Maji inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ziliidhinishiwa shilingi bilioni 267.3 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji 396, hadi Februari, 2018 shilingi bilioni 91.08 zilipelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo miradi 71 ilitekelezwa na kukamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 14 na jumla ya vituo 990 vya kuchotea maji vimejengwa ambavyo vitahudumia wananchi wapatao laki 247,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kukabiliana na Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi; Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Misaada ya Uingereza (UKAID) kupitia Shirika lake la Maendeleo *(Department for International Development-DfID)* na Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo *(International Institute for Environment and Development-IIED)* na Shirika la Kikazi la *Catalyst* la Arusha inatekeleza mradi wa kukabiliana na kujenga ustahimilivu wa athari za mabadiliko ya Tabianchi. Lengo kubwa la mradi huu ni kuhakikisha mipango ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali inafungamanishwa na masuala ya mabadiliko ya Tabianchi ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umetekelezwa katika Halmashauri tatu za Mkoa wa Arusha ambapo ni Halmashauri tatu za Mkoa wa Arusha ambapo ni Halmashauri za Wilaya za Monduli, Ngorongoro na Longido. Kupitia mradi huu Halmashauri zinajengewa uwezo na ujenzi wa miundombinu ili kuhakikisha ustahimilivu na kukabiliana na

athari za mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya miradi 34 imetekelezwa ambapo baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa skimu za maji msererekо, ujenzi wa mifereji ya kudhibiti mafuriko, ujenzi wa ukarabati wa malambo na mabirika ya kunyweshea mifugo, ujenzi wa masoko ya mifugo na ukarabati na uhifadhi wa vyanzo vya maji. Kazi nyingine zilizofanyika ni ujenzi wa maabara za mifugo, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao na ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji. Miradi hiyo ambayo inanufaisha wananchi 436,569 umegharimu shilingi bilioni mbili hadi kukamilika kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais. TAMISEMI, Taasisi ya kwanza ni Tume ya Walimu hadi kufikia Desemba, 2017, kupitia Tume ya Utumishi ya Walimu, walimu 4,054 walisajiliwa, walimu 2,173 walithibitishwa kazini na walimu 1,084 wamewezeshwa kukamilisha taratibu za kustaafu. Aidha, mashauri ya nidhamu 250 yalipokelewa na mashauri 156 yamefanyiwa kazi na kutolewa maamuzi sawa na asilimia 60.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2017 walimu 869 wamefunguliwa mashtaka ya kinidhamu, mashauri 401 yapo kwenye hatua mbalimbali ya maamuzi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vijijini na Mijini *TARURA* umeanzishwa rasmi kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 211 la tarehe 12/05/2017. Wakala unasimamia ujenzi wa barabara na madaraja, ukarabati wa matengenezo ya mtandao wa barabara za Halmashauri zenye urefu wa kilometa 108,946.2 vijijini na mijini. Kati ya barabara hizo, kilometa 56,000 zinafanyiwa mchakato wa kuzihakiki ili hatimaye ziweze kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili zitambulike kisheria na kilometa 52,946.2 tayari zimetambuliwa na zimeshatangazwa na Gazeti la Serikali. Lengo la Serikali kuanzisha *TARURA* ni kuleta ufanisi katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara ambazo hapo awali zilikuwa zikihudumiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* inatekeleza majukumu yake kupitia asilimia 30 ya fedha ya Mfuko wa Barabara ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala umeidhinishiwa shilingi bilioni 230.8 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye kilometa 34,024**.** Hadi Februari, 2018, *TARURA* imepokea shilingi bilioni 98.5 ambapo zimetumika kutengeneza barabara zenye urefu wa kilometa 4,183.31, ujenzi wa madaraja 35, makalavati makubwa 43, *drift* nne na makalavati madogo 364. Wakala unategemea kuongeza mtandao wa barabara za lami katika Halmashauri kutoka kilometa 1,585.51 zilizopo sasa hadi kufikia kilometa 2,059.83 ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Elimu Kibaha linaendelea kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake ambayo ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo yaani ujinga, umaskini na maradhi. Hadi Februari, 2018 Shirika limetoa huduma kwa wagonjwa 33,652 wakiwemo wagonjwa 2,806 waliolazwa na wagonjwa 22 waliofanyiwa huduma ya matibabu ya mdomo sungura. Vilevile, kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha na Hospitali ya Tumbi, Shirika liliendelea kutoa mafunzo ya kada mbalimbali za maafisa tabibu, afya ya jamii, wauguzi na wakunga kwa ngazi ya stashahada na wauguzi wasaidizi kwa ngazi ya cheti ambapo kwa sasa chuo kina wanafunzi 265 wanaoendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Serikli za Mitaa Hombolo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 3,485 ambapo wanafunzi wa kike walikuwa ni 2,067 na wa kiume 1,178**.** Aidha, chuo kinaendesha mafunzo mbalimbali ya muda mfupi katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi na Mashirika ya Umma. Vilevile chuo kimeendelea kutoa ushauri wa kitaalam kwenye maeneo mbalimbali ya kujenga uwezo hususan utoaji taarifa, tathmini na upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2017/2018 mfuko wa Pensheni ya Serikali za Mitaa ulipanga kukusanya mapato

ya kiasi cha shilingi bilioni 611.67. Hata hivyo, makisio hayo yalifanyiwa marekebisho baada ya miezi sita na kuwa shilingi bilioni 543.34 kutokana na kuondolewa kwa wafanyakazi wasio na sifa katika utumishi wa umma. Kiasi kilichopungua ni shilingi bilioni 68.33. Hadi Desemba, 2017 makusanyo halisi yalifikia shilingi bilioni 254.65 sawa na asilimia 41.6 ya lengo. Thamani ya Mfuko inatarajiwa kukua kwa asilimia 16 kutoka shilingi trilioni 1.75 ya mwaka wa fedha 2017/2018 hadi shilingi trilioni 2.4 ifikapo Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko unaendelea na shughuli mbalimbali za uwekezaji wenye tija mpaka sasa mfuko umekamilisha uwekezaji mkubwa kwa kushirikiana na mamlaka husika za Serikali za Mitaa ambapo jengo la kisasa la kitega uchumi limekamilika katika Jiji la Mwanza pale *Rock Mall* pamoja na ujenzi wa *stand* ya kisasa eneo la Msamvu katika Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mabasi Yaendao Haraka Dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wakala umefanikiwa kufanya maandalizi ya Awamu ya Pili na ya Tatu ya ujenzi wa miundombinu ya *DART* ambapo taratibu za ununuzi zimefanyika ili kuwapata Wakandarasi wa kujenga miundombinu hiyo. Wakala unaendelea kuimarisha usimamizi na usalama wa miundombinu ya mradi katika vituo vikuu vitano, vituo vidogo 27, na madaraja ya kutembea kwa miguu matatu, pamoja na karakana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizofanyika ni kuendelea na ukamilishaji wa taratibu za kumpata mtoa huduma wa pili yaani *SP2*, mafunzo ya viwango vya ubora wa kimataifa kwa watumishi wa wakala; ujenzi wa uzio kuzunguka vituo vikuu vitatu vya Ubungo, Kivukoni na Morocco ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya nauli na usalama wa abiria ambao umepangwa kukamilika Juni, 2018.

Aidha, Wakala umefunga Kituo cha Mawasiliano cha muda ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya mwenendo wa mabasi katika mfumo wa *DART.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *DART* umeliwezesha Jiji la Dar es Salaam kupata tuzo ya Usafiri Endelevu na kuwa Jiji Bora duniani *(Sustainable Transport Award)* kwa mwaka 2018. *(Makofi)*

Vigezo vilivyotumika kupata tuzo hiyo ni pamoja na kupanga mradi kwa ufanisi mkubwa, kujenga miundombinu mizuri, iyozingatiwa mahitaji ya watumiaji mbalimbali na kutoa elimu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka kwa watumiaji kupitia Mpango Mkakati wa Wakala. Kutokana na ufanisi wa utekelezaji wa mradi wa *DART*, nchi mbalimbali zimekuja Tanzania kujifunza mafanikio na changamoto za mradi huu zikiwemo nchi za Zambia, Zimbabwe, Uganda, Kenya, Ethiopia, Senegal na Rwanda. Aidha, tuzo hiyo imeipa Tanzania heshima ya kuandaa Mkutano wa Kimataifa wa Masuala ya Usafirishaji mijini utakaofanyika Juni, 2018 hivyo kufungua fursa ya kiuchumi na kiuwekezaji na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa *DART* kutoka wastani wa abiria 76,000 kwa siku hapo mwezi Mei, 2016 mradi ulipoanza kufikia abiria 209,000 kwa siku mwezi Machi, 2018. Vilevile umepunguza muda wa safari kutoka Kimara hadi Kivukoni kutoka wastani wa masaa mawili kwa mabasi ya kawaida hadi wastani wa dakika 40 kwa mabasi ya mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mkakati wa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, maandalizi na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019, azma ya kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Ajenda ya Dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/2021, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa

kuzindua Bunge Novemba, 2015 na maagizo mbalimbali ya viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kutekeleza vipaumbele mbalimbali, vikiwemo vifuatavyo:-

(i) Kuimarisha amani na utulivu nchini, kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji na wananchi na Ugatuaji wa Madaraka yaani *D by D;*

(ii) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi za Rais – TAMISEMI;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya kila Taasisi yaliyohainishwa kwenye mpango wa mikakati yao;

(iv) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla;

(v) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali, programu za miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, uvuvi na sekta zinginezo;

(vii) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi;

(viii) Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na;

(ix) Kusimamia maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanywa na Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Tawala za Mikoa zitatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;

(ii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Wasaidizi wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya pamoja na Maafisa Tarafa;

(iii) Kuendeleza mikutano ya Kisheria ya Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mikoa *(RCC);*

(iv) Kushughulikia migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali za kujenga uchumi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuanzisha na kurasimisha utengaji wa maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda, kilimo, ufugaji, makazi, hifadhi za wanyamapori, misitu na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanywa na Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zitatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kujenga na kukarabati miundombinu ya kijamii na kiuchumi hususan katika sekta za elimu, maji, afya, kilimo, mifugo, uvuvi, barabara na sekta nyingine kwa kushirikisha nguvu ya wananchi;

(ii) Kuendesha Mikutano ya Kisheria ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji na Mtaa ili kuimarisha masuala ya Utawala Bora na Uwajibikaji;

(iii) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayosaidia kuongeza mapato ya Halmashauri**;**
(iv) Kuwezesha Vikundi vya Vijana na Wanawake kupata mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake;

(v) Kusimamia mpango wa utoaji wa elimumsingi bila malipo katika shule za Msingi na Sekondari; na

(vi) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya uwekezaji na maendeleo ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Taasisi ya yaliyoko Ofisi chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI tukianza na usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka - *DART,* katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuanza Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya *DART* inayoelekea eneo la Mbagala Jijini Dar es Salaam utakaohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe zenye urefu wa kilometa 20.3. Ujenzi umepangwa kuanza Desemba, 2018 baada ya kumpata mkandarasi. Mradi huu utatekelezwa kupitia mkopo wa dunia kupitia dola za Marekani milioni 141.71 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika;

(ii) Kuanza Awamu ya Tatu ya ujenzi wa miundombinu ya *DART* inayoelekea eneo la Gongolamboto utahusisha barabara ya Nyerere, Uhuru, Bibi Titi, Azikiwe, Shaurimoyo, Lindi na Maktaba zenye urefu wa kilometa 20.6 kwa mkopo wa dola za Marekani milioni 148.2 kutoka Benki ya Dunia. Kazi ya ujenzi imepangwa kuanza Desemba, 2018;

(iii)Kuanza usanifu wa Awamu ya Nne ya ujenzi wa miundombinu ya *DART* kwa mkopo wa dola za Marekani milioni 97.9 kutoka Benki ya Dunia. Usanifu utahusisha barabara za Sam Nujoma, Bagamoyo, Bibi Titi na Ali Hassan Mwinyi zenye urefu wa kilometa 25.9;

(iv)Ujenzi wa maegesho katika maeneo ya mfumo wa wakala;

(v)Kuimirisha upatikanaji wa Mfumo wa *Intelligent Transport System (ITS)* wa Serikali na kuwajengea uwezo watumiaji wake;

(vi)Kutekeleza Mpango Kazi wa Fidia ya Makazi kwa waathirika wa mradi wa awamu ya II na III ni pamoja na kulipa fidia kwa ajili ya mradi wa awamu ya II, III na IV; na

(vii)Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa Mabasi Yaendayo haraka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Tume ya Utumishi ya Walimu imepanga kutekeleza kazi yafuatayo:-

(i) Kuwezesha Makao Makuu na Wilaya ya 139 kufanya vikao vya kisheria vya kusikiliza mashauri ya nidhamu na kuthibitisha walimu kazini;

(ii) Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa utunzaji wa taarifa za walimu;

(iii) Kuwajengea uwezo watumishi wa Tume ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(iv) Kuratibu na kufanya ufuatiliaji wa tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya 139; na

(v) Kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa wa Walimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa huduma za afya za kinga na tiba katika Hospitali ya Tumbi;

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya Afya ya mazingira, uuguzi na utabibu kwa wanafunzi 265 katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;

(iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi 1,710 wa sekondari na wanafunzi 904 wa shule za msingi;

(iv) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya hospitali;

(v) Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi ili kiweze kutoa huduma zaidi kwa jamii kulingana na uhitaji uliopo; na

(vi) Ukarabati Mabanda ya mifugo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa vitendo katika shamba darasa la mifugo na mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)* umepanga kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Matengenezo ya kawaida ya barabara za changarawe na udongo kilometa 13,163.89;

(ii) Matengenezo ya sehemu korofi kilometa 6,201.22;

(iii) Matengenezo maalum ya barabara kilometa 3,925.94;

(iv) Ukarabati wa madaraja 117, mifereji mirefu wa meta 67,844 na makalvati 1,881;

(v) Matengenezo ya kawaida kwenye barabara za lami kilometa 54.72 na ujenzi wa kilometa 34.2 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo kimepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kudahili wanafunzi wapya 2,500;

(ii) Kufanya shughuli za utafiti katika maeneo ya mifumo, uongozi na usimamizi wa rasilimali fedha na watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Ununuzi wa vitabu nakala 500 na kompyuta 25 kwa ajili ya Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

(iv) Kuajiri watumishi wapya 72;

(v) Kukusanya mapato ya ndani kupitia vyanzo vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kutoa mikopo kwenye Halmashauri;

(ii) Kufanya ufuatiliaji wa uwasilishaji wa marejesho ya mikopo na michango kutoka kwenye Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi;

(iii) Kubuni vyanzo vipya vya mapato;

(iv) Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili waweze kufahamu majukumu ya Bodi na huduma zinazotolewa; na

(v) Kuboresha muundo wa Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa mikopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa umepanga kufanya shughuli zifuatazo:-

(i) Kuandikisha wanachama wapya wapatao 21,128;

(ii) Kufanya uwekezaji katika viwanda vya Nyama cha *Nguru Hills Ranch;*

(iii) Kuanzisha Ofisi ndogo za uratibu katika Mikoa ya Tabora na Kagera;

(iv) Kiwanda cha kuchakata Tangawizi, Same; na

(v) Kiwanda cha Maturubai Morogoro, sekta ya mafuta na gesi na viwanda vingine kwa kushirikiana na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Shirika la Masoko Kariakoo litatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya shughuli za uwekezaji katika viwanja vinavyomilikiwa na Shirika ambavyo viko Mbezi Beach, Tabata Bima, Mbezi Makonde na soko dogo lililopo katikati ya Jiji la Dar es Salaam; na

(ii) Kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato yaani Local *Government Revenue Collection Information System* ili kuongeza mapato ya Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/19, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imedhamiria kutekeleza kazi maalum zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa Hospitali mpya 67 za Halmashauri katika Halmashauri 67 ambazo hazina Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba nirudie; tumejipanga mwaka huu tutajenga hospitali mpya 67 katika Halmashauri 67 ambazo hazina Hospitali ya Wilaya

(ii) Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka 2019;

(iii) Kutekeleza miradi ya kimkakati katika Halmashauri 21 zilizokidhi vigezo kwa ajili ya kuongeza mapato ya Halmashauri;

(iv) Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri 22 ambazo hazina Ofisi;

(v) Ununuzi wa boti saba kwa ajili ya utatuzi wa changamoto za usafiri majini katika Halmashauri za Wilaya za Ludewa, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa;

(vi) Ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 85 kwa kiwango cha lami kupitia Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Sambamba na hilo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itafanya uboreshaji mkubwa wa Bonde la Msimbazi ambapo litahakikisha linajenga miundombinu ya kuhakikisha endepo mvua itanyesha maji yote yataweza kuelekea baharini ambapo huo ndiyo mpango wa mwaka huu wa fedha 2018/2019. *(Makofi)*

(vii) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mwingine ni Ujenzi wa kilometa 80.96 za lami pamoja na Ujenzi wa mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 16.47,

(viii) Ujenzi wa *stand* ya mabasi Mkoani Dodoma pamojana ujenzi wa soko la kisasa hapa Makao Makuu ya nchi Ddoma na ununuzi wa vifaa vya kukusanyia taka katika Halmashauri saba za Manispaa kupitia Miji mikakati ya *TSCP;*

(ix) Ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 220 kupitia Programu ya Kuimarisha Miji katika Halmashauri za Manispaa na Miji 18 ambapo kuweka taa za barabarani kwenye barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami;

(x) Kuratibu ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati 100 kwa kila Mkoa katika Mikoa 26;

(xi) Kutenga ekari 228,543 kwa kila Mkoa katika Mikoa yote 26 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo vya kati na vikubwa na kuwapatia mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya vijana na kinamama kwa fedha inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia eneo hili; tutawapatia mikopo sisyo na riba vijana na wakina Mama inayotoka katika asilimia 10 ambayo fedha hizi zinatokana kwa wananchi wenyewe, zinakwenda kwa Halmashauri halafu zinarudi tena kwao fedha hizi tumeweka utaratibu kwamba haiwezekani tunawapelekea Wananchi hawa halafu tunawatoza riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nishukuru; naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kushukuru tena wewe Mwenyewe unaengoza Bunge hili leo, nimshukuru Mheshimiwa Spika, nimshukuru Naibu Spika, Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Kipekee niishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Kamati kwa kazi kubwa mnaendelea kuifanya na hadi leo hii tuna-*table* Bajeti yetu hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wadau mbalimbali wakiwemo wafuatao:-

(i) Benki ya Dunia;
(ii) Benki ya Maendeleo ya Afrika;
(iii) Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DfID);*
(iv) Jumuiya ya Nchi za Ulaya;
(v) Shirika la Maendeleo la Japan;
(vi) Shirika la Maendeleo la Canada;
(vii) *UNFPA;*
(viii) *UN-Habitat;*
(ix) Shirika la Maendeleo ya Ubelgiji;
(x) Shirika la Maendeleo la Ujerumani;
(xi) Shirika la Maendeleo la Marekani;

(xii) Shirika la Maendeleo la Sweden;
(xiii) *UNICEF;*
(xiv) *UNDP*;
(xv) *Plan international;*
(xvi) *Feed the Children* na;
(xvii) *CDTF* pamoja wadau wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru wote pamoja na nchi zote waliochangia katika mfuko wa pamoja wa kuisadia bajeti ya Serikali. Mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yamepatikana kutokana na ushirikiano mzuri wa Wadau wa Maendeleo ambao waliendelea kushirikiana katika utekelezaji wa Programu na Miradi mbalimbali katika Sekta za afya, elimu, maji, barabara, fedha, kilimo na maboresho mbalimbali katika Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kushirikiana na wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi ili kutimiza azma ya kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia miradi inayotekelezwa na kuzingatia vipaumbele vya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutambua kazi kubwa inayofanywa na Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais-TAMISEMI nikianzia na Mheshimiwa Joseph George Kakunda (Mbunge), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI anayeshughulikia masuala ya huduma za elimu, maji na maliasili. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mbunge), Naibu Waziri anayeshughulikia huduma za afya, miundombinu na uwekezaji, naomba kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi Mussa Iyombe - Katibu Mkuu, Bwana Tixon Nzunda - Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Elimu, Mheshimiwa Dkt. Zainab Chaula - anayesimamia Idara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa wote, Makatibu Tawala wote, Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, ninawashukuru viongozi na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na watumishi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika ngazi zote kwa

kutekeleza kwa umakini majukumu yao katika kuboresha huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa kuendelea kuwa wavumilivu mara zote nilipokuwa mbali nao kwa majukumu ya Kitaifa ambayo nimepewa. Naahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Aidha, naishukuru sana familia yangu, nawashukuru wazazi wangu na Mama yangu Mzazi binti Mwalimu kwa kuendelea kunitia moyo katika kutekeleza wa majukumu yangu haya ya kulitumikia Taifa hili na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwako maombi ya fedha zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 185 zinaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya shilingi 758,362,711,799. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi 6,586,915,753,733 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Fungu namba 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu namba 2, Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 185 ambapo fedha kwa ajili ya mishahara ni shilingi 4,134,200,811,930 na fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo ni shilingi 649,309,982,303 na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 1,803,404,959,500 ambazo fedha za

ndani ni shilingi 1,276,262,429,500 na fedha za nje ni shilingi 500,527,142,530.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii niliyowasilisha, naomba pia kuwasilisha majedwali yanayofafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, taasisi zake, Mikoa na Halmashauri zote 185.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii pia inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni *www.tamisemi.go.tz*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPITIO, MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**I. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima kubwa namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza nchi yetu kwa falsafa ya uchumi wa viwanda na utekelezaji makini wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015. Vilevile, nawapongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (MB) kwa uongozi wao mahiri na miongozo ambayo imetoa dira katika kuboresha utendaji Serikalini.

2. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe mwenyewe na Naibu Spika kwa uongozi wenu imara na madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya njema na hekima katika kuuongoza Mhimili huu muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Damas Daniel Ndumbaro Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Justine Joseph Monko Mbunge wa Singida Kaskazini, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia Mbunge wa Kinondoni na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel Mbunge wa Siha kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako tukufu ili wawatumikie wananchi waliowachagua. Vilevile nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge hongereni sana.

3. **Mheshimiwa Spika,** mnamo Novemba 2017, Bunge lako Tukufu liliondokewa na Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Songea Mjini. Kwa masikitiko makubwa napenda kutumia fursa hii kukupa pole wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu mahiri. Aidha, natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wote waliofiwa na wapendwa wao katika ajali za magari, pikipiki na nyinginezo. Mwenyezi Mungu azilaze Roho za marehemu mahali pema peponi Amina.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Mwanne Mchemba Mbunge wa Viti Maalum, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Kuchaguliwa kwao kwa mara nyingine kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kunadhihirisha kukubalika kwao na umahiri wao wa uongozi katika Kamati hii. OR-TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Kamati hii katika

kuboresha utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi. Kamati imepokea, kuchambua kwa kina na hatimaye kupitisha makadirio ya Bajeti ya OR-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

5. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya OR-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/18. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya OR - TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 02 pamoja na mafungu 26 ya Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

## II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

6. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, OR-TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri iliidhinishiwa shilingi **Trilioni 6.57** kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **Trilioni 4.27** ni Mishahara, shilingi **bilioni 519.45** ni Matumizi Mengineyo na shilingi **Trilioni 1.78** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **Trilioni 1.31** ni fedha za ndani na shilingi **bilioni 467.67** ni fedha za nje. Hadi Februari, 2018 fedha zilizopokelewa ni shilingi **Trilioni 3.33** sawa na **asilimia 50.68** ya bajeti yote.

### Maduhuli ya OR-TAMISEMI na Mikoa

7. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, OR-TAMISEMI iliidhinishiwa kukusanya Maduhuli ya shilingi **milioni 14.0.** Hadi Februari, 2018, makusanyo halisi yalikuwa shilingi **milioni 10.3** sawa na **asilimia 74** ya lengo. Taasisi zilizo chini ya OR-TAMISEMI zimekusanya maduhuli ya shilingi **bilioni 9.0** kati ya lengo la kukusanya shilingi **bilioni 22.8** sawa na **asilimia 44**. Aidha, Maduhuli yaliyokusanywa na Mikoa yalikuwa shilingi **bilioni 3.3** sawa na **asilimia 96** ya makadirio

ya kukusanya shilingi **bilioni 3.51** katika kipindi hicho. Kuimarika kwa makusanyo ya maduhuli ya Mikoa kumetokana na ufanisi wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa GoT-HOMIS unaotumika katika Hospitali za Mikoa, matumizi ya Tiba kwa Kadi (TIKA) katika kufanya malipo na kuimarika kwa usimamizi.

**Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

**8.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya shilingi **bilioni 687.30** kutoka vyanzo vya mapato ya ndani. Hadi Februari, 2018 shilingi **bilioni 343.82** zimekusanywa sawa na asilimia **50.0** ya makadirio ***(kama inavyooneshwa katika jedwali Na. 1).*** Kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la shilingi **bilioni 90.68** ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **bilioni 253.12** zilizokusanywa hadi Februari, 2017. Ongezeko la makusanyo limechangiwa na kuimarishwa kwa usimamizi, elimu na uhamasishaji kwa walipa kodi, ushuru mbalimbali pamoja na matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yangu ya Mwaka wa Fedha 2017/18, nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri zote zitakamilisha kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato ifikapo tarehe 30 Juni, 2017. Nafurahi kuliarifu Bunge lako kuwa Halmashauri zote 185 zimeunganishwa na zinatumia Mfumo wa Kukusanya Mapato unaojulikana kama *Local Government Revenue Collection Information System (LGRCIS)*.

**Matumizi**

**10.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2018, OR-TAMISEMI pamoja na Taasisi zake imepokea jumla ya shilingi **bilioni 245.17** sawa na **asilimia 53** ya bajeti ya shilingi **bilioni 459.41** iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2017/18. Aidha, katika kipindi hicho, Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea jumla ya shilingi **bilioni 6.92** kati ya shilingi **bilioni 12.42** zilizoidhinishwa na Bunge sawa na **56.** Kwa upande wa Mikoa, fedha zilizoidhinishwa na Bunge ni

shilingi **bilioni 285.13** ambapo kiasi kilichopokelewa ni shilingi **bilioni 156.18** sawa na **asilimia 55.** Vilevile, Halmashauri ziliidhinishiwa shilingi **Trilioni 5.83** ambapo tayari jumla ya shilingi **Trilioni 3.17** zimepokelewa hadi Februari, 2018 ikiwa ni sawa na **asilimia 54**.

**11.** **Mheshimiwa Spika,** fedha zilizopokelewa na kukusanywa zimetumika kutekeleza majukumu ya msingi ya OR-TAMISEMI, Taasisi zilizo chini ya OR-TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa ajili ya kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

**Utawala Bora**

**12.** **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya kuwajengea uwezo na utawala bora Wakuu wa Mikoa yote 26 yametolewa Tanzania Bara. Aidha, Makatibu Tawala wa Mikoa **26**, Wakuu wa Wilaya **139,** Wakurugenzi wa Halmashauri **185,** Maafisa Utumishi **185** na Maafisa Mipango **185** wamepata mafunzo kuhusu majukumu na mipaka ya kazi zao, maadili ya uongozi, utawala bora, usimamizi wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali. Mafunzo hayo yamesaidia kuboresha utendaji na kuondoa mwingiliano wa majukumu baina ya Viongozi na Watendaji. Aidha, Viongozi na Watendaji hao wamekumbushwa wajibu wa kusimamia maendeleo na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika maeneo yao ya utawala.

**Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**13.** **Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 27 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaelekeza kuwa ni wajibu wa kila Mtanzania kulinda mali za umma na kuhakikisha zinatumika kwa maslahi ya Watanzania wote. OR-TAMISEMI imeendelea kusimamia matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Katiba ya Nchi, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011, Kanuni zake za Mwaka 2013 na marekebisho yake ya Mwaka 2016.

**14.** **Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeendelea kuimarika. Kwa mujibu wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kati ya Halmashauri **185** zilizokaguliwa Mwaka wa Fedha 2016/17, Halmashauri **166** sawa na **asilimia 90** zimepata hati safi, Halmashauri **16** zimepata hati zenye mashaka na Halmashauri 3 tu ndizo zimepata hati chafu ikilinganishwa na ukaguzi wa Mwaka wa Fedha 2015/16 ambapo kati ya Halmashauri **171** zilizokaguliwa, Halmashauri **138** sawa na asilimia **81** zilipata hati safi, Halmashauri **32** zilizopata hati zenye mashaka na Halmashauri **1** ilipata hati chafu.

**15.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI imeimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa inakuwa na thamani ya fedha zilizotumika katika miradi ya maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, ufuatiliaji umefanyika katika Mikoa yote **26** na Halmashauri **182** ambao ulihusisha kukagua miradi na shughuli mbalimbali za utawala bora. Vilevile, ukaguzi maalum kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma umefanyika katika Halmashauri za Wilaya za Hanang', Kilindi, Mbulu, Tunduru, Morogoro, Nkasi, Same, Chalinze, Bumbuli, Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Halmashauri za Manispaa za Ilala, Ubungo, Temeke na Kinondoni na Mpanda.

**16.** **Mheshimiwa Spika**, hatua mbalimbali za kudhibiti ubadhirifu na ukiukwaji wa Sheria zimechukuliwa ambapo watumishi 434 waliobainika kwa ubadhirifu na ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma wamechukuliwa hatua za kinidhamu na wengine 28 michakato ya nidhamu inaendelea ili waweze kufikishwa Mahakamani.

**17.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI imeendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti kupitia mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha (Epicor) ambapo Halmashauri zilizounganishwa kwenye mfumo huo zimeongezeka kutoka 168 katika Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi Halmashauri zote 185 katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Mfumo umeongeza uwazi na uwajibikaji katika mchakato

mzima wa malipo. Aidha, Serikali imeanzisha mfumo wa ***Tanzania Interbank Settlement System – TISS*** ambapo malipo yote ya Serikali yanafanyika kutoka akaunti zilizofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania kwenda moja kwa moja kwa mlipwaji. Mfumo wa *TISS* umeunganishwa katika Mikoa **11** ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro, Lindi, Mtwara, Mwanza, Songwe, Pwani na Tanga yenye jumla ya Halmashauri **77.** Mikoa 15 iliyobaki na Halmashauri zake itaunganishwa kwenye mfumo katika Mwaka wa Fedha 2018/ 19.

**Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI inaratibu uanzishaji, utunzaji na uendelezaji wa maeneo ya uwekezaji katika kila Mkoa na Halmashauri. Halmashauri zinaendelea kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya kujenga uchumi wa viwanda. Hadi Februari, 2018 Halmashauri **184** zimetenga maeneo yenye ukubwa wa hekta **196,710** kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa. Aidha, katika utekelezaji wa agizo la ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati **100** kwa kila Mkoa, jumla ya viwanda vipya **1,285** vimejengwa kati ya Mwezi Novemba, 2017 hadi Machi, 2018 ambapo ni sawa na **asilimia 49.4** ya utekelezaji.

**Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA**

**19.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI imeendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA iliyopo kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utendaji na uwajibikaji. Mfumo mpya wa *Facility Financial Accounting and Reporting System (FFARS)* umeandaliwa ili kuwezesha upelekaji wa fedha na utoaji wa taarifa katika vituo vya kutolea huduma katika ngazi za msingi za Serikali za Mitaa. Aidha, Mfumo wa kuandaa Mipango na Bajeti za Halmashauri (PlanRep-Web based) umeboreshwa na kutumika kuandaa bajeti za Halmashauri zote 185 kwa Mwaka wa Fedha 2018/19. Mifumo hii ya kielektroniki imeongeza ufanisi katika utendaji kazi,

imepunguza gharama, imeongeza udhibiti wa rasilimali, uwajibikaji, upatikanaji wa taarifa na hivyo kuwezesha Viongozi kufanya maamuzi kwa wakati.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, mafunzo ya kujenga uwezo yametolewa kwa watumishi **262** wa Mikoa na **1,507** wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafunzo hayo yametolewa kuhusu matumizi ya mifumo ya PlanRep, *FFARS, Basic Education Management Information System (BEMIS), Government of Tanzania Hospital Management Information System (GoT-HOMIS)* na *Local Government Revenue Collection Information System (LGRCIS).* Matumizi ya TEHAMA yamesaidia katika upatikanaji wa takwimu za msingi kwa ajili ya kusaidia kufanya maamuzi mbalimbali ya Serikali, uwazi na uwajibikaji. OR-TAMISEMI itaendelea kubuni, kuratibu, kujenga, kuboresha na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu, uchakataji, uchambuzi, utunzaji na utoaji wa taarifa zilizo sahihi kutumika katika mipango kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha uwajibikaji na uadilifu.

## Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**21.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake umetengewa shilingi **bilioni 61.6** ikiwa ni **asilimia 10** ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya mikopo ya vikundi **18,233.** Hadi Februari, 2018 kiasi cha shilingi **bilioni 15.6** zimetolewa kwa vikundi **8,672** vya Wanawake na Vijana.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI kupitia programu ya *LocaL Investment Climate (LIC)* inawawezesha wananchi kiuchumi kwenye Sekta za Kilimo, Biashara na Uvuvi katika Mikoa ya Kigoma na Dodoma. Maeneo yanayopewa kipaumbele ni uzalishaji na uchakataji wa mazao ya Mchikichi, Zabibu, mbogamboga, muhogo, mpunga, Alizeti na ufugaji wa samaki. Hadi Februari, 2018 jumla ya **shilingi bilioni 2.89** zimetumika katika kuendesha shughuli za

programu hiyo. Aidha, jumla ya wananchi **1,000** wamewezeshwa kuandaa maandiko ya kibiashara.

**Utoaji wa Huduma za Afya**

**23.** **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya afya, OR-TAMISEMI inahusika na uratibu pamoja na usimamizi wa Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati ili kuhakikisha zinatoa huduma bora za afya kwa wananchi. Hospitali za Halmashauri zilizopo ni **120** kati ya Hospitali **184** zinazohitajika sawa na **asilimia 65** ya lengo. Kati ya Hospitali hizo, **77** zinamilikiwa na Serikali na **43** zinamilikiwa na Mashirika Binafsi ambazo ni Hospitali Teule zilizoingia mkataba wa utoaji huduma na Halmashauri.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Vituo vya Afya vilivyopo ni **696** sawa na asilimia **15.7** ya lengo la kuwa na Vituo vya Afya **4,420**. Kati ya hivyo, vituo **513** vinamilikiwa na Serikali na vituo **183** vinamilikiwa na Sekta Binafsi na Mashirika ya Dini. Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya **208** ili kuviwezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji kwa ajili ya kuboresha huduma zote za Vituo vya Afya. Kati ya Vituo hivyo **15** ni vipya na **14** ni zahanati zilizopandishwa hadhi, vituo vitatu **(3)** ni maboma ambayo yalikuwa hayajakamilika. Ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya **44** umekamilika, vituo **139** vitakamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2018 ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2)*** na vituo 25 vitaanza ujenzi Aprili, 2018. Vituo hivyo vitagharimu shilingi **bilioni 93.5** hadi kukamilika. Sambamba na ujenzi, vituo hivyo vimetengewa shilingi **bilioni 50.2** kwa ajili ya kununulia vifaa tiba pamoja na samani ili kuviwezesha kuanza kutoa huduma. Aidha, shilingi **bilioni 13.0** zimetumika kwa ajili ya kuboresha mifumo ya kupeleka fedha vituoni ikiwemo mishahara ya Wasaidizi wa Hesabu **535** kwenye vituo vya Afya na Zahanati zenye wagonjwa wengi.

**25.** **Mheshimiwa Spika**, mpango uliopo ni kukamilisha ukarabati na ujenzi wa vituo vyote ili kuboresha huduma za Afya na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Kazi hiyo inatekelezwa kwa uratibu na usimamizi wa OR-TAMISEMI

ikishirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wa maendeleo wa Mfuko wa Pamoja wa Afya. Vigezo vilivyotumika kuchagua vituo hivyo ni pamoja na idadi ya watu katika Kata, umbali kutoka kituo cha kutolea huduma kilichopo na hali ya kijiografia ya eneo husika.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** idadi ya Zahanati zilizopo nchini ni **6,640** sawa na **asilimia 53** ya lengo la kuwa na Zahanati **12,545** zinazohitajika. Kati ya hizo, zahanati **4,554** sawa na **asilimia 47.9** zinamilikiwa na Serikali na Zahanati **2,086** zinamilikiwa na Sekta Binafsi. Katika Mwaka wa Fedha 2017/ 18, Serikali iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **shilingi bilioni 35.5** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Zahanati, kipaumbele kikiwa ni kukamilisha ujenzi wa maboma yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imekamilisha ujenzi wa nyumba **578** za watumishi wa afya katika vituo vya afya **268** kwenye Halmashauri **51.** Nyumba nyingine **262** zinaendelea kujengwa na imepangwa ziwe zimekamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2018. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za Afya kinakuwa na nyumba angalau mbili ifikapo Mwaka 2020 ili kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi.

**Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeongeza bajeti ya dawa, vifaa, vifaa tiba, chanjo na vitendanishi kutoka shilingi **bilioni 31** zilizotengwa Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi shilingi **bilioni 269** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Kati ya fedha hizo, shilingi **bilioni 98.08** zimetengwa kwa ajili ya huduma ya afya ya msingi kwenye Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati.

**29.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/ 17, kiasi cha shilingi **bilioni 17.3** zilizoidhinishwa kwa ajili ya dawa na vifaa tiba katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilibaki Bohari ya Taifa ya Dawa (MSD) kutokana na

kukosekana kwa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Hadi Desemba, 2017 vituo vya kutolea huduma za Afya katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa vimetumia shilingi **bilioni 35.3** zikijumuisha bakaa iliyobaki MSD katika Mwaka wa Fedha 2016/17 kwa ajili ya dawa na vifaa tiba. Upatikanaji wa dawa muhimu umeongezeka kufikia asilimia **92** ikilinganishwa na asilimia **81** katika kipindi kama hicho Mwaka 2016.

**30.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI imeanza matumizi ya mfumo wa jazia kwa kutumia Washitiri (Prime Vendor) katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Shinyanga ambao lengo ni kuhakikisha dawa zinakuwepo katika vituo vya kutolea huduma za Afya endapo zimekosekana MSD. Azma ya Serikali ni kuhakikisha mfumo huu unatumika katika Mikoa yote 26 nchini.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

**31.** **Mheshimiwa Spika,** Usimamizi wa huduma za Ustawi wa Jamii unatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010. Katika kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo Mwaka 2017, OR-TAMISEMI ilitoa Waraka kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwakumbusha na kuwataka Wadau wote katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza maelekezo ya Sheria hiyo ili kuimarisha ustawi wa makundi yote ya jamii hususan Watu Wenye Ulemavu. Watu Wenye Ulemavu wapatao **221,090** wakiwemo wanawake **110,290** na wanaume **110,800** wametambuliwa na kupatiwa huduma zikiwemo vifaa vya shule, kofia za kuzuia jua na mafuta ya ngozi kwa Watoto Wenye Ualbino **1,836.**

**32.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imewajengea uwezo Maafisa Ustawi wa Jamii **35** kuhusu utoaji wa huduma ya ulinzi na usalama wa mtoto na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa watoto **4,536** wakiwemo wanawake **2,211** na wanaume **2,325** katika makambi ya Ntuta, Nyarugusu na Mtendeli yaliyoko Mkoani Kigoma. Mkakati huu unakusudia kuboresha ustawi wa jamii kwa makundi yote.

**33.** **Mheshimiwa Spika,** huduma za matunzo ya Watu Wenye Ulemavu zinatolewa katika makazi maalum **17** yanayomilikiwa na Serikali na makazi **24** yanayohudumiwa na Mawakala wa hiari. Huduma hizo ziko kwenye Mikoa ya Mara, Mwanza, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Kigoma, Kagera, Arusha, Kilimanajaro na Rukwa. Watu **100,000** Wenye Ulemavu wanahudumiwa katika makazi hayo. Aidha, huduma za ushauri nasihi na huduma za mazoezi tiba na unasihi zimetolewa kwa Watu **1,150** Wenye Ulemavu kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii.

## Mfuko wa Afya ya Jamii

**34.** **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wanachama **12,278,406** wamejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) katika Mwaka 2017. Wananchi katika Halmashauri **154** kati ya **185,** wanatumia kadi za CHF na TIKA katika maeneo ya miji. Hadi Machi, 2018 jumla ya shilingi **bilioni 22.5** zilikuwa zimekusanywa na Halmashauri. Halmashauri zimetunga Sheria Ndogo ambazo zimeweka viwango vya kuchangia kati ya shilingi **5,000** hadi **30,000** kwa kila mwanachama. Halmashauri zote zimeelekezwa kuhakikisha fedha hizo zinatumika katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba ili kuboresha huduma za Afya kwa wananchi.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Wazee **1,652,206** wasiokuwa na uwezo wametambuliwa katika Mikoa **22** ambapo kati yao **462,513** wamepatiwa kadi za CHF kwa ajili ya matibabu bila malipo. Halmashauri **117** zinaendelea na utambuzi wa Wazee ili kuwapatia kadi za CHF. Mpango uliopo ni kuhakikisha Halmashauri zote **184** zinawatambua Wazee wasiokuwa na uwezo ili kuwapa matibabu bila malipo.

## Usimamizi wa Elimu ya Msingi na Sekondari Nchini

## Elimu ya Awali na Msingi

**36.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI inaendelea kuboresha utoaji wa elimu katika ngazi zote za elimu ya Awali, Msingi hadi Sekondari. Hadi Machi, 2018 shule za msingi

zilizopo ni **16,140** ambapo kati ya hizo shule **16,004** zina madarasa ya elimu ya awali ikilinganishwa na shule **14,946** zilizokuwepo Mwaka wa Fedha 2016/17. Kwa ujumla shule zenye madarasa ya awali ni **asilimia 99.2** ya lengo. Wanafunzi wa elimu ya Awali walioandikishwa hadi Machi, 2018 ni **1,283,790** (Wavulana 647,467 na Wasichana 636,323) sawa na **asilimia 85.7** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,498,043** (Wavulana 746,102 na Wasichana 751,941) hadi tarehe 31 Machi, 2018 ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3).***

**37.** **Mheshimiwa Spika,** uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza hadi kufikia Machi, 2018 umefikia wanafunzi **1,751,221** (Wavulana 880,391 na Wasichana 870,830) ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi **1,732,303** (Wavulana 871,918 na Wasichana 860,385) sawa na **asilimia 100.1** ya lengo ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 4).*** Wito unatolewa kwa Wazazi/Walezi na jamii kwamba wanao wajibu wa kuhakikisha kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anaandikishwa na kuanza masomo.

**38.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Serikali kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa elimu na wananchi, imekamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa **2,278** kwa shule za msingi. Ujenzi huo umeongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **120,766** vilivyokuwepo Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi vyumba vya madarasa **123,044** kufikia Machi 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 1.8.** Hivyo, mahitaji ya vyumba vya madarasa yamepungua hadi **264,594** ikilinganishwa na **266,872** Mwaka 2017. Aidha, nyumba za walimu zimeongezeka kutoka nyumba **43,075** zilizokuwepo Mwaka 2017 hadi **43,365** sawa na ongezeko la nyumba **290** zilizojengwa hadi Machi, 2018.

**39.** **Mheshimiwa Spika,** matundu ya vyoo yameongezeka kutoka **167,496** hadi **173,770** sawa na ongezeko la matundu ya vyoo **6,274** yaliyojengwa kufikia Machi, 2018. Ongezeko hilo limepunguza upungufu uliokuwepo kutoka matundu ya vyoo **350,110** Mwaka 2017 hadi **343,832** kufikia Machi, 2018. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2017/18, jumla ya Ofisi za

Walimu **316** na maktaba **165** zimejengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** walimu wa shule za msingi waliokuwepo nchini Mwaka wa Fedha 2016/17 ni **175,946** ambapo mahitaji yalikuwa ni walimu **273,463** hivyo upungufu ulikuwa ni walimu **97,517.** Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali imefanikiwa kuajiri walimu wapya **2,767.** Aidha, Serikali imewahamisha walimu wa ziada **8,834** wa masomo ya Sanaa na Lugha kutoka shule za sekondari kwenda katika shule za msingi na kufanya upungufu wa walimu kuwa **85,916** ikilinganishwa na upungufu wa walimu **97,517** katika Mwaka 2017.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** jumla ya wanafunzi **1,192,655** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kitaifa wa Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) katika Mwaka 2017 wakiwemo Wavulana **590,380** na Wasichana **602,275.** Wanafunzi waliofanya Mtihani huo walikuwa **1,158,499** (Wavulana 569,718 na Wasichana 588,781) sawa na **asilimia 97.1** ya lengo. Kati ya Wanafunzi waliofanya Mtihani huo, jumla ya wanafunzi **1,086,156** (wavulana 513,916 na wasichana 554,240) sawa na **asilimia 93.76** walifaulu na kujiunga na Darasa la Tano. Hivyo, ufaulu umeongezeka kutoka **asilimia 93.36** Mwaka 2016 hadi **asilimia 93.76** Mwaka 2017.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** wanafunzi waliohitimu Darasa la Saba Mwaka 2017 walikuwa **909,950,** wakiwemo wasichana **480,784** na wavulana **429,166**. Kati ya hao, wanafunzi **662,035** wakiwemo wasichana **341,020** na wavulana **321,015** walifaulu mtihani huo sawa na **asilimia 72.75.** Ufaulu umeongezeka kutoka **asilimia 70.84** Mwaka 2016 hadi **asilimia 72.75** Mwaka 2017 kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuimarishwa kwa usimamizi wa shule.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/ 18, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata **17,518** kuhusu mbinu za kufundisha Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Aidha, mafunzo

ya uongozi yametolewa kwa Walimu Wakuu **5,333** na mafunzo ya uandaaji mipango ya elimu yametolewa kwa Maafisa Elimu na Maafisa Mipango katika Halmashauri **51**. Vilevile, walimu **4,452** na Maafisa Elimu Kata **998** kutoka katika Mikoa saba wamepatiwa vifaa vya TEHAMA (tablets) **5,450** kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa kukusanya takwimu. Katika kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa Elimu ngazi za Kata, Maafisa Elimu Kata **2,025** wamepatiwa Pikipiki ili kurahisisha utendaji wa majukumu yao. Aidha, Wataalam **314** wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwatambua na kuwa hudumia watoto wenye mahitaji maalum.

**Elimu ya Sekondari**

**44.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2018 wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza walikuwa **661,059** (wavulana 320,849 na wasichana 340,210) ikinganishwa na wanafunzi **555,291** (wavulana 283,751 na wasichana 271,540) waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Mwaka 2017 sawa na ongezeko la wanafunzi **105,768** ambao ni **asilimia 19.05.** Hadi Machi, 2018 wanafunzi **586,830** (wavulana 285,847 na wasichana 300,983) wameripoti katika shule walizopangiwa sawa na **asilimia 88.8** ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 5)*** na wanafunzi **74,229** bado hawajaripoti katika shule walizopangiwa. OR-TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza wanafuatiliwa ili kuhakikisha wanajiunga na shule walizochaguliwa.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** nyumba za walimu zimeongezeka kutoka **12,922** zilizokuwepo Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi nyumba za walimu **13,196** sawa na ongezeko la nyumba za walimu **274** zilizojengwa hadi Februari, 2018. Vyumba vya madarasa vimeongezeka kutoka **39,490** kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi vyumba **40,278** kufikia Februari, 2018 ikiwa ni ongezeko la vyumba **788.** Aidha, matundu ya vyoo yameongezeka kutoka **51,327** kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi kufikia matundu **53,398** hadi Februari, 2018 ikiwa ni ongezeko la matundu ya vyoo **2,071**. Katika

kipindi hicho, miundombinu mingine iliyojengwa ni maktaba **176,** mabweni **543**, majengo ya utawala **36** na maabara **165.** Utekelezaji umefanyika kupitia fedha za Programu ya Elimu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) pamoja na fedha za ndani za Halmashauri. Serikali inaendelea na ukarabati wa shule kongwe **89** ambapo shule **43** ukarabati wake umekamilika. Ukarabati unahusisha kuondoa miundombinu iliyochakaa ikiwemo paa, kupiga rangi, kuboresha mifumo ya maji safi na maji taka, umeme na kujenga miundombinu mipya kulingana na mahitaji.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** walimu waliopo katika shule za sekondari nchini ni **88,865**. Walimu wa masomo ya Sanaa waliopo ni **69,395** ikilinganishwa na mahitaji ya walimu **48,245** sawa na ziada ya walimu **20,712**. Kwa upande wa masomo ya sayansi na hisabati, walimu wanaohitajika ni **35,136** na walimu waliopo ni **19,459** sawa na upungufu wa walimu **15,677.**

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutoa fedha za Elimumsingi Bila Malipo kila Mwezi tangu mpango huu uanze kutekelezwa Desemba, 2015. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Februari, 2018 Serikali imefanikiwa kutoa jumla ya shilingi **bilioni 172.4** kugharamia Mpango wa Elimumsingi bila Malipo ambapo kati ya hizo shilingi **bilioni 77.2** zimetolewa kwa shule za msingi na shilingi **bilioni 89.2** zilitolewa kwa shule za sekondari nchini. Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo umesaidia watoto wenye umri wa kwenda shule kupata fursa ya kusoma. Wazazi wamebaki na jukumu la kumwezesha Mwanafunzi kupata madaftari, kalamu, sare za shule, chakula na nauli kwa wanafunzi wa shule za kutwa.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** kati ya wanafunzi **521,759** (wasichana 270,174 na wavulana 251,585) waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Kidato cha Pili, wanafunzi **486,742** (wasichana 254,538 na wavulana 232,204) walifanya mtihani huo. Wanafunzi waliofaulu ni **433,453** (wasichana 224,736 na wavulana 208,717) sawa na **asilimia 89.05** na kufanikiwa kuendelea na Kidato cha Tatu. Kwa

upande wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, jumla ya wanafunzi **287,713** (wasichana 143,728 na wavulana 143,985) walifaulu mtihani huo katika Mwaka 2017 sawa na **asilimia 77.09** ikilinganishwa na wanafunzi **374,950** (wasichana 191,956 na wavulana 182,994) waliofanya Mtihani huo. Ufaulu katika Mtihani wa Kidato cha Nne umeongezeka kutoka **asilimia 75.99** Mwaka 2016 hadi **asilimia 77.09** kwa Mwaka 2017. Kati ya wanafunzi **62,725** waliofanya mtihani wa Kidato cha Sita Mwaka 2017, wanafunzi **61,308** walifaulu sawa na **asilimia 97.74** ikilinganishwa na wanafunzi **63,525** waliofaulu Mwaka 2016.

**Usimamizi na Uendelezaji Vijiji na Miji**

**49.** **Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa miji ni fursa ya maendeleo kijamii, kiuchumi na kimazingira. Mipango ya matumizi bora ya ardhi imeandaliwa katika Vijiji **1,764** ikilinganisha na Vijiji **12,545** nchini sawa na **asilimia 14.** Aidha, upimaji wa mipaka ya Vijiji umefanyika katika Vijiji **11,256** kati ya Vijiji **12,545** sawa na **asilimia 90.** Vilevile, Halmashauri **161** kati ya **184** zipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya Mipango ya Jumla ya uendelezaji miji ili kuhakikisha kunakuwa na ukuaji endelevu wa miji kuepuka uwepo wa miji ambayo haijapangwa vizuri. Aidha, Miji Midogo **800** inayochipukia imebainishwa ili iweze kuendelezwa kabla haijavurugika.

**50.** **Mheshimiwa Spika**, OR-TAMISEMI imekamilisha uandaaji wa mwongozo wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa ukaguzi wa majengo ambao umesambazwa kwenye Mikoa na Halmashauri zote. Mwongozo huo utapunguza muda wa utoaji wa vibali vya ujenzi ambapo kibali kitatolewa kati ya siku **7** hadi **30** kutegemeana na aina ya jengo ikilinganishwa na siku **60** hadi **309** hapo awali. Mwongozo umesisitiza wadau wote wanaohusika na utoaji wa idhini ya vibali kuwa katika eneo moja ili kuondoa urasimu. Utekelezaji wa mwongozo huo utaiwezesha Tanzania kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa kupunguza muda wa upatikanaji wa huduma hiyo.

## Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

**51.** **Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Wananchi wa Tanzania unategemea kwa kiasi kikubwa sekta ya kilimo. Sekta hii ni muhimili wa uchumi wa Viwanda na kuchangia kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati, kupunguza umaskini na kuongeza uhakika wa chakula. Kwa sasa **asilimia 65.5** ya Wananchi wa Tanzania wanategemea sekta ya kilimo kwa maendeleo yao ya Kiuchumi na Kijamii.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inachangia sehemu kubwa ya mapato ya uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia ushuru wa mazao ya kilimo na ushuru wa huduma katika sekta ya Mifugo na Uvuvi. Mikoa na Halmashauri imeitikia mwito wa kusimamia kilimo cha mazao makuu matano ya biashara katika maeneo yao. Mazao hayo ni Pamba, Korosho, Kahawa, Chai na Tumbaku. Usimamizi huu utachangia ongezeko la mavuno ya mazao hayo katika msimu wa mavuno ujao.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** maelekezo yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kushirikiana pamoja na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha wanawatafuta na kuwafikisha mbele ya vyombo vya Sheria wale wote wanaochafua ubora wa mazao, iwe ni kuweka mawe, maji, mchanga na uchafu wowote katika pamba, korosho au zao lingine lolote. Aidha, ni jukumu la Vyama vya Ushirika na kila mkulima kuhakikisha mazao hayahujumiwi.

## Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

**54.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeongeza fedha za ruzuku ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka shilingi **bilioni 156** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu katika Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi shilingi **bilioni 251.0** kwa Mwaka wa Fedha 2017/18. Halmashauri zimeboresha miradi iliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2017/18 kwa kuchagua miradi michache yenye tija ambayo itatekelezwa na kukamilika ili ianze kutoa huduma. Mkakati huu umesaidia kuondoa changamoto ya kuwa na miradi

viporo kila Mwaka. **Asilimia 95** ya fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za afya, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, ujenzi wa majengo ya utawala, vitega uchumi vya kibiashara, sekta ya maji, sekta ya kilimo, mifugo na sekta ya ardhi na maliasili. Utekelezaji wa miradi hiyo umepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2018 ili ianze kutoa huduma. Fedha zinazobaki sawa na **Asilimia 5** zimetengwa kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyopangwa.

### Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania

**55. Mheshimiwa Spika,** Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Miji nane (8) ya Kimkakati ulikamilika katika Mwaka wa Fedha 2015/16. Mpango huu umeongezewa muda wa utekelezaji kwa miaka miwili (2) kwa gharama ya shilingi **bilioni 291.2.** Programu itatekelezwa kwenye Majiji ya Arusha, Mbeya, Mwanza na Tanga na Halmashauri za Manispaa za Dodoma, Kigoma Ujiji, Ilemela na Mtwara Mikindani ili kuchochea ukuaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi katika Miji nchini. Hadi kufikia Januari, 2018 shilingi **bilioni 21.17** zimetolewa kati ya shilingi **bilioni 81.5** zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha 2017/18 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara. Jumla ya kilometa **12.74** za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri nane zinazotekeleza mradi. Aidha, ujenzi wa nyongeza ya mashimo **6** (6 Cells) katika madampo matano ya kisasa katika Miji mitano ya Dodoma, Arusha, Mbeya, Mtwara Mikindani na Kigoma unakamilika. Vilevile, ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa **7.25** pamoja na uwekaji wa taa za barabarani katika barabara zilizojengwa nao pia umekamilika.

### Programu ya Kuzijengea Uwezo Halmashauri za Miji

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kuzijengea Uwezo Halmashauri za Miji inaendelea kutekelezwa katika Miji 18 ambayo ni Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Singida, Musoma, Iringa, Bukoba, Kibaha, Mpanda na Lindi na Halmashauri za

Miji ya Njombe, Babati, Geita, Korogwe na Bariadi. Kupitia programu hii, jumla ya kilometa **64.38** za barabara zimejengwa kati ya kilometa **220** za barabara zilizopangwa kujengwa. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa **67.03** ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inatekeleza Programu ya Kuendeleza Miji 18 ambao unagharimu shilingi **bilioni 571.2** kwa kipindi cha Miaka mitano (5). Katika kuboresha na kupanga Miji, uandaaji wa Mipango Kabambe ya uendelezaji wa Miji katika Miji 18 unaendelea. Hadi kufikia Januari, 2018 Mipango Kabambe ya Miji mitatu (3) imezinduliwa, Mipango Kabambe ya Miji mitano (5) imewasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kuidhinishwa na Mipango Kabambe ya Miji saba ipo katika maandalizi. Hadi kufikia Desemba, 2017 kiasi cha shilingi **bilioni 91.9** zimetolewa na kutumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara za lami, mifereji, uwekaji wa taa za barabarani, madampo na ununuzi wa magari ya taka ngumu.

**Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam**

**58.** **Mheshimiwa Spika,** mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam umepangwa kutekelezwa kwa miaka mitano kwa gharama ya shilingi **bilioni 660.** Serikali inaendelea kutekeleza malengo ya Programu ya Kuendeleza Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam ambapo jumla ya barabara zenye urefu wa **kilometa 15** zimejengwa likiwemo tuta la **kilometa 1.5** lenye daraja la **meta 16** na makalvati kwenye bonde la mto Mzinga linalounganisha maeneo ya Kijichi na Tuangoma. Aidha, usanifu wa miradi ya barabara zenye urefu wa **kilometa 110** umekamilika. Jumla ya shilingi **bilioni 17.7** zimetumika kutekeleza miradi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, Serikali inaendelea na usanifu wa mradi wa Bonde la Mto Msimbazi unaofanywa na Kampuni mbili za *COWI Tanzania Ltd* na *ECORYS* ya nchini *Netherland* ili kumpata Mkandarasi wa kujenga na kuboresha

miundombinu ya bonde hilo. Kazi ya usanifu imepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2018. Mradi huu utatekelezwa kwa mkopo wa Dola za **Kimarekani milioni 20** kutoka *Department for International Development (DfID)* ikiwa ni mkakati wa kupunguza athari za mazingira na mafuriko katika Bonde la Mto Msimbazi.

**Mradi wa Kuondoa Vikwazo vya Upitikaji (Improving Rural Access in Tanzania).**

**60.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, mradi wa kuondoa vikwazo uliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilioni 10.95** kwa ajili ya matengenezo maalum ya **kilometa 122.2** kwenye Halmashauri **9** ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Kyerwa, Kishapu, Babati, Kondoa, Magu, Mpwapwa, Bariadi, Kibiti na Songwe. Hadi Februari, 2018 jumla ya shilingi **bilioni 4.36** zimetumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa **kilometa 24**. Aidha, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), imetumia shilingi **bilioni 15.74** kujenga **kilometa 11.45** za barabara na **kilometa 78** zinaendelea kujengwa.

**Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma (PFMRP V)**

**61.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imekuwa ikitekeleza Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) kwa vipindi tofauti tangu mwaka 1998 ambapo PFMRP Awamu ya IV ya utekelezaji ilikamilika Juni, 2017. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Programu imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:- kuimarisha Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha (IFMS – EPICOR 9.05) ambao umefungwa katika Halmashauri zote 185, kufanya mapitio ya Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuzihuisha Sheria ndogo kulingana na wakati na Sheria mama, kuandaa Mwongozo wa namna bora ya kuwatambua wafanya biashara wadogo wadogo (Wamachinga) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mfumo (LGRCIS) pamoja na ununuzi wa Mashine za

Kieletroniki za kukusanya mapato (POS) kwa ajili ya Halmashauri zenye uwezo mdogo katika ukusanyaji wa mapato.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa Mwongozo kwa lugha ya Kiswahili wa Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuanzishwa kwa mfumo wa utoaji taarifa za Fedha zinazopekelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (Fiscal Transfer Web Portal) ambayo imeunganishwa kwenye Tovuti ya OR-TAMISEMI ili kuweka uwazi wa taarifa hizo na kuandaa na kusambazwa kwa Miongozo ya Maeneo muhimu sita (6) ya Usimamizi wa fedha itakayotumika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Ukaguzi wa ndani na nje, ununuzi, Mikopo na Uwekezaji, Ukusanyaji wa mapato, Mipango na Bajeti na Taarifa za Kihasibu na za Fedha.

**Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

**63.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI inaendelea kusimamia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi Mwaka 2020/21. Programu hii imelenga kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa maeneo ya mijini na vijijini kwa kuboresha miundombinu, usimamizi na uendelezaji endelevu wa rasilimali za maji.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Halmashauri ziliidhinishiwa shilingi **bilioni 267.3** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji **366**. Hadi Februari 2018, shilingi **bilioni 91.08** zilipokelewa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Katika kipindi hicho miradi **71** imetekelezwa na kukamilika kwa gharama ya shilingi **bilioni 14.0**. Miradi iliyokamilika inajumuisha miradi ya mserereko **6** na miradi **43** inayoendeshwa kwa Nishati. Miradi hiyo ina jumla ya vituo **990** vya kuchotea maji ambavyo vinahudumia wananchi **247,500**.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuimarisha na kuunda vyombo huru vya watumiaji maji kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Hadi Februari, 2018, jumla ya Jumuiya za Watumiaji Maji **565** zimeundwa na kufanya idadi ya Jumuiya zilizopo kuwa **2,796.** Lengo la kuundwa kwa Jumuiya hizo ni kuwa na mifumo thabiti ya kusimamia uendelevu wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Shirika la Maendeleo la Uingereza inatekeleza mfumo wa malipo kwa matokeo *(Payment by Results -PbR)* uliozinduliwa katika mwaka wa fedha 2016/17. Mfumo huo unahusisha utoaji wa fedha kwa Halmashauri kulingana na ufanisi, usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kuchotea maji. Kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, jumla ya Halmashauri **74** zilikidhi vigezo vya usimamizi wa miradi ya maji na kupata fedha shilingi **bilioni 1.7.** Hadi Februari, 2018 jumla ya Halmashauri **95** zimekidhi vigezo na kupewa jumla ya shilingi **bilioni 8.55** kwa ajili ya ujenzi na ukabarati wa miundombinu ya maji katika mwaka huu wa fedha wa 2017/18. Aidha, Halmashauri zingine zilizobaki zitaendelea kujengewa uwezo ili nazo ziweze kukidhi vigezo.

## Mradi wa Kukabiliana na Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi

**67.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (UKAID) kupitia Shirika lake la Maendeleo (Department for International Development-DfID) na Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (International Institute for Environment and Development-IIED) na *Shirika la Hakikazi Catalyst* la Arusha inatekeleza mradi wa kukabiliana na kujenga ustahimilivu wa athari za mabadiliko ya Tabianchi. Lengo kubwa la mradi huu ni kuhakikisha mipango ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali inafungamanishwa na masuala ya mabadiliko ya Tabianchi ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo Mwaka 2030.

**68. Mheshimiwa Spika,** Awamu ya Kwanza ilianza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2012/13 na kuhusisha Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Arusha ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Monduli, Ngorongoro na Longido. Kupitia mradi huu Halmashauri zinajengewa uwezo na ujenzi wa miundombinu ili kuhakikisha ustahimilivu wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi. Jumla ya miradi **34** imetekelezwa ambapo baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa skimu ya maji msererereko, ujenzi wa mifereji ya kudhibiti mafuriko, ujenzi na ukarabati wa malambo na mabirika ya kunyweshea mifugo, ujenzi wa masoko ya mifugo na ukarabati na uhifadhi wa vyanzo vya maji. Kazi nyingine zilizofanyika ni ujenzi wa maabara za mifugo, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao na ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji. Miradi hiyo ambayo inanufaisha wananchi **436,569** imegharimu shilingi **bilioni 2.0** hadi kukamilika.

## IV. TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI

### Tume ya Utumishi wa Walimu

**69. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Desemba, 2017, walimu **4,054** walisajiliwa, walimu **2,173** walithibitishwa kazini na walimu **1,084** wamewezeshwa kukamilisha taratibu za kustaafu. Aidha, mashauri ya nidhamu **250** yalipokelewa na mashauri **156** yamefanyiwa kazi na kutolewa uamuzi sawa na **asilimia 60.2.**

**70. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2017 walimu **869** wamefunguliwa mashtaka ya nidhamu. Mashauri **401** yapo kwenye hatua mbalimbali ya uamuzi kwa mujibu wa Sheria.

### Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA)

**71. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural and Urban Roads Agency–TARURA)* umeanzishwa rasmi kwa Sheria ya Wakala za Serikali Sura 245 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 211 la tarehe 12/05/2017. Wakala ulianza kutekeleza majukumu yake Julai,

2017. Wakala unasimamia ujenzi wa barabara na madaraja, ukarabati na matengenezo ya mtandao wa barabara za Halmashauri zenye urefu wa kilometa **108,946.2** vijijini na mijini. Kati ya barabara hizo, kilometa **56,000** zinafanyiwa mchakato wa kuzihakiki ili hatimaye ziweze kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili zitambulike ki-sheria na kilometa **52,946.2** tayari zinatambulika na zimeshatangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Lengo la Serikali kuanzisha TARURA ni kuleta ufanisi katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara ambazo awali zilikuwa zinasimamiwa na Halmashauri.

**72. Mheshimiwa Spika,** TARURA inatekeleza majukumu yake kupitia Fedha za Mfuko wa Barabara ambapo katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Wakala umeidhinishiwa shilingi bilioni **230.8** kwa ajili ya matengenezo ya barabara kilomita **34,024.** Hadi Februari, 2018, TARURA imepokea shilingi **bilioni 98.5** ambazo zimetumika kutengeneza barabara zenye urefu wa kilometa **4,183.31,** ujenzi wa madaraja **35,** Makalavati makubwa **43,** *Drift* 4, na Makalavati madogo **364.** Wakala unategemea kuongeza mtandao wa barabara za lami katika Halmashauri kutoka kilometa **1,585.51** zilizopo sasa hadi kilometa **2,059.83** ifikapo Mwaka 2020.

**Shirika la Elimu Kibaha**

**73. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Elimu Kibaha linaendelea kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake ambayo ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo yaani Ujinga, Umaskini na Maradhi. Hadi Februari, 2018, Shirika limetoa huduma kwa wagonjwa **33,652** wakiwemo wagonjwa **2,806** waliolazwa. Pia Hospitali ilihudumia majeruhi wa ajali za barabarani **352,** na majeruhi wasio wa ajali za barabarani wapatao **129**. Shirika limeanzisha huduma ya matibabu ya Mdomo Sungura *"Cleft Lip and Palate"* ambapo wagonjwa **22** wameshanufaika na huduma hii. Huduma hii inagharamiwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali lijulikanalo kama *SmileTrain* la nchini Marekani. Vilevile, kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha na Hospitali ya Tumbi, Shirika liliendelea kutoa mafunzo kwa kada za maafisa tabibu, Afya ya Jamii, uuguzi na ukunga kwa ngazi ya stashahada, na

wauguzi wasaidizi kwa ngazi ya cheti ambapo kwa sasa Chuo kinao wanafunzi **265** wanaoendelea na masomo.

**74.** **Mheshimiwa Spika**, Shirika limefanikiwa kutoa elimu na malezi kwa wanafunzi **2,614.** Wanafunzi **904** walipata elimu ya msingi na wanafunzi **1,710** walipata elimu ya sekondari. Kwa upande wa maktaba, wanafunzi pamoja na wadau wengine **20,499** walipata huduma za kujisomea vitabu na majarida mbalimbali. Aidha, mafunzo ya vitendo yanaendelea kutolewa na Shirika kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi chenye wanachuo **279.** Mafunzo yanayotolewa ni Kilimo, Mifugo, Uashi, Ufundi Bomba, Useremala, Ushonaji, Upishi, Ufundi wa Magari, Uundaji na Ufuaji vyuma na Umeme wa majumbani.

### Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo

**75.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/18, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi **3,485** ambapo wanafunzi wa kike ni **2,067** na wa kiume **1,178.** Aidha, Chuo kiliendesha mafunzo mbalimbali ya muda mfupi katika Tawala za Mikoa, Halmashauri pamoja na Taasisi na Mashirika ya Umma. Vilevile, Chuo kimetoa ushauri wa kitaalam kwenye maeneo mbalimbali ya kujenga uwezo hususan utoaji taarifa, tathmini na upimaji.

### Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

**76.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Bodi ilikadiria kukusanya mapato ya ndani ya shilingi **bilioni 5.71.** Hadi Februari, 2018 Bodi imefanikiwa kukusanya shilingi **bilioni 1.11** sawa na **asilimia 20** ya lengo. Aidha, Bodi imefanikiwa kutoa mkopo wa shilingi **milioni 450.00** katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

### Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa

**77.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ulipanga kukusanya mapato ya kiasi cha shilingi **bilioni 611.67.** Hata

hivyo, makisio hayo yalifanyiwa marekebisho baada ya miezi sita na kuwa shilingi **bilioni 543.34** kutokana na kuondolewa wafanyakazi wasio na sifa katika utumishi wa umma. Kiasi kilichopungua ni shilingi **bilioni 68.33.** Hadi Desemba, 2017 makusanyo halisi yamefikia shilingi **bilioni 254.65** sawa na **asilimia 41.6** ya lengo. Thamani ya Mfuko inatarajiwa kukua kwa **asilimia 16** kutoka shilingi **trilioni 1.75** ya Mwaka wa Fedha 2017/18 hadi shilingi **trilioni 2.4** ifikapo Juni, 2019.

**Shirika la Masoko Kariakoo**

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa ajili ya kusimamia na kuendesha masoko ya mazao ya chakula, zana za kilimo na pembejeo za kilimo katika Jiji la Dar es Salaam. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Shirika lilikadiria kukusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi **bilioni 3.6** kutokana na ushuru wa mazao, kodi ya pango na ada ya kutumia soko. Hadi Februari, 2018 Shirika limekusanya shilingi **bilioni 1.7** sawa na **asilimia 47** ya lengo.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** fedha hizo zimetumika kulipa mishahara ya watumishi wa Shirika, uendeshaji wa biashara, kulipa kodi ya mapato, ujenzi wa maduka **94,** utatuzi wa mgogoro wa viwanja vya Shirika Mbezi Beach, ukarabati wa nyumba za Shirika na barabara kuzunguka Shirika, kumaliza mashauri **16** yaliyokuwa Mahakamani, kufunga mitambo ya CCTV na kulipa madeni ya Shirika kiasi cha shilingi **milioni 176.7.**

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam**

**80.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Wakala umefanikiwa kufanya maandalizi ya Awamu ya Pili na Tatu ya ujenzi wa miundombinu ya DART ambapo taratibu za ununuzi zimefanyika ili kuwapata Wakandarasi wa kujenga miundombinu hiyo. Wakala umeendelea kuimarisha usimamizi na usalama wa miundombinu ya mradi katika vituo vikuu (5), vituo vidogo ishirini na saba (27), madaraja ya watembea kwa miguu matatu (3) pamoja na karakana. Aidha, umesimikwa mfumo wa kielektroniki wa masjala pamoja na mfumo wa usimamizi na udhibiti wa

fedha – Epicor 10.1 kwa lengo la kuboresha utendaji, ufanisi na uwajibikaji.

**81. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zilizofanyika ni kuendelea na ukamilishaji wa taratibu za ununuzi wa kumpata mtoa Huduma wa pili (SP2), mafunzo ya viwango vya ubora wa Kimataifa kwa watumishi wa Wakala; ujenzi wa uzio kuzunguka vituo vikuu vitatu (3) vya Ubungo, Kivukoni na Morocco ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya nauli na usalama wa abiria ambao umepangwa kukamilika Juni 2018. Aidha, Wakala umefunga Kituo cha Mawasiliano cha muda ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya mwenendo wa mabasi katika mfumo wa DART.

**82. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi wa DART umeliwezesha Jiji la Dar es Salaam kupewa tuzo ya ***Usafiri Endelevu na kuwa Jiji Bora duniani (Sustainable Transport Award)*** kwa Mwaka 2018**.** Vigezo vilivyotumika kupata tuzo hiyo ni pamoja na kupanga mradi kwa ufanisi mkubwa, kujenga miundombinu mizuri, kuzingatiwa kwa mahitaji ya watumiaji mbalimbali na kutoa elimu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka kwa watumiaji kupitia Mpango Mkakati wa Wakala. Kutokana na ufanisi wa utekelezaji wa mradi wa DART, Nchi mbali mbali zimekuja Tanzania kujifunza mafanikio na changamoto za mradi huu zikiwemo nchi za Zambia, Zimbabwe, Uganda, Kenya, Ethiopia, Senegal na Rwanda. Aidha, tuzo hiyo imeipa Tanzania heshima ya kuandaa Mkutano wa Kimataifa wa Masuala ya Usafirishaji mijini utakaofanyika Juni 2018 hivyo kufungua fursa za kiuchumi, uwekezaji na utalii.

**83. Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa DART kutoka wastani wa abiria **76,000** kwa siku Mei, 2016 mradi ulipoanza kutekelezwa hadi abiria **209,000** kwa siku Machi, 2018. Ongezeko la watumiaji wa DART limeongeza mapato kutoka wastani wa shilingi **milioni 8.13** Mei, 2016 hadi wastani wa shilingi **bilioni 3.6** kwa Mwezi Agosti, 2017. Vilevile, muda wa safari kutoka Kimara hadi Kivukoni kwa usafiri wa mabasi ya kawaida umepungua

kutoka **saa 2** za awali hadi wastani wa dakika **40** baada ya mabasi ya DART kuanza kufanya kazi na gharama za nauli zimepungua kutoka takriban **shilingi 20,000** kwa gari binafsi hadi shilingi **1,300** kwa siku. Aidha, msongamano wa magari barabarani umepungua hususan katika barabara ya Morogoro.

**84. Mheshimiwa Spika,** mradi umetoa fursa za ajira kwa zaidi ya watu **1,000** pamoja na watoa huduma wakiwemo watumishi wa UDA-RT, Maxcom, kampuni ya ulinzi, usafi na maegesho ya magari katika eneo la Kimara. Aidha, matumizi ya teknolojia yakiwemo matumizi ya kadi badala ya fedha taslimu yamerahisisha abiria kuingia na kutoka kwenye vituo na kudhibiti upotevu wa mapato.

## V. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

**85. Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya Mpango na Bajeti ya OR-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19, azma ya kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015, Agenda ya Dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuzindua Bunge Novemba, 2015 na maagizo mbalimbali ya Viongozi.

**86. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/ 19, OR -TAMISEMI, itaendelea kutekeleza vipaumbele mbalimbali, kama ifuatavyo:-

i) Kuimarisha amani na utulivu nchini, kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

ii) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

iii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi (Core Business) ya kila Taasisi yaliyoainishwa kwenye Mipango Mikakati yao;

iv) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya Biashara na Uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;

v) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali, programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vi) Kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyingine;

vii) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi;

viii) Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na;

ix) Kusimamia maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**Tawala za Mikoa**

**87. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Tawala za Mikoa zitatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;

(ii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa,

Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Tarafa;

(iii) Kuendesha mikutano ya Kisheria ya Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Mkoa (RCC) ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi zote;

(iv) Kuratibu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Mwaka 2019;

(v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisekta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;

(vi) Kuratibu masuala mtambuka yanayotekelezwa kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vii) Kushughulikia migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(viii) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali za uchumi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ix) Kuandaa Mipango Mikakati ya Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Kuzingatia Mpango wa Pili wa Maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015;

(x) Kuanzisha na kurasimisha utengaji wa maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda, kilimo, ufugaji, makazi, hifadhi za wanyamapori, misitu na vyanzo vya maji;

(xi) Kusimamia rasilimali watu, fedha na vifaa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(xii) Kuanzisha na kusimamia madawati ya kuratibu malalamiko kuhusu huduma zinazotolewa kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**88. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/ 19, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zitatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kujenga na kukarabati miundombinu ya kijamii na kiuchumi hususan katika sekta za elimu, maji, afya, kilimo, mifugo, uvuvi, barabara na sekta nyingine kwa kushirikisha nguvu ya wananchi;

(ii) Kuendesha Mikutano ya Kisheria ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa ili kuimarisha masuala ya utawala bora na uwajibikaji;

(iii) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato;

(iv) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati itakayosaidia kuongeza mapato ya Halmashauri**;**

(v) Kuwezesha Vikundi vya Vijana na Wanawake kupata mikopo kupitia Mifuko ya Maendeleo ya Vijana na Wanawake;

(vi) Ukamilishaji wa miradi viporo, majengo ya Ofisi na makazi ya Viongozi na watumishi hasa katika maeneo mapya ya utawala;

(vii) Kuanza maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Mwaka 2019;

(viii) Kusimamia mpango wa utoaji wa elimumsingi bila malipo katika shule za Msingi na Sekondari;

(ix) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya uwekezaji na maendeleo ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa;

(x) Utunzaji wa mazingira na hifadhi ya vyanzo vya maji; na

(xi) Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na kuanzisha mazao mbadala ili kupunguza hasara pamoja na kuwezesha viwanda vya usindikaji.

## VI. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OR - TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)89.**
**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka-Dar es Salaam umepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuanza Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya DART utakaohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe zenye urefu wa **kilometa 20.3.** Ujenzi umepangwa kuanza Desemba, 2018 baada ya kumpata Mkandarasi. Mradi huu utatekelezwa kupitia mkopo wa Dola za Marekani **milioni 141.71** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika;

(ii) Kuanza Awamu ya Tatu ya ujenzi wa miundombinu ya DART utakaohusisha barabara za Nyerere, Uhuru, Bibi Titi, Azikiwe, Shaurimoyo, Lindi na Maktaba zenye urefu wa **kilometa 23.6** kwa mkopo wa dola za Marekani **milioni 148.2** kutoka Benki ya Dunia. Kazi ya ujenzi imepangwa kuanza Desemba, 2018;

(iii) Kuanza usanifu wa Awamu ya Nne ya ujenzi wa miundombinu ya DART kwa mkopo wa dola za Marekani **milioni 97.9** kutoka Benki ya Dunia. Usanifu utahusisha barabara za Sam Nujoma, Bagamoyo, Bibi Titi na Ali Hassan Mwinyi zenye urefu wa **kilometa 25.9;**

(iv) Ujenzi wa Maegesho katika maeneo ya mfumo wa Wakala;

(v) Kukamilisha taratibu za upatikanaji wa Mtoa Huduma wa Pili (SP2), Mkusanyaji Nauli, Msimamizi wa Fedha pamoja Mshauri Mwelekezi'' Transaction Advisor'' kwa ajili ya awamu ya tatu;

(vi) Kuhakikisha upatikanaji wa Mfumo wa ´´Intelligent Transport System (ITS)" wa Serikali na kuwajengea uwezo watumiaji wake;

(vii) Kutekeleza Mpango Kazi wa Fidia ya Makazi kwa waathirika wa mradi wa awamu ya pili na tatu ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kwa ajili ya mradi wa awamu ya 2, 3 na 4;

(viii) Uboreshaji na ujenzi wa vituo mlisho (*bus stops*); maeneo ya kugeuzia mabasi (*bus turning facilities*) pamoja na kuweka mipaka karakana ya Jangwani; na

(ix) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam.

**Tume ya Utumishi wa Walimu**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwezesha Makao Makuu na Wilaya **139** kufanya vikao vya Kisheria vya kusikiliza mashauri ya nidhamu na kuthibitisha walimu kazini;

(ii) Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa utunzaji wa taarifa za Walimu;

(iii) Kuwajengea uwezo Watumishi wa Tume ili kutekeleza Majukumu yao ipasavyo;

(iv) Kuratibu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya **139;** na

(v) Kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa wa Walimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Shirika la Elimu Kibaha**

**91. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa huduma za afya za kinga na tiba katika hospitali ya Tumbi;

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya Afya ya mazingira, uuguzi na utabibu kwa wanafunzi **265** katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;

(iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **1,710** wa Sekondari na Wanafunzi **904** wa shule za msingi;
(iv) Kuendelea kutoa huduma za maendeleo ya jamii ili kuiwezesha Taasisi kuondokana na umaskini kwa kutoa mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya wananchi Kibaha na shamba darasa la mifugo na mazao;

(v) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya hospitali;

(vi) Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa jamii kulingana na uhitaji uliopo;

(vii) Kujenga miundombinu ya shule ikiwemo maabara katika shule ya sekondari ya wasichana ya Kibaha na vyoo vya nje katika shule ya sekondari Kibaha; na

(viii) Kukarabati mabanda ya mifugo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa vitendo katika shamba darasa la mifugo na mazao.

**Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) umepanga kufanya kazi zifuatazo:-

i) Matengenezo ya kawaida ya barabara za changarawe na udongo kilometa **13,163.89;**

ii) Matengenezo ya sehemu korofi kilometa **6,201.22;**

iii) Matengenezo maalum ya barabara kilometa **3,925.94;**

iv) Ukarabati wa madaraja **117,** mifereji urefu wa meta **67,844 na** makalvati **1,881**;

v) Matengenezo ya kawaida kwenye barabara za lami kilometa **54.72** na ujenzi wa kilometa **34.2** kwa kiwango cha lami;

vi) Kujenga uwezo wa Wahandisi katika maeneo ya usanifu na usimamizi wa Mikataba; na

vii) Kuimarisha maabara iliyopo pamoja na kununua vifaa vya upimaji wa kazi za barabara.

**Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo**

**93.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo kimepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kudahili wanafunzi wapya **2,500;**

ii) Kufanya shughuli za utafiti katika maeneo ya mifumo, uongozi na usimamizi wa rasilimali fedha na watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iii) Ununuzi wa vitabu nakala **500** na kompyuta **25** kwa ajili ya Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA);

iv) Kuajiri watumishi wapya **72**; na

v) Kukusanya mapato ya ndani kupitia vyanzo vilivyopo.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**94.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa itatekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kutoa mikopo kwenye Halmashauri;

ii) Kufanya ufuatiliaji wa uwasilishaji wa marejesho ya mikopo na michango kutoka kwenye Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi;

iii) Kubuni vyanzo vipya vya mapato;

iv) Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili waweze kufahamu majukumu ya Bodi na huduma zinazotolewa;

v) Kuboresha muundo wa Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa mikopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi zaidi; na

vi) Kuandaa mwongozo wa kuboresha utoaji wa mikopo kwa vikundi mbalimbali kupitia Mfuko wa Wanawake na Vijana.

**Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa**

**95.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa umepanga kufanya shughuli zifuatazo:-

(i) Kuandikisha wanachama wapya **21,128;**

(ii) Kuendelea kukusanya michango ya wanachama;

(iii) Kukusanya mapato kutokana na uwekezaji**;**

(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Mfuko;

(v) Kufanya uwekezaji katika kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills Ranch;

(vi) Kuanzisha Ofisi Ndogo za uratibu katika Mikoa ya Tabora na Kagera;

(vii) Kiwanda cha kuchakata Tangawizi Same; na

(viii) Kiwanda cha maturubai Morogoro, sekta ya mafuta na gesi na viwanda vingine kwa kushirikiana na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii.

**Shirika la Masoko Kariakoo**

**96. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Shirika la Masoko Kariakoo litatekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kufanya marekebisho ya Sheria Na. 36 ya Mwaka 1974 iliyoanzisha Shirika;

ii) Kufanya shughuli za uwekezaji katika viwanja vinavyomilikiwa na Shirika ambavyo viko Mbezi Beach, Tabata Bima, Mbezi Makonde na soko dogo lililopo katikati ya Jiji la Dar es Salaam; na

iii) Kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato (Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS) ili kuongeza mapato ya Shirika.

**MALENGO MAHSUSI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

**97. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, OR-TAMISEMI itatekeleza kazi maalum zifuatazo:-

i) Ujenzi wa Hospitali **67** za Halmashauri katika Halmashauri **67** ambazo hazina Hospitali hizo ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6);***

ii) Maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Mwaka 2019;

iii) Kutekeleza miradi ya kimkakati katika Halmashauri **21** zilizokidhi vigezo kwa ajili ya kuongeza mapato ya Halmashauri;

iv) Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri **22** ambazo hazina Ofisi ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6)***;

v) Ununuzi wa boti saba (**7**) kwa ajili ya kutatua changamoto za usafiri majini katika Halmashauri za Wilaya za Ludewa, Kibiti, Rufiji, Mafia, Ukerewe, Kigoma na Nyasa ***(kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6)***;

vi) Ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilometa 85** kwa kiwango cha lami kupitia Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari;

vii) Ujenzi wa **kilometa 80.96** za lami pamoja na ujenzi wa mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa **kilometa 16.47**, ujenzi wa stendi ya mabasi Mkoani Dodoma na ununuzi wa vifaa vya kukusanyia taka katika Halmashauri saba za Manispaa kupitia Mradi wa Miji ya Kimkakati (TSCP);

viii) Ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilometa 220** kupitia Programu ya Kuimarisha Miji katika Halmashauri za Manispaa na Miji **18** pamoja na kuweka taa za barabarani kwenye barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami;

ix) Kuratibu ujenzi wa viwanda **100** kwa kila Mkoa katika Mikoa yote **26**;

x) Kutenga **ekari 228,543** kwa kila Mkoa katika Mikoa yote **26** kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo, kati na vikubwa; na

xi) Kuondoa riba kwenye mikopo kwa vikundi vya Vijana na Wanawake kwa fedha inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani katika Halmashauri.

## Shukrani

**98.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kukushukuru tena wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote. Kipekee niishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wetu wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA), UNFPA, UN-Habitat, Shirika la Maendeleo ya Ubelgiji (BTC), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA), UNICEF, UNDP, pamoja na nchi zote zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Kusaidia Bajeti ya Serikali. Mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya OR-TAMISEMI yamepatikana kutokana na ushirikiano mzuri wa Wadau wa Maendeleo ambao waliendelea kushirikiana katika utekelezaji wa Programu na Miradi mbalimbali katika Sekta za afya, elimu, maji, barabara, fedha, kilimo na maboresho ya mfumo wa Serikali za Mitaa. OR-TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ili kutimiza azma ya kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia miradi inayotekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi wenyewe.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutambua kazi kubwa inayofanywa na Viongozi wenzangu katika OR-TAMISEMI nikianzia na Mheshimiwa Joseph George Kakunda (Mb.), Naibu Waziri Ofisi ya Rais –TAMISEMI anayeshughulikia masuala ya huduma za elimu, maji na utawala, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb.), Naibu Waziri anayeshughulikia huduma za afya, miundombinu na uwekezaji, Mhandisi Mussa I. Iyombe, Katibu Mkuu, Bw. Tixon T. Nzunda, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Elimu, na Dkt. Zainab A.S. Chaula, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Afya, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Aidha, ninawashukuru Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya OR-TAMISEMI na watumishi wa OR-TAMISEMI katika ngazi zote kwa utekelezaji makini wa majukumu yao katika kuboresha huduma kwa wananchi.

**100. Mheshimiwa Spika,** kipekee napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa kuendelea kuwa wavumilivu mara zote nilipokuwa mbali nao kwa majukumu ya Kitaifa. Naahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote. Aidha, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu haya ya kuwatumikia wananchi.

## VII. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/19

### Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani101.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, OR - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 185 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya shilingi Bilioni **Mia Saba Hamsini na Nane, Milioni Mia Tatu Sitini na Mbili, Mia Saba Kumi na Moja Elfu, Mia Saba Tisini na Tisa (shilingi 758,362,711,799.00).** Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

### Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

| Na. | OFISI/TAASISI | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| 1. | OR – TAMISEMI | **20,000,000.00** |
| 2. | Taasisi | **22,623,519,091.00** |
| 3. | Mikoa | **130,563,708.00** |
| 4. | Halmashauri | **735,588,629,000.00** |
| **JUMLA** | | **758,362,711,799.00** |

12

**Mheshimiwa Spika,** sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka

wa Fedha 2018/19 jumla ya shilingi **Trilioni Sita, Bilioni Mia Tano Themanini na Sita, Milioni Mia Tisa Kumi na tano, Mia Saba Hamsini na tatu Elfu, Mia Saba Thelathini na Tatu (Shilingi 6,586,915,753,733.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu fungu Na. 02 na mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 185. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 ni kama ifuatavyo:-

**Muhtasari wa Fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19**

| AINA YA MATUMIZI | FEDHA ZINAZOOMBWA |
|---|---|
| **OR-TAMISEMI** | |
| **A) Mishahara** | |
| Makao Makuu | 8,736,397,905 |
| Taasisi | 14,916,444,000 |
| **Jumla Ndogo Mishahara** | **23,652,841,905** |
| **B) Matumizi Mengineyo** | |
| Makao Makuu | 17,896,530,002 |
| Taasisi | 1,318,870,806 |
| **Jumla Ndogo Matumizi Mengineyo** | **19,215,400,808** |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida (A+B)** | **42,868,242,713** |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU** | |
| Mishahara | 7,893,115,025 |
| Matumizi Mengineyo | 4,622,145,495 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida (TSC)** | **12,515,260,520** |
| **MIKOA NA HALMASHAURI** | |
| **MIKOA:** | |
| Mishahara | 159,941,766,000 |
| Matumizi Mengineyo | 45,219,821,000 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **205,161,587,000** |
| **HALMASHAURI:** | |
| Mishahara | 3,942,713,089,000 |
| Matumizi Mengineyo (Ruzuku SK) | 190,390,615,000 |
| Matumizi Mengineyo (Own source) | 389,862,000,000 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | **4,522,965,704,000** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| **OR-TAMISEMI** | |
| Fedha za Ndani | 283,642,430,000 |
| Fedha za Nje | 61,471,111,000 |
| **Jumla OR-TAMISEMI** | **345,113,541,000** |
| **MIKOA** | |
| Fedha za Ndani | 80,120,000,000 |
| Fedha za Nje | 13,064,414,000 |
| **Jumla Mikoa** | **93,184,414,000** |
| **HALMASHAURI** | |
| Fedha za Ndani (SK) | 566,773,370,500 |
| Fedha za Ndani (MH) | 345,726,629,000 |
| **Jumla Ndogo** | **912,499,999,500** |
| Fedha za Nje | 452,607,005,000 |
| **Jumla Maendeleo Halmashauri** | **1,365,107,004,500** |
| **Jumla Maendeleo Mikoa na Halmashauri** | **1,458,291,418,500** |
| **Jumla Miradi ya Maendeleo** | **1,803,404,959,500** |
| **JUMLA KUU** | **6,586,915,753,733** |

**103. Mheshimiwa Spika,** pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya OR-TAMISEMI, Taasisi, Mikoa na Halmashauri.

**104. Mheshimiwa Spika,** hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya OR-TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Imetolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Suleiman Said Jafo hoja imeungwa mkono. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Sekretarieti ya Maadli ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Ushauri wa Mafuta na Gesi (Fungu 11), Menejiment ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 9), Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha mopango wa utekelezaji wa Makadirio ya fedha kwa Ofisi ay Rais, Menejimenti ya

Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uwezo wa kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Namuahidi Mheshimiwa Rais kwamba nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Newala Mjini kwa ujumla kwa kuendelea kunipa ushirikiano ninapoendelea kuwawakilisha. Vilevile naishukuru familia yangu, mke wangu Anna na wajukuu zangu ambao wananikosa kucheza nao mara kwa mara wakati babu yao anapotekeleza majukumu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mabadiliko ya Kamati ya Kudumu ya Bunge yaliyofanyika, naomba kuwapongeza mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum - Tabora kwa kuendelea katika nyadhifa zao. Pia nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuchanguliwa katika nafasi zao zenye dhamana ya kusimamia Kamati katika kuishauri Serikali na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2017/2018 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Maoni na ushauri wa Kamati hiyo yametuwezesha na yataendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapakazi na utendaji wenye matokeo katika utumishi wa umma.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyotuongoza na anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi wake shupavu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri wetu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji, usimamizi na uratibu wa kazi kila siku za Serikali na kuwa kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupongeze wewe binafsi, naomba kumpongeza Mheshimiwa Spika, kumpongeza Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge ukiwepo na wewe uliyekalia kiti sasa kwa umahiri na kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mawaziri wenzangu wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na dira ya mandeleo ya mwaka

2025. Kwa namna ya pekee nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Suleiman Jafo (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mmitaa na Manaibu wake Mheshimiwa Joseph George Kakunda, nilisahau hapa kuweka George na Mheshimiwa Josephat Kandege kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais kwa sababu tunafanya katika Ofisi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochanguliwa hivi karibuni Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Songea Mjini), Mheshimiwa Justine Joseph Monko (Singida Kaskazini), Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa (Longido), Mheshimiwa Alfreda Kahigi (viti maalum), Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, (Viti Maalum), Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili (Viti Maalum), Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim (Viti Maalum), Mheshimiwa Shamsa Aziz Mtamba (Viti Maalum), Mheshimiwa Sonia Jumaa Magongo (Viti Maalum) na Mheshimiwa Zainab Mndolwa (Viti Maalum).

Aidha, nawapongeza Wabunge wenzangu walioshinda uchaguzi na kuapishwa katika mkutano huu wa Bunge la bajeti ambao ni Mheshimiwa Maulid Mtulia Mbunge wa Kinondoni na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel Mbunge wa Siha. *(Makofi)*

Vile vile, kwa masikitiko makubwa sana natoa pole kwa msiba wa Mheshimiwa Leonidas Tulubeti Gama Mbunge wa (Songea Mjini), tunaomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Balozi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Charles Mwankupili, Kaimu Katibu Mkuu Ikulu, Ofisi ya Rais, Ikulu, Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bi. Dorothy Mwaluko, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na watumishi wote kwa kazi nzuri

wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru nchi wahisani na washirika wa maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo na wananchi. Hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kushukuru na kuwataja kama ifuatavyo; Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujerumani, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ireland, Israel, Kenya, Rwanda, Somalia, Afrika Kusini, Botswana, Msumbiji, Malawi, Mali, Ghana, Ethiopia, Jamhuri ya Watu wa Kongo, Nigeria, Sierra Leone, Liberia, Ivory Coast, Namibia, Niger, Togo, Zimbabwe, Trinidad na Tobago, na Ubelgiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kushukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Benki ya Dunia, *OFID-OPEC Fund for International Development*, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan *(Japanese Social Development Fund), DfID, KOICA, GIZ, DFATZ, USAID, SIDA, UNDP,* Jumuiya ya Madola*, DANIDA, NORAD,* Mfuko wa Fedha wa Kimataifa *(IMF)* na Taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa watumishi wote wa umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa. Uzalendo wao na imani yao kwa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano umewezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi, kwa ufanisi mkubwa na ubora zaidi na watumishi wa umma kote mliko mimi Waziri wenu nawapongezeni kwa kazi nzuri mnayofanya tuendelee kuwatumikia vizuri wananchi wetu walio tuajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya

Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nyakati mbalimbali kuhusu kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya Serikali na utumishi wa umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ufisadi, uzembe, uvivu, ukiukwaji wa maadili na utumishi hewa na wasio na sifa stahiki kwa kuwawajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazoendelea kuchukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa watumishi wa umma wote kufanya kazi kwa weledi, juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Tunaendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora, kwa haraka na kwa staha ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo ajali na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Pia napenda wakumbuka askari wetu wapiganaji wenzangu wa kulinda amani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo waliofariki wakiliwakilisha Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka wa fedha wa 2017/2018 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa 2017/2018 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Shughuli zilizotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais - Ikulu na Taasisi zake,katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu ilidhinishiwa shilingi bilioni 16.2 kwa ajili ya shughuli za Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2018 shilingi bilioni 12.9 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yake, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) inayojumuisha taasisi zilizo chini ya Ikulu iliidhinishiwa shilingi bilioni 747.8 Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 368.3 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 379.5 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 shilingi bilioni 574.4 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 335 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 238.8 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maelezo kwa kila Taasisi kwa muhtasari, tarifa kamili ya utekelezaji wa shughuli za ikulu na taasisi zake zipo kuanzia ukurasa wa 10hadi wa 33 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Huduma zilitolewa kwa Rais na familia yake. Aidha, ushauri ulitolewa kwa Mheshimiwa Rais kuhusu ratiba ya kila siku, masuala ya siasa, uchumi, jamii, sheria, diplomasia na ushauri mwingine wowote wenye lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Shughuli za Baraza la Mawaziri zilifanyika ambapo mikutano 38 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, mikutano 61 zilichambuliwa; Mikutano 15 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu ilifanyika na nyaraka 39 zilichambuliwa, mikutano 15 ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 10 ziliwasilishwa. Mikutano minne ya Baraza la Mawaziri ilifanyika; nyaraka 30 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi, mikutano minne ya Kamati ya Katiba ya Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo Miswada 14 ilijadiliwa.

(iii) Hotuba 27 za Mheshimiwa Rais zilichapishwa na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Vipindi Maalum vya televisheni 12 kuhusu shughuli za Mheshimiwa Rais na Serikali yake zilitengenezwa na kurushwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari;

(iv) Taarifa kwa vyombo vya habari kutoka ofisi binafsi ya Rais *(Press Releases)* 318 zikiambatana na picha zilichapishwa na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na mitandao ya kijamii;

(v) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu umeanza kutekelezwa ambapo elimu kwa Wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu imetolewa kwa mikoa 16, Wizara zote na taasisi za umma 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kutokana na jitihada za TAKUKURU na wadau wa kuzuia na kupambana na rushwa nchini tatizo la Rushwa limeanza kupungua kiasi katika nchi yetu katika upimaji wa hali ya rushwa uliofanywa na Mashirika ya Kimataifa ambao umeonesha Tanzania kufanya vizuri miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki ikishika nafasi ya pili baada ya Rwanda.

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Uchunguzi wa majalada 325 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuombewa kibali. Majalada 214 kati ya 325 yaliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, majalada mengine yanaendelea kufanyiwa kazi;

(ii) Kesi 725 zilifikishwa mahakamani ikiwemo mpya 201. Katika kipindi hicho, kesi 219 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 81 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 138 watuhumiwa walitiwa hatiani, aidha, kesi 14 ziliondolewa mahakamani Kesi 499 zinaendelea mahakamani;

(iii) Kazi 339 za uchambuzi wa mifumo na warsha/ vikao 179 vya wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa ilifanyika katika sekta 24;

(iv) Miradi ya maendeleo 195 yenye thamani ya shilingi bilioni 154.1 ilifuatiliwa katika Sekta za Elimu, Afya, Maji na Ujenzi. Miradi 73 yenye thamani ya shilingi bilioni 30.9 ilibainika kuwa na mapungufu katika utekelezaji .Tayari uchunguzi umeanzishwa kwenye miradi 31 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.

(v) Elimu kuhusu athari za rushwa na juhudi za Serikali za kuidhibiti ili kupata uungwaji mkono ilitolewa.

(vi) Maandalizi yamefanyika ya kuanza ujenzi wa Ofisi za TAKUKURU katika Wilaya saba, ambazo ni Chamwino, Ruangwa, Manyoni, Namtumbo, Ngorongoro, Masasi na Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi ya Uongozi katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 ;

(i) Mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi (*Post Graduate-Diploma in Leadership)* iliyozinduliwa rasmi tarehe 21 Aprili yameendelea kutolewa;

(ii) Kozi nane za muda mfupi zimetolewa kwa viongozi 238 wa umma ili kuimarisha utendaji kazi;

(iii) Programu ya Kuwajengea uwezo Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa iliandaliwa na kutekelezwa. Programu hii ililenga kuwajengea uwezo katika masuala ya maadili, utawala bora na uwajibikaji; mawasiliano fanisi; utendaji wenye matokeo; uongozi wa kimkakati; usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani, mahusiano kati ya viongozi wa kisiasa na watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), katika kipindi cha utekelezaji:-

(i) Wakulima 589 na viongozi 89 wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika benki na taasisi zingine za fedha katika halmashauri tatu. Aidha, mafunzo yaliyotolewa yakuwawezesha uanzishwaji wa SACCOS nne (4), Vikundi 56 vya uzalishaji na wakulima 140 kufungua akaunti katika benki;

(ii) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Kituo Kimoja cha Urasimishaji wa Biashara kimeanzishwa ambapo huduma Serikali zinapatikana sehemu moja matokeo chanya yanaonyesha ukurasa wa 25 wa kitabu cha hotuba yangu.

(iii) Wafanyabiashara 100 katika Wilaya za Kusini Unguja wafanyabaishara 50 na Micheweni, Pemba 50 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Aidha, MKURABITA iliwezesha Wafanyabiashara hao kutoka Unguja na Pemba kushiriki kwenye Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika nchini Burundi mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni kama zifuatazo:-

(i) Kaya maskini 1,363,448 zimetambuliwa tangu kuanza kwa Mpango. Aidha, baada ya uhakiki, kaya maskini 1,118,751 zenye watu milioni tano ziliandikishwa. Kati ya kaya/watu wote waliomo katika Mpango, asilimia 54 ni wanawake. Mpango huu unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Aidha, shilingi bilioni 185 zilihaiulisha kama ruzuku kwa wanakaya masikini zilizoandikishwa Tanzania bara na Zanzibar.

(ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeleza miradi 3,682 kutoka katika vijiji 2,091, mitaa 331 na shehia 168, jumla yake ni 2,590 ambapo kaya za walengwa 288,385 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar.

(iii) Zoezi la uhakiki wa kaya masikini ambao ni endelevu limebainika kuwepo kwa kaya 7713 nchini zilikosa sifa kwa sababau mbalimbali hivyo zimeondolewa kwenye mpango. Sababu ya kuondolewa zipo kwenye ukurasa wa 29 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa kujitegemea, baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni kama zifuatazo;

(i) Mikopo 1,949 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 imetolewa kwa vijana waliohitimu mafunzo *VETA* na *SIDO.*

(ii) Walengwa 3,341 wa mfuko walipata mafunzo ya ujasiliamali na namna ya kujitambua na kuratibu na taratibu za mkopo wa mfuko.

(iii) Vituo vya huduma vimefunguliwa Kilolo (Iringa), Ruangwa (Lindi) na tawi la Dodoma limefunguliwa mwezi machi mwaka huu ambapo walengwa 86 wa mfuko walipata mafunzo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Fungu 32 linalojumuisha wakala

zilizo chini yake iliidhinishiwa jumla ya bilioni 33.6 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 26.6 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni saba kwa ajili ya uatkelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hadi kufikia Machi, 2018 shilingi bilioni 26.9 zilikuwa zimepokelewa na kutumika kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.9 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 20.9 matumizi mengineyo, shilingi bilioni tatu mishahara aidha, shilingi bilioni tatu ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora pamoja na Wakala zake ilitekeleza shughuli kama zilivyo kwa kina kwenye kitabu changu ukurasa wa 35 hadi 54. Baadhi yao kama ifuatavyo:-

(i) Menejimenti ya Utumishi wa Umma; uwezo wa taasisi za Serikali umejengewa katika maeneo ya kuandaa sera za kisekta zilizowianisha ili kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji, mafunzo kwa vitendo yamewezeshwa na timu ya Taifa ya wataalam wa sera.

(ii) Miundo na mgawanyo wa majukumu ya ofisi Wizara 22, Idara zinajitegemea 21, Wakala wa Serikali 19 na taasisi za mashirika ya umma 20 imehuishwa.

(iii) Utoaji vibali vya uhamisho 4,163 kushikizwa vinne kuazimwa 1,452 likizo bila malipo 206 kwa watumishi wameshughulikiwa. Aidha, mapendekezo ya nafasi ya uteuzi 289, vibali vya uteuzi 84 kwa utumishi viongozi wanapendekezwa na waajiri kuteuliwa mikataba ya ajira 45 imeshughulikiwa.

(iv) Usimamizi wa ajira za watumishi wa umma umefanyika kwa aajiri wote ambapo watumishi wapya 15,000 wameajiriwa wakiwemo waalimu 4,348 wa masomo ya sayansi; watumishi 3,152 kada ya afya hii ili kuziba pengo la waliobainika kughushi vyeti.

(v) Maafisa Utumishi na Maafisa Utawala wapatao 1,595 wamechukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufungiwa dhamana ya kuingia katika mfumo wa *Human Capital Management Information System* kufikishwa mahakamani na wengine kesi zao zinachunguzwa TAKUKURU.

(vi) Watumishi 30 wa idara mbili zilizokuwa zimesalia Dar es Salaam wamehamishiwa Makao Makuu Dodoma hatua hiyo imefanya huduma zote za Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwamba sasa zimehamia Dodoma kuanzia Aprili mwaka huu, tumehamia kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma, katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zimetekelezwa; mafunzo ya kujiandaa kufanya mtihani wa utumishi wa umma yalifanyika na watumishi 566 kati ya 810. Uongozi na maendeleo, menejimenti na usimamizi wa ofisi, watumishi wa umma 2,283 kati ya 2790. Vilevile yalitolewa mafunzo ya muda mrefu katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, *computer*, utunzaji wa fedha za umma na menejimenti na rasilimali watu; usimamizi wa manunuzi ya umma, uongozi na utawala bora kwa washiriki 10,760 kati ya 15,810.

Pia Chuo kimepatiwa eneo kubwa wa mita za mraba 3900 mjini Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na kumbi za mikutano na semina. Aidha, chuo kimepatiwa eneo la ukubwa hekari 26 eneo la Pande katika Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa ajili ya kujenga majengo ya chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala ya Mafunzo kwa Ajili ya Mtandao *(TaGLA);* shughuli zilizofanyika huduma ya muunganisho ya mtandao wa mafunzo kwa njia ya video, *(video conference)* imetolewa kwa washiriki 526 kutoka Wizara, mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali na Mikoa yote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti; Wakala wa Serikali Mtandao *(e-government);* Wakala imetekeleza shughuli zifuatazo; Serikali imeboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ikiwa ni pamoja na kuifanyia ukaguzi wa usalama na utendaji.

Mifumo hii ni pamoja na mfumo wa ukusanyaji wa mapato Serikalini, *Government e-payment Gate Way* ambapo hadi sasa taasisi 28 za umma zimeunganishwa na zinatumia kukusanya mapato ya Serikali. Pia mfumo wa kutolea tiketi za kielektroniki umeanza kutumika na Shirika la Meli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mfumo wa kutoa huduma za Serikali kupitia simu ya mkononi kwa kupiga simu namba *152*00# umeboreshwa. Kuanzia Julai, 2017 taasisi 42 za umma zimewezesha kutoa huduma kwa njia ya simu za mkononi. Aidha, taasisi zinazotumia mfumo hadi sasa zimefikia 118.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; taasisi mpya 15 za umma zimeunganishwa kwenye mfumo wa Ofisi Mtandao uliobuniwa na kutengenezwa na Wakala wa Serikali Mtandao. Hadi sasa taasisi za Serikali 31 zimejiunga na mfumo huo ulioandaliwa na wataalam wetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, taasisi mpya 32 zimeunganishwa katika mfumo wa mawasiliano wa Serikali kwa njia ya barua pepe *(Government Mailing System)* kuanzia Julai, 2017 na kuwezesha kuwa na mawasiliano salama kwa njia ya barua pepe kwa taasisi za Serikali. Taasisi 360 za Serikali zinatumia mfumo huu tangu ulipozinduliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, mwaka wa fedha 2017/2018 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa bilioni 8.6. Kati ya fedha hizo, bilioni 6.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018 shilingi bilioni 3.3 matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa miradi ya maendeleo shilingi milioni 336 ilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zilizotekelezwa kwa kirefu ni kama ilivyo kwa kina kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 55 hadi 58. Baadhi yao kwa kifupi ni kama zifuatazo:-

(i) Malalamiko 150 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya viongozi wa umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Uchunguzi wa awali umefanyika na malalamiko 119 yanayohusu ukiukwaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma.

(ii) Usambazaji wa fomu la tamko la Serikali na madeni viongozi wa umma kwa njia ya tovuti imeanza ambapo fomu hizo zilipatikana katika mtandao. Jumla ya viongozi wa umma 16,050 ambao ni sawa na asilimia 98 wamerejesha fomu za tamko la rasilimali na madeni kufikia Machi, 2018. Sekretarieti imeanza maandalizi ya mchakato wa ujazaji fomu kwa njia ya mtandao *(online application).*

(iii) Viongozi 2,000 walipangwa kuhakikiwa katika mwaka wa fedha 2017/2018. Awamu ya kwanza ya uhakiki wa viongozi 1,000 inatarajiwa kuanza mwezi Aprili. Aidha, zoezi la kuchambua nyaraka za uthibitisho wa tamko linalotolewa na viongozi wa umma limeanza kwa kuwataka viongozi husika kuwasilisha nyaraka hizo kwaajili ya maandalizi ya zoezi la uhakiki na ufuatiliaji wa mienendo ya kimaadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa umma iliidhinishiwa shilingi bilioni 3.1, shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi milioni 750 fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 shilingi milioni 897 zilikuwa zimepokelewa na kutumika, kati ya fedha hizo shilingi milioni 589 kwa ajili ya mishahara shilingi 307 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa umma ilitengeneza shughuli kama ilivyo kwa kina katika kitabu changu ukurasa 59 mpaka 61. Baadhi yake katika kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira, ofisi iliendesha usaili mara sita kwa niaba ya waajiri 261. Waombaji 2,223 walifaulu; pili, mfumo wa kielektroniki wa maombi ya kazi ulihuishwa ili uweze kuwasiliana na mifumo mengine; tatu,

ofisi za sekretarieti ya ajira tawi la Zanzibar imeimarishwa na baadhi ya usaili wa mchujo umeanza kufanyika Zanzibar, mathalani usajili wa mchujo wa *TRA* ulifanyika Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizo shilingi bilioni 2.4 zilikuwa za mishahara, shilingi bilioni 4.4 nyingine na matumizi mengineyo. Hadi Machi mwaka huu shilingi bilioni 4.1 za matumizi ya kawaida zilikuwa zimetolewa. Kati ya hizo zilikuwa milioni 391 za kulipa madeni ya miaka iliyopita, shilingi bilioni 3.7 zilikuwa za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, Tume ya Utumishi wa Umma imetekeleza majukumu yafuatayo; ukaguzi wa kawaida umefanyika katika taasisi mbalimbali; pili, vikao vitatu vya Tume vimefanyika na kutoa maamuzi kwa watumishi waliopeleka malalamiko yao.

Mheshimiwa Mweyekiti, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2017/2018 iliidhinishiwa shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida; kati ya fedha hizo shillingi milioni 709 mishahara, bilioni moja kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi walipokea shilingi milioni 978; kati ya hizo, shilling milioni 674 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi milioni 303 mshahara. Katika kipindi cha Julai, 77 hadi leo Bodi imetekeleza majukumu yake, nimeyaeleza kwa kirefu kutoka ukurasa wa 68 na 69.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, Kumbukumbu Nyaraka za Taifa imeidhinishiwa jumla bilioni 4.3, kati ya fedha hizo, bilioni 2.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, bilioni 2 miradi ya maendeleoo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 shilingi bilioni 1.3 zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi milioni 705 kwa ajili ya mishahara. Shilingi milioni 607 kwa ajili ya matumizi mengine na shilingi bilioni mbili kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Idara ya Kumbukumbu imetekeleza shughuli kama ilivyo kwenye kitabu changu cha hotuba ukurasa wa 67 hadi 71.

Moja, baadhi yake mfumo wa utunzaji kumbukumbu wa kiutendaji umeweka katika taasisi za umma;

Pili, hatua zinazolenga kuondoa mrundikano wa kumbukumbu wa kuboresha utunzaji wa taarifa muhimu za watumishi zimechukuliwa;

Tatu, Wizara 18 zimewezesha kuhamisha masijala kwenda Dodoma katika utekelezaji agizo la Serikali; na

Nne, mfumo wa kidigitali wa uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka umesimikwa katika Kituo cha Kumbukumbu cha Taifa Dodoma, Jengo la Kumbukumbu ya Nyaraka Makao Makuu nalo linaendelea kukarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Ushauri ya Mafuta na Gesi, katika mwaka wa fedha huo Bunge liliidhinisha shilingi milioni 711 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Shilingi bilioni 171 fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika katika mwaka wa kuanzia Julai, 2017/2018. Shughuli zilizotekelezwa zinapatikana ukurasa wa 71hadi 73.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2017/2018; baada ya kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti, sasa naomba kutoa mapendekezo ya mpango wa bajeti mwaka 18/19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Bajeti mwaka 2018/2019 kwa mafungu hayo niliyoyataja imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kama tulivyosema Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Mwongozo wa Taifa kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka pamoja na maeneo mengine ya kuzingatiwa kama ilivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Ikulu; katika mwaka 2018/2019 imepanga kutekeleza mambo tumeandika ukurasa wa 74 mpaka 88 wa kitabu changu. Kwa kifupi, wataendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake; wataendelea kutoa huduma ya ushauri, kumshauri Rais ili aweze kufanya maamuzi mbalimbali; wataendelea kuratibu utekelezaji mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa, tutaendelea kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Mikutano ya Baraza la Mawaziri; tutaendelea kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, MKURABITA na Mfuko wa Rais wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kukarabati nyumba 12 za watumishi Ikulu ndogo Dodoma, Chamwino na uboreshaji wa Ikulu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imepanga kufanya yafuatayo;

(i) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazopokelewa.

(ii) Wataendelea kuifanyia mapitio Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

(iii) Wataendelea na shughuli za ujenzo wa Ofisi za TAKUKURU katika Wilaya kumi ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uongozi imepanga kutekeleza yafuatayo; kutoa mafunzo ya stashahada za uzamili na uongozi; kuwajengea uwezo wataalam wa Serikali kuhusu majadiliano ya mikakati yenye thamani kubwa; kutoa mafunzo ya muda mfupi katika kozi 20 na kuwajengea uwezo viongozi katika uongozi wa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa MKURABITA; wataendelea kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora

ya hati za hatimiliki za kimila kwa wakulima mbalimbali; wataanzisha vituo vitano vya urasimishaji biashara; na wataanza urasimishaji wa wachimbaji wadogo wadogo wa madini katika maeneo Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* watafanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya vijiji 4,408, mitaa 1,189 na shehia 99; kuhaulisha ruzuku kwa kaya maskini 1,100,000 katika vipindi vya mizunguko sita vya malipo katika Halmashauri za Tanzania Bara na Zanzibar na watafanya uhakiki wa walengwa wanaostahili kuwemo katika Mpango na kuondoa wale ambao hawastahili kuendelea kuwepo.

Nne, kuendelea na maandalizi ya kipindi cha pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa miaka mitano kuanzia 2019/2020 mpaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea utaendelea kutoa mafunzo ya wajasiriamali kuitambua na kuratibu mikopo inayotolewa na mfuko kwa walengwa 6,000 na mafunzo ya uendeshaji wa miradi, pia kutoa mafunzo kwa wateja 3,000 ya kufanya miradi endelevu. Pia itaendelea kutoa mikopo kwa vijana waliohitimu mafunzo *VETA* na *SIDO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa fedha 2018/2019 Fungu 20, Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba shilingi 22,644,912,748 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Fungu la Rais Ofisi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba shilingi bilioni 576,213,769 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 401,158,280,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 175 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala zilizo chini yake; Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi kama tulivyoeleza kwenye kitabu ukurasa wa 89 mpaka 101. Kazi ya kuhuisha miundo ya maendeleo ya utumishi; kuanzisha

na kuhuisha miundo ya mgawanyo wa majukumu ya taasisi za Serikali; kufanya usanifu wa mfumo mpya wa *Human Capital Management Information System;* kuratibu uanzishwaji wa vituo vitatu vya awali vya huduma ya pamoja; kutoa vibali vya uhamisho na maombi ya vibali vya likizo bila malipo, kuazimwa na kushikizwa kwa watumishi; kusimamia ajira ya watumishi wa umma, kufanya ufuatiliaji utekelezaji wa masuala ya anuai jamii na kutumia *framework* maalum katika utumishi wa umma na kuhamasisha masuala ya anuai ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma kitaendelea kutoa mafunzo kujiandaa kufanya mitihani kama kazi walizozifanya mwaka jana wataendelea nazo; kutoa mafunzo ya muda mrefu washiriki 12,886 na kuendelea ujenzi wa ghorofa mbili litakalotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi *campus* ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mafunzo kwa njia ya mtandao watatoa mafunzo ya muunganisho wa mtandao kuwezesha utoaji wa huduma kwa washiriki 2,700; wataendelea kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kwa gharama nafuu kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Serikali Mtandao katika kipindi hicho wataendelea kushirikiana na taasisi za Serikali ili kujenga na kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato na maduhuli ya Serikali, kusimamia na kuboresha usalama wa mifumo ya TEHAMA, kusimamia, kuboresha, kupanua miundombinu shirikishi ya Serikali mtandao kwa taasisi zote za Serikali; kusimamia, kuboresha na kupanua matumizi ya mifumo, miundombinu shirikishi ya TEHAMA; na kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na kisekta kubadilishana taarifa na kuondoa urudufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ufanisi Fungu 32, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kiasi cha shilingi 41,403,499,261 kwa ajili ya matumizi

ya kawaida na miradi ya maendeleo; kati ya fedha hizo shilingi 30,464,699,261 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 10,939,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi itaendelea kupokea matamko ya viongozi wa umma kuhusu rasilimali na kuhakiki; itaendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya taarifa za ukiukwaji wa maadili na itaendelea na ujenzi wa Ofisi Makao Makuu ya Sekretarieti ya Maadili hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, mwaka wa fedha unaokuja Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili inaomba kuidhinishiwa shilingi 11,511,874,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya miradi ya maendeleo, kati za fedha hizo, shilingi 7,461,874,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 4,050,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira wataendelea kusimamia na kuendesha michakato ya ajira na kuimarisha mfumo wa maombi ya kazi na mrejesho. Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa shilingi 3,116,083,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi milioni 750 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma wataendelea kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za ukaguzi maalum na wataendelea kufanya mikutano ya kisheria ya Tume ili kutoa uamuzi, ukaguzi, rufaa, malalamiko na masuala mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu, Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa shilingi 4,403,479,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara katika Utumishi inaomba kutumia shilingi 1,652,435,000 kwa ajili ya matumizi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka maelezo yangu yako ukurasa 108 mpaka 110 na wataendelea kuweka, kuhuisha mifumo ya utunzaji; wataendelea kuweka mfumo wa kielektroniki; watakamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu Kanda ya Ziwa Mwanza; ukarabati wa jengo la Idara ya Makao Makuu Upanga, Dar es Salaam. Ili kutekeleza majukumu wanaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 8,148,504,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya bajeti ya mwaka 2018/2019 ya mafunzo yaliyotajwa yamezingatia vipaumbele na matakwa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025. Ofisi yangu itaendelea kujenga utumishi wa umma unaohudumia kwa ufanisi viwango vya ubora, stahiki, jamii…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba umalizie, muda wetu umekaribia kuisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo yangu yote yaliyomo katika hotuba yaingie katika *Hansard,* lakini kwa sababu hiki ni kikao cha kuomba kuidhinishiwa fedha naomba uniruhusu nisome kifungu ninachoombea fedha Wizara yangu na taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla kuu ya bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo; jumla kuu, Matumizi ya Kawaida shilingi 473,121,195,009; Matumizi ya miradi ya Maendeleo shilingi 195, 973, 361,000. Jumla kuu ya fedha ninazoomba Bunge liidhinishe kwa ajili ya Wizara yangu ni shilingi 669,094,556,009.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyatafakari, kuyajadili na kuyaidhinisha.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA *KAPT* (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/19 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Ushauri wa Mafuta na Gesi (Fungu 11), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09), na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uwezo wa kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; ninamuahidi kuwa nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Newala Mjini kwa ujumla kwa kuendelea kunipa ushirikiano ninapoendelea kuwawakilisha. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa dhati ya moyo wangu kwa ushirikiano wanaonipatia na kwa kuwa wavumilivu ninapotekeleza majukumu yangu.

3. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia mabadiliko ya Kamati za Kudumu za Bunge yaliyofanyika, naomba kumpongeza

Mwenyekiti na Makamu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kuendelea katika nafasi zao. Pia, nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa katika nafasi zao zenye dhamana ya kusimamia kamati katika kuishauri Serikali na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jasson Samson Rwekiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum Tabora kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/18 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Maoni na ushauri wa Kamati hiyo umetuwezesha na utaendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapa kazi na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma. Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Zanzibar, kwa uongozi wake shupavu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji, usimamiaji na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali na kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri na kazi nzuri wanayoifanya ya kuliongoza Bunge lako Tukufu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Nawapongeza pia Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kwa namna ya pekee, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Selemani Said Jafo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Ma-Naibu wake Mheshimiwa Josephat Kakunda (Mb) na Mheshimiwa Joseph Kandege (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

10. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa Mheshimiwa Dkt Damas Daniel Ndumbaro (Songea Mjini) Mheshimiwa Justin Joseph Monko (Singida Kaskazini), Mheshimiwa Stephen Lemomo Kiruswa (Longido), Mheshimiwa Alfredina Kahigi (Viti Maalum), Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye (Viti Maalum), Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili (Viti Maalum), Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim (Viti Maalum), Mheshimiwa Shamsa Aziz Mtamba (Viti Maalum), Mheshimiwa Sonia Jumaa Magongo (Viti Maalum) na Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir (Viti Maalum). Aidha, nawapongeza wabunge wenzetu walioshinda uchaguzi wa hivi karibuni, ambao ni Mheshimiwa Maulid Mtulia Mbunge wa Kinondoni na Mheshimiwa Dkt Godwin Mollel Mbunge wa Siha. Vile vile, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa Mheshimiwa Leonidas Gama (Songea Mjini),

tunaomba Mola aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina!

11. ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Balozi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Charles Mwankupili, Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bi. Dorothy Mwaluko, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati.

12. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kushukuru na kuwataja wachache ambao ni:- China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujerumani, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ireland, Israel, Kenya, Rwanda, Somalia, Afrika Kusini, Botswana, Msumbiji, Malawi, Mali, Ghana, Ethiopia, Jamhuri ya Watu wa Kongo, Nigeria, Sierra Leone, Liberia, Ivory Coast, Namibia, Niger, Togo, Zimbabwe, Trinidad na Tobago, na Ubelgiji. Vilevile, nashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, OFID-OPEC Fund for International Development, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), DfID, KOICA, GIZ, DFATD, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, NORAD, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

13. ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa. Uzalendo wao na imani yao kwa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano

umewezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi, kwa ufanisi na Ubora mkubwa.

14. ***Mheshimiwa Spika****,* naomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nyakati mbali mbali kuhusu kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya  Serikali na Utumishi wa Umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia Sheria, Kanuni Miongozo na Taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma. Vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ufisadi, uzembe, uvivu, ukiukwaji wa maadili na utumishi hewa na wasio na sifa stahiki kwa kuwawajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazoendelea kuchukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa Watumishi wa Umma wote kufanya kazi kwa weledi, juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Tunaendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora, kwa haraka na kwa staha ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

15. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo ajali na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Pia, nawakumbuka Askari wetu wa kulinda amani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo waliofariki wakiliwakilisha Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

16. ***Mheshimiwa Spika****,* hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 pamoja na

Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA 2017/18

17. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa 2017/18 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. Shughuli zilizotekelezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

### *OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE*

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu ilidhinishiwa **Shilingi 16,267,586,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2018 **Shilingi 12,927,942,594** zilipokelewa na kutumika.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) inayojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa **Shilingi 747,885,035,000** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 368,314,145,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 379,570,890,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 **Shilingi 574,402,064,096** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 335,587,953,722** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 238,814,110,374** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo kwa kila Taasisi:-

### (a) Ikulu

20. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Huduma zilitolewa kwa Rais na familia yake. Aidha, ushauri ulitolewa kwa Mhe. Rais kuhusu ratiba ya kila siku, masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia na ushauri mwingine wowote wenye lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Shughuli za Baraza la Mawaziri zilifanyika ambapo:- Mikutano 38 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 61 zilichambuliwa. Mikutano 15 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 39 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 15 ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 40 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Mikutano minne (4) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 30 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi. Aidha, mikutano nane (8) ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 14 ilijadiliwa;

(iii) Hotuba 27 za Mheshimiwa Rais zilichapishwa na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Vipindi Maalum vya Televisheni 12 kuhusu shughuli za Mheshimiwa Rais na Serikali yake vilitengenezwa na kurushwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari;

(iv) Taarifa kwa Vyombo vya Habari (Press Releases) 318 zikiambatana na picha zilichapishwa na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na mitandao ya kijamii;

(v) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu (2017 – 2022) umeanza kutekelezwa ambapo:- Nakala 80,000 za vitabu vya Mkakati vilisambazwa kwa wadau mbalimbali. Vile vile, Elimu kwa Wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu imetolewa kwa Mikoa 16, Wizara zote na Taasisi za Umma 51;

(vi) Rufaa 85 za Watumishi wa Umma na Mamlaka za Nidhamu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa uamuzi ambapo kati ya hizo, Rufaa 45 zilitolewa uamuzi na wahusika kujulishwa. Aidha, malalamiko 475 ya Watumishi wa Umma

na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo; na

(vii) Mikutano minne (4) ya uratibu na uendeshaji wa maboresho ilifanyika kujadili mafanikio, changamoto na mipango ya baadae ya maboresho.

### (b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni pamoja na kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya rushwa. Kutokana na jitihada za TAKUKURU na wadau wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini, tatizo la Rushwa limepungua kiasi katika nchi yetu katika upimaji wa hali ya rushwa uliofanywa na Mashirika ya Kimataifa ambao umeonesha Tanzania kufanya vizuri miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki ikishika nafasi ya pili baada ya Rwanda. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Uchunguzi wa majalada 325 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuombewa kibali. Majalada 214 kati ya 325 yaliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, majalada mengine yanaendelea kufanyiwa kazi;

(ii) Kesi 727 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 201. Katika kipindi hiki, kesi 219 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 81 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 138 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Aidha, kesi 14 ziliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali. Kesi 494 zinaendelea mahakamani;

(iii) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa katika maeneo ya kodi na ukusanyaji mapato na manunuzi ulifanyika. Kazi hizo ni uzingatiaji wa matumizi ya Mashine za Kielekroniki katika ukusanyaji wa kodi na uchambuzi wa mianya ya rushwa katika utaratibu wa ukasimishaji wa mapato kwa kutumia mawakala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na tathmini ya hali ya rushwa katika utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ngazi ya Serikali za Mitaa kwenye Sekta ya Elimu na Afya;

(iv) Kazi 329 za uchambuzi wa mifumo na Warsha/vikao 179 vya wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa vilifanyika katika Sekta 24; Aidha, kazi 73 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na mapendekezo ya uchambuzi wa mifumo zilifanyika;

(v) Miradi ya maendeleo 195 yenye thamani ya Shilingi bilioni 154.1 ilifuatiliwa katika Sekta za Elimu, Afya, Maji na Ujenzi. Lengo la ufuatiliaji huu lilikuwa ni kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kama zilivyokusudiwa na thamani ya fedha inapatikana. Katika ufuatiliaji huu miradi 73 yenye thamani ya Shilingi bilioni 30.9 ilibainika kuwa na mapungufu katika utekelezaji wake. Uchunguzi umeanzishwa kwenye miradi 31 yenye thamani ya Shilingi bilioni 10. Aidha, Miradi 42 ilifanyiwa marekebisho ya kasoro zilizokuwepo na hivyo kiasi cha Shilingi milioni 40 zilizokuwa zilipwe kwa wakandarasi zilitumika kurekebisha miradi hiyo ili iwe na ubora uliokusudiwa. Pia TAKUKURU ilipendekeza wasimamizi wa miradi 13 wachukuliwe hatua za kinidhamu na mamlaka kutokana na kasoro zilizobainika katika miradi waliyoisimamia. Vile vile, Shilingi bilioni 58.4 ziliokolewa kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU na kurejeshwa Serikalini kutokana na kudhibiti rushwa katika eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali, uzuiaji wa malipo hewa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

(vi) Elimu kuhusu athari za rushwa na juhudi za Serikali za kuidhibiti ili kupata uungwaji mkono ilitolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina 2,613, mikutano ya hadhara/

mijadala ya wazi 1,323, vipindi vya redio na televisheni 144, maonesho 128 na taarifa kwa umma 32 zilitolewa kupitia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 205 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na nakala za machapisho 16,000 zilisambazwa. Katika uelimishaji huo wananchi 611,335 walifikiwa ana kwa ana bila kuhusisha waliofikiwa kwa njia ya redio, runinga na machapisho. Vile vile, Elimu kwa umma imeendelea kutolewa kwa njia mbali mbali kwa kushirikiana na wadau kupitia matangazo kwenye vyombo vya usafiri na kwenye madaftari ya wanafunzi yaliyokuwa na ujumbe wa kupambana na rushwa na kupitia vyombo vya habari matangazo matano (5) yanayokemea vitendo vya rushwa nchini yalitolewa;

(vii) Vijana walijengewa uwezo wa kimaadili ili kushiriki kuzuia na kupambana na rushwa. Vile vile, vijana walio shuleni, vyuoni na ambao hawapo shuleni walipatiwa elimu kuhusu rushwa na kuwasisitiza kujiunga na klabu za wapinga rushwa. Klabu mpya za wapinga rushwa 603 zilifunguliwa na 1,363 ziliimarishwa;

(viii) TAKUKURU imeendelea kutoa Huduma ya kupokea malalamiko na taarifa kutoka kwa wananchi kwa saa ishirini na nne (call centre) ambapo Wananchi wameweza kuifikia TAKUKURU kwa kupiga simu namba 113, kutuma ujumbe kwenda namba hiyo au kutoa taarifa kwa kupiga *113# yaani mfumo wa USSD *(Unstructured Supplementary Service Data).* Katika kipindi husika, malalamiko 119,285 yamepokelewa ambapo malalamiko 25,201 yalikuwa kwa njia ya simu, 87,681 kupitia ujumbe mfupi wa simu na 6,403 kupitia USSD;

(ix) Watumishi 252 walipatiwa mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu kwa ufanisi; na

(x) Maandalizi yamefanyika ya kuanza ujenzi wa Ofisi za TAKUKURU katika Wilaya saba, matarajio ni kujenga katika Wilaya za Chamwino, Ruangwa, Manyoni, Namtumbo, Ngorongoro, Masasi na Mpwapwa.

## (c) Taasisi ya UONGOZI

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi (Post Graduate-Diploma in Leadership) iliyozinduliwa rasmi tarehe 21 Aprili, 2017 yameendelea kutolewa. Stashahada hii inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine na kujenga sifa binafsi za kiongozi. Programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichoko Helsinki, Finland. Hadi kufikia Machi, 2018 moduli nane (8) zimetolewa. Awamu ya kwanza imehusisha Maafisa Waandamizi 30 wa Jeshi la Polisi ambao wamehitimu tarehe 21 Machi, 2018. Aidha, awamu ya pili ya mafunzo haya ambayo inahusisha Maafisa Waandamizi 30 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma mbalimbali imeanza;

(ii) Kozi nane (8) za muda mfupi zimetolewa kwa Viongozi 238 wa Umma ili kuimarisha utendaji kazi. Kozi hizi zimetolewa katika maeneo ya Uongozi wa kimkakati; Utawala; Mitazamo na Dira; Majadiliano ya Mikataba yenye thamani kubwa; Kiongozi Muadilifu na Uongozi Binafsi na Wenye Maadili;

(iii) Programu ya Kuwajengea uwezo Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa iliandaliwa na kutekelezwa. Programu hii ililenga kuwajengea uwezo katika masuala ya Maadili, Utawala Bora na Uwajibikaji; Mawasiliano Fanisi; Utendaji wenye Matokeo; Uongozi wa Kimkakati; Usimamizi wa Vihatarishi na Udhibiti

wa Ndani; Mahusiano kati ya Viongozi wa Kisiasa na Watendaji. Programu hii ilitolewa kwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya wote;

(iv) Kwa kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi, makongamano matano (5) ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa yalifanyika kwa lengo la kukutanisha viongozi ili kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Viongozi 826 walishiriki kutoka Tanzania na nchi za Kenya, Rwanda, Somalia, Afrika Kusini, Botswana, Msumbiji, Malawi, Mali, Ghana, Ethiopia, Jamhuri ya Watu wa Kongo, Nigeria, Sierra Leone, Liberia, Ivory Coast, Namibia, Niger, Togo, Zimbabwe, Trinidad na Tobago, Amerika, Uingereza, Ujerumani, Ubelgiji, Sweden, Canada na Australia. Mikutano ifuatayo ilifanyika:-

(a) Kongamano la Kikanda la Viongozi wa Afrika kuhusu "Amani na Usalama kwa Afrika Jumuishi na Endelevu" lilifanyika tarehe 24-25 Agosti, 2017. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mstaafu Benjamin Mkapa na Ofisi ya Rais Mstaafu Thabo Mbeki wa Afrika ya Kusini. Kongamano hili lilihudhuriwa na Viongozi 200 wakiwemo Marais Wastaafu kutoka Tanzania, Malawi, Nigeria, Tunisia, Afrika ya Kusini na Namibia; Wakuu wa Taasisi za Kikanda za SADC, EAC, UNECA, na AfDB; wafanyabiashara, Wakuu wa Taasisi za Kiraia, na wasomi kutoka nchi 22;

(b) Kongamano la Kimataifa kuhusu "Masuala ya Jinsia kutoka kwenye Nadharia kuelekea kwenye Vitendo" lilifanyika tarehe 2 - 4 Novemba, 2017 na kuhudhuriwa na viongozi, watunga sera, watendaji na watafiti 180 kutoka ndani na nje ya Bara la Afrika. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF);

(c) Mkutano wa Kitaifa kuhusu "Namna ya Kujenga Uchumi Endelevu kwa Kutumia Rasilimali kwa Ufanisi" uliandaliwa tarehe 29 Septemba, 2017 kwa kushirikiana na Chatham House ya Uingereza. Viongozi 28 walihudhuria mkutano huu;

(d) Kongamano la Kitaifa kuhusu "Maboresho katika Sekta ya Umma na Ugatuaji wa Madaraka" lilifanyika tarehe 24 - 25 Oktoba, 2017, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Viongozi 118 kutoka Wizara, Idara za Serikali na Taasisi za Umma walihudhuria; na

(e) Mdahalo wa Kitaifa kuhusu "Harakati za Kujikomboa Kiuchumi kwa Bara la Afrika" lilifanyika tarehe 21 Disemba, 2017 kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wanataaluma, viongozi na wanachuo takriban 300 walihudhuria mdahalo huo.

(v) Vipindi saba (7) vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi na mitandao ya kijamii kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu. Vipindi hivi vinaoneshwa na kuonekana Bara zima la Afrika;

(vi) Utafiti unaohusu "Mikakati na Sera za Kukuza Uchumi wa Viwanda vya Kijani" umekamilika. Aidha, utafiti kuhusu "Viwezeshi na Vikwazo vya Uongozi Barani Afrika" uliofanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza umekamilika. Utafiti huu ulihusisha nchi tano (5) ambazo ni Tanzania, Uganda, Afrika ya Kusini, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokarasi ya Kongo. Utafiti mwingine kwenye maeneo manne unaohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu unaendelea kufanyika;

(vii) Machapisho kuhusu Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mhe. Benjamin Mkapa liko katika hatua za mwisho, na linalohusu maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Ali Hassan Mwinyi linaendelea kuandaliwa. Lengo kuu ni kutoa machapisho (memoirs) kuhusu maisha binafsi na michango ya Marais wastaafu;

(viii) Uratibu wa uwezeshaji wa vikao kazi vya usanifu wa Awamu ya Tatu ya Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma inayotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018 unaendelea;

(ix) Programu Jumuishi ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa hususan katika Sekta ya Uziduaji (Mafuta, Gesi Asili na Madini) ilitekelezwa kama ifuatavyo:

(a) Mafunzo kwa ajili ya kuijengea uwezo Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi na Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi Bagamoyo (Special Economic Zone) yalitolewa. Mafunzo hayo yalifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Columbia, Marekani;

(b) Mikutano miwili iliyokutanisha viongozi 148 kutoka Tanzania na nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika ilifanyika. Mikutano hiyo ilihusu “Jinsi ya Kuongeza Thamani katika Sekta ya Uziduaji” na “Usimamizi wa Mazingira katika Sekta ya Uziduaji Tanzania;

(c) Taasisi imekamilisha utafiti kwenye maeneo matatu ambayo ni “Uwiano Bora katika Uwekezaji na Utumiaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Mafuta na Gesi Asili”; “Utayari wa Tanzania wa kuwa na Uchumi wa Mafuta” na “Mtazamo wa Kimataifa kuhusu

Gesi Asilia na Athari zake katika Uanzishwaji wa Miradi ya Gesi Asilia Nchini";

(d) Uratibu na uwezeshaji wa shughuli za Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi unaendelea kufanyika. Timu hiyo kwa sasa inaendelea na majadiliano na Makampuni ya Mafuta ya Kimataifa;

(e) Uratibu na uwezeshaji wa Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi Bagamoyo (Special Economic Zone) umefanyika. Timu hiyo imeanza majadiliano na Makampuni yanayoshiriki kwenye mradi huu.

**(d) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Wakulima 589 na viongozi 89 wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi zingine za Fedha katika Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Mpwapwa na Serengeti. Aidha, mafunzo yaliyotolewa yamewezesha uanzishwaji wa SACCOS nne (4), Vikundi 56 vya uzalishaji na Wakulima 140 kufungua akaunti katika benki;

(ii) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Kituo Kimoja cha Urasimishaji wa Biashara *(One Stop Formalization Centre)* kimeanzishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ambapo huduma

muhimu za utoaji leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN), usajili wa jina la biashara (BRELA), huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinapatikana sehemu moja. Aidha, wafanyabiashara 870 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Hadi kufikia Machi, 2018 Kituo kimesajili biashara 380 ambapo Shilingi milioni 4.5 zimekusanywa kutokana na ada za leseni. Vile vile wafanyabiashara 79 wamepata leseni na 200 wamefungua akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kujiongezea mitaji;

(iii) Wafanyabiashara 100 katika Wilaya za Kusini Unguja (50) na Micheweni, Pemba (50) wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara ambapo wafanyabiashara 10 wamesajili Majina ya Biashara na kupata Leseni za kuendesha Biashara. Aidha, MKURABITA iliwezesha Wafanyabiashara 13 waliorasimisha biashara zao Unguja na Pemba kushiriki kwenye Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Nchini Burundi mwezi Desemba, 2017;

(iv) Kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar, MKURABITA imeanza kufanya utafiti kuhusu Sekta isiyo Rasmi nchini kwa lengo la kubaini ukubwa na thamani ya Sekta isiyo Rasmi kwa sasa. Aidha, utafiti wa Majaribio umefanyika katika Mikoa sita (6) ya Tanzania Bara na miwili (2) Zanzibar. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Tanga, Mjini Magharibi na Kusini Pemba. Utafiti huu wa majaribio ulilenga kuona kama methodolojia, sampuli na madodoso yaliyoandaliwa yanaweza kuleta matokeo tarajiwa juu ya ukubwa wa Sekta isiyo Rasmi kwa sasa. Aidha, vikao vya wadau vimefanyika Tanzania Bara na Zanzibar ili kupata maoni ya wadau juu ya dhana ya utafiti, methodolojia na madodoso. Utafiti mkubwa utaendelea kufanyika nchi nzima katika Mikoa yote

26 ya Tanzania Bara na Mikoa mitano (5) ya Zanzibar kuanzia mwezi Machi hadi Juni, 2018. Matokeo ya utafiti huu yatatolewa katika ngazi ya taifa na mkoa;

(v) Mkakati wa Mawasiliano umepitiwa kwa kushirikiana na wataalam kutoka Wizara za Kisekta ili kuongeza ufanisi katika kufanya mawasiliano kwa Umma. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Chuo cha Utumishi wa Umma, Tume ya Mipango Zanzibar, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na

(vi) Vipindi 12 vya radio na runinga vimeandaliwa kuhusu MKURABITA na uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia urasimishaji rasilimali ardhi na biashara ambapo vipindi nane (8) vimerushwa kupitia kituo cha televisheni cha TBC1 na radio za TBC Taifa pamoja na *Radio Free Africa (RFA).* Urushaji wa vipindi vinne (4) vilivyobaki unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2018.

## (e) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

25.***Mheshimiwa Spika*****,** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji. Kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 ni kama ifuatavyo:

(i) Kaya maskini 1,363,448 zimetambuliwa tangu kuanza kwa Mpango. Aidha, baada ya uhakiki, kaya maskini 1,118,751 zenye watu milioni 5 ziliandikishwa. Kati ya kaya/watu wote waliomo katika Mpango, asilimia 54 ni wanawake. Mpango huu unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, Shilingi bilioni 185.1 zilihawilishwa kama ruzuku kwa kaya maskini zilizoandikishwa Tanzania Bara na Zanzibar. Hatua mbalimbali za kinidhamu

zilichukuliwa na Mamlaka husika dhidi ya watumishi waliobainika kuhusika na uandikishaji wa walengwa waliokosa sifa. Hatua hizo ni pamoja na kusimamishwa kazi, kupewa onyo kali na wengine kuachishwa kazi. Kwa wananchi ambao walithibitika kutokuwa maskini, waliondolewa kwenye mpango;

(ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeleza miradi 3,682 kutoka katika Vijiji 2,091, Mitaa 331 na Shehia 168, jumla yake ni 2,590 ambapo kaya za walengwa 288,385 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi bilioni 31.4. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji, na hifadhi ya mazingira. Aidha, watoa huduma 2,820 wa ngazi ya jamii wamefundishwa namna ya kusimamia miradi ya kutoa ajira za muda katika Maeneo 19 ya Utekelezaji;

(iii) Zoezi la uhakiki wa Kaya Maskini ambalo ni endelevu limebaini kuwepo kwa kaya 7,713 nchini zilizokosa sifa kwa sababu mbali mbali. Hadi kufikia Machi, 2018 kaya hizo ziliondolewa kwenye Mpango. Mgawanyo wa kaya na sababu za kuondolewa ni kama ifuatavyo:-

(a) Kaya zilizokuwa na mwanakaya mmoja ambaye alifariki au wote wamefariki ni 4,404;

(b) Kaya zilizohamia Vijiji/Mitaa/Shehia ambapo Mpango haujaanza kutekelezwa ni 1,263;

(c) Kaya ambazo hazikujitokeza mara mbili mfululizo kupokea ruzuku ni 449;

(d) Kaya ambazo wananchi walithibitisha kuwa siyo maskini ni 1,219; na

(e) Kaya ambazo baadhi ya wanakaya ni Wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Jamii, Halmashauri za Vijiji/ Kamati za Mitaa, Viongozi na Watendaji ni 378.

(iv) Miradi 163 ya miundombinu ya elimu, afya na maji yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.72 inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri 13 za Mikoa ya Arusha na Njombe inayofadhiliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Mataifa Yanayozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC). Aidha, wawezeshaji wa ngazi ya Halmashauri na wajumbe wa kamati za usimamizi za jamii walipewa mafunzo kuhusu taratibu za utekelezaji na usimamizi wa miradi katika maeneo yao;

(v) Miongozo ya utekelezaji wa shughuli za kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya ilikamilika na kuanza kutumika katika utekelezaji. Miongozo hiyo ilitumika kutoa mafunzo ya stadi za ujasiriamali na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa yametolewa kwa wawezeshaji 600 kutoka katika maeneo ya utekelezaji 20 ambako Mpango huu umeanza. Vikundi 5,399 vya kuweka akiba na kuwekeza vyenye wanachama 114,728 viliundwa na Shilingi bilioni 1.07 zimetumika;

(vi) Mfumo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Utambuzi, Uandikishaji, Malipo na Malalamiko ya Walengwa umekamilika na umeanza kutumika katika Maeneo ya Utekelezaji 42. Utaratibu wa kuongeza wigo wa huduma hii kwa maeneo yaliyobaki umekamilika na upo tayari kwa utekelezaji. Mifumo ya TASAF imeunganishwa na mifumo mingine ya kitaifa kama vile NIDA na Malipo Mtandao (Government e-Payment Gateway). Aidha, Kituo cha huduma kwa wateja kimeanzishwa TASAF Makao Makuu;

(vii) Programu 88 za radio na 26 za televisheni kuhusu shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini zimeendelea kutolewa kwa umma kupitia Kituo cha radio cha TBC Taifa na Televisheni ya TBC1;

(viii) Katika kujenga uwezo wa wadau muhimu katika kutekeleza Mpango kwa ufanisi, mafunzo yalitolewa kwa waajiriwa wapya 32 na maofisa ufuatiliaji 129. Aidha, washiriki 472 walipatiwa mafunzo ya malipo ya kielektroniki. Kati yao 442 ni kutoka kwenye Halmashauri 16 zilizochaguliwa kuanza utekelezaji wa malipo kielektroniki na 30 ni kutoka TASAF Makao Makuu;

(ix) Utafiti kwenye maeneo mbalimbali wenye lengo la kupima ufanisi wa utekelezaji wa Mpango na matokeo yake umefanyika. Utafiti huu ulifanywa kwa pamoja na Ofisi ya Takwimu ya Taifa kwa Tanzania Bara na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar. Utafiti huo ulihusu Tathmini ya Mpango; tathmini ya Mpango kwa maendeleo ya vijana; na tathmini kuhusu ushiriki na uwezeshwaji wa wanawake. Utafiti huu ambao ni wa msingi umekamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili. Matokeo ya utafiti kwa Awamu ya pili yatakamilika Mwezi Machi, 2018; na

(x) Ukaguzi wa ndani ulifanyika ili kuhakikisha kama fedha zilitumika ipasavyo katika utekelezaji wa Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu. Ukaguzi ulifanyika TASAF Makao Makuu pamoja na Maeneo yote 161 ya Utekelezaji. Aidha, Wakaguzi wa nje kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) walifanya ukaguzi wa uhawilishaji fedha kwa walengwa, manunuzi, uendeshaji na thamani ya fedha. Matokeo ya ukaguzi huo yalikuwa mazuri na kuwezesha kupata HATI SAFI

## (f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea yameendelea kutekelezwa kupitia huduma ya utoaji wa mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Aidha, Huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara yameendelea kutekelezwa. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo 1,949 yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.6 imetolewa kwa vijana waliohitimu mafunzo katika Vyuo vya Ufundi Stadi vinavyotambuliwa na VETA na SIDO na wanawake wajasiriamali katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Njombe na Lindi;

(ii) Walengwa 3,441 wa Mfuko walipata mafunzo ya ujasiriamali wa namna ya kujitambua na taratibu za mikopo ya Mfuko;

(iii) Vituo vya huduma (Satellites) vimefunguliwa Kilolo (Iringa) na Ruangwa (Lindi);

(iv) Tawi la Dodoma limefunguliwa mwezi Machi, 2018 ambapo walengwa 86 wa Mfuko walipata mafunzo ya awali;

(v) Utafiti kuhusu huduma za mikopo kwa walengwa kwenye Mikoa ya Dodoma na Iringa ulifanyika na kubaini utayari na uhitaji wa huduma za mikopo ni mkubwa na hivyo ni fursa nzuri kwa Mfuko; na

(vi) Maofisa mikopo 17 walipata mafunzo ya utoaji huduma na sera za mikopo.

## OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZAKE

27. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32) linalojumuisha Wakala zilizo chini yake liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 33,695,038,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,695,038,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 **Shilingi 26,956,443,042.64** zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizi **Shilingi 23,956,443,042.64** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; **Shilingi 20,923,718,820.82** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 3,032,724,221.82** ni Mishahara. Aidha, **Shilingi 3,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

28. ***Mheshimiwa Spika****,* Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi, pale wanapotoa huduma mbalimbali kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

29. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

### (a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(i) Uwezo wa Taasisi za Serikali umejengwa katika maeneo ya kuandaa sera za kisekta zilizowianishwa ili kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji. Mafunzo kwa vitendo yamewezeshwa na Timu ya Taifa ya Wataalam wa Sera kwa Wizara zilizokuwa na mahitaji ya kuhuisha sera za sekta inazozisimamia;

(ii) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Ofisi/Wizara 22, Idara Zinazojitegemea 21, Wakala za Serikali 19 na Taasisi na Mashirika ya Umma 20 imehuishwa. Miundo iliyohuishwa iliwasilishwa kwenye vikao vya Kamati ya Rais ya Utekelezaji (PIC) kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa ushauri kabla ya kuidhinishwa ili iweze kutekelezwa;

(iii) Tathmini imefanyika kubaini hali halisi ya utekelezaji wa shughuli za Serikali za ufuatiliaji na tathmini kwa wizara 11 na Idara zinazojitegemea 15;

(iv) Utaalamu wa uchambuzi kazi katika uhuishaji wa Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Taasisi 7 za Serikali umetolewa. Taasisi zilizowezeshwa ni Mamlaka ya Elimu na Mafunzo Stadi (VETA), Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Wakala ya Vipimo

(WMA), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Afya) na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Aidha, Ofisi imewezesha taasisi 2 za Serikali (Wakala ya Mbegu za Miti – TTSA na Chuo cha Uongozi) kuhuisha Mikataba ya Huduma kwa Mteja (Client Service Charter);

(v) Uwezo wa namna ya kuimarisha na kuboresha mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini umejengwa kwa Taasisi 18. Vile vile, matumizi ya matokeo ya tathmini na ufuatiliaji kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea imefanyika;

(vi) Mapitio ya Miongozo ya viwango vya utendaji kazi kwa Taasisi za Serikali yamefanyika. Miongozo hiyo inajumuisha: Mwongozo wa Uandishi wa Nyaraka mbalimbali za Kiserikali; Mwongozo wa Kitambulisho cha Mtumishi wa Umma na Mwongozo wa Viwango vya Karatasi Maalum za Barua zenye Anuani (Letterheads) za Taasisi za Umma;

(vii) Uandaaji wa nyaraka za kuanzishwa na kuzinduliwa Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) iliyopo chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI umewezeshwa; Vile vile, nyaraka za kuanzishwa kwa Wakala ya Mpiga Chapa wa Serikali (TGPA) imewezeshwa na kuwasilishwa kwenye Mamlaka stahili kwa ajili ya kuidhinishwa;

(viii) Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umefanyiwa mapitio na kubaini matatizo mbalimbali yanayosababisha mfumo huo kutofanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Vile vile, changamoto za kiteknolojia na za mahitaji ya wadau zilizopo kwenye mfumo huo kwa sasa zilitatuliwa;

(ix) Tathmini ya wataalamu wa TEHAMA Serikalini imefanyika kwa watumishi 139 wa Wizara zote wa

fani ya TEHAMA ikiwa ni awamu ya kwanza. Lengo la tathmini hiyo ni kubaini idadi na sifa za wataalamu wa TEHAMA waliopo Serikalini na kuweka mipango madhubuti ya kusimamia na kuendeleza rasilimali hiyo ili iweze kuwa na ujuzi na weledi unaotakiwa katika kubuni, kujenga, kuendesha na kusimamia mifumo na mitandao ya Serikali Mtandao;

(x) Mwongozo wa kusimamia Utekelezaji wa Serikali Mtandao wa mwaka 2018 umetolewa na nakala 200 zimesambazwa kwenye Taasisi za Serikali. Lengo la Mwongozo huu ni kutoa utaratibu na viwango vya kuzingatiwa katika kubuni, kutengeneza na kuendesha mifumo, mitandao na miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi za Serikali ili kuondoa urudufu, kuwezesha ubadilishaji wa taarifa na kuhakikisha usalama wa data na taarifa za Serikali;

(xi) Uratibu wa Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano (RCIP) iliyokuwa inafadhiliwa na Benki ya Dunia kwenye eneo la Serikali Mtandao ambapo Programu hiyo ilikamilika rasmi mwezi Desemba, 2017. Mifumo sita ya Serikali Mtandao ilitekelezwa kupitia Programu hiyo ambayo ni mifumo ya Usajili wa Vizazi na Vifo; Matibabu Mtandao; Ofisi Mtandao; Nyaraka Mtandao; Ununuzi Mtandao; na Usajili wa Biashara kwa Mtandao. Pia Mtandao wa Mawasiliano unaounganisha Taasisi 72 za Serikali Kuu na Taasisi 77 za Serikali za Mitaa ulitekelezwa kupitia Programu hiyo. Aidha, mafunzo yaliyohusu maeneo mbalimbali ya ufundi na utumiaji wa mifumo na mitandao ya TEHAMA yalitolewa kwa watumishi 2,067 wa kada mbalimbali kutoka taasisi mbalimbali za Serikali;

(xii) Maandalizi ya Programu mpya ya “Digital Tanzania” kwenye eneo la Serikali Mtandao yameratibiwa. Programu hiyo ambayo itafadhiliwa na Benki ya Dunia ina lengo la kuongeza matumizi ya TEHAMA na Serikali Mtandao kama chachu ya kuharakisha utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Taifa katika kuongeza

ajira, kuwezesha uchumi wa viwanda na maendeleo ya jamii, na kufikia malengo ya Dira ya Taifa, 2015;

(xiii) Utoaji wa vibali vya uhamisho 4,163, kushikizwa 4, kuazimwa 1,452, likizo bila malipo 206 kwa watumishi umeshughulikiwa. Aidha, mapendekezo ya nafasi za uteuzi 289, vibali vya uteuzi 84 kwa watumishi viongozi na wanaopendekezwa na waajiri kuteuliwa, mikataba ya ajira 45 imeshughulikiwa.

Vile vile, hoja mbalimbali 496 kuhusu uteuzi, mikataba ya ajira, uhamisho, likizo bila malipo na mishahara binafsi zimejibiwa;

(xiv) Malalamiko yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma yapatayo 1,696 yamepokelewa, kati ya hayo malalamiko 1,343 ambayo ni sawa na asilimia 79 yameshughulikiwa. Malalamiko yaliyowasilishwa yanahusiana na masuala ya upandishaji vyeo, ajira, mafao ya hitimisho la kazi, nidhamu, fidia ya kuumia au kufariki kazini na unyanyasaji. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuelimisha na kuzikumbusha Mamlaka za Ajira na Nidhamu jukumu la kushughulikia masuala ya watumishi kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu;

(xv) Tathmini ya Mikataba ya Utendaji Kazi imefanyika katika Taasisi za Umma nane (8) na kubaini changamoto za utekelezaji Mikataba na kutoa ushauri kwa Taasisi husika ambazo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM); Tume ya Utumishi wa Umma (PSC); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (PSRS); Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA); Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (PSRB); Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (RAMD); Chuo cha

Utumishi wa Umma (TPSC); na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA);

(xvi) Taasisi za Umma sita zimejengewa uwezo kuhusu Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS). Taasisi hizo ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha; Mamlaka ya Taifa ya Hifadhi ya Ngorongoro; Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula; Chuo cha Utumishi wa Umma; Mamlaka ya Elimu Tanzania; na Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT-PID);

(xvii) Ufuatiliaji wa matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) katika Idara za Afya na Elimu umefanyika katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ambapo hadi kufikia Februari 2018 jumla ya watumishi **107** wamepatiwa mafunzo hayo;

(xviii) Uhakiki wa mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma ikiwemo mikoa yote umefanyika kupitia Mfumo wa "HCMIS" na kuweza kubaini mahitaji ya watumishi 52,436 wa kada mbalimbali. Aidha, Serikali imeanza mchakato wa kuajiri watumishi hao kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele na kuimarisha kada zenye upungufu mkubwa kama vile afya (14,102), Elimu (16,516), Kilimo (1,487), Mifugo (1,171), Uvuvi (320), Polisi (2,566), Magereza (750), Uhamiaji (1,500), Zimamoto (1,177), hospitali za mashirika ya kidini na hiari (174) na wengineo (12,673);

(xix) Usimamizi wa ajira za Watumishi wa Umma umefanyika kwa Waajiri wote ambapo watumishi wapya 15,000 wamejiriwa, wakiwemo na jumla ya walimu 4,348 wa masomo ya sayansi na watumishi 3,152 wa kada ya Afya, ili kuziba pengo lililosababishwa na kuondolewa kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara kwa watumishi wa umma waliobainika kughushi vyeti;

(xx) Maofisa Utumishi na Maofisa Tawala wapatao **1,595** wamechukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufungiwa dhamana ya kuingia katika Mfumo wa "HCMIS", kufikishwa mahakamani na wengine kesi zao zipo TAKUKURU;

(xxi) Mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa "HCMIS" yametolewa kwa Maofisa Rasilimaliwatu **55** kutoka kwa waajiri mbalimbali ili kuwapatia ujuzi stahiki;

(xxii) Fursa za mafunzo kupitia wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa umma zimetolewa. Fursa hizo zimewezesha watumishi 970 (wanawake 249 na wanaume 721) kuhudhuria mafunzo mbalimbali yakiwemo ya muda mfupi na mrefu nje ya nchi kupitia Serikali za India, China, Japan, Indonesia, Misri na Korea Kusini;

(xxiii) Taasisi 7 za Serikali zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu na Urithishanaji wa Madaraka katika Utumishi wa Umma. Taasisi hizo ni:- Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), *Wakala wa Barabara Tanzania* (TANROADS), Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi Tanzania (PSPTB), RAS Shinyanga, Geita, Mbeya pamoja na halmashauri zake;

(xxiv) Kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, nafasi mbalimbali za kazi kutoka mashirika ya kimataifa na kikanda ambayo Serikali yetu ni mwanachama zilitangazwa ili watanzania wenye sifa waweze kuomba. Miongoni mwa nafasi zilizotangazwa ni kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), International Conference on the Great Lakes Region (ICGLR), African Caribbean and Pacific Group of States Secretariat (ACP), na International Telecommunication Union (ITU). Kati ya nafasi hizo zilizotangazwa, watanzania wanne walipata kazi,

katika Jumuiya ya Afrika Mashariki 2 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2;

(xxv) Usanifu wa Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma umeendelea kufanyika kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (DFID) na Benki ya Dunia. Maandalizi ya nyaraka za programu yanaendelea kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi;

(xxvi) Ujazaji wa kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi 180,429 kutoka taasisi 180 za umma umesimamiwa na taarifa za watumishi 34,815 kutoka Taasisi 146 zimeingizwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS);

(xxvii) Mafunzo ya Maadili yametolewa kwa watumishi 1,529 wa Taasisi 18 za Umma;

(xxviii) Ufuatiliaji wa uzingatiaji Maadili umefanyika katika Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 31;

(xxix) Huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu11 na wajane watano (5) zimetolewa katika kipindi chote kwa mujibu wa Sheria;

(xxx) Watumishi 30 wa Idara 2 zilizokuwa zimesalia Dar es Salaam wamehamishiwa Makao Makuu Dodoma. Hatua hiyo inafanya huduma zote za Menejimenti ya Utumishi wa Umma kutolewa Dodoma kuanzia Aprili, 2018;

(xxxi) Ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa Mwongozo wa kudhibiti Viru vya Ukimwi (VVU), UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambuzwa (MSY) mahali pa kazi wa 2014 umefanyiwa ufuatiliaji katika Sekretarieti za Mikoa minne (4) na Halmashauri za Wilaya (3) Majiji (2) na Manispaa (4), ambazo ni Mkoa wa Manyara (Babati Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Babati), Mkoa wa Arusha (Arusha Jiji, Hamashauri za Wilaya za Meru na

Arusha), Mkoa wa Kilimanjaro (Moshi Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi), Mkoa wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Jiji, Manispaa za Temeke na Kigamboni); na

(xxxii) Uhamasishaji kupitia vipindi 6 vya runinga na vipindi 2 vya redio kuhusu utekelezaji wa Miongozo ya kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi wa Umma wa mwaka 2014 na ule wa Huduma kwa watumishi wa Umma wenye Ulemavu wa 2008 umefanyika kwa waajiri na watumishi.

### (b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Astashahada. Aidha, Chuo kinafanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kutoa machapisho mbalimbali ya kitaalam katika Utumishi wa Umma. Chuo kinatoa mafunzo kwenye Kampasi sita zilizoko kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya. Aidha, chuo kimeanzisha shahada za Uhazili na Utunzaji Kumbukumbu.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

(i) Mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma yalifanyika kwa Watumishi 566 kati ya 840;

(ii) Mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi yalifanyika kwa watumishi wa umma 2,283 kati ya 2,790;

(iii) Mafunzo ya muda mrefu kwa Washiriki 10,760 kati ya 15,810 yalitolewa katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya Raslimaliwatu, usimamizi wa manunuzi ya umma, uongozi na utawala bora;

(iv) Ushauri wa kitaalam umetolewa kwa Taasisi 12, na maandiko 18 ya ushauri elekezi wa kitaalam yameandaliwa na kuwasilishwa kwa Taasisi zilizoomba huduma hiyo;

(v) Makala 7 za kitaalam katika Utumishi wa Umma zimechapishwa katika majarida mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Jarida moja la Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC Journal) lipo katika hatua ya uchapishaji;

(vi) Chuo kimedhamini mafunzo ya muda mrefu kwa Watumishi 32 wa Chuo cha Utumishi wa Umma (19 Shahada ya uzamivu; 9 Shahada ya uzamili; 4 Shahada ya kwanza) na kuwezesha watumishi 96 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi;

(vii) Chuo kimepatiwa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 3,900 mjini Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na kumbi za mikutano na semina. Aidha, Chuo kimepatiwa eneo la ukubwa wa ekari 26 eneo la Pande katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.

(viii) Ukarabati wa mfumo wa umeme na kuweka mfumo wa mawasiliano ya ndani ya kielektroniki (LAN) katika majengo ya Kampasi ya Dar es Salaam; na

(ix) Ukarabati wa jengo la Shaban Robert la Kampasi ya Tabora ulifanyika na kukamilika;

## (c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

(i) Wakala imeendeleza ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika kutoa mafunzo yenye tija kwa maendeleo ya Taifa;

(ii) Mafunzo yametolewa kwa washiriki 1,331 kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na sekta binafsi. Mafunzo haya yalitolewa katika maeneo ya Uongozi, Utawala Bora, Uhasibu na Ukaguzi, Maadili, Anuai za Jamii, Mazingira, Kupunguza Umaskini na Afya;

(iii) Huduma ya muunganisho wa mtandao wa mafunzo kwa njia ya video (Video conference) imetolewa kwa washiriki 526 kutoka Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali na mikoa yote Tanzania bara;

(iv) Huduma ya muunganisho wa mtandao imetolewa kuwezesha midahalo, mikutano 21 ya mafunzo na mijadala ya ndani na nje ya nchi katika maeneo ya kinga dhidi ya Malaria, Ujenzi wa Reli mpya na utoaji ushahidi Mahakamani;

(v) Vituo vya kutoa huduma vimefunguliwa katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Morogoro. Utaratibu wa kukamilisha vituo vya kutolea huduma Dodoma na mikoa mingine unaendelea; na

(vi) Watumishi watano (5) wamepata mafunzo ya muda mfupi hapa nchini ya kuongeza uwezo wa utendaji katika maeneo ya Utawala Bora. Watumishi wawili wanapata Mafunzo ya muda mrefu katika kozi ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Uhasibu.

## (d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) ina jukumu la kutekeleza Sera ya Teknolojia ya Habari na

Mawasiliano (TEHAMA) ya Mwaka 2016 katika Utumishi wa Umma ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Wakala ina jukumu la kuratibu na kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Wakala imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Wakala, ikishirikiana na taasisi nyingine za Serikali imeboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuifanyia ukaguzi wa usalama na utendaji. Mifumo hii ni pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji wa mapato Serikalini (Government e-Payment Gateway – GePG) ambapo hadi sasa jumla ya Taasisi 28 za umma zimeunganishwa na kuutumia kukusanya mapato ya Serikali na mfumo wa kutolea ticket za kielektroniki ulioanza kutumiwa na Shirika la Meli za Serikali (MSCL);

(ii) Mfumo wa kutoa huduma za Serikali kupitia simu za mkononi (Government Mobile Platform) umeboreshwa. Mfumo huu unawarahisishia wananchi kupata huduma za Serikali popote walipo, unaokoa muda wa kwenda kufuata huduma kwenye ofisi za serikali, unapunguza gharama za kupata huduma husika na kupunguza mianya ya rushwa kwa kuondoa ulazima wa afisa wa Serikali kuonana uso kwa uso na mtoaji huduma. Katika kutekeleza hili, Wakala imetengeneza miundombinu ya kutoa huduma ya Ujumbe Mfupi (Short Message Service (SMS) Gateway) na kwa Menyu ((Unstructured Supplementary Service Data (USSD) Gateway) kupitia namba maalum *152*00#. Kuanzia Julai, 2017 Taasisi 42 za umma zimewezeshwa kutoa huduma kwa njia ya simu za mkononi kupitia miundombinu hii. Aidha, jumla ya taasisi zote zinazotumia mfumo hadi sasa zimefikia 118; mfano NHIF, TRA, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Ardhi zinatumia huduma hii kutoa

ankara na risiti za malipo yanayofanyika kupitia mfumo wa malipo wa Wizara ya fedha (GePG);

(iii) Taasisi mpya 15 za Umma zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) uliobuniwa na kutengenezwa na Wakala ya Serikali Mtandao. Hadi sasa, jumla ya Taasisi za Serikali 31 zimejiunga na mfumo huu. Mfumo huu unamuwezesha Afisa wa Serikali kufanya kazi mahali popote palipo na Ofisi ya Serikali iliyoungwa kwenye mtandao wa Serikali. Hali hiyo imeongeza ufanisi wa ubadilishanaji wa nyaraka mbali mbali katika Taasisi za Serikali. Vile vile, mafunzo yametolewa kwa taasisi zote zilizounganishwa katika huduma hii;

(iv) Taasisi za Serikali zimeendelea kuunganishwa kwenye Mfumo wa Mawasiliano wa Serikali kwa Njia ya Barua pepe (Government Mailing System [GMS]) na kuwezesha kuwa na mawasiliano salama kwa njia ya barua pepe kwenye Taasisi za Serikali. Taasisi mpya 32 zimeunganishwa katika mfumo huu kuanzia Julai, 2017 na Watumishi wake wamepewa mafunzo ya utumiaji sahihi wa mfumo. Taasisi 360 za Serikali zimeunganishwa na zinatumia mfumo huo tangu ulipozinduliwa;

(v) Taasisi 10 za Umma zimewezeshwa kuhifadhi Mifumo kwenye Vituo Vikuu vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya Serikali (Government Data Centres) yenye usalama na uhakika wa upatikanaji wa taarifa za Serikali;

(vi) Mchakato wa kuziunganisha Taasisi za Serikali 77 zilizopo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) wenye kuziunganisha Taasisi za Serikali katika mtandao mmoja wa mawasiliano ya kielektroniki (taarifa, sauti na video) ili kupunguza gharama za mawasiliano na kuboresha usalama wa taarifa. Kufikia sasa, zaidi ya taasisi 150 zimeshaunganishwa kwenye mtandao huo;

(vii) Ushauri wa kitaalamu umetolewa kwa taasisi 49 za Serikali katika maeneo mbalimbali ya matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa Serikali;

(viii) Uwezo wa watumishi wa Taasisi za umma 234 umejengwa hasa kwa wanaohusika na TEHAMA kwa kuwapatia mafunzo yanayowapa ujuzi wa kubuni, kujenga na kusimamia miundombinu na mifumo mbalimbali inayotumiwa na Taasisi husika;

(ix) Elimu kwa Umma kuhusu dhana ya Serikali Mtandao imetolewa kwa kupitia uandaaji na urushaji wa vipindi vya elimu, habari na mawasiliano. Vipindi 35 vimerekodiwa na vinaendelea kurushwa kwenye runinga. Aidha, tathmini ya utendaji wa Wakala katika kipindi cha miaka mitano imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau; tathmini hii pia inapatikana katika tovuti ya Wakala; na

(x) Watumishi 43 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ya kuongeza uwezo wa kiutendaji katika maeneo ya mbalimbali ya kitaalamu na uongozi. Aidha watumishi 18 wa Wakala wako katika mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za uzamili na uzamivu katika maeneo mbalimbali kulingana na kada zao. Watumishi 08 wamehudhuria mafunzo ya kitalaam (Profesional Certification) kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika maeneo yao ya kiutendaji;

## OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 8,640,422,004**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 6,990,422,004** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,650,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 **Shilingi 3,312,399,958** Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 336,000,000** zilipokelewa na kutumika.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Malalamiko 154 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 119 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 35 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Uchunguzi wa awali umefanyika kwa malalamiko 119 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, malalamiko 35 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

(ii) Usambazaji wa fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma kwa njia ya tovuti imeanza ambapo fomu hizo zilipatikana katika mtandao *www.ethicssecretariat.go.tz.* Jumla ya Viongozi wa Umma 16,050 ambao ni sawa na asilimia 98 wamerejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kufikia Machi, 2018. Aidha, kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, Sekretarieti imeanza maandalizi ya mchakato wa ujazaji fomu kwa njia ya mtandao (Online Application);

(iii) Viongozi 2,000 walipangwa kuhakikiwa katika mwaka wa fedha 2017/18. Awamu ya kwanza ya uhakiki wa viongozi 1,000 inatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2018. Mwongozo wa Uhakiki ulioandaliwa Mei, 2017 umeboreshwa na uko kwenye hatua za uchapaji. Aidha, zoezi la kuchambua nyaraka za uthibitisho wa Tamko linalotolewa na Viongozi wa Umma limeanza kwa kuwataka Viongozi husika kuwasilisha nyaraka hizo kwa ajili ya maandalizi ya zoezi la uhakiki na ufuatiliaji wa mienendo ya kimaadili;

(iv) Elimu kwa umma ilitolewa kwa viongozi wa Taasisi za Umma 667, pamoja na Watumishi wa Umma na wananchi 2,505 kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi

wa Umma ikijumuisha Hati ya Ahadi ya Uadilifu. Vipindi vitano (5) vya radio vilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Klabu 80 za Maadili zilianzishwa katika Shule za Msingi (50), Sekondari (25) na Vyuo (5) katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa upande wa Mikoa; Dodoma Klabu 15 za Maadili zilianzishwa katika Shule za Msingi (7), Sekondari (6) na Vyuo (2); Iringa Shule za Msingi (10); Morogoro Shule za Sekondari (3); na Mtwara Shule za Msingi (10);

(v) Siku ya Maadili Kitaifa iliadhimishwa Kitaifa Mkoani Dodoma tarehe 10 Desemba, 2017 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya utawala bora, uwajibikaji, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na maadili. Aidha, elimu kwa viongozi wa Taasisi za Umma na wananchi ilitolewa kupitia wiki ya huduma kwa wateja, matembezi ya watumishi, midahalo mbalimbali inayohusu maadili na kupitia vipindi vya redio na runinga. Aidha, sherehe hizi ziliadhimishwa katika mikoa mbali mbali nchini;

(vi) Watumishi 30 wa Sekretarieti wa kada mbalimbali wamejengewa uwezo katika eneo la utunzaji wa siri, masijala na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka za ofisi. Aidha, jumla ya watumishi 91 ambao sio wachunguzi walipata mafunzo kuhusu hatua za awali za kufanya uchunguzi;

(vii) Rasimu ya kanuni za Maadili kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeandaliwa na maoni ya wadau mbalimbali yanaendelea kupokelewa ili kuboresha kanuni husika;

(viii) Ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili Makao Makuu Dodoma umeanza; na

(ix) Kwa kushirikiana na TBC makala ya Siku ya Maadili inayohusu mapambano dhidi ya ukiukwaji wa maadili kwa viongozi wa umma, rushwa na mabadiliko ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 13 ya

mwaka 1995 imeandaliwa na kukamilika. Makala hiyo ina lengo la kukuza maadili katika jamii, uelewa wa haki za binadamu, uwajibikaji, utawala bora na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa.

## OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

38. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Sekretarieti ya Ajira ni: Kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika Utumishi wa Umma na kufanya usaili, kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira, kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa kanzidata za wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira; kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam wenye weledi kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma.

39. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa Jumla ya **Shilingi 3,115,975,000** ambapo **Shilingi 2,365,975,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 750,000,000** ni fedha za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Jumla ya **Shilingi 897,570,504.70** zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 589,743,500** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 307,827,004.70** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Katika kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira inayowezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika, Ofisi iliendesha usaili mara 6 kwa niaba ya waajiri 261 ili kujaza nafasi mbalimbali. Jumla ya waombaji 2,223 waliofaulu usaili walipangiwa vituo vya kazi;

(ii) Kanzidata ya kutunza taarifa za waliopangiwa vituo vya kazi imeimarishwa, taarifa za kada zenye wataalam wenye ujuzi maalum (rare profession) na taarifa za wahitimu wa vyuo vikuu zimeendelea kuandaliwa na kutunzwa kwa ajili ya rejea;

(iii) Usaili wa watendaji wakuu wa Mamlaka ya Maji safi na Maji taka-Dar es Salaam, Wakala wa Uchimbaji Visima na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI) umefanyika;

(iv) Usimamizi wa uendeshaji wa usaili katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za umma umefanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za ajira. Mamlaka za Serikali za Mitaa 139 zimesimamiwa katika kujaza nafasi ambazo Katibu wa Sekretarieti ya Ajira amekasimu kwao. Taasisi za Umma ambazo ajira zake zimesimamiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Bohari Kuu ya Dawa na Shirika la Masoko Kariakoo;

(v) Sekretarieti kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCCA), Shirika la Uendelezaji Uwanja wa Ndege Kilimanjaro (KADCO), Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ajira zinazoratibiwa na Ofisi ya Rais Ikulu za mradi wa "Building Sustainable Ant Corruption Action in Tanzania imefanya usaili wa nafasi mbalimbali;

(vi) Mfumo wa kielektroniki wa maombi ya kazi ulihuishwa ili uweze kuwasiliana na mifumo mingine. Hadi sasa, usanifu wa kuunganisha mfumo huu na mfumo wa Vitambulisho ya Taifa (NIDA) umefanyika;

(vii) Sekretarieti kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) imeboresha mfumo wa maombi ya kazi katika maeneo ya 'mwombaji nafasi za Ajira' kama mnufaika katika mfumo na 'Sekretarieti ya Ajira' kama msimamiaji wa mfumo ili kuongeza ufanisi

wa mfumo. Maboresho ya mfumo ni zoezi endelevu kutokana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji;

(viii) Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira tawi la Zanzibar imeendelea kuimarishwa na baadhi ya usaili wa michujo umeanza kufanyika Zanzibar ili kupunguza gharama za wasailiwa kutoka Zanzibar. Mathalani usaili wa mchujo wa TRA ulifanyika Zanzibar; na

(ix) Watumishi wameendelea kujengewa uwezo kwa kutumia fedha za ndani na kwa ufadhili wa Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi, 2018 watumishi 11 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya watumishi hao, watumishi saba (7) wamefadhiliwa na Washirika wa Maendeleo;

## OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

41. ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Utumishi wa Umma ni Tume REKEBU na inao wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma yanaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji unaozingatia malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/18 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi **4,909,515,670** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,425,530,000** zilikuwa za mishahara na Shilingi **2,483,985,670** zilikuwa za Matumizi Mengineyo. Hadi Machi, 2018 kiasi cha Shilingi **4,103,934,563.69** za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimetolewa. Kati ya hizo Shilingi **361,540,312.69** zilikuwa za kulipa madeni ya miaka iliyopita na Shilingi **3,742,394,251** zilikuwa za matumizi ya kawaida kwa mwaka husika, ambapo Shilingi **1,498,787,400** kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **2,243,606,851** za Matumizi Mengineyo.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Tume ya Utumishi wa Umma imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Ukaguzi wa kawaida umefanyika katika Taasisi 144 kati ya Taasisi 150;

(ii) Ukaguzi maalumu umefanyika katika Taasisi 8 kati ya 10 zilizotarajiwa;

(iii) Vikao vitatu (3) vya Tume vimefanyika na kutolea uamuzi rufaa 145 kati ya 212 zilizokuwepo;

(iv) Malalamiko 106 yameshughulikiwa kati ya 225 yaliyokuwepo;

(v) Elimu ilitolewa kwa wadau kupitia ziara za Makamishna katika Mkoa wa Lindi, kutoa vipeperushi 1,300 kuhusu Tume ya Utumishi wa Umma na kutoa nakala 392 za Miongozo ya kushughulikia masuala ya ajira na nidhamu katika Utumishi wa Umma. Vile vile, elimu kwa umma ilitolewa kupitia vyombo vya habari vya runinga, redio, magazeti na Tovuti ya Tume ambapo vipindi vitano (5) vya runinga na redio viliandaliwa na kurushwa. Aidha, Tume imeshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu;

(vi) Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa Robo ya Kwanza (Julai – Septemba, 2017) na Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Mwaka 2016/17 ziliandaliwa; na

(vii) Elimu kwa watumishi 115 kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa imetolewa. Vile vile, watumishi 17 wa Tume wamepata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika masuala ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na watumishi 55 wamepata mafunzo maalum ya Ukaguzi wa Rasilimaliwatu;

## OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

44. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 162 la tarehe 3 Juni, 2011. Aidha, uanzishwaji wa Bodi ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma (2010). Bodi ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa mamlaka husika.

45. ***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka wa fedha 2017/18, Bodi ya Mishahara na Masilahi (Fungu 09) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,721,977,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 709,170,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,012,817,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi Machi, 2018 Bodi imepokea **Shilingi 978,485,368.56**, kati ya fedha hizo, **Shilingi 674,947,600** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 303,537,768.56** ni mishahara.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Bodi imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Maandalizi ya Utafiti wa Hali ya Masilahi nchini yamefanyika ili kushauri kuhusiana na namna bora ya kutoa motisha kwa kuzingatia utendaji katika Utumishi wa Umma;

(ii) Taarifa mbili za gharama za maisha zinazotumika kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha zimeandaliwa;

(iii) Wajumbe 7 na watumishi 20 wa Bodi walipata mafunzo kuhusu masuala ya Mishahara katika zoezi la Tathmini ya Kazi kutoka kwa Wataalam wa Serikalini na Mtaalam Mwelekezi ili kuweza kuelewa dhana nzima ya kazi hii na ilivyotekelezwa; na

(iv) Rasimu ya Taarifa ya mwisho ya Tathmini ya Kazi imeshaandaliwa, utaratibu wa kuwasilishwa kwenye vikao vya juu Serikalini zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2018.

## OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

47. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2017/ 2018, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 4) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,375,726,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,375,726,000** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2018 **Shilingi 1,322,820,447.3** zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 705,194,873.28** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 617,625,574.05** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 2,000,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo.

49. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Idara ya Kumbukumbu imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji umewekwa katika Taasisi za Umma Kumi (10) ambazo ni Ofisi za Wakuu wa Wilaya Momba, Songwe, Kibiti, Malinyi na Tanganyika, Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), Uongozi Institute, Chuo cha Taifa cha Utalii, Jeshi la Zimamoto na Wakala wa Mabasi ya Yaendayo Kasi (DART);

(ii) Hatua zinazolenga kuondoa mlundikano wa kumbukumbu na kuboresha utunzaji wa taarifa muhimu za Watumishi (Vital Personnel Information Management) zimechukuliwa kwa Taasisi 13 za Umma ambazo ni Ofisi za Halmashauri za Wilaya Ruangwa, Kilwa, Uvinza, Buhigwe, Kigoma Ujiji, Kalambo, Sumbawanga, Kishapu, Shinyanga, Kyerwa na Biharamulo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

(iii) Mfumo wa Kiutendaji wa masijala umewekwa katika Ofisi za Mashirika ya Posta na Bandari, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Bohari Kuu ya Madawa;

(iv) Wizara 18 zimewezeshwa kuhamisha Masijala kwenda Dodoma katika kutekeleza agizo la Serikali;

(v) Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu yametolewa kwa Watumishi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Jeshi la Polisi, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Chuo cha Utumishi wa Umma, Tume ya Nguvu za Atomiki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Uongozi Institute, na Wakala wa Mabasi ya Mwendo Kasi (DART);

(vi) Mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ofisi (e-Office System) yametolewa kwa watumishi 6 wa Tume ya Utumishi ya Walimu;

(vii) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao ofisi imesimamia utekelezaji wa matumizi ya Mfumo wa kielektroniki wa masijala (e-file system) katika Taasisi za Umma 31;

(viii) Tathmini ya hali ya utunzaji kumbukumbu ilifanyika katika Taasisi za Umma 36 na ushauri wa kitaalamu kutolewa;

(ix) Miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu imetengenezwa katika Taasisi ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GLCA) na Mahakama ya Kuu ya Tanzania. Vile vile, miongozo ya Taasisi ya TASAF, Chuo cha Usafirishaji (NIT) na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) inaendelea kukamilishwa;

(x) Nyaraka na machapisho 593 yenye umuhimu wa kudumu kwa Taifa yamekusanywa na kuhifadhiwa kutoka Taasisi za Umma, Taasisi binafsi na watu binafsi (Idara imeweza kukusanya Majalada 2 ya British Early Secretariat na Vitabu 3 vya Wilaya (District Books), majalada 3 ya German records na nakala 136 za nyaraka kutoka Kilwa, Tanga, Morogoro na Lindi, machapisho kutoka Taasisi 5 binafsi ambazo ni: Majira Publications, The Guardians, Tanzania Standard New Papers (TSN), Mwananchi Communication) na TAMWA;

(xi) Vitu mbali mbali 410 na kumbukumbu 230 za Waasisi wa Taifa zenye umuhimu wa kihistoria kwa taifa zimetambuliwa, zimekusanywa na kuhifadhiwa makao makuu;

(xii) Mfumo wa Kidijitali wa Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka umesimikwa katika Kituo cha Kumbukumbu cha Taifa - Dodoma;

(xiii) Majaribio ya mfumo kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Taifa yamefanyika na watumishi 26 wa Idara wamejengewa uwezo wa matumizi ya mfumo huo kielektroniki katika usimamizi wa taarifa. Vile vile, majalada 800 ya nyaraka yameingizwa kwenye mfumo.

(xiv) Majalada 2,280 ya kumbukumbu tuli za Ofisi ya Rais-TAMISEMI yamehakikiwa ili kubaini yenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na yale ambayo umuhimu wake umekoma ili ziteketezwe;

(xv) Jengo la Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka Makao Makuu limefanyiwa ukarabati; na

(xvi) Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa wa kuanzia mwaka 2018/19 – 2022/23 umeandaliwa .

## OFISI YA USHAURI WA MAFUTA NA GESI (OGAB)

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Chombo hiki ni cha Taifa chenye jukumu la kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uchumi wa mafuta na gesi kwa Baraza la Mawaziri.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Bunge iliidhinisha **Shilingi 711,073,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2018 **Shilingi 171,794,720** fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Machi, 2018 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Ushauri wa kitaalam umetolewa katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi katika Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya Uchumi wa Mafuta na Gesi na mambo mengine yanayohusiana na Uchumi wa Mafuta na Gesi;

(ii) Utafiti juu ya manufaa ya kiuchumi wanayoyapata wawekezaji wenye viwanda kutokana na kutumia gesi asilia kama nishati yanavyomfikia mwananchi na

Taifa katika kukuza uchumi umefanyika na kukamilika mwezi Julai, 2017. Ripoti ya matokeo ya utafiti huo imewasilishwa mwezi Novemba, 2017;

(iii) Ushauri wa kitaalam ulitolewa kuhusu aina ya utaalam unaotakiwa kwenye majadiliano ya mikataba, ukubwa wa timu, mikakati na mbinu zitakazotumika na kushiriki kama waangalizi katika majadiliano ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Sekta ya Mafuta na Gesi;

(iv) Vikao vya majadiliano vitatu (3) vinavyohusu mradi wa gesi asilia ya kimiminika (Liquified Natural Gas-LNG project) vilivyofanyika kati ya Julai na Oktoba ,2017 vilishirikisha wajumbe kutoka OGAB; na

(v) Mkutano ya Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Ushiriki wa Watanzania katika Uwekezaji *(National Multi-sector Local Content Steering Committee)* uliofanyika Dodoma Tarehe 3 Agosti, 2017 na warsha kuhusu masuala ya miradi ya kimkakati ya utafutaji wa mafuta na gesi iliyoandaliwa na TPDC Tarehe 14 Agosti, 2017 ulishirikisha wajumbe kutoka OGAB.

## C. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2018/19 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

53. ***Mheshimiwa Spika*****,** baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/18, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2018/19.

54. ***Mheshimiwa Spika*****,** Mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19 kwa Mafungu yafuatayo 20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 04 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:

## OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

### (a) Ikulu

55. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

(ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuandaa mkutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

(vii) Kutengeneza na kurusha hewani Vipindi Maalum 20 vya Televisheni, kuchapisha na kutangaza Hotuba na Picha za Mheshimiwa Rais kwenye vyombo vya habari;

(viii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi.

(ix) Kuendesha mikutano miwili (2) ya Watendaji na Maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(x) Kuratibu na kuendesha mikutano nane (8) ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;

(xi) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;

(xii) Kukarabati nyumba 12 za watumishi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino na nyumba moja iliyopo Dodoma Mjini;

(xiii) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino; na

(xiv) Kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mwanza, Arusha, Mbeya, na nyumba mbili za wafanyakazi Tabora.

## (b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(ii) Kuendesha kesi 492 zinazoendelea na mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;

(iii) Kuifanyia mapitio Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa na ufisadi;

(iv) Kufanya utafiti wa msingi kuhusu hali ya rushwa nchini, utafiti na udhibiti wa mianya ya rushwa katika uendeshaji na usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa; utafiti wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa maliasili;

(v) Kufanya uchambuzi wa mifumo katika Sekta na Idara mbalimbali katika ngazi ya mikoa na wilaya;

(vi) Kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kwenye Taasisi za Umma zinazotolewa na Serikali na Wabia wa Maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(vii) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa na ufisadi na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(viii) Kushirikisha kundi la vijana katika shughuli zinazowajenga kimaadili na kupambana na rushwa ili kuwa na jamii inayoichukia rushwa;

(ix) Kuushirikisha umma katika kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa kwa kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii;

(x) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika Taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, Mkoa na Makao Makuu;

(xi) Ujenzi wa majengo ya Ofisi za TAKUKURU katika Wilaya 10; Kahama, Karatu, Karagwe, Rombo, Mbinga, Mafia, Mbogwe, Mlele, Uvinza, na Ubungo.

(xii) Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuongeza ufanisi.

## (c) Taasisi ya UONGOZI

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo ya "Stashahada ya Uzamili ya Uongozi" (Post Graduate-Diploma in Leadership), kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;

(ii) Kutekeleza Programu ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu majadiliano ya mikataba yenye thamani kubwa;

(iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa. Kozi 20 zitatolewa;

(iv) Kuandaa mikutano minne (4) ya kimataifa na kikanda; miwili (2) ya kitaifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(v) Kuandaa vipindi vya televisheni 12 vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika Bara zima la Afrika;

(vi) Kufanya utafiti kwenye maeneo tisa (9) kuhusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(vii) Kuandaa machapisho yatakayoelezea maisha na uzoefu wa Kiongozi maarufu Mstaafu;

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu pale utakapohitajika;

(ix) Kuendelea kuratibu na kuwezesha timu za Kitaifa za Majadiliano ya Mikataba yenye thamani kubwa; na

(x) Kwa kushirikiana na OR – MUU kuanzisha Kituo cha Tathmini kwa lengo la kuboresha mfumo wa uteuzi wa viongozi wa kati na waandamizi katika Utumishi wa Umma.

## (d) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

58. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, MKURABITA imejipanga kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Miliki za Kimila kwa wakulima 800 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 80 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya nne (4) za Mvomero, Chamwino, Uyui na Magu. Aidha, Mipango Kazi ya jamii ya vijiji vilivyorasimishwa itatekelezwa kwa kuanzisha mashamba darasa na kuunda vikundi vya uzalishaji;

(ii) Kuanzisha Vituo vitano (5) vya Urasimishaji Biashara ili kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu sehemu moja katika Halmashauri za Wilaya Tano (5) za Geita, Njombe, Singida, Tanga na Mtwara. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa kwa wafanyabishara 5,000 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;

(iii) Kufanya urasimishaji wa biashara katika Wilaya za Micheweni na Kusini Unguja ambapo wafanyabiashara 1,000 watapata mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara zao. Aidha, taratibu za kuanzisha vituo viwili (2) vya urasimishaji biashara zitafanyika kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu sehemu moja;

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri za Wilaya za Mbozi na Momba kwa kushirikiana na TAMISEMI;

(v) Kuandaa na kutoa hati miliki katika Halmashauri za Miji ya Morogoro, Arusha, Tunduma, Babati, Iringa, Njombe na Miji midogo ya Tandala na Ikonda. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa ardhi mjini utafanyika Chakechake na Unguja mjini. Jumla ya Hati Milki 6,500 zitaandaliwa na kutolewa;

(vi) Kukamilisha uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za kimila 11,766 katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji, Musoma, Butiama, Mbulu, Chamwino, Nyang'wale, Makete, Bukoba Vijijini, Mpwapwa na Newala;

(vii) Kufanya urasimishaji wa ardhi vijijini eneo la Chanjamjawiri katika Wilaya ya Chake Chake Pemba na eneo la Mahonda katika Wilaya ya Kaskazini B Unguja ambapo Hati za Miliki 2000 zitaandaliwa na kutolewa;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji tisa (9) katika Halmashauri za Wilaya sita (6) ambazo ni Mvomero, Mpwapwa, Manyoni, Nachingwea, Mbinga na Chamwino. Aidha, ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji vinne (4) utaendelea katika Halmashauri za Wilaya mbili (2) za Newala na Mbarali;

(ix) Kuanza urasimishaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini katika maeneo ya Mkoa wa Geita;

(x) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa shughuli za MKURABITA katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Zanzibar;

(xi) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara katika Wizara za Kisekta; na

(xii) Kuandaa vipindi 26 vya redio na televisheni kuhusu utekelezaji wa Shughuli za urasimishaji Tanzania Bara na Zanzibar.

## (e) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, TASAF imejipanga kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza ya Mpango. Zoezi hili linategemea kuzifikia kaya za walengwa zipatazo 355,000;

(ii) Kufanya maandalizi ya zoezi la kutambua kama hali za ustawi wa maisha ya walengwa wa Mpango wa kunusuru Kaya Maskini zimeboreka au la. Zoezi hili litatoa fursa ya kuwaondoa wale watakaobainika kuwa sio maskini tena kwa vigezo vitakavyotumika kupitia utaratibu wa wazi utakaoandaliwa na kukubalika na wadau wote;

(iii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 1,100,000 katika vipindi vya mizunguko 6 ya malipo katika Halmashauri za Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba, Zanzibar. Uhawilishaji wa fedha utafanywa kwa kufuata Kalenda ya Malipo ya kila baada ya miezi miwili;

(iv) Kufanya uhakiki wa walengwa wanaostahili kuwemo katika Mpango na kuwaondoa mara moja wale wote wasiostahili kuwemo kwa sababu mbalimbali;

(v) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 292,188 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa kazi za ajira za muda kwa Kaya Maskini. Walengwa hawa watatoka katika Halmashauri 44 pamoja na Unguja na Pemba;

(vi) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati na Miongozo ya Kuweka Akiba na Kuwekeza Katika maeneo ya utekelezaji. Wawezeshaji 2,340 katika Halmashauri 117 watapatiwa mafunzo ya kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Jumla ya vikundi 30,000 vya walengwa vitaundwa, kupewa mafunzo na vitendea kazi;

(vii) Miradi 134 ya afya, elimu, maji, ujasiriamali na barabara za vijijini itatekelezwa chini ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu. Wafanyakazi 850 wa Halmashauri na Sekretatieti ya Mikoa na Wajumbe wa Kamati 134 za Usimamizi za Jamii watapewa mafunzo juu ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi. Aidha, miradi 160 itatekelezwa katika Halmashauri 13 za Mikoa ya Arusha na Njombe kupitia programu inayofadhiliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Mataifa Yanayozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC);

(viii) Kutayarisha mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya Kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki). Njia hii ya malipo itawezesha fedha kutumwa moja kwa moja kwa mlengwa na kumfikia kwa haraka. Aidha, mifumo ya Habari, mawasiliano, uendeshaji na utoaji taarifa wa shughuli za Mpango itaendelea kuimarishwa na kuboreshwa kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu;

(ix) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu;

(x) Kufanya utafiti shirikishi katika maeneo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi ili kubaini fursa na vikwazo katika kufikia lengo la jamii kujipatia maendeleo. Hii itahusisha kukusanya takwimu mbalimbali katika ngazi za jamii kwa ajili ya utafiti huo;

(xi) Kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na TASAF Makao Mkuu, mikoa, halmashauri na jamii ili kuweza kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi;

(xii) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini za shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango;

(xiii) Kufanya mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini; na

(xiv) Kuendelea na maandalizi ya Kipindi cha Pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN II) kitakachotekelezwa kwa miaka mingine mitano kuanzia 2019/20 – 2023/24.

## (f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa Mafunzo kwa walengwa 6,000 kuhusu ujasiriamali, namna ya kujitambua na taratibu za mikopo ya Mfuko inayotolewa na mfuko kuhusu uendeshaji wa miradi endelevu na kutoa mafunzo kwa wateja 3,000 kuhusu kufanya miradi endelevu;

(ii) Kutoa mikopo 5,400 kwa Vijana waliohitimu mafunzo katika Vyuo vya Ufundi Stadi vinavyotambuliwa na

VETA na SIDO na wanawake wajasiriamali katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Njombe, Lindi, Iringa na Kagera;

(iii) Kufungua tawi Bukoba Vijijini;

(iv) Kufungua Vituo vya huduma (Satellites) Bagamoyo (Pwani) na Iringa Mjini;

(v) Kufanya utafiti wa uanzishwaji wa huduma katika Halmashauri za Wilaya za Bukoba, Urambo, Bagamoyo, Kakonko na Tanga; na

(vi) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi yanayolenga utoaji wa huduma na sera za mikopo.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba **Shilingi 22,644,912,748** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba **Shilingi 576,213,769,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**.** Kati ya fedha hizi, **Shilingi 401,158,280,000** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 175,055,489,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZILIZO CHINI YAKE

### (a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2018/19 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa. Aidha, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo wa Serikali katika kuratibu Sera mbalimbali zilizopo ili ziweze kuleta maendeleo kutokana na kuwianishwa kwake (Policy Coherence);

(ii) Kuhuisha miundo ya Maendeleo ya Utumishi na kuwianisha na kuoanisha mishahara katika Utumishi wa Umma baada ya zoezi la Tathmini ya Kazi kukamilika.

(iii) Kuanzisha na kuhuisha Miundo na Mgawanyo wa Majukumu kwa Taasisi za Serikali zilizobaki ili kuboresha utoaji huduma kwa Umma kwa kuondokana na urudufu wa majukumu. Vile vile, ofisi itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo iliyokwisha idhinishwa;

(iv) Kufanya tathmini ya hali halisi ya Ufuatiliaji na tathmini (M&E) kwa Wakala za Serikali;

(v) Kujenga uwezo wa kimafunzo kuhusu uimarishaji wa mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri; Taasisi Zinazojitegemea na Wakala za Serikali;

(vi) Kufanya Tathmini ya Utendaji kazi na kuziimarisha Wakala za Serikali zilizopo;

(vii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mifumo na Viwango vya Utendaji Kazi na kutoa ushauri wa kitaalam katika taasisi za Serikali;

(viii) Kuanza usanifu wa mfumo mpya wa HCMIS (home grown system) utakaokidhi mahitaji ya Serikali ya sasa na ya mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea kutokea duniani ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto za kiufundi za sasa za HCMIS;

(ix) Kuratibu uanzishwaji wa Vituo 3 vya awali vya HUDUMA PAMOJA kwa ajili ya kutolea Huduma za Serikali sehemu moja (One Stop Service Centre) katika jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Dodoma;

(x) Kufanya tathmini ya wataalamu wa fani ya TEHAMA Serikalini wakijumuishwa wa Wakala, Idara Zinazojitegemea, Ofisi za Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali;

(xi) Kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji, uendelezaji, uendeshaji na matumizi ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2018;

(xii) Kufuatilia uzingatiaji wa Mwongozo wa kusimamia Utekelezaji wa Serikali Mtandao wa mwaka 2018 katika Taasisi za Serikali;

(xiii) Kuhuisha Mpango Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Serikali Mtandao wa mwaka 2013 (National e-Government Strategy, 2013) na kuandaa Mpango Mkuu wa Utekelezaji wa Serikali Mtandao (e-Government Master Plan) wa miaka mitano;

(xiv) Kuratibu utekelezaji wa Programu mpya ya "Digital Tanzania" kwenye eneo la Serikali Mtandao;

(xv) Kusimamia na kuratibu fursa za mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa watumishi wa umma kufanya kazi kwa ufanisi;

(xvi) Kutoa Mwongozo wa kuwezesha Taasisi za Umma kuwa na Mpango wa Rasilimaliwatu wa muda wa kati na muda mrefu (Medium and Long term Human Resource Plan);

(xvii) Kuimarisha utoaji wa taarifa kupitia tovuti na barua kuhusu upatikanaji wa nafasi za kazi katika mashirika ya kimataifa pindi nafasi zinapojitokeza;

(xviii) Kushughulikia na kutoa vibali vya uhamisho wa watumishi miongoni mwa waajiri katika Utumishi wa Umma na kushughulikia maombi ya vibali vya likizo bila malipo, kuazimwa na kushikizwa yanayowasilishwa na waajiri pamoja na watumishi. Sambamba na kutoa vibali vya uteuzi kwa watumishi waandamizi wanaopendekezwa na waajiri kushika nyadhifa za Uongozi katika Utumishi wa Umma;

(xix) Kushughulikia malalamiko yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma na kuchukua hatua stahiki kwa kushirikiana na waajiri;

(xx) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara “HCMIS” katika ngazi zote za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuhuisha mfumo huo kuendana na mahitaji ya sasa na teknolojia iliyopo;

(xxi) Kutoa mafunzo ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa watumishi wa Idara za Kilimo na Mifugo na kufuatilia utekelezaji wa Mfumo katika Idara za Afya na Elimu katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa;

(xxii) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma watakaoajiriwa kwa kuzingatia vipaumbele na kuimarisha maeneo yenye upungufu mkubwa;

(xxiii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa matumizi sahihi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS);

(xxiv) Kufanya uhakiki wa mahitaji sahihi ya Rasilimaliwatu katika Mikoa mitano (5) na kutoa mafunzo kwa Maafisa Rasilimaliwatu 30 kutoka katika Taasisi za Umma;

(xxv) Kuhuisha Kanuni za Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2005;

(xxvi) Kufanya ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 20, Sekretarieti ya Mkoa 1 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 3. Vile vile Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu;

(xxvii) Kufanya ufuatiliaji na uhamasishaji wa masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuwezesha Serikali kuwa na rasilimaliwatu bora na itakayowezesha kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuandaa 'framework' ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala ya Anuai za jamii katika Utumishi wa Umma;

(xxviii) Kujenga uelewa wa Menejimenti na Viongozi wa Kisiasa wa Taasisi za Umma kuhusu utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini;

(xxix) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) kwenye Taasisi za Umma;

(xxx) Kutoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5) kwa mujibu wa sheria;

(xxxi) Kuhamisha watumishi 28 waliosalia Dar es Salaam kuja Dodoma; na

(xxxii) Kukamilisha maandalizi ya nyaraka za Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma na kuratibu uidhinishwaji.

### (b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)

**64**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 1,400;

(ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Manejimenti na Usimamizi wa ofisi kwa Watumishi wa Umma 3,385;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa Watumishi wa Umma 1,170;

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 12,866 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye maeneo 21 kwa Taasisi za Umma;

(vi) Kufanya utafiti wa maeneo 8 yanayolenga kuboresha Utumishi wa Umma;

(vii) Kuandaa machapisho mbalimbali kama vile majarida, vitabu, na makala za kitaalamu katika Utumshi wa Umma katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala;

(viii) Kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 23 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi zifuatazo;13 Shahada ya Uzamivu na 10 shahada ya uzamili;

(ix) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 194 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika maeneo ya Uongozi na Utawala Bora katika Utumishi wa Umma na maeneo mengine kulinga na taaluma zao;

(x) Kuendeleza ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) litakalotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi ya Tabora;

(xi) Kuandaa Mahitaji ya kufanya ukarabati wa majengo na uzio katika Kampasi ya Tabora;

(xii) Kuandaa Mpango wa Matumizi (Master Plan) ya eneo la Tanga;

(xiii) Kukarabati jengo la Chuo lililopo Dodoma; na

(xiv) Kufanya malipo ya awamu ya kwanza gharama za ununuzi wa jengo la Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

## (c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma za maunganisho ya mtandao kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa Washiriki 2,700 katika maeneo ya Uongozi, Utawala Bora, Utoaji Huduma na Uwajibikaji, Huduma za Fedha na Ukaguzi, Maadili, Anuai za Jamii, Mazingira, Kupunguza Umaskini na Afya;

(ii) Kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia za kisasa na kwa gharama nafuu kwa ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuimarisha mtandao wa Wakala kikanda ili kuwafikia wateja walioko mikoani kwa urahisi;

(iv) Kuanza ujenzi wa Ofisi za Wakala Dodoma;

(v) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Wakala ili kukidhi ongezeko la wateja na mabadiliko ya haraka ya teknolojia;

(vi) Kuratibu mikutano ya kazi ya Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara, Wakala za Serikali na taasisi

nyingine za umma kwa kutumia huduma ya daraja-video (bridging video services) na kutoa ushauri wa kitaalamu; na

(vii) Kufanya utafiti na majaribio ya teknolojia rafiki katika nyanja za mawasiliano ya video na mafunzo na kuziboresha.

## (d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2018/19, Wakala ya Serikali Mtandao inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kushirikiana na Taasisi za Serikali ili Kujenga na Kuboresha Mifumo ya ukusanyaji mapato na maduhuli ya Serikali;

(ii) Kusimamia na kuboresha Usalama wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini;

(iii) Kuanzisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao Makao Makuu Dodoma;

(iv) Kusimamia, Kuboresha na Kupanua Miundombinu Shirikishi ya Serikali Mtandao kwa Taasisi zote za Serikali, hii ni pamoja na kuendelea kusambaza Miundombinu ya Mtandao wa Serikali (GovNet), Ujenzi wa mfumo utakaowezesha mifumo mbalimbali ya TEHAMA Serikalini kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus (GESB), Mfumo mkubwa kwa ajili ya kuhifadhi data za Serikali kwa pamoja (Government Data Central Repository or Government Data Warehouse (GDW), Miundombinu ya Pamoja ya Kuhifadhi mifumo ya Serikali Mtandao (Government Cloud);

(v) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtandao kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na watumiaji wa huduma

za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Serikali 140 ili kuongeza uelewa na uwezo wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(vi) Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ili kuhakikisha kwamba uwekezaji unaofanywa na Serikali kwenye TEHAMA unazaa matokeo yaliyokusudiwa;

(vii) Kusimamia, kuboresha na kupanua matumizi ya Mifumo na Miundombinu shirikishi ya TEHAMA Serikalini ili kuongeza ufanisi na usalama wa taarifa za Serikali pamoja na kupunguza gharama ya uhifadhi na uendeshaji wa mifumo ya Taasisi za Serikali. Mifumo na Miundombinu hiyo ni pamoja na Kituo Kikuu cha Data cha Serikali (Government Data Centre) kwa kuongeza taasisi mpya 27, Mfumo wa barua pepe Serikalini (GMS) kwa kuongeza taasisi mpya 25 kufikia 385, Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-office) kwa kuongeza taasisi mpya 21, Mfumo wa kutoa huduma kwa Umma kupitia simu za Mkononi (Government Mobile Platform (GMP) kufikia 163 kutoka 118;

(viii) Kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa kwa kutumia Viwango na Miongozo ya TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano; hili litafanywa kwa ushirikiano wa karibu na mamlaka husika za utambuzi wa watu; na

(ix) Kuendelea kujenga uwezo wa wataalam wake ambapo watumishi 50 watapatiwa mafunzo ya ubobezi kwenye maeneo ya usalama, miundombinu na utengenezaji wa Mifumo. Watumishi 10 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Stashahada, watumishi wawili (2) katika ngazi ya

uzamivu na watumishi tisini na tano (95) watapatiwa mafunzo ya muda mfupi katika maeno mbalimbali ya kiutendaji.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2018/19 kwa ufanisi, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kiasi cha **Shilingi 41,403,499,261** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 30,464,499,261** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 10,939,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kupokea Matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Matamko hayo yanajazwa kwa njia ya mtandao (online application) baada ya kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (Ethics Management Information System – EMIS)

(ii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;

(iii) Kuchunguza tuhuma ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 2,000;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kutoe elimu kwa Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na

(ix) Kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Makao Makuu Dodoma.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 11,511,874,000 kwa ajili ya** Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 7,461,874,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,050,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kushiriki kama Wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na Taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwa Taasisi husika;

(iii) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira za Muungano;

(iv) Kuimarisha Ofisi za kanda ikiwemo Ofisi ya Dar es salaam baada ya kuhamia Dodoma;

(v) Kufanya utafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji kazi wa ofisi;

(vi) Kuimarisha mfumo wa maombi ya kazi na mrejesho kwa waombaji kwa kutumia TEHAMA.

(vii) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya "psychometric test";

(viii) Kutoa taarifa na elimu kwa Umma ili kukuza uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2018/19, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi **3,116,083,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **2,366,083,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **750,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2018/19, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya Ukaguzi wa kawaida katika Taasisi 150 na Ukaguzi Maalum katikaTaasisi 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi taarifa za ukaguzi, rufaa, malalamiko

na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

(iii) Kuelimisha Taasisi za Umma na Watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kupitia, ziara za Makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na Tovuti;

(iv) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/18 na kuiwasilisha kwa Rais; na

(v) Kutoa elimu na mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi 24 wa Tume.

73. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2018/19, Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi **4,403,479,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

## OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

74. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/19, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya utafiti wa Hali ya Masilahi katika Utumishi wa Umma nchini na Mifumo ya kupima utendaji kazi ili kushauri namna bora ya kutoa Motisha kwa kuzingatia utendaji ili kuongeza ufanisi katika kuhudumia wananchi;

(ii) Kuandaa taarifa 4 za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kima cha chini cha mshahara wenye staha; taarifa hizi zinawezesha kushauri kuhusu mshahara wa chini unaoendana na gharama halisi za maisha; na

(iii) Kutekeleza mapendekezo yanayotokana na zoezi la Tathmini ya Kazi na Uhuishaji wa Madaraja katika Utumishi wa Umma.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza mpango wa bajeti wa Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Fungu 09: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kutumia **Shilingi 1,652,435,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

## OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

76. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuweka na kuhuisha Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za Kiutendaji na za Watumishi katika Taasisi za Umma (Wizara 17, Mikoa 25, Halmashauri 16) ili kuboresha Utoaji wa huduma;

(ii) Kujenga uwezo wa Taasisi za umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa Menejimenti za Taasisi za umma na mafunzo kwa waratibu na watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

(iii) Kuweka mfumo wa kielektroniki wa masijala (e-file system) katika Taasisi thelathini na tatu (33) za Umma;

(iv) Kufanya ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi thelathini na nane (38) za Umma;

(v) Kusaidia Taasisi za umma kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu;

(vi) Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka Taasisi za umma na watu binafsi;

(vii) Kutambua, Kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

(viii) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Taifa kwa kuingiza kumbukumbu na nyaraka katika mfumo wa Kidijitali wa Kuhifadhi Nyaraka (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;

(ix) Kufanya uhakiki (appraisal) wa kumbukumbu tuli zaTaasisi tatu (3) za Umma zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ilikubaini zenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zile ambazo umuhimu wake umekoma ili ziteketezwe;

(x) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu katika Kanda ya Ziwa Mwanza;

(xi) Kuendeleza ukarabati wa jengo la Idara Makao Makuu Upanga Dar es Salaam na ukarabati wa Ghala la Taifa la kuhifadhi nyaraka (National Repository);

(xii) Kufanya utekelezaji wa Mipango ya hadhari ya kudhibiti na kukabiliana na majanga kwenye Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu na Ghala la Nyaraka la

Taifa. Vile vile, kuweka vifaa vya kudhibiti hali ya hewa kwenye maghala ya kuhifadhia nyaraka;

(xiii) Kufunga mitambo ya kupiga picha nyaraka kwa ajili ya kuhifadhi kwenye mifumo ili kulinda nakala halisi na kuweka urithi wa Taifa. Pia, kujenga Maabara ya kisasa ya kukarabati nyaraka na kufanya ukarabati wa nyaraka; na

(xiv) Kuimarisha uwezo wa utendaji wa Watumishi wa Idara.

78. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha wa 2018/19, Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 8,148,504,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**.** Kati ya fedha hizi, **Shilingi 2,969,632,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 5,178,872,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## D. MAJUMUISHO

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Mipango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/19 ya mafungu yaliyotajwa imezingatia vipaumbele na matakwa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuiwezesha Nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025. Ofisi yangu itaendelea kujenga Utumishi wa Umma kuanzi sasa utakaohudumia kwa ufanisi, viwango na ubora stahiki jamii ya uchumi wa kati baadala ya kusubiri mpaka mwaka 2025. Lengo hilo la muda mrefu linawekewa misingi kuanzia sasa kwa kuimarisha misingi ya uwazi, uchapa kazi, uwajibikaji na nidhamu katika Utumishi wa Umma ili kuondokana na matumizi mabaya ya rasilimali, ukiukwaji wa maadili na urasimu katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, tunaimarisha mifumo ya usimamizi wa utekelezaji na matumizi ya TEHEMA katika utendaji wa Serikali. Tunaamini kuwa Utumishi wa Umma wenye ufanisi, viwango na ubora ni chachu ya maendeleo kwa Taifa lolote duniani. Hivyo basi, ni matumaini yangu kuwa Utumishi wa Umma na Utawala

bora utaendelea kuimarishwa siku hadi siku ili kutoa huduma bora zenye viwango stahiki kwa haraka na staha. Tutaendelea kusisitiza uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu mbali mbali ili kujenga uwajibikaji na kupiga vita rushwa kwa nguvu zaidi.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** mazingira ya utulivu na amani ni fursa adhimu katika kujenga uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote. Mazingira hayo hujengwa katika misingi ya utumishi uliotukuka, utawala bora, utawala wa Sheria na Mifumo thabiti ya Usimamizi wa utekelezaji. Kwa nchi yetu na kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, hayo yanatekelezwa na Ofisi yangu inayojumuisha, Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaunga mkono kwa dhati juhudi za Mheshimiwa Rais za kupiga vita ubadhirifu wa mali ya Umma na ufisadi. Tunaunga mkono hatua zinazochukuliwa na viongozi katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma ili kurejesha nidhamu ya Utumishi wa Umma na kuboresha huduma kwa wananchi. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge na watu wenye mapenzi mema kwa Nchi yetu waendelee kuunga mkono juhudi hizi. Tumeanza kuona mafanikio lakini bado tunayo kazi kubwa ya kufanya mbele yetu.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kwako naomba kutoa taarifa kwa kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kuwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imekamilisha kuhamia Dodoma, hivyo hakuna utoaji huduma Dar es Salaam. Jengo la Utumishi la Dar es Salaam linatumiwa na Wakala ya Serikali Mtandao.

83. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha wa 2018/19, sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi yetu kwa mwaka wa fedha 2018/19 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

**a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu**

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 22,644,912,748 |
| **Jumla** | **Sh.** | **22, 644,912,748** |

**b. Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 401,158,280,000 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 175,055,489,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **576,213,769,000** |

**c. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 30,464,499,261 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 10,939,000,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **41,403,499,261** |

**d. Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 7,461,874,000 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 4,050,000,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **11,511,874,000** |

**e. Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 2,366,083,000 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 750,000,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **3,116,083,000** |

**f. Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 4,403,479,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **4,403,479,000** |

**g. Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 1,652,435,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **1,652,435,000** |

**i. Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 2,969,632,000 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 5,178,872,000 |
| **Jumla** | **Sh.** | **8,148,504,000** |

84. ***Mheshimiwa Spika*****,** Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2018/19, ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Jumla kuu - Matumizi ya Kawaida | Sh. | 473,121,195,009 |
| Jumla kuu - Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 195,973,361,000 |
| **Jumla kuu kwa Mafungu yote** | **Sh.** | **669,094,556,009** |

85. ***Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge***, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

86. ***Mheshimiwa Spika***, Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge mchana huu kuna tangazo dogo tu kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club.* Anawaomba Wajumbe wa kamati ya Utendaji ya Bunge *Sports Club* Wajumbe wa Kamati Ndogo ya Uratibu wa Michezo na Burudani pamoja na wasemaji walioteuliwa wabaki ukumbini hapa mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge mchana huu saa saba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 07:00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Tunaendelea na majadiliano. Sasa tunamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ili awasilishe Taarifa yake. Mwenyekiti, karibu. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya uchambuzi wa bajeti Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la januri 2016 kwa kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla wa mafungu 28 yafuatayo:-

(1) Fungu 56 – Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(2) Fungu 02 – Tume ya Utumishi wa Walimu *(TSC);* na

(3) Mafungu 26 ya mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI inajikita katika maeneo manne ambayo ni kama yalivyotajwa kwenye Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na ufafanuzi wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa na Bunge shilingi trilioni 1.78 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni pamoja na; Programu ya Uimarishaji Miji, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri), pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Ndani kwa njia ya Kieletroniki kama ifuatavyo:-

Moja, Mradi Na. 6405 – Programu ya Uimarishaji Miji. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 3.32 na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga. Mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa Kilomita 13.1 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu kilomita 4.3 zilikuwa zimekamilika, ambazo ni sawa na asilimia 33 ya utekelezaji wa mradi huo. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa mifereji rafiki kwa ajili ya maji taka, ujenzi wa njia za waenda kwa miguu, uwekezaji wa taa na alama za barabarani.

Pili, Mradi Na. 4946 – *Local Government Own Source Projects,* Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 471.4 na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu. Mradi huu ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuwawezesha kiuchumi wanawake na vijana kupitia 10% ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea kikundi cha vijana ambacho kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kimeanzisha Kiwanda cha Chaki kilichopo Mjini Maswa. Mradi huu una mtaji wa shilingi milioni 100, ambapo Kikundi hicho cha vijana kinamiliki asilimia 40 ya hisa na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inamiliki 60%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mradi huo umeingizwa katika kundi la miradi ya kimkakati ya Halmashauri na umetengewa kiasi cha shilingi bilioni nne kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanda hicho na kuanzisha uzalishaji wa bidhaa nyingine za kimkakati kama vile vifaa tiba na vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu. Mradi Na. 4946 – *Local Government Own Source Projects,* Mfumo wa Ukusanyaji Mapato kwa njia za Kieletroniki. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha Fungu 85 – Mkoa wa Tabora ili kuiwezesha Serikali kuongeza mapato kwa njia ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi na kasi ya utekelezaji mfumo huu ambao sasa unatumika katika Halmashauri zote 185 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kwamba katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilipanga kukamilisha ununuzi wa mashine 85 za kukusanyia mapato *(Point of Sales)* na tayari imeishanunua mashine 59 sawa na 69% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na matumizi ya mfumo huu Kamati iliweza kutembelea na kukagua maeneo ya biashara katika soko kuu la tabora lenye jumla ya mashine tisa za kukusanyia mapato na stendi ya mabasi yaendayo mikoani ambapo inatumia mashine mbili tu za *POS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuhusu matokeo ya ukaguzi, mradi Na. 6405 *Program* ya Uimarishaji Miji. Kamati ilikagua ujenzi huo wa barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na kubaini mambo yafuatayo:-

(a) Mafanikio; moja, kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami katikati ya Mji wa Shinyanga; pili, kuongezeka kwa biashara na uwekezaji katika maeneo ya kati ya mji kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara; na tatu, kuongezeka thamani kwa maeneo ya makazi yaliyo jirani na barabara zinazojengwa.

(b) Changamoto; Kasoro za Mkataba kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na Mkandarasi zinachelewesha mradi huo na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji; pili, Usanifu wa awali wa mradi haukuzingatia mahitaji halisi ya wakazi wa maeneo mradi unapotekelezwa; tatu, mradi kutekelezwa kwa gharama kubwa ikilinganishwa na ubora wa kazi; nne, mifereji rafiki ya maji ambayo itakuwa inajaa udongo kwa urahisi na hivyo kushindwa kusafirisha maji taka kutokana na kujengwa chini ya kiwango; tano, Halmashauri kukosa Wahandisi wa ujenzi na hivyo kukosa usimamizi madhubuti wa miradi ya barabara; sita, ushirikiano hafifu baina ya Halmashauri na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA);* na saba uwepo wa viashiria vya rushwa katika utoaji wa zabuni za ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mradi Na. 4946 – *Local Government Own Source Projects*, Uwezeshaji wa Kiuchumi, Wanawake na Vijana. Baada ya Kamati kutembelea kikundi hicho cha vijana cha Maswa, yako mambo kadhaa yalibainika, kama ifuatavyo:-

(a) Mafanikio; ajira za moja kwa moja na fursa ya kumiliki hisa kwa vijana ambapo vijana 28 wameajiriwa na kati ya hao sita wanamiliki hisa katika kiwanda hicho. Pili, mradi huu ni miongoni mwa vyanzo vya mapato vya Halmashauri; tatu, kiwanda hiki kimeweza kusambaza chaki katika mikoa nane ya Tanzania Bara na Zanzibar na hivyo kupunguza matumizi ya chaki kutoka nje; nne, mradi huo umekuwa chachu ya Halmashauri nyingi kuanzisha viwanda vya aina hii kutokana na kuwa sehemu ya mafunzo.

(b) Changamoto; moja, teknolojia duni ambayo inafanya kiwanda hicho kuzalisha chaki chini ya kiwango;

kukosekana kwa malighafi mkoani Simiyu na hivyo kulazimika kuzifuata mkoani Singida; tatu, mazingira ya ushindani yasiyo sawa yanayosababishwa na uingizaji wa chaki kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mradi Na. 4946 – *Local Government Own Source Projects*. Kamati ilitembelea baadhi ya maeneo katika Manispaa ya Tabora ili kujionea ukusanyaji wa mapato na kubaini yafuatayo:-

(a) Mafanikio; Moja, mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki umeimarisha utunzaji wa kumbukumbu na hivyo kupunguza upotevu wa taarifa muhimu za hesabu; pili, kupunguza gharama za ukusanyaji mapato; tatu, mfumo umeongeza uwazi na hivyo kuiwezesha Serikali kudhibiti ubadhirifu wa mapato uliokuwa unasababishwa na Wakala wasio waaminifu.

(b) Changamoto; moja, matatizo ya mtandao kukata wakati wa kutoa huduma kwa wateja hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato; pili, mfumo huu kushindwa kuzungumza na mifumo ya kibenki na hivyo kuzifanya benki kushindwa kuingiza malipo kwenye mfumo kwa njia ya *cheque* na *TISS;* tatu, kukosekana kwa Wakala wa Benki kwa ajili ya makusanyo ya mapato ya Halmashauri; na nne, mfumo kushindwa kudhibiti fedha za Halmashauri moja kuingiliana na taarifa za Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018:-

(i) Hazina itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi ilinayopangwa;

(ii) Wanasheria wa Halmashauri wajengewe uwezo katika eneo la mikataba ili kuziwezesha Halmashauri kuingia mikataba yenye manufaa kwa Taifa na kuepuka ubadhirifu;

(iii) Ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika uibuaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo umeendelea kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo, kwani wanajiona siyo sehemu ya miradi hiyo;

(iv) Kukosekana kwa programu endelevu ya elimu ya ujasiriamali na uwezeshaji kwa wanawake na vijana, kumefanya vikundi hivyo washindwe kutumia vizuri fedha za mikopo;

(v) Urasimu usio wa lazima Serikalini umeendelea kuchelewesha utekelezaji wa miradi;

(vi) Kukosa umakini katika usanifu wa awali wa miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama; na

(vii) Mfumo wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa njia ya kieletroniki umeonesha mafanikio makubwa kwa kuongeza na kudhibiti mapato ya Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Fungu – 56, pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22.7 kutoka vyanzo vya ndani. Hadi Februari, mwaka huu 2018, jumla ya shilingi bilioni 9.9 zilikuwa zimekusanywa na Fungu – 56, kiasi ambacho ni sawa na 43% ya lengo. Sababu za makusanyo hafifu ya maduhuli ni pamoja na:-

(i) Mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vya Ofisi;

(ii) Halmashauri nyingi kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;

(iii) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kushindwa kupata shilingi bilioni 1.2 ilizotarajia kuzipata kutoka *CRDB*; na

(iv) Kukosekana kwa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kwamba kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka fedha 2016/2017 ambacho kilikuwa ni asilimia 28.1. Aidha, Kamati inatia shaka iwapo kwa kipindi kilichobaki malengo ya makusanyo yatafikiwa. Hii inatoa taswira kwamba bado Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijaweza kuwa na makadirio sahihi kuhusu kiasi cha mapato kinachotakiwa kukusanywa au kuna uzembe wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya mtazamo huu ni kwamba, utekelezaji wa shughuli zinazopangwa na Ofisi hii kwa kutegemea fedha za ndani utaendelea kusuasua. Kamati inaendelea kushauri kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, izingatie makadirio halisi ya makusanyo kutokana na vyanzo vilivyopo ili kuweza kuwa na makusanyo halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mikoa na Serikali za Mitaa, hadi kufikia Februari, 2018 makusanyo yalikuwa ni shilingi bilioni 347.1 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 50 ya lengo. Ingawa kiasi hiki kiko chini ya lengo angalau kwa asilimia 70 hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka huu, bado kiwango cha makusanyo katika Serikali za Mitaa kimeonekana kuwa kikubwa. Sababu inaweza kuwa ni kutokana na Halmashauri kuwa na vyanzo vingi vya makusanyo na wingi wa watu ikilinganishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba:-

(i) Fedha zinazotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji fedha uliowekwa;

(ii) Kiasi cha fedha kinachotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni kikubwa ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na

(iii) Fedha hazipatikani kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti ya ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia Februari, 2018 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, pamoja na taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea shilingi bilioni 245.1 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 53 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2018 kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa ni shilingi bilioni 29.07 sawa na asilimia 69 ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa kulinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita wa 2016/2017 kiasi hicho kimeongezeka kwa 5% kutoka 64%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba hadi kufikia Februari, mwaka huu, 2018 Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, imepokea jumla ya shilingi bilioni 216.1 kutoka Hazina, sawa na 52% ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika kipindi hicho. Kiasi hicho kimepungua kwa takriban 4% ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliotangulia ambapo kilifikia 56% ya lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba kwa wastani wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017 ulikuwa na 60.5% kiwango ambacho ni sawa na kilichopatikana katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, bado upatikanaji wa fedha umeshindwa kufikia lengo la angalau 25% kwa kila robo ya mwaka wa fedha, ambapo ingepaswa kuwa zaidi ya 75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida umeendelea kuwa juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Hii ni ishara kwamba miradi ya maendeleo itaendelea kuathirika kutokana na kuchelewa kwa fedha. Hali hii inaweza kuwaingiza Watendaji wa Halmashauri katika migogoro na watoa huduma na Wakandarasi kwa kushindwa kulipa kwa wakati. Ufafanuzi zaidi ya ulinganisho huu umeonekana kwenye jedwali Na. 01 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo 12 ili yaweze kuzingatiwa katika utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti ya ofisi hii kuleta ufanisi na maendeleo. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya kupitia majibu yaliyowasilishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Kamati imeridhishwa na jitihada za Serikali katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zilizobainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuepuka utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hadi Februari, 2018 Halmashauri 21 ziliweza kubuni miradi ya kimkakati, kama vile ujenzi wa stendi za mabasi, masoko na kilimo cha umwagiliaji. Serikali imetenga shilingi bilioni 131.5 katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya Halmashauri hizo.

(ii) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinatumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo hadi kufikia Desemba, 2017 Halmashauri zote 185 sawa na 100% zilikuwa zimeanza kutumia mfumo huu katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo baadhi ya maoni ambayo licha ya kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati

inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Halmashauri ziandae na kutunza takwimu sahihi kuhusu vikundi vya wanawake na vijana vinavyonufaika na 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Aidha, Halmashauri ziongeze kiwango kinachotolewa kwani kiko chini. Hadi mwezi Februari 2018 kiwango kilichotolewa kilikuwa 25.5%. *(Makofi)*

(ii) Halmashauri zishirikiane na MKURABITA kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, ili kuepusha migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

(iii) Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi kwa kuepusha ongezeko la gharama za miradi kutokana na malipo kucheleweshwa. Hadi Februari mwaka huu, 2018 fedha za maendeleo zilizopokelewa na Halmashauri zilikuwa 51% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchmbuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha unaokuja Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha amani na utulivu nchini, kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma, *D by D;*

(ii) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

(iii) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla na kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji katika kilimo na viwanda;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuratibu shughuli za usimamizi wa maendeleo ya elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyingine;

(vi) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka zilizo chini ya ofisi hiyo; na

(vii) Kusimamia maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka kesho, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 6.58. Narudia zinaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 6.58. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.52 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.79 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, shilingi trilioni 4.13 sawa na asilimia 62.8 ni kwa ajili ya Mishahara, na shilingi bilioni 649.3 sawa na asilimia 9.8 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 758.3. Mapato hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 44.7 sawa na asilimia 5.9 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mgawanyo uliopo katika jedwali Na. 03 la Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa uchambuzi huu, makusanyo yote yameongezeka kwa shilingi bilioni 44.7 ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaomalizika. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Aidha, ongezeko hilo litachangia kwa kiasi kikubwa na Halmashauri ambazo

maduhuli yanayotarajiwa kuongezeka kwa shilingi bilioni 48.28 sawa na asilimia 6.5 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la asilimia 5.9 kwa mwaka unaomalizika, makusanyo ya mikoa yamebainika kushuka kwa kiwango kikubwa sana, shilingi bilioni 3.3 sawa na asilimia 96.2 ya lengo lililokusudiwa. Sababu iliyoelezwa mbele ya Kamati ni kwamba Hospitali za Rufaa za Mikoa zimehamishiwa Wizara ya Afya na hivyo makusanyo yote yaliyokuwa yakikusanywa chini ya kifungu hiki chini ya mfumo wa *GoT – HoMIS* kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais,TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa pamoja zinaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trilioni 6.58 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1.79 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shilingi bilioni 12.5 ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu *(TSC).* Kiasi cha Fedha kinachoombwa kuidhinishwa kimeongezeka kwa shilingi bilioni 4.3 sawa na asilimia 0.07 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hilo ni dogo sana ikilinganishwa na ongezeko la mwaka wa fedha 2017/2018 ambalo lilikuwa asilimia 8.52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umebaini kwamba fedha za maendeleo zilizopokelewa, zimeongezeka kwa asilimia 0.91 kutoka shilingi trilioni 1.79 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi shilingi 1.79 katika mwaka wa 2018/2019. Uchambuzi umebaini kwamba bajeti yote pamoja na ile ya maendeleo iliyokuwa ikiongezeka katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, lakini kwa kiwango cha kupungua *(increasing at decreasing rate),* asilimia 12 mwaka 2016/2017, asilimia 8.5 mwaka 2017/2018 na asilimia 0.07 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, uchambuzi ulibaini kwamba bajeti ya Taifa iliongezeka kwa asilimia 2.5 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/2017, wakati bajeti ya TAMISEMI imeongezeka kwa asilimia 0.07 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uchambuzi umebaini kwamba, bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni sawa na asilimia 20.27 ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeendelea kupungua katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kutoka uwiano asilimia 24 mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kiwango hicho cha sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupungua huko, bado ni jambo lisilopingika kwamba Ofisi ya TAMISEMI ndiyo Wizara inayobeba sehemu kubwa ya bajeti ya nchi yetu ikilinganishwa na Wizara nyingine zote. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati ingetamani kuona bajeti ya Ofisi hii inaongezeka mwaka hadi mwaka badala ya kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii ni kama unavyooneshwa katika Jedwali Na. 4 ambalo ni Kiambatisho A cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2017/2018 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(1) Serikali ihimize Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kufidia pengo kubwa la mapato lililotokana na Serikali Kuu kuchukua baadhi ya vyanzo vilivyokuwepo ambavyo vilikuwa tegemezi kwa Halmashauri nchini. Aidha, baadhi ya Halmashauri zilikusanya chini ya asilimia 25 hadi mwezi Februari, 2018. Miongoni mwa Halmashauri hizo ni Mbinga *DC* asilimia 13, Siha *DC* asilimia 20 na Mji wa Kishapu asilimia 23.

(2) Serikali itenge fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa maboma katika Halmashauri nchini ambayo yamejengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Kuendelea kuyaacha majengo hayo bila kuyakamilisha kunawakatisha tamaa wananchi kushiriki katika kazi za maendeleo.

(3) Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza au kuondoa kodi ya taulo za kike *(tampon tax)* ili kuwawezesha watoto wa kike hasa kutoka familia maskini kumudu gharama ya taulo hizo na kuweza kuhudhuria masomo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2008 *UNICEF* ulibaini kwamba asilimia 10 ya watoto wa kike katika Shule za Msingi na Sekondari Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub-Saharan Africa) huacha masomo kwa kushindwa kumudu gharama za taulo za kike. Baadhi ya nchi barani Afrika, kama vile Kenya, Mauritius na Shelisheli zimefanikiwa kupunguza kwa kiwango kikubwa kadhia hii kwa watoto wa kike. *(Makofi)*

(4) Serikali iendeleze ujenzi wa wodi maalum (mama ngojea) ili kuwezesha wajawazito kupata uangalizi wa kitabibu kwa karibu wanapokaribia kujifungua. Hii itasaidia kupunguza vifo vya akinamama na watoto wakati wa kujifungua *(maternity mortality rates)*.

(5) Halmashauri ichangie kikamilifu katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, kwani nyingi zimeshindwa kufanya hivyo. Hadi Februari, 2018 Halmashauri zilichangia shilingi bilioni 1.1 sawa na asilimia 20 ya lengo la shilingi bilioni tano.

(6) Serikali isaidie Mikoa na Halmashauri mpya nchini kupata majengo ya ofisi, watumishi na vitendea kazi na kuboreshewa miundombinu ya barabara ili lengo la kuanzishwa kwake ziweze kutimia. Mfano wa maeneo hayo ni Mikoa ya mipya ya Katavi, Njombe na Songwe. (Makofi)

(7) Ofisi ya Rais, TAMISEMI iendelee kutoa ufafanuzi wa Agizo la Mheshimiwa Rais kuhusu michango katika Shule za Serikali. Bado jambo hili lina mkanganyiko na linaathiri utoaji wa elimu katika baadhi ya maeneo ambayo wazazi waliamua wenyewe kuchangia elimu.

(8) Ofisi ya Rais, TAMISEMI isimamie na kuhakikisha Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri nchini zinazingatia Waraka unaozitaka kupanga ratiba za vikao vya kazi na ushauri vya Mikoa, Wilaya na Halmashauri *(RCC, DCC, Full Council and Finance Committee)* bila kuingilia ratiba ya Vikao vya Bunge. (Makofi)

(9) Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria itakayowezesha kusimamia kikamilifu asilimia kumi (10) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi wanawake na vijana. *(Makofi)*

(10) Serikali isimamie kikamilifu Halmashauri ili kuhakikisha zinaboresha mazingira ya kutolea elimu kwa kujenga miundombinu ya kielimu hasa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo, ambavyo upungufu wake unachangia kuathiri utoaji wa elimu.

(11) Kamati inashauri Serikali kuongeza mgawo wa fedha wa Barabara *(road fund)* kwa ajili ya *TARURA* kutoka asilimia 30 ya sasa hadi asilimia 50.

(12) Ofisi ya Rais, TAMISEMI ihakikishe *TARURA* inashirikisha Halmashauri (Watendaji, Madiwani na Wabunge) katika shughuli inazopanga kutekeleza ili kuondoa mkinzano ambao umeshuhudiwa kwa baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge wote kwa kuchaguliwa tena kuendelea na kazi zao. Hii ni ishara

kwamba utendaji wao katika kipindi kilichopita ulikuwa mzuri na ndiyo maana Wabunge tumekuwa na imani na nyie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa kutuchagua tena mimi na Makamu Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge, ili tuendelee kuongoza Kamati kwa kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ishara kwamba wanatuamini na wako tayari kushirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu. Natambua kwamba cheo siyo fursa, bali ni dhamana. Ukiaminiwa, basi sharti nawe ujiamini. Tunalo deni kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ina mafungu mengi ya bajeti ambayo yanashughulikiwa. Kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwepo wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi hadi kufikia usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza wajibu wao kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu wa pekee, natamani sana kutaja majina yao, lakini kwa sababu ya ufinyu wa muda naomba majina yao yaingie kwenye *record* za *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Said Jafo; Naibu Mawaziri, Mheshimiwa George Kakunda, Mheshimiwa Josephat Kandege kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati ambao umesaidia katika kutekeleza majukumu yetu. Kwa kweli viongozi hawa ni hazina kubwa katika ustawi wa Serikali za Mitaa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Mhandisi Musa Iyombe,

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wakuu wote wa Mikoa, Sekretarieti za Mikoa chini ya ushirikiano wao na Kamati wakati wote wa uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina Sanga; Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Victor Leonard na Ndugu Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Catherine Kitutu, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawashukuru watumishi wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga kwa kuandaa na kutoa vitabu vya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa mwaka wa 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JASSON SAMSON RWEIKIZA (MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya pili ya Kamati ataisoma Makamu wangu, Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante.

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

______________________________

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kuisimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - UUB) pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Aidha, Kifungu cha 7(1) (a), kinafafanua jukumu mahususi la Kamati kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ambayo yanaielekeza Kamati kwa siku zisizozidi saba (7) kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

Kamati ilitekeleza jukumu hilo na kisha kuingia katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya

Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla ya Mafungu Ishirini na Nane (28) yafuatayo:-

(i) Fungu 56: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(ii) Fungu 02: Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);
(iii) Fungu 70 – Mkoa wa Arusha;
(iv) Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam;
(v) Fungu 63 – Mkoa wa Geita;
(vi) Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya;
(vii) Fungu 90 – Mkoa wa Songwe;
(viii) Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa;
(ix) Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara;
(x) Fungu 85 – Mkoa wa Tabora;
(xi) Fungu 84 – Mkoa wa Singida;
(xii) Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro;
(xiii) Fungu 71 – Mkoa wa Pwani;
(xiv) Fungu 36 – Mkoa wa Katavi;
(xv) Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza;
(xvi) Fungu 73 – Mkoa wa Iringa;
(xvii) Fungu 87 – Mkoa wa Kagera;
(xviii) Fungu 54 – Mkoa wa Njombe;
(xix) Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma;
(xx) Fungu 76 – Mkoa wa Lindi;
(xxi) Fungu 95 – Mkoa wa Manyara;
(xxii) Fungu 77 – Mkoa wa Mara;
(xxiii) Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu;
(xxiv) Fungu 86 – Mkoa wa Tanga;
(xxv) Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma;
(xxvi) Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma;
(xxvii) Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga; na
(xxviii) Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro;

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa Taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa baada ya Kamati hii kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha unaoisha pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha unaoanza, Taarifa hii ya Kamati

kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne (4) yafuatayo:-

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Thabo Mvuyelwa Mbeki wakati akielezea sera za taifa hilo na maendeleo yanayoweza kuletwa na Serikali za Mitaa, aliwahi kusema maneno yafuatayo, na hapa ninanukuu;

> *"...the policies might be there but are people benefiting from the policies? You find that in many instances, though the policies exist, they are not having the necessary impact. That is a particular challenge in Local Governmet, because that is where all the services get deliverd."*

Kwa tafsiri isiyo rasmi anachokisema Thabo Mbeki ni kwamba;

> *"Sera zinaweza kuwepo, lakini watu wananufaika nazo? Katika matukio mengi utakuta kwamba, ingawa sera zipo lakini hazina tija. Hiyo ndiyo changamoto haswa katika Serikali za Mitaa, kwa sababu ndiko huduma zinakotolewa."*

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kunukuu maneno hayo ni kutokana na ukweli kwamba, nchi yetu pia ni miongoni mwa Mataifa ambayo yaliamua kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa Madaraka *(Decentralization by Devolution)* kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za Mitaa. Lengo la ugatuaji huo ni

kusogeza huduma kwa wananchi katika ngazi za chini. Hata hivyo, lengo hilo linaposhindwa kutekelezwa ndipo wananchi wanapohoji maana nzima ya kutekeleza dhana ya ugatuaji wa madaraka.

Kwa mantiki hiyo, Serikali inapaswa kuandaa mikakati na mipango thabiti ya uboreshaji wa huduma muhimu za kijamii katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ili kufanikisha azma ya kuboresha maisha ya Watanzania na kuwa na maendeleo endelevu kwa Taifa letu.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,783,206,586,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi hii katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Miradi hiyo ni pamoja na, Programu ya Uimarishaji Miji *(Urban Local Government Authorities Strengthening Program - ULGSP)* ; Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri) pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Ndani kwa njia ya Kieletroniki *(Local Government Revenue Collection Information System - LGRCIS)* kama ifuatavyo:-

#### 2.1.1 Mradi Na. 6405 Programu ya Uimarishaji Miji (ULGSP)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 3,328,956,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha **Fungu 83** – Mkoa wa Shinyanga.

Mradi huu ambao unalenga kuendeleza miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Shinyanga, unahusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa Kilomita 13.1 kwa kiwango cha lami. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu kilomita 4.37 zilikuwa zimekamilika, hii ikiwa ni sawa na asilimia 33.4 ya utekelezaji wa mradi.

Aidha, mradi utahusisha **ujenzi wa** mifereji rafiki kwa ajili ya maji taka, ujenzi wa njia za waenda kwa miguu, uwekezaji wa taa na alama za barabarani.

### 2.1.2 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects "Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana".

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 471,452,580/=** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha **Fungu 47** - Mkoa wa Simiyu. Mradi huu ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuwawezesha Kiuchumi Wanawake na Vijana, kupitia asilimia (10%) ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nchini. Kupitia utaratibu huu Wanawake na Vijana wamejengewa uwezo wa kubuni miradi na kupata mitaji ya kuitekeleza na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Kamati ilitaka kujiridhisha na utekelezaji wa Mradi huu na hivyo ilitembelea Kikundi cha Vijana ambacho kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kimeanzisha Kiwanda cha Chaki kilichopo Maswa Mjini. Katika Kiwanda hicho, Kamati ilipata fursa ya kujionea shughuli za uzalishaji na ufungashaji *(production and packaging)*.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba katika mradi huo wa ubia ambao una mtaji wa thamani ya **Shilingi Milioni 100**, Kikundi hicho cha vijana kinamiliki asilimia 40 ya hisa na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inamiliki asilimia 60.

Vijana hao walianza na mtaji wa **Shilingi 1,000,000** kabla ya kupata fedha kutoka mfuko wa uwezeshaji wa Vijana wenye thamani ya **Shilingi Milioni 30**.

Aidha, mradi huo umeingizwa katika kundi la miradi ya kimkakati ya Halmashauri na umetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 4** kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanda hicho na kuanzisha uzalishaji wa bidhaa nyingine za kimkakati kama vile vifaa tiba na vifaa vya ujenzi.

### 2.1.3 Mradi Na. 4946 – Local Government Own Source Project (Mfumo wa Ukusanyaji Mapato kwa njia ya Kieletroniki - *LGRCIS*)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha **Fungu 85** - Mkoa wa Tabora. Lengo la mradi huu ni kuiwezesha Serikali kuongeza mapato kwa kuboresha njia na Mfumo wa ukusanyaji wa mapato *(revenue collection system)*.

Kupitia mradi huu Serikali imeachana na matumizi ya vitabu na Mawakala katika ukusanyaji wa mapato, jambo ambalo limewezesha kuepuka upotevu mkubwa wa mapato kutokana na upotevu wa kumbukumbu na mawakala wasio waaminifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi na kasi ya kuanzisha Mfumo huu ambao sasa unatumika katika Halmashauri zote 185 nchini. Mfumo wa ukusanyaji mapato ya ndani kwa njia ya kielektroniki *"Local Government Revenue Collection Information System"* ulianzishwa rasmi katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha (2017/2018) Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilipanga kukamilisha lengo la ununuzi wa mashine 85 za kukusanyia mapato (POS). Hadi wakati Kamati inakagua utekelezaji wa Mfumo huo tayari Halmashauri ilikuwa imeishanunua mashine 59, sawa na asilimia 69.4 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na matumizi ya mfumo huu Kamati iliweza kutembelea na kukagua maeneo ya biashara katika Soko kuu la Tabora lenye jumla ya mashine 9

za kukusanyia mapato *(POS),* na Stendi ya Mabasi yaendayo Mikoani ambayo inatumia mashine mbili tu za POS.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hiyo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tukufu juu ya mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Mradi Na. 6405 Program ya Uimarishaji Miji (ULGSP)

**Mheshimiwa Spika,** katika Halmashauri ya Shinyanga ambako Kamati iliweza kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu wa kuimarisha miundombinu, ukaguzi huo ulibaini mambo yafuatayo:-

**(a) Mafanikio;**

(i) Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami katikati ya Mji wa Shinyanga;

(ii) Kuongezeka kwa biashara na uwekezaji katika maeneo ya kati ya Mji kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara; na

(iii) Kuongezeka thamani kwa maeneo ya makazi yaliyo jirani na barabara zinazojengwa.

**(b) Changamoto;**

(i) Kasoro za Mkataba kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na Mkandarasi, zinachelewesha mradi huo na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji;

(ii) Usanifu wa awali *(feasibility study)* wa mradi haukuzingatia mahitaji halisi ya wakazi wa maeneo mradi unapotekelezwa;

(iii) Mradi kutekelezwa kwa gharama kubwa ikilinganishwa na ubora wa kazi;

(iv) Mifereji (mifereji rafiki) ya maji ambayo itakuwa inajaa udongo kwa urahisi na hivyo kushindwa kusafirisha maji taka kutokana na kujengwa chini ya kiwango;

(v) Halmashauri kukosa wahandisi wa ujenzi na hivyo kukosa usimamizi madhubuti wa miradi ya barabara;

(vi) Ushirikiano hafifu baina ya Halmashauri na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (*TARURA)*; na

(vii) Uwepo wa viashiria vya rushwa katika utoaji wa zabuni za ujenzi wa mradi huo.

### 2.2.2 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.(Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana)

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi uliofanywa na Kamati katika mradi huu uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto.

**(a) Mafanikio;**

(i) Ajira za moja kwa moja na fursa ya kumiliki hisa kwa Vijana ambapo Vijana 28 wameajiriwa na kati ya hao 6 wanamiliki hisa katika kiwanda hicho;

(iii) Mradi huu ni miongoni mwa vyanzo vya mapato vya Halmashauri;

(iv) Kiwanda hiki kimeweza kusambaza chaki katika Mikoa Nane (8) ya Tanzania Bara na Zanzibar na hivyo kupunguza matumizi ya chaki kutoka nje;

(v) Mradi huo umekuwa chachu ya Halmashauri nyingi kuanzisha Viwanda vya aina hii kutokana na kuwa sehemu ya mafunzo.

**(j) Changamoto;**

(i) Teknolojia duni ambayo inafanya Kiwanda hicho kuzalisha chini ya kiwango;

(ii) Kukosekana kwa malighafi mkoani Simiyu, na hivyo kulazimika kuzifuata mkoani Singida; na

(iii) Mazingira ya ushindani yasiyo sawa yanayosababishwa na uingizaji wa chaki kutoka nje ya nchi.

2.2.3 **Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects (Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwa njia ya Kielektroniki).**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa katika Halmshauri zote nchini, lakini Kamati iliweza kutembelea Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na kubaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

**(a) Mafanikio:-**

(i) Mfumo wa *LGRCIS* umerahisisha utunzaji wa kumbukumu na hivyo kupunguza upotevu wa taarifa muhimu za hesabu;

(ii) Kupunguza gharama za ukusanyaji mapato; na

(iii) Mfumo umeongeza uwazi na hivyo kuiwezesha Serikali kudhibiti ubadhirifu wa mapato uliokuwa unasababishwa na Mawakala wasio waaminifu.

**(b) Changamoto:-**

(i) Matatizo ya mtandao kukata wakati wa kutoa huduma kwa wateja, hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato;

(ii) Mfumo wa *LGRCIS* kushindwa kuzungumza na Mifumo ya Benki na hivyo kuzifanya Benki kushindwa kuingiza malipo kwenye Mfumo kwa njia ya CHEQUE na TISS;

(iii) Kukosekana kwa Wakala wa Benki kwa ajili ya makusanyo ya mapato ya Halmashauri; na

(iv) Mfumo kushindwa kudhibiti taarifa za Halmashauri moja kuingiliana na taarifa za Halmashauri nyingine.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Tabora, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na inapenda kuyatolea maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Hazina itoe fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kuendelea kuwakosesha wananchi huduma zilizokusudiwa;

(ii) Wanasheria wa Halmashauri wajengewe uwezo katika eneo la Sheria za Mikataba *(law of contracts)* ili kuziwezesha Halmashauri kuingia mikataba yenye manufaa kwa Taifa na kuepukana na ubadhilifu;

(iii) Ushirikishwaji mdogo wa Wananchi katika uibuaji na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo *(feasibility study)* umeendelea kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo, kutokana na Wananchi kujiona kwamba siyo sehemu ya miradi hiyo;

(iv) Kukosekana kwa programu endelevu ya elimu ya ujasiriamali na uwezeshaji kwa Vijana kumefanya idadi kubwa ya vikundi hivyo vishindwe kutumia vizuri fedha za mikopo;

(v) Urasimu *(cumbersome procedures)* usio wa lazima Serikalini umeendelea kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Mfano, utaratibu wa watoa huduma na wakandarasi kuwasilisha madai kwa njia ya cheti *(certificates)* umekuwa ukichelewesha malipo na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi;

(vi) Kukosa umakini katika usanifu wa awali *(feasibility study)* wa Miradi ya Maendeleo kunaathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama; na

(vii) Mfumo wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa nja ya Kieletroniki *(LGRCIS)* umeonesha mafanikio makubwa kwa kuongeza na kudhibiti mapato ya Halmashauri nchini. Hata hivyo, mfumo huu unahitaji maboresho ili kuondoa dosari zilizobainika.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

Njia zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati vikao vya Kamati.

Kwa ufafanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **22,766,063,908** kutoka vyanzo vya ndani. Kwa Fungu 56 mapato yalikadiriwa kukusanywa kutoka kwenye mauzo ya vifaa chakavu na zabuni. Aidha, kwa upande wa Taasisi mapato yalitarajiwa kutokana na tozo mbalimbali, ukusanyaji wa madeni, nauli za mabasi, ada za Wanafunzi katika Vyuo, ushuru wa mauzo ya bidhaa mbalimbali, na kodi ya pango kwa wapangaji wa majengo ya Taasisi.

Hadi kufikia Februari, 2018 jumla ya **Shilingi 9,951,491,965.88** zilikuwa zimekusanywa na Fungu 56, kiasi ambacho ni sawa na **asilimia 43.7** ya mapato yaliyotarajiwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Kamati ilitaka kujua ni kwanini kumekuwa na makusanyo hafifu ya maduhuli, na sababu zilizotolewa ni pamoja na:-

(i) Mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vya Ofisi;

(ii) Halmashauri nyingi kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;

(iii) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kushindwa kupata **Shilingi Bilioni 1.2** ilizotarajia kuzipata kutoka CRDB;

(iv) Kukosekana kwa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka Fedha 2016/2017 ambacho kilikuwa ni asilimia 28.13. Ingawa kiwango kilichokusanywa kimeshindwa kufikia angalau asilimia 70 ambayo ilipaswa kuwa imefikiwa katika robo ya tatu, bado ni kikubwa hasa kwa kuzingatia

kwamba malengo yaliyowekwa yalikuwa ni makubwa zaidi ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha uliotangulia.

Aidha, Kamati inatia shaka iwapo kwa kipindi kilichobaki malengo ya makusanyo yatafikiwa. Hii inatoa taswira kwamba bado Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijaweza kuwa na makadirio sahihi kuhusu kiasi cha mapato kinachotakiwa kukusanywa au kuna uzembe wa ukusanyaji wa mapato. Tafsiri ya mtazamo huu ni kwamba, utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Ofisi hii kwa kutegemea fedha za ndani utaendelea kusuasua.

Kamati inaendelea kushauri kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI izingatie makadirio halisi ya makusanyo kutokana na vyanzo vilivyopo ili kuweza kuwa na makusanyo halisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mikoa na Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Februari, 2018 makusanyo yalikuwa ni **shilingi 347,186,363,928,** kiasi ambacho ni sawa na asilimia 50 ya lengo.

Ingawa kiasi hiki kiko chini ya lengo la angalau asilimia 70 hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha, bado kiwango cha makusanyo katika Serikali za Mitaa kimeonekana kuwa kikubwa. Sababu inaweza kuwa ni kutokana na Halmashauri kuwa na vyanzo vingi vya makusanyo na wingi wa watu ikilinganishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Taasisi zake.

### 3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba:-

(i) Fedha zinazotolewa ni kidogo ikilinganishwa na Mpango wa upatikanaji fedha (*cash flow plan*) uliowekwa;

(ii) Kiasi cha Fedha kinachotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni kikubwa ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na

(iii) Fedha hazipatikani kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 245,177,039,868.65/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 53** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kilichopatikana katika kipindi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 ambapo ilikuwa ni asilimia 57.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia februari, 2018 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **Shilingi 29,072,505,060.65,** sawa na asilimia 69 ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa kulinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2016/17 kiasi hicho kimeongezeka kwa asilimia 5 kutoka asilimia 64.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 216,104,534,808.00** kutoka Hazina, sawa na asilimia 52 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika kipindi hicho. Kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 4 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa

katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/17 ambacho kilifikia asilimia 56 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kwa wastani wa upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) katika Mwaka wa Fedha 2017/18 ulikuwa ni **asilimia 60.5**, kiwango ambacho ni sawa na kilichoshuhudiwa katika Mwaka wa Fedha 2016/17.

Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, bado upatikanaji wa fedha umeshindwa kufikia lengo la angalau asilimia 25 kwa kila robo ya mwaka wa fedha, ambapo ingepaswa kuwa zaidi ya asilimia 70.

Aidha, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida umeendelea kuwa juu ikilinganishwa na fedha zinazotolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hii inaashiria kwamba miradi ya maendeleo itaendelea kuathirika kutokana na kuchelewa kwa fedha. Na hali hiyo, inaweza kuwaingiza Watendaji wa Halmashauri katika migogoro na Watoa huduma na Wakandarasi kutokana na kushindwa kulipwa kwa wakati, baada ya kuwa wamekamilisha kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa fedha iliyoidhishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na fedha iliyopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2018, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Ufafanuzi zaidi wa ulinganisho huu umeoneshwa kupitia **Jedwali Na. 01**

**Jedwali Na.01:** Bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na Fedha zilizopatikana hadi Februari, 2018.

| Mgawanyo wa Bajeti | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 | Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2018 | Asilimia ya Kiasi kilichopokelewa hadi Februari,2018 |
|---|---|---|---|
| OC | 23,810,002,200.00 | 14,944,710,887.80 | 63 |
| Mishahara | 18,347,579,957.00 | 14,127,794,172.85 | 69 |
| Maendeleo | 417,256,688,000.00 | 216,104,534,808.00 | 52 |
| **Jumla** | **459,414,270,157.00** | **245,177,039,868.65** | **53** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2017/2018)

### 3.1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika mapitio na uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo kumi na mbili (12) ili yaweze kuzingatiwa katika utekelezaji vipaumbele vya bajeti ya Ofisi hii kuleta ufanisi na maendeleo;

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati baada ya kupitia majibu yaliyowasilishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeridhishwa na jitihada za Serikali katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zilizobainishwa.

Kuzingatiwa kwa maoni na ushauri wa Kamati kumechangia uboreshaji wa huduma za msingi kwa maendeleo ya Jamii. Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanyia kazi ushauri kwa baadhi ya maeneo ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na:-

(i) Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuepuka utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Ofisi ya Rais TAMISEMI imezielekeza Halmashauri kubuni miradi ya kimkakati kwa lengo la kuongeza mapato ya ndani. Hadi kufikia Februari, 2018 Halmashauri 21 ziliweza kubuni miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa stendi za mabasi, masoko, maeneo ya maegesho, machinjio na kilimo cha umwagiliaji ambayo imekidhi vigezo vya kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi **Bilioni 131.5** katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya Halmashauri hizo;

(ii) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinatumia Mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani *(Local Governemnt Revenue Collection Information System -*

*LGRCIS)*, ambapo hadi kufikia Disemba, 2017 Halmashauri zote 185 sawa na asilimia 100 zilikuwa zimeanza kutumia

Mfumo huu katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, karibu kila Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine za kukusanyia mapato (POS) kwa lengo la kuimarisha mfumo huo.

**Mheshimiwa Spika,** yapo baadhi ya maoni ambayo licha ya kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na:-

(i) Kuhakikisha Halmashauri zinaandaa na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na namba vikundi vya Wanawake na Vijana, vinavyopokea na kurejesha fedha zinazotokana na Asilimia kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri;

Aidha, Halmashauri zitekeleze kwa ukamilifu utengaji wa fedha hizo na kuzipeleka kwa wahusika. Taarifa zinaonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 utengaji wa fedha hizo ulikuwa ni asilimia 25.5, kiwango ambacho kiko chini sana. Ni ushauri wa Kamati kwamba, jambo hili linahitaji msisitizo wa Serikali;

(ii) Halmashauri kushirikiana na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kuandaa mpango wa matumizi bora ya Ardhi, kwa kuainisha maeneo ya Kilimo, Ufugaji na matumizi mengine, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji; na

(iii) Serikali kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati ili kuwezesha Halmashauri kulipa madeni ya Watoa huduma na Wakandarasi kwa wakati na hivyo kuepusha ongezeko la gharama katika miradi inayotekelezwa. Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Halmashauri kwa ajili ya maendeleo (asilimia 51) kinaashiria

kwamba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri utaendelea kuathirika.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/ 2018

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia yafuatayo :-

(i) Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa;

(ii) Vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; na

(iii) Malengo Endelevu ya Maendeleo *(Sustainable Development Goals*); na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha unaokuja 2018/2019, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha amani na utulivu nchini, kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa Wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

(ii) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi (Core Business) ya kila Taasisi yaliyoainishwa kwenye Mipango Mikakati yao;

(iv) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa Uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya Biashara na Uwekezaji hasa katika Kilimo na Viwanda;

(v) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali, programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyingine;

(vii) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuendeleza Rasilimali Watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi;

(viii) Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na

(ix) Kusimamia maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6,582,946, 851,733/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

**4,522,965,704,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1,799,436,057,500/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,134,200,811,930/=** sawa na asilimia 62.8 ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 649,309,982,303/=** sawa na asilimia 9.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. **Jedwali Na. 02** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Jedwali Na. 02** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 .

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2018/2019)

## 4.2 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 758,362,711,799.** Mapato hayo yameongezeka kwa **Shilingi 44,778,191,187** sawa na **asilimia 5.9** ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mgawanyo utakaooneshwa katika **Jedwali Na. 03** hapo chini.

**Mheshimiwa Spika,** makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na mishahara. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

**Jedwali Na.3 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya ndani**

| Ofisi/ Taasisi | Bajeti 2017/18 | Bajeti 2018/19 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| OR – TAMISEMI na Taasisi | 22,766,063,908 | 22,643,519,091.00 | 122,544,817 | 0.53 |
| Mikoa | 3,511,759,704 | 130,563,708.00 | 3,381,195,996 | 96.2 |
| Halmashauri | 687,306,661,000 | 735,588,629,000.00 | 48,281,968,000 | 6.5 |
| **Jumla** | 713,584,520,612 | 758,362,711,799.00 | 44,778,191,187 | **5.9** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (2018/2019)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa uchambuzi huu makusanyo yote yameongezeka kwa **Shilingi 44,778,191,187** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaomalizika. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Aidha, ongezeko hilo linarajiwa kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri [illegible] a kukusanywa [illegible]**1,968,000** sawa [illegible] ya Halmashauri.

Nimtazamo wa Kamati kwamba, huenda sababu ya ongezeko hilo ni kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa [illegible] e za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, ni wazi kwamba watu wengi na vyanzo vingi vya mapato vinapatikana katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kubainika kwa ongezeko la jumla la **asilimia 5.9** ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka unaomalizika, makusanyo ya Mikoa yamebainika kushuka kwa kiwango cha kutisha cha asilimia 96.2 (Shilingi 3,381,195,996).

Kamati ilipotaka maelezo ya kwanini mapato ya Mikoa yameshuka kwa kiwango hicho, ilielezwa kwamba

sababu ni Hospitali za Rufaa za Mikoa kuhamishiwa Wizara ya Afya na hivyo makusanyo yote yaliyokuwa yakikusanywa kwa mfumo wa GoT – HoMIS kuondoka.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa pamoja zinaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 6, 582,946, 851,733** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,522,965,704,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,799,436,057,500** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha hizo zinazoombwa kuidhinishwa, **Shilingi 12, 515,260,520** ni kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Fedha kinachoombwa kuidhinishwa kimeongezeka kwa **Shilingi 4,319,381,367** sawa na asilimia 0.07 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018. Hata hivyo, ongezeko la Mwaka huu ni dogo sana ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/18 ambapo ongezeko lilikuwa asilimia 8.52%.

Uchambuzi umebaini kwamba, katika fedha za Miradi ya Maendeleo, kuna ongezeko la asilimia 0.91 kutoka **Shilingi 1,783,206,586,000** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi **Shilingi 1,799,436,057,500** katika Mwaka wa fedha 2018/2019.

Uchambuzi umebaini kwamba, ongezeko la bajeti yote pamoja na ile ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitatu limekuwa ni likiongezeka kwa kupungua (increasing at decreasing rate). i.e. kutoka asilimia 12 mwaka 2016/17, asilimia 8.5 mwaka 2017/18 na asilimia 0.07 kwa mwaka wa fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika,** katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 uchambuzi ulibaini kwamba, wakati bajeti ya Taifa ikiongezeka kwa asilimia 2.53 kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2016/17, bajeti ya TAMISEMI katika kipindi hicho imeongezeka kwa asilimia 0.07.

Aidha, uchambuzi umebaini zaidi kwamba, bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na **asilimia 20.27** ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeendelea kupungua katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kutoka Mwaka wa Fedha 2015/16 ambapo uwiano ulikuwa **asilimia 24** hadi kiwango hicho cha sasa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kupungua huko, bado ni jambo lisilopingika kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo Wizara inayobeba sehemu kubwa ya bajeti ya nchi yetu ikilinganishwa na Wizara nyingine, kutokana na kusimamia kila Sekta katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati ingetamani kuona Ofisi hii inaongezewa fedha katika bajeti yake.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama unavyooneshwa katika **Jedwali Na.4** ambalo ni Kiambatisho "**A"** cha Taarifa hii.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya Maendeleo na kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihimize Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kufidia pengo kubwa la mapato lililotokana na Serikali Kuu kuchukua baadhi ya vyanzo vilivyokuwa tegemezi kwa Halmashuri nchini kama vile kodi ya majengo *(property*

*tax)*. Kamati imebani kushuka kwa kiwango cha kutisha kwa makusanyo ya ndani ya kwa baadhi ya Halmashauri ambapo hadi mwezi Februari, 2018 (ikiwa ni robo ya tatu) Halmashauri hizo zilishindwa kufikia asilimia 25 ya makusanyo. Mingoni mwa Halmashauri hizo ni Mbinga DC (13%), Siha DC (20%) na Mji Kishapu (23%).

(ii) Serikali itenge fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa maboma, katika Halmashauri nchini ambayo yamejengwa kwa kushirikisha nguvu za Wananchi. Kuendelea kuyaacha majengo hayo bila kuyakamilisha kunawakatisha tamaa Wananchi kushiriki katika kazi za maendeleo, na kuwafanya waendelee kukosa huduma muhimu za kijamii ambazo wanazitegemea.

(iii) Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza au kuondoa kodi ya taulo za kike *(tampon tax)* ili kuwawezesha Watoto wa Kike hasa kutoka familia maskini kumudu gharama ya taulo hizo na kuweza kuhudhuria masomo kikamilifu.

Aidha, Serikali iweke mkakati wa kuanzisha viwanda vya ndani kwa ajili ya kuzalisha taulo hizo *(tampons)* kutokana na fursa ya malighafi ya pamba inayozalishwa kwa wingi nchini.

Utafiti wa Shirika la Umoja Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) mwaka 2008 ulibaini asilimia 10 ya watoto wa kike wanaodahiliwa katika elimu ya msingi na sekondari katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara *(Sub Saharan Countries)* huacha masomo kwa sababu ya kukosa au kushindwa kumudu gharama za taulo za kike *(pads/ tampons).*

Aidha, utafiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ulibaini kwamba, kutokana na kushindwa kumudu gharama za taulo za kike, Wanafunzi wa kike wamekuwa wakikumbwa na athari za kushindwa kuhudhuria masomo kwa siku kati ya 3 hadi 5 kwa mwezi, kupata mimba za utotoni na ufaulu hafifu.

Baadhi ya nchi barani Afrika, kama vile Kenya, Mauritius na Shelisheli zimefanikiwa kupunguza kwa kiwango kikubwa kadhia hiyo kwa watoto wa kike;

(iv) Serikali iendeleze ujenzi wa wodi maalum (mama ngojea) ili kuwezesha Wajawazito wanaotoka mbali na maeneo ya huduma za afya, kupata uangalizi wa karibu kutoka kwa Wataalam wa afya wanapokaribia kujifungua. Hatua hiyo itasaidia kupunguza vifo vya Mama na Mtoto wakati wa kujifungua *(maternity motarity deaths)* ambavyo huchangiwa na kukosa huduma za msingi za afya kama vile upasuaji *(operation)*.

(v) Serikali ihimize Halmashauri nchini kuchangia kikamilifu katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, kwani nyingi zimeshindwa kufanya hivyo. Hadi kufikia Februari, 2018 Halmashauri zilikuwa zimechangia **Shilingi Bilioni 1.11** tu sawa na asilimia 20 ya makadirio ya kiasi kilichopaswa kuchangiwa. Hali hiyo inakwamisha bodi hiyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

(vi) Serikali isaidie Mikoa na Halmashauri mpya nchini kupata majengo ya Ofisi, Watumishi na vitendea kazi na kuboreshewa miundomibu ya barabara ili lengo la kuanzishwa kwake liweze kufikiwa. Ni wazi kuwa maeneo hayo mapya ya utawala yalianzishwa kwa lengo la kusogeza huduma za kijamii karibu na Wananchi na kuhamasisha maendeleo katika maeneo husika. Mfano wa maeneo hayo ni Mikoa ya mipya ya Katavi, Njombe na Songwe;

(vii) Ofisi ya Rais, TAMISEMI iendelee kutoa ufafanunuzi wa Agizo la Mheshimiwa Rais kuhusu michango ya Wazazi katika Shule za Serikali za Msingi na Sekondari nchini. Bado jambo hili linaendelea kuleta mkanganyiko miongoni mwa Wazazi na Walimu, na linaathiri utoaji wa elimu katika baadhi ya maeneo ambayo Wazazi walikuwa wameamua wenyewe kuchangia elimu.

(viii) Ofisi ya Rais, TAMISEMI isimamie na kuhakikisha Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri nchini zinazingatia

kikamilifu Waraka unaozitaka kuzingatia ushiriki wa Wabunge katika vikao vya kazi na ushauri vya Mkoa, Wilaya na Halmashauri *(RCC, DCC, Full Council and Finance Committee)*. Waraka huo unazitaka Sekretarieti hizo kupanga ratiba za vikao hivyo bila kuingiliana na Vikao vya Bunge. Aidha, hatua kali zichukuliwe dhidi ya watakaoendelea kukiuka masharti ya waraka huo;

(ix) Serikali ichukue hatua za makusudi ili kukabili tatizo la ucheleweshaji na upatikanji wa fedha kutoka Hazina *(disbursement)*, kwani unaathiri mtiririko wa bajeti *(cash flow plan)* na hivyo kukwamisha utekelezaji wa malengo na mipango mingi ya Serikali. Aidha, Serikali iweke vipaumbele vichache ambavyo itamudu kuvitekeleza kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti uliopo;

(x) Serikali iendelee kuzisisitiza Halmashauri kutenga asilimia kumi (10%) ya makusanyo yake ya ndani kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake na Vijana. Aidha, hatua kali zichukuliwe kwa Halmashauri ambazo zimeendelea kupuuza agizo hilo.

(xi) Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Muswada wa kusudio la kutunga Sheria itakayowezesha kusimamia kikamilifu utengaji, utoaji na urejeshaji wa fedha zinazotokana na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake na Vijana;

(xii) Serikali isimamie kikamilifu Halmashauri ili kuhakikisha zinaboresha mazingira ya kutolea elimu kwa kujenga miundombinu ya kielimu hasa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo, ambayo upungufu wake unachangia kuathiri utoaji wa elimu. Ni aibu katika karne hii Walimu na Wanafunzi kuchangia matundu ya vyoo. Aidha, uchache wa matundu ya vyoo unachangia watoto kuacha masomo *(drop outs)* kutokana na kushindwa kujisitiri wanapokuwa katika siku zao;

(xiii) Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuanzisha Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kwani utasaidia sana kuboresha na kuendeleza miundombinu ya barabara katika Miji na Vijiji. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya fedha kidogo inayopelekwa kwa Wakala hii. Kamati inashauri mgawo wa fedha za Mfuko wa Barabara (road fund) kwa ajili ya TARURA uongezeke kutoka asilimia 30 ya sasa hadi 50.

(xiv) Serikali iiwezeshe TARURA kuajiri Watumishi wa kutosha hasa wa kada za uhandisi ili kuondoa changamoto ya Wakala kuchukua Watumishi wa Halmashauri na hivyo kuathiri utendaji wa Halmashauri hizo.

(xv) Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe TARURA inashirikisha Halmashauri (Watendaji, Madiwani na Wabunge) katika shughuli inazopanga kutekeleza ili kuondoa mkinzano ambao umeshuhudiwa kwa baadhi ya Halmashauri nchini kutoelewa shughuli zinazopangwa kutekelezwa na Wakala huo katika maeneo yao.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge wote kwa kuchaguliwa tena kuendelea na nafasi zao. Hii ni ishara kwamba, utendaji wao katika kipindi kilichopita ulikuwa mzuri na ndiyo umewapa imani Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwachagua tena.

Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati kwa kutuchagua tena mimi na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Mwanne Ismail Mchemba (Mb) ili tuendelee kuongoza Kamati kwa kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge. Hii ni ishara kwamba, wanatuamini na wako tayari kushirikiana nasi katika kutekeleza shughuli za Kamati. Ninatambua kwamba, “cheo sio fursa bali ni dhamana” na “ukiaminiwa basi nawe unapaswa kujiamini.” Tunalo deni kwa Wajumbe, na njia

pekee ya kulipa deni hilo ni kuenzi imani na ushirikiano wao kwetu, kwa kuwatumikia kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwingine hadi jioni. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza wajibu wao kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia Wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim,Mb
7. Mhe.Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
8. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate,Mb
9. Mhe. Mwatum Dau Haji,Mb
10. Mhe. Saada Mkuya Salum,Mb
11. Mhe. Salum Khamis Salum,Mb
12. Mhe. Venance Methusela Mwamoto,Mb
13. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb
14. Mhe. Anna Joram Mhagama, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb

22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
25. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati napenda kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Seleman Said Jafo (Mb) kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha kwa Kamati hii ambao umechangia kwa sehemu kubwa kwa Kamati kutekeleza shughuli zake. Yeye pamoja na Naibu Mawaziri wake, Mhe. George Joseph Kakunda (Mb) na Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) ni hazina kubwa katika ustawi wa Serikali za Mitaa na maendeleo ya Taifa hili.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Mhandisi Musa Iyombe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa utendaji wao uliotukuka katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, na kwa uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Catherine Kitutu, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii. Vilevile, nawashukuru Watumishi

wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga, kwa kuandaa na kutoa Vitabu vya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**

11 Aprili, 2018

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, uje kuwasilisha taarifa ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Karibu Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kifungu 117(11) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Ili kukidhi masharti ya kifungu cha 6(4) pamoja na kifungu cha 7(1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya uchambuzi wa bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejikita katika maeneo manne yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati; Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa miradi ya maendeleo iliyolengwa kukaguliwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa shilingi bilioni 390.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu matano kama yanavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea miradi ya *TASAF*, MKURABITA na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania. Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi uliotembelewa ni Mradi Na. 6220 – *Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF).* Mradi huo ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 378.6 na kutekelezwa chini ya Kifungu cha 1003 cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ambao unatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa, Tanzania Bara na Wilaya, zote za Zanzibar uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji ambayo imejikita kusaidia kaya maskini za Watanzania kujimudu na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu awamu ya tatu ya *TASAF* ianze, takriban Watanzania milioni tano wameandikishwa na wananufaika na ruzuku. Jumla ya shilingi bilioni 147.6 zilitolewa kama ruzuku kwa wananchi hao. Aidha, mpango huo umetoa ajira za muda kwa kaya za walengwa 288,385 kupitia miradi 3,682 zenye thamani ya shilling bilioni 13.3 katika Halmashauri 42 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilitembelea kukagua Mitaa ya Nyalikungu na Mnadani na Kijiji cha Shanwa, Wilayani Maswa, Mkoani Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.5 na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 kiitwacho *Policy and Planning* cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Lengo la Mpango huu ni kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendelezaji wa biashara unaotambuliwa na kukubalika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA imewajengea wakulima 589 na viongozi 89 uwezo wa kutumia Hakimiliki za Kimila ili waweze kupata mitaji katika benki na taasisi nyingine za kifedha katika Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Mpwapwa na Serengeti. Aidha, wafanyabiashara 870 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji wa biashara katika Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar jumla ya wafanyabiashara 100 katika Wilaya za Kusini, Unguja 50 na Micheweni, Pemba 50 wamepata mafunzo ya

urasimishaji na uendeshaji wa biashara na 10 tayari wamesajili majina ya biashara na kupata leseni za biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, MKURABITA kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar, imeanza kufanya utafiti kuhusu sekta isiyo rasmi kwa lengo la kubaini ukubwa na thamani ya sekta hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Msalala, Mkoani Shinyanga kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji ya MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Aidha, Chuo kinajihusisha na utafiti wa kutoa ushauri wa kitaalam na kutoa machapisho mbalimbali ya kitaalam kwenye Utumishi wa Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo kupitia Kampasi sita zilizoko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Iringa, Tanga na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitembelea Kampasi ya Tabora ambayo ilikuwa ikitekeleza ukarabati wa jengo la Shaban Robert.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi; kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (*Support to Tanzania Social Action Fund - TASAF),* katika Wilaya ya Maswa, Kamati ilitembelea Kijiji cha Shanwa ambacho kina jumla ya Kaya 248 zinazonufaika na utaratibu wa kunusuru kaya maskini. Idadi hiyo ya kaya imepungua kwa asilimia 19 ikilinganishwa na kaya 308 zilizokuwa zinanufaika awali, kabla ya zoezi la uhakiki na kuondoa kaya zisizokuwa na sifa. Hizo zimepelekea jumla ya shilingi bilioni 8.8 kutokana na awamu ya 16 ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TASAF* imeshiriki katika kuboresha elimu ya sekondari kwa kuchangia ujenzi wa

vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyalikungu kwa kutoa jumla ya shilingi milioni 29.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia utaratibu wa kuwezesha mahudhurio ya shule kwa watoto wanaotokana na kaya maskini, Mfuko huo umewezesha wanafunzi 49 wa Kidato cha Kwanza na hadi cha nne kushiriki kikamilifu katika masomo yao ya sekondari, kulipia gharama za mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishuhudia namna ambavyo baadhi ya wanufaika wa mpango wametumia fedha za ruzuku kujenga na kuboresha makazi yao. Miongoni mwa wanufaika hao ni Bibi Monica Katabi Gwilasa (miaka 60), ambaye ametumia ruzuku kama chachu ya kujenga nyumba ya tofali ya vyumba vitatu na kuezeka kwa bati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto kadhaa ambazo zinaonekana kama kwenye ukurasa wa 11 hadi wa 13 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Msalala ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 13 na wa 15 wa Taarifa ya Kamati. Aidha, jedwali Na. 01 linatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara yake kwenye kampasi ya Tabora Kamati ilibaini yafuatayo: Chuo cha Utumishi wa Umma kinamiliki maeneo yake na kipo katika hatua ya mwisho ya kupata Hatimiliki. Hii ni tofauti na kampasi nyingine kama vile Mbeya na Tanga ambazo zinatumia majengo ya kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo kina upungufu wa watumishi wa kudumu, vitendea kazi na vyumba vya madarasa. Uchakavu wa miundombinu ya maji na umeme

umeongeza gharama za uendeshaji. Mwitikio hafifu kutoka Wizara na Taasisi za Umma katika kutumia huduma ya chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi na maendeleo, maoni ya Kamati ni kwamba mpango wa ruzuku kwa kaya maskini utafanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zitatumika kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za wafadhili. Bado mchango wa Serikali ni mdogo, kwani tangu kuanza kwa mpango huu katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia shilingi bilioni 4.3 tu, kati ya zaidi ya shilingi bilioni 63.5 iliyopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 6.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini wanaweza kujikwamua kiuchumi iwapo watatumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi kama vile biashara, ufugaji au kilimo. Iwapo *TASAF* itahakiki na kusajili kaya maskini zilizosahaulika katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, itasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya vituo na zahanati binafsi kukataa kuwahudumia wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii *(CHF)* kunakatisha tamaa wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini ambao waliamua kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujiunga na *CHF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuhakiki na kuondoa watu wasio na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya masikini litafanikiwa iwapo litashirikisha wanajamii, viongozi wa Serikali za Mitaa na kuzingatia haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti finyu kwa MKURABITA inaathiri utendaji wa mpango huo, hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki na Taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu hadhi ya hati za hakimiliki za Kimila kutumia kama dhamana ya mikopo, zitatoa mikopo kwa wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zikipatiwa wataalam wa ardhi, zitasaidia MKURABITA kuhakikisha zoezi la kurasimisha ardhi na kutoa hati za kumiliki watahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Mfuko wa Kujitegemea wa Rais utatengewa fedha za kutosha, utaweza kufikisha huduma zake katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kunufaisha wanawake, vijana na wengine zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Tabora kitapatiwa watumishi wa kudumu na vitendea kazi kitaboresha huduma na kupunguza gharama kulipia watumishi wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa na utekelezaji wa Bajeti Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa 2017/2018 umebaini kwamba fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha *(cash flow plan)*. Fedha kutoka Hazina kwa ajili ya maendeleo ni pungufu ikilinganishwa na matumizi ya kawaida na fedha hazipatikani kwa wakati, hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya bajeti ya ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 417.8 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 50.8 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2017 na 2016 na kubaini kwamba kiasi cha fedha kimepungua takriban shilingi bilioni

109.3 sawa na asilimia 20.74 ikilinganishwa na shilingi bilioni 527.1 zilizopatikana katika kipindi hicho kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi unabainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 206.7 kutoka Hazina. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 52.8 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo. Kiasi hicho ni pungufu kwa asilimia 16 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya maendeleo ambapo kilikuwa ni shilingi bilioni 246.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imebaini kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla haukuwa mzuri. Vilevile katika kipindi chote hicho jumla ya shilingi bilioni 298.6 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 69.3 ya fedha iliyoidhinishwa. Tafsiri hapa ni kwamba kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilikuwa kikubwa zaidi ikilinganishwa na fedha za maendeleo zilizopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo 21 kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya mambo hayo yaliyozingatiwa ni kuhusu Serikali kuchangia utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo katika mwaka huu wa fedha, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 750.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya taasisi za kifedha kutokuwa tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Hati za Kimila, ambapo MKURABITA imeanzisha kuelimisha na kuhakikisha benki na taasisi za fedha kuhusu hali ya hati hizo kama dhamana kwa wakulima 105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza bajeti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo katika mwaka ujao wa fedha Serikali imeongeza jumla ya Shilingi bilioni 2.9 kwa chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iajiri watumishi ili kuziba pengo lililosababishwa na kuondolewa kwa watumishi wasio na sifa badala ya uhakiki wa watumishi ambao Serikali imeanza na inakamilisha utaratibu wa kuajiri watumishi 52,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yenye jumla ya mafungu nane imepanga kutekeleza malengo 209 na baadhi ya malengo ni kama yanavyoonekana kwenye ukurasa wa 26 hadi 28 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora, inaomba kuidhinisha jumla ya shilingi bilioni 669. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 473.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 195.9 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 34.2 sawa na asilimia 7.2 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 438.9 sawa na asilimia 92.7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti inayoombwa kuidhinishwa katika mwaka ujao wa fedha imepungua kwa shilingi bilioni 152.2 sawa na asilimia 18.5 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ilikuwa na shilingi bilioni 821.3. Kiasi cha fedha kilichopungua ni kikubwa zaidi

kwani ni takriban mara tatu ya kiasi kilichopungua katika mwaka wa fedha unaoishia, ambacho kilikuwa ni kiasi cha asilimia 6.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi umebaini, kiasi kinachoombwa kimepungua kwa shilingi bilioni 194.9 sawa na asilimia 49 ikilinganishwa na kiasi hicho cha shilingi bilioni 390.9 cha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa bajeti ya Wizara kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019; uchambuzi wa Kamati ulilenga kubaini kuwa kiasi gani ongezeko la Bajeti ya Taifa kiliathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika mwaka ujao wa fedha ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali asilia, ulinganishi na utofautishaji. Ili kurahisisha maelezo, Kamati imetumia *chart* na mambo yaliyobainika ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2018/2019 ambayo ni shilingi bilioni 669 ni sawa na asilimia 2.6 ya bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2017/2018 ni shilingi bilioni 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 unaonesha ongezeko la bajeti kwa 2% ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 0.6 katika fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, wakati wa bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo siyo sawa na asilimia 0.6 ya Bajeti ya Taifa. Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya

Utumishi wa Umma yanaoneshwa sawia kwa kutumia *chart* mraba Na. 1 na Na. 2 kama ilivyo kwenye vitabu vya taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati; baada ya kupitia taarifa ya ukaguzi wa miradi na maendeleo, taarifa ya utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 4,004, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufanywa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweze kunufaisha mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)*, kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyojisajiri na kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianze maandalizi ya kuwezesha mpango wa ruzuku kwa kaya maskini kuwa endelevu hata baada ya Wafadhali kujiondoa katika kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipunguze urasimu katika udhibiti watumishi kwa nafasi za uteuzi kwani baadhi wanakaimu kwa zaidi ya miaka miwili kwa madai ya kusubiri upekuzi *(vetting)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze mishahara kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Maendeleo ya Jamii watumike kuelimisha wanufaika wa mipango ya ruzuku kwa kaya maskini namna ya kutumia sehemu za ruzuku hiyo kujikwamua kiuchumi kama vile kuanzisha kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iangalie namna ya kuwawezesha Wazee katika vituo vya kutunzia wazee, kunufaika na mpango wa kaya masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika. Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea uwezeshwe kifedha ili kutanua wigo wa shughuli zake nchini na hivyo kuwafikia wanawake na vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kiwezeshwe kukamilisha awamu ya mwisho ya ujenzi wa jengo ambao unaendeleo katika Kampasi ya Tabora. Aidha, Kampasi hiyo ipatiwe vitendea kazi na watumishi wa kudumu ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari ili kujenga kizazi chenye maadili na uzalendo ambacho kitachukia na kupinga vitendo vya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe upendeleo wa mgawo wa watumishi watakaoajiriwa kwa baadhi ya Halmashauri ambazo zimebainika kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa kati ya asilimia 32 hadi 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iiwezeshe kikamilifu Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kukusanya na kuhifadhi taarifa na kumbukumbu muhimu kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Miongoni mwa njia za kukusanya taarifa hizo ni kutembelea na kuhoji watu wenye umri mkubwa ambao wameshuhudia mambo mengi ambayo ni muhimu kwa Taifa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe kampasi za Chuo cha Utumishi wa Umma zilizopo kabla ya kuanzisha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi, itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwako binafsi, Spika, Naibu Spika na Wenyekiti wengine wa Bunge, kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, naomba uhitimishe.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge wote kwa kuchaguliwa tena kuendelea na nafasi zao. Hii ni ishara tosha kwamba, utendaji wao katika kipindi kilichopita ulikuwa mzuri na ndiyo umewapa imani Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwachagua tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati kwa kutuchagua tena mimi na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Jasson Rweikiza ili tuendelee kuongoza Kamati kwa kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge. Hii ni ishara tosha kwamba wanatuamini na wako tayari kushirikiana nasi katika kutekeleza shughuli za Kamati.

Tunawaahidi kwamba tutaenzi imani na ushirikiano wao kwetu na njia pekee ya kufanya hivyo ni kuwatumikia kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti (Mafungu 36) ambayo inayashughulikia; na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi, wakati mwingine hadi jioni. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza wajibu wao kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara ya utayari wao katika kutuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati namshukuru Mheshimiwa Kapteni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamu, naomba uhitimishe, utoe hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Watendaji wa Ofisi wakiongozwa na Katibu Mkuu Utumishi, Dkt. Lauren Ndumbaro kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina Sanga; Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Victor Leonard na Ndugu Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Catherine Kitutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa

Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanne Ismail Nchemba, Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Ili kukidhi masharti ya Kifungu cha 6(4) pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uchambuzi wa bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati

ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge. Baada ya hatua hiyo, Kamati ilijielekeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/18 na kulinganisha na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya Mafungu Nane (8) yafuatao:-

i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;

ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;

iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;

vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na

viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejikita katika maeneo manne yafuatayo:-

(v) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

(vi) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(vii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

(viii) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

***Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa***

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa **Tsh. 390, 970, 890, 000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu matano kama ifuatavyo:-

**i)** **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – **Tshs. 379,570,890,000/=**;

**ii)** **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma – **Tshs. 7,000,000,000/=**;

**iii)** **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 1,650,000,000/=**;

**iv)** **Fungu 67**: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - **Tshs. 750,000,000/=**; na

**v)** **Fungu 4:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – **Tshs. 2, 000,000,000/=**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia sharti la kikanuni linalozitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kipindi kisichozidi siku Saba (7), Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na

Utawala Bora. Miradi iliyotembelewa inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 378,570,890,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mradi huu ambao unatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji wake ambayo imejikita kusaidia kaya maskini za Watanzania kujimudu kiuchumi kwa kupunguza umaskini wa kipato; kuboresha maisha na ustawi wa jamii, na kuhamasisha uwajibikaji na kuzingatia dhana ya utawala bora.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, tangu kuanza kwa awamu ya tatu ya TASAF takribani Watanzania **milioni 5** kutoka kaya maskini 1,118,751 wameandikishwa na wananufaika na ruzuku. Aidha, jumla ya **shilingi bilioni 147.6** zilitolewa kama ruzuku kwa kaya maskini zilizoandikishwa kupitia mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa zaidi kuwa mpango huu umetoa ajira za muda kwa kaya za walengwa 288,385 kupitia utekelezaji wa miradi 3,682 yenye thamani ya **shilling bilioni 13.3.** Miradi hiyo inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar kwa kuhusisha Vijiji 2,091, Mitaa 331 na Shehia 168.

Aidha, zoezi la uhakiki wa kaya maskini kwa lengo la kuhakikisha wanaonufaika ni wale wenye sifa stahiki, limekuwa likifanyika muda wote na hadi kufikia mwezi

Februari, 2018 kaya zipatazo 7,573 zilibainika kukosa sifa, hivyo kuondolewa katika mpango huu.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu Kamati ilitembelea na kukagua Mitaa ya Nyalikungu na Mnadani na Kijiji cha Shanwa, Wilayani Maswa, mkoani Simiyu.

**Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

Mheshimiwa Spika, **mradi huu ulitengewa jumla ya** shilingi 1,500,000, 000/= **na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 kiitwacho *"Policy and Planning"* cha** Fungu 30 **– Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.**

Mpango huu umeendelea kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Kupitia mpango huu wanyonge wanawezeshwa kurasimisha mali walizonazo (ardhi na biashara) na kuzitumia kujikwamua kiuchumi. Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, MKURABITA imewajengea wakulima 589 na viongozi 89 uwezo wa kutumia Haki Miliki za Kimila ili kupata mitaji katika benki na taasisi zingine za fedha katika Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Mpwapwa na Serengeti.

Aidha, wafanyabiashara 870 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara katika Wilaya ya Urambo, baada ya MKURABITA kushirikiana na Halmashauri ya wilaya hiyo kuanzisha kituo kimoja cha urasimishaji wa biashara (*one stop formalization centre*). Kupitia kituo hicho, wananchi wananufaika kwa kupata sehemu moja huduma za leseni za biashara, Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN), ujasili wa jina la biashara (BRELA), huduma za kibenki na mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Zanzibar jumla ya wafanyabiashara 100 katika Wilaya za Kusini Unguja (50)

na Micheweni, Pemba (50) wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Kati ya hao wafanyabiashara 10 wamefanikiwa kusajili majina ya biashara na kupata leseni za biashara.

Aidha, MKURABITA kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar, imeanza kufanya utafiti kuhusu sekta isiyo rasmi kwa lengo la kubaini ukubwa na thamani ya sekta hiyo kwa sasa. Utafiti wa majaribio umefanyika katika mikoa Sita (6) ya Tanzania Bara (Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Tanga) na mikoa miwili (2) ya Zanzibar (Mjini Magharibi na Kusini Pemba), ili kuona kama methodolojia, sampuli na madodoso yaliyoandaliwa yanaweza kuleta matokeo tarajiwa juu ya ukubwa wa sekta isiyo rasmi kwa sasa. Vilevile, utafiti mkubwa unaendelea kufanyika nchi nzima kuanzia Machi hadi Juni, 2018 na matokeo yake yatatolewa katika ngazi ya mkoa na taifa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga ili kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji wa MKURABITA.

## Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinajihusisha na utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam na kutoa machapisho mbalimbali ya kitaalam kwenye utumishi wa Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo kupitia Kampasi Sita (6) zilizoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Singida, Tanga na Tabora.

Ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitembelea Kampasi ya Tabora ambayo ilikuwa ikitekeleza ukarabati wa jengo la Shaban Robert.

***Matokeo ya Ukaguzi***

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

**Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini "Support to Tanzania Social Action Fund"**

**Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Maswa, Kamati ilitembelea Kijiji cha Shanwa ambacho kina jumla ya Kaya 248 zinazonufaika na utaratibu wa kunusuru kaya maskini. Idadi hiyo ya kaya imepungua kwa asilimia 19 ikilinganishwa na kaya 308 zilizokuwa zinanufaika awali, kabla ya zoezi la uhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa. Kaya hizo zimepokea ruzuku ya jumla ya **shilingi bilioni 8.85** kutokana na awamu 16 za malipo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile TASAF imeshiriki kwa kiasi kikubwa katika kuboresha elimu ya Sekondari kwa kuchangia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyalikungu kwa kutoa jumla ya **shilingi milioni 29.6.**

Aidha, kupitia utaratibu wa kuwezesha mahudhurio ya shuleni kwa watoto wanaotoka kaya maskini, mfuko huu umewezesha **Wanafunzi 49** kushiriki kikamilifu katika masomo yao ya sekondari. Wanafunzi hao walio katika kidato cha kwanza hadi cha nne wanalipiwa gharama za masomo na mfuko huu, ambazo ni pamoja na sare za shule, madaftari, kalamu, viatu na matumizi mengine.

Kupatikana kwa mahitaji hayo muhimu kumesaidia kuboresha mahudhurio shuleni, na hivyo kupunguza utoro na mdondoko (drop out) kwa wanafunzi hao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia namna ambavyo baadhi ya wanufaika wa mpango wametumia fedha za ruzuku kujenga na kuboresha makazi yao. Miongoni mwa wanufaika hao ni Bibi Monica Katambi Gwilasa (miaka 60), ambaye ametumia ruzuku kama chachu ya kujenga nyumba ya tofali ya vyumba vitatu na kuezeka kwa bati.

Mnufaika huyo alieleza Kamati jinsi alivyogeuza ruzuku aliyokuwa akiipata kuwa mtaji na kuanzisha biashara ndogo ndogo zilizompatia kipato na hivyo kuweza kujenga nyumba hiyo.

Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza. Kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**(viii) Mafanikio;**

(i) Kupungua kwa kiwango cha umaskini katika kaya kutokana na ongezeko la upatikanaji wa mahitaji ya msingi;

(ii) Ongezeko la idadi ya watoto wanaoandikishwa shuleni;

(iii) Kupungua kwa tatizo la ajira za watoto wadogo;

(iv) Watoto kutoka Kaya maskini zinazonufaika wanapata mahitaji muhimu ya shule na hivyo kuhudhuria shuleni kwa zaidi ya asilimia 80;

(vi) Walengwa wa mpango wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, kilimo, ufugaji na biashara na kuongeza kipato ambacho kimewasaidia kuboresha maisha;

(vii) Ongezeko la mahudhurio ya kliniki kwa watoto wa chini ya miaka mitano (5) kutoka asilimia 80 hadi 97; na

(viii) Walengwa wengi kutumia sehemu ya ruzuku kujiunga katika Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na hivyo kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya.

**(ix) Changamoto;**

(i) Mahitaji makubwa ya fedha za usimamizi wa mpango ikilinganishwa na kiasi kinachopokelewa;

(ii) Walengwa wengi wa mpango kuhamia maeneo mengine bila kutoa taarifa kwa uongozi;

(iii) Malalamiko kutoka kaya maskini ambazo hazijaingizwa kwenye mpango;

(iv) Fomu za utimizaji wa masharti ya afya na elimu kutojazwa kwa usahihi; na

(v) Baadhi ya wanakamati wa CMC kujitoa kutokana na ujira/posho kidogo wanayoipata.

**Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika,** katika Halmashauri ya Msalala ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 01** linatoa muhtasari wa hali utekelezaji wa mpango huu.

**Jedwali Na. 01: Mashamba yaliyopimwa katika vijiji vya Lunguya na Segese na Lunguya**

**Chanzo:** Taarifa za MKURABITA kuhusu urasimishaji wa ardhi na biashara.

**a) Mafanikio**

i) Kupungua kwa migogoro ya ardhi katika vijiji hivyo;

ii) Kuongezeka kwa usalama wa milki ya ardhi za wakulima waliorasimisha ardhi yao;

iii)Wanawake wamemilikishwa hati miliki za ardhi peke yao au pamoja na wenza wao;

iv) Baadhi ya wananchi wamekuza mitaji ya biashara kutokana na mikopo waliyoipata kwa kutumia Hati Miliki za Kimila kama dhamana; na

v) Mafanikio katika vijiji hivi yamekuwa chachu ya kuendeleza urasimishaji katika vijiji vingine 14 ambapo mashamba 24 yamepimwa na Hakimiliki kuandaliwa;

**a) Changamoto;**

i) Ukosefu wa fedha unakwamisha utekelezaji wa MKURABITA;

ii) Ukosefu wa Afisa Ardhi Mteule wa kusajili Hati Miliki za Kimila, unachelewesha kukamilika kwa hati hizo. Mfano; katika urasimishaji uliofanyika mwaka 2014 Hati Miliki zake zimetolewa mwaka huu, 2018;

iii)Upotevu wa takwimu za ardhi na kukosekana kwa Wataalam kutokana na mgawanyiko wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, iliyozaa Msalala na Ushetu;

iv) Kasi ndogo ya utayarishaji wa Hati Miliki kutokana na uhaba wa Watumishi wa Ardhi; Mfano, katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati, kati ya mashamba 2158 yaliyopimwa ni Hati Miliki 274 tu (sawa na asilimia 12.69) ndiyo zimeandaliwa;

v) Baadhi ya Wananchi kushindwa kugomboa Hati za Miliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa;

vi) Wamiliki wa Hati za Hakimiliki za Kimila kukosa ujuzi wa kuandaa maandiko ya miradi ambayo yatawawezesha kupata mikopo kutoka benki na taasisi nyingine za kifedha.

**Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utumishi wa Umma, kilianzishwa mwaka 2000 baada ya kuunganishwa kwa Chuo cha Uhazili Tabora *(Tabora Secretarial College*) ambacho kilianzishwa rasmi mwaka 1973 kwa ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Sweden, na Chuo cha Watumishi wa Serikali (*Civil Service Training Centre*) kilichokuwa Dar es Salaam.

Kwa sasa chuo hiki chenye Kampasi Sita ambazo ziko mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara, Singida, Tanga na Tabora, ni nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma.

Katika ziara yake, kwenye Kampasi ya Tabora Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Chuo kinamiliki maeneo yake na kipo katika hatua za mwisho za kupata Hatimiliki. Hii ni tofauti na Kampasi nyingine kama vile Mbeya na Tanga ambazo zinatumia majengo ya kupanga;

ii) Chuo kina upungufu wa watumishi wa kudumu, vitendea kazi na vyumba vya madarasa;

iii) Uchakavu wa miundombinu ya maji na umeme unaongeza gharama za uendeshaji;

iv) Upungufu wa vitendea kazi na vyumba vya madarasa; na

v) Mwitikio hafifu kutoka Wizara na Taasisi za Umma katika kutumia huduma za chuo hicho;

***Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2017/2018***

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

i) Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini utafanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zitatumika kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za Wafadhili. Bado mchango wa Serikali ni mdogo kwani tangu kuanza kwa mpango huu katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia **Shilingi bilioni 4.35** kati ya zaidi ya **shilingi bilioni 63.5** ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **6.85**;

ii) Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini wanaweza kujikwamua kiuchumi iwapo watatumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi kama vile biashara, ufugaji au kilimo. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Jamii katika halmashauri isaidie kuwaelimisha walengwa hao;

iii) Iwapo TASAF itahakiki na kusajili Kaya maskini zilizosahaulika katika Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, itasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko miongoni mwa Jamii;

iv) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechangia kuboresha mahudhurio ya Watoto wa Kaya maskini shuleni na kliniki. Mfano; Wanafunzi 49 katika Shule ya Sekondari Nyalikungu (Wilayani Maswa) wanahudhuria kikamilifu masomo kutokana na mpango wa ruzuku kwa kaya maskini;

v) Hatua ya Vituo na Zahanati binafsi kukataa kuwahudumia wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kunakatisha tamaa wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini ambao waliamua kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujiunga na CHF;

vi) Zoezi la kuhakiki na kuondoa watu wasio na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, litafanikiwa iwapo litashirikisha wanajamii, viongozi wa Serikali za Mitaa na kuzingatia haki;

vii) Bajeti finyu kwa MKURABITA inaanthiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji;

viii) Watendaji wa Halmashauri waliojengewa uwezo na MKURABITA, wanaweza kuendeleza zoezi la urasimishaji iwapo watawezeshwa kwa kupatiwa vifaa na raslimali fedha;

ix)Benki na taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu hadhi ya Hati za Hakimiliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, zitatoa mikopo kwa Wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo;

x) Halmashauri zikipatiwa wataalam wa ardhi, zitasaidia MKURABITA kuharakisha zoezi la kurasimisha ardhi na kutoa Hati za Hakimiliki kwa wahusika;

xi)Iwapo Mfuko wa Kujitegemea wa Rais utatengewa fedha za kutosha utaweza kufikisha huduma zake katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kunufaisha Wanawake na Vijana wengi zaidi;

xii) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Tabora kitapatiwa watumishi wa kudumu, na vitendea kazi kitaboresha huduma na kupunguza gharama kulipa watumishi wa mkataba na washiriki;

**UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

***Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais,

Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

**Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa:-

i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan);

ii) Fedha zinazotolewa kutoka Hazina kwa ajili ya maendeleo ni pungufu kwa asilimia 14 ikilinganishwa na fedha za matumuzi ya kawaida; na

iii) Fedha hazipatikani kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (na mafungu yake) kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2018 (kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/18) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja

na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 417, 779, 331, 561/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 50.89** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2017/2018 na mwaka 2016/2017 na kubaini kuwa kiasi hicho cha fedha kimepungua kwa takribani **shilingi 109,336,885,951** (sawa na asilimia **20.74)** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/17 ambacho kilikuwa ni **shilingi 527,116,217,512**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebainisha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 206,720, 967,511/=** kutoka Hazina. Kiasi hicho ni sawa na asilimia **52. 87** ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa **asilimia 16.26** ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni **shilingi 246,780,369,584/=**.

Aidha, Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani asilimia **50.37** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kwa tafsiri rahisi ni kwamba, kiasi kilichopaswa kupatikana kwa kila robo ya mwaka wa fedha hakikuweza kupatikana. Kwa kuzingatia asilimia 25 ya bajeti kwa kila robo, ilitarajiwa kwamba hadi kipindi hicho fedha iliyoidhinishwa ingekuwa imepatikana kwa takribani **asilimia 70**.

Vilevile, katika kipindi hicho jumla **shilingi 298,604,842,833/=** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **69.39** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Tafsiri ya mwenenendo huo ni kwamba, kiasi cha

fedha za matumizi ya kawaida kilikuwa kikubwa zaidi ikilinganishwa na fedha za maendeleo zilizopatikana katika kipindi kama hicho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina siyo mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani, kiasi kinachotolewa kimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Aidha, kasumba ya fedha za matumizi ya kawaida kuwa nyingi ikilinganishwa na fedha za maendeleo imeendelea kuwepo.

**Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo Ishirini na Moja (21) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu:-

i) Serikali kutoa mchango wake wa fedha katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo katika mwaka huu wa fedha Serikali imetoa jumla ya **shilingi milioni 750** kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo;

ii) Baadhi ya Taasisi za kifedha kutokuwa tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Hati za Hakimiliki za Kimila; ambapo MKURABITA imeanza kuelimisha na kuhamasisha benki na taasisi za kifedha kuhusu uhalali wa hati hizo kama dhamana kwa ajili ya mikopo. Aidha, taasisi hizo za fedha zinatumika kuwaelimisha wamiliki wa ardhi wenye hati hizo namna ya kuandaa mpango kazi kuhusu mikopo watakayoichukua. Tayari wakulima 105 kutoka Halmashauri

ya Wilaya za Kilosa na Mji wa Njombe wamekopeshwa **shilingi bilioni 3.8** kutoka Benki ya Kilimo kwa dhamana ya hati hizo;

iii) Kuongeza bajeti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ambapo katika mwaka ujao wa fedha Serikali imeongeza jumla ya **shilingi bilioni 2.95** kwa chombo hiki.

iv) Serikali iajiri watumishi ili kuziba pengo lililosababishwa na kuondolewa kwa watumishi wasio na sifa baada ya uhakiki wa Watumishi, ambapo Serikali imeanza na inakamilisha utaratibu wa kuajiri watumishi 52,436.

**UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

***Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2018/2019, kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Nane (20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 04) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo **209** katika mwaka ujao wa fedha na baadhi ya malengo ni pamoja:-

i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

ii) Kumshauri Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;

iii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) kwa kushirikisha wadau wa sekta ya Umma na sekta binafsi;

iv) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);

v) Kuifanyia mapitio Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa na ufisadi;

vi) Kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kwenye Taasisi za Umma zinazotolewa na Serikali na Wabia wa Maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

vii) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na hivyo kujenga jamii inayochukia rushwa;

viii) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa Kaya maskini zipatazo 355,000 katika Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96, ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza;

ix) Kuanzisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao, Makao Makuu Dodoma;

x) Kuendelea kupokea na kuhakiki matamko ya viongozi wa Umma kuhusu raslimali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Matamko haya sasa yanajazwa kwa njia ya mtandao (*online application*) baada ya kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili *(Ethics Management Information System - EMIS*).

xi) Kuandaa taarifa nne (4) za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kima cha chini cha mshahara wenye staha. Taarifa hizi zitawezesha kushauri kuhusu mshahara wa chini unaoendana na gharama halisi za maisha; na

xii) Kuweka na kuhuisha Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za kiutendaji *(Keyword Filling System)* za Watumishi *(Personanel Records Management System)* katika Taasisi za Umma 58 ili kuboresha utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 669,094,556,009.** Kati ya fedha hizo **shilingi 473,118,195,009.** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 195,973,361,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi 34,247,334,360** sawa na asilimia 7.23 ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 438,870,860,649** sawa asilimia 92.77 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa katika mwaka ujao wa fedha imepungua kwa **shilingi 152,227,791,665** (asilimia 18.53) ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/18 ambayo ilikuwa **shilingi 821, 322, 347, 674.**

Kiasi cha fedha kilichopungua ni kikubwa zaidi kwani ni takribani mara tatu ya kiasi kilichopungua katika mwaka wa fedha unaoisha ambacho kilikuwa ni asilimia **6.89**.

Aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba kiasi kinachoombwa kuidhinishwa kimepungua kwa **shilingi 194,997,529,000** (asilimia 49.88) ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 390,970,890,000** kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/18.

Uchambuzi umebaini zaidi kwamba, kiasi kilichopungua ni kikubwa sana kwani ni zaidi ya mara tatu ya kilichobainika kupungua katika mwaka wa fedha unaomalizika ambacho kilikuwa **asilimia 16.13**

***Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kufanya ulinganisho na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi wa Kamati ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la Bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha.

Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Mambo yaliyobainika ni haya yafuatayo:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ni **shilingi bilioni 669** ni sawa na asilimia 2.06 ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2017/18 ni **shilingi bilioni 32,476;**

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/19 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 2.45, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2017/18; lakini bajeti ya jumla ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/19 imepungua kwa asilimia 18.59 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2017/18;

iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 0.06 katika fedha za maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2018/19, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala

Bora, ambayo ni sawa na asilimia 0.60 ya Bajeti ya Taifa, imepungua kwa asilimia 49.88 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/18.


Aidha, **Jedwali Na. 02** linafafanua zaidi juu ya ulinganisho baina ya maeneo hayo mawili.

**Jedwali Na. 02:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa Mwaka 2018/19


| BAJETI KUU YA TAIFA 2017/2018 | | | BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2017/2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mgawanyo | Bajeti Kuu (Tsh.Bilioni) | Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu | Mgawanyo | Bajeti ya Wizara | Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara |
| OC | 2895 | 8.92 | OC | 438,870,860,649 | 65.59 |
| Deni la Taifa | 9,705 | 29.88 | - | - | - |
| Mshahara | 7,627 | 23.49 | Mshahara | 34,247,334,360 | 5.12 |
| Maendeleo | 12,248 | 37.71 | Maendeleo | 195,973,361,000 | 29.29 |
| **Jumla** | **32,476** | **100** | **Jumla** | **669,094,556,009** | **100** |

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yanaweza kuoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-



**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19




**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

i) Zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mradi wa ruzuku kwa kaya maskini, lifanyike mapema ili kaya maskini katika maeneo hayo kunufaika na mpango wa ruzuku. Takwimu zinaonesha yapo maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango;

ii) Serikali iwezeshe wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa

Afya ya Jamii (CHF), kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyosajiliwa. Aidha, kadi hizo zitambuliwe kwenye Hospitali/Vituo vya Afya na Zahanati binafsi kama ilivyo kwa aina nyingine za bima za afya;

iii) Serikali ianze maandalizi ya kuwezesha mpango wa ruzuku kwa kaya maskini kuwa endelevu (*Business Continuity Plan – BCP*) ili uendelee hata baada ya Wafadhali kujiondoa katika kuchangia. Iwapo hili halitafanyiwa kazi mapema, ipo hatari ya kuzuka taharuki miongoni mwa wanufaika iwapo mpango utasita ghafla;

iv) Serikali ipunguze urasimu katika kuthibitisha watumishi wa nafasi za uteuzi. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya watumishi katika ofisi za umma wamekuwa wakikaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miaka miwili, kwa madai ya kusubiri upekuzi "vetting". Hali hiyo inawavunja moyo watumishi nao na kuathiri utendaji wao kwani hushindwa kufanya maamuzi ya msingi;

v) Serikali iongeze mshahara kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Sote ni mashahidi kwamba, Serikali haijaongeza mshahara wa Watumishi wa umma kwa mwaka wa tatu sasa;

vi) Halmashauri zitumie Maafisa Maendeleo ya Jamii kuelimisha wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini namna wanavyoweza kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujikwamua kiuchumi. Baadhi ya maeneo walengwa wamefanikiwa kuanzisha kilimo na ufugaji kwa kutumia sehemu ya ruzuku hiyo;

vii) Kwa kuwa wazee wengi katika vituo vya kutunzia Wazee hawajimudu kiuchumi na hivyo kuwa na vigezo vya kunufaika na mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, Kamati inashauri Serikali iangalie namna ya kuwawezesha Wazee katika vituo hivyo kunufaika na mpango huo;

viii) Zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika;

ix) Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa, ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa ardhi na biashara za wananchi. Hadi mwezi Februari, 2018 MKURABITA ilikuwa imepokea asilimia 52.85 tu ya fedha yote iliyoidhinishwa katika mwaka huu wa fedha ambayo ilikuwa ni **shilingi bilioni 4.4;**

x) Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii;

xi) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) uwezeshwe kifedha ili kutanua wigo wa shughuli zake nchini na hivyo kuwafikia Wanawake na Vijana wengi zaidi;

xii) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kiwezeshwe kukamilisha awamu ya mwisho ya ujenzi wa jengo ambao unaendeleo katika Kampasi ya Tabora. Aidha, Kampasi iapatiwe vitendea kazi na watumishi wa kudumu ili kupunguza gharama za uendeshaji na kulipa watumishi wa mkataba na washiriki;

xiii) Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari ili kujenga kizazi chenye maadili na uzalendo ambacho kitachukia na kupinga vitendo vya rushwa;

xiv) Serikali itoe upendeleo wa mgawo wa watumishi watakaoajiriwa kwa baadhi ya Halmashauri ambazo maeneo ambayo yamebainika kuwa na upungufu mkubwa wa Watumishi, wa kati ya asilimia 32 hadi 65;

xv) Serikali iiwezeshe kikamilifu Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kukusanya na kuhifadhi taarifa na kumbukumbu muhimu kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Miongoni mwa njia za kukusanya taarifa hizo ni kutembelea na kuhoji watu wenye umri mkubwa ambao wameshuhudia mambo mengi ambayo ni muhimu kwa taifa na vizazi vijavyo;

xvi) Serikali iimarishe kampasi za Chuo cha Utumishi wa Umma zilizopo kabla ya kuanzisha nyingine, ili kuwezesha chuo hicho kutoa huduma bora; na

xvii) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima ambayo inaweza kuibuka.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge wote kwa kuchaguliwa tena kuendelea na nafasi zao. Hii ni ishara kwamba, utendaji wao katika kipindi kilichopita ulikuwa mzuri na ndiyo umewapa imani Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwachagua tena.

Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati kwa kutuchagua tena mimi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Mwanne Ismail Mchemba (Mb) ili tuendelee kuongoza Kamati kwa kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge. Hii ni ishara kwamba, wanatuamini na wako tayari kushirikiana nasi katika kutekeleza shughuli za Kamati. Tunawaahidi kwamba tutaenzi imani na ushirikiano wao kwetu, na njia pekee ya kufanya hivyo ni kuwatumikia kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ina mafungu mengi ya Bajeti (mafungu 36) ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwingine hadi jioni.

Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza wajibu wao kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba,Mb – M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. George Malima Lubeleje,Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim,Mb
7. Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
8. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate,Mb
9. Mhe. Mwatum Dau Haji,Mb
10. Mhe. Saada Mkuya Salum,Mb
11. Mhe. Salum Khamis Salum,Mb
12. Mhe. Venance Methusela Mwamoto,Mb
12. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb
13. Mhe. Anna Joram Mhagama, Mb
14. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
15. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
16. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
17. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
18. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
19. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
20. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
21. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
22. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb

23. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
24. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Utumishi, Dr. Lauren Ndumbaro kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Catherine Kitutu, kwa kuratibu vizuri shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. Vilevile, nawashukuru watumishi wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga, kwa kuandaa na kutoa vitabu vya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S. Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**

11 Aprili, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza mjadala wetu wa jumla na tutaanza na Mheshimiwa Joseph Selasini, baadaye Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Hamidu Bobali na Mheshimiwa George Lubeleje wajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu na ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu, niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais alipochagua vijana kuongoza katika sehemu mbalimbali, nadhani kusudio lake lilikuwa vijana waoneshe uwezo kwa sababu ya ujana wao, uwezo wa kufikiri, kukimbia na kutenda kwa haraka. Ni kwa sababu hiyo nataka niwapongeze Mawaziri hawa watatu; Mheshimiwa Jafo pamoja na wenzake Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Kakunda kwa kazi wanayofanya. Wizara hii ni kubwa sana, lakini kwa muda mfupi wameweza kukimbia nchi nzima na kufanya hayo mengi waliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba kwa mara ya pili leo hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imekosekana. Sasa jambo hili siyo afya kwa Bunge na wala siyo rekodi nzuri ambayo inaandikwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Uongozi wa Bunge uchukue hatua dhidi ya jambo hili, kwa sababu jambo hili likiendelea linafedhehesha demokrasia ndani ya Bunge na vizazi vijavyo vitatuona kwamba tumeweka *precedent* mbaya sana katika nchi yetu na Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda sana nizungumze suala la elimu. Suala la elimu sasa ni jambo ambalo linazungumzwa na wengi katika nchi yetu na miezi michache iliyopita, Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin Mkapa alitoa rai lifanyike kongamano kwa ajili ya kujadili elimu ya nchi hii ambayo inaporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami leo ningependa kusema kwamba ni lazima elimu yetu tuibadilishe tujikite kwenye elimu yenye ujuzi kwa watoto wetu; elimu yenye malengo ambayo itawezesha watoto wetu wakimaliza hata *primary school* wajue kwamba ni nini ambacho wameandaliwa kwenda kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wahenga wenzangu ndani ya Bunge, wanakumbuka kwamba baadhi yetu tulimaliza darasa la saba tukiwa tuna ufundi wa namna fulani. Tulikuwa tunajua kutengeneza meza, bustani mbalimbali, masweta, mashuka na kadhalika, lakini leo hii mtoto anamaliza darasa la saba hajui chochote. Hata kilimo ambacho anaambiwa akafanye hajui, mtoto anamaliza *form four* hajui chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana turejee kwenye elimu ya zamani ya kujitegemea. Nasema tuache kuendesha elimu kwa matamko. Siku chache zilizopita, tumesikia habari ya kuondolewa michango mbalimbali kwenye mashule; ni sawa kuna michango ambayo ilikuwa inakera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza sana kuhusu mchango wa chakula mashuleni. Upo utafiti unaosema kwamba akili za watoto wetu zimedumaa kwa asilimia 42 kwa sababu ya lishe duni. Hii vile vile inatokana na elimu tunayowapa. Zamani tulikuwa tunalima bustani tunakula mboga mashuleni; tulikuwa tunafuga sungura, tunakula sungura mashuleni; tulikuwa tunafuga kuku, tunakula mayai shuleni; na tulikuwa tunafuga ng'ombe tunakunywa maziwa shuleni. Sasa ni mdudu gani aliyeingia katika nchi yetu akaondoa mambo haya katika Shule za Msingi matokeo yake watoto wetu sasa tunawadundulizia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa watoto wetu wote chakula. Wale ambao mmesoma zamani mtakumbuka jinsi Mwalimu Nyerere alivyoenda kwa Rais J. F. Kennedy wakati ule

tukapata shayiri na maziwa watoto wakasoma, kiwango cha elimu kilipanda namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni huduma. Pamoja na kwamba tunajenga *standard gauge,* reli; tunanunua ndege na kadhalika, kama hatutaangalia tukahudumia elimu yetu sawasawa, Taifa hili litakwenda kuangamia. Mifano tunayo, sasa hivi bajeti inajadiliwa katika nchi zote za Afrika Mashariki. Ukienda Kenya wanajadili kuhusu ajira kwa vijana na akinamama, wanajadili habari ya uwekezaji katika *assembling* ya viwanda vya magari. Ukienda Uganda wanajadili habari ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tupo katika Bunge, Watanzania wanajadili habari ya watoto waliotelekezwa. Ni kwa sababu akili zetu tumezi-*corner* kwenye kujadili vitu vidogo vidogo badala ya kujadili *issues* kubwa za kuisaidia nchi yetu. Kwa hiyo, naomba kabisa Wizara iangalie namna ya kututoa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nizungumze habari ya asilimia kumi ya wanawake na watoto. Naunga mkono yale yaliyosemwa na Kamati yangu, lakini tumekuwa tukiwalaumu Wakurugenzi hapa. Hawa Wakurugenzi, leo nataka niseme kwamba Wakurugenzi katika nchi yetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na sababu ni kwamba fedha za kuendesha Halmashauri hawapati. Matokeo yake wanaangalia ile asilimia kumi ndiyo inayowasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna Halmashauri ambazo hazilipi posho kwa Madiwani; na sababu ni kwamba fedha ambazo walikuwa wanategemea kwenye vyanzo mbalimbali, Serikali Kuu imechukua, yaani ni kana kwamba hawa Wakurugenzi wamefungwa mikono na miguu halafu wanaambiwa wakimbie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, pamoja na utekelezaji wa hayo Kamati iliyosema, lakini ni lazima Serikali iangalie uamuzi wake wa kuzinyang'anya hizi Halmashauri

vyanzo vyake vya mapato. Ni kweli asilimia kumi inasaidia, katika Jimbo langu najua. Jimboni kwangu Warombo ni watu wanaohangaika dunia nzima wamo, Halmashauri zote Tanzania Warombo wapo kwa sababu wamezoea hivyo. Wangepata hizi pesa, zingewasaidia zaidi. Kwa hiyo, naunga mkono itungwe sheria, lakini pia iwepo akaunti maalum ambapo hizi pesa zitaingia ziweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu *TARURA*. Naunga mkono *TARURA* kwa sababu hapo nyuma fedha za barabara zilikuwa zinagawiwa kisiasa. Diwani anataka barabara yake anakwenda ana-*influence* kule, inajengwa. Diwani ambaye hawezi kufanya hivyo, anashindwa. Sasa nasema tu kwamba ili kuondoa malalamiko *TARURA* ishirikishe Halmashauri kwa kutoa taarifa mbalimbali ya kazi wanazofanya ndani ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuwe na Bodi ya *TARURA* ngazi ya Wilaya na bajeti ya *TARURA* iongezwe kutoka asilimia 30 ya Mfuko wa Barabara sasa, angalau ifike asilimia 50 na uanzishwe mfuko wa matengenezo ya barabara ya dharura kwa sababu barabara hizi za za vijijini ni tofauti na zile barabara kuu. Hizi za vijijini zinaharibika mara kwa mara mvua inaponyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze kuhusu utawala bora. Tumeshuhudia ugomvi na kutoelewana katika Halmashauri mbalimbali kati ya Wakurugenzi, Madiwani pamoja na Watendaji wengine. Tunaiomba Serikali kwa mara nyingine itafute namna ya kuondoa hii migogoro, kwa sababu kwenye migogoro kazi haiwezi kufanyika. Wakurugenzi ambao wanafikiri wanataka kufanya siasa, wanafikiri wanataka kuua Wabunge, ni vizuri Serikali iwa-*identify* wakae pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kwa Halmashauri zote, unakuta Wakurugenzi wamekaa pale, Mkurugenzi wa Halmashauri X ana uhusiano na Mkurugenzi wa Halmashauri Y huko, wanachoreana namna ya kupata Ubunge, matokeo yake wanaingiza migogoro katika Halmashauri, Halmashauri

haziendi kwa sababu huyu ana tamaa. Wachunguzeni ili iamuliwe, kama wanataka kufanya siasa, wafanye siasa. Vinginevyo tunao wajibu kabisa wa Kimungu wa kuhudumia watu wetu na siyo kuvutana kwa ajili ya nani awe nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, yapo maagizo yanayotolewa na viongozi wetu. Kwa mfano, Mawaziri wetu wametoa maagizo kuhusu Halmashauri ya Tunduma kwa barua mara mbili, Mkuu wa Wilaya hatekelezi, Mkurugenzi hatekelezi, Madiwani na Halmashauri iliyochaguliwa na wananchi haifanyi kazi na haikai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unashindwa kuelewa, hii dharau ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwa Mawaziri wetu inatoka wapi? Kwa sababu Waziri anamwakilisha Rais na Waziri anapotamka maana yake anaangalia sera, sheria na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie viburi vya baadhi ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji ili Halmashauri zetu ziweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna kamata kamata ya...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe kaka yangu taarifa kwamba juzi Mkuu wa Mkoa wa Manyara alitengua amri au agizo la Waziri wa Maliasili. Kwa hiyo, ndiyo *level* ya kiburi hicho tunachozungumza. Naomba uchukue taarifa yangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ninachosema, tusipoangalia kutakuwa...

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa vizuri Mheshimiwa ametoa taarifa na mimi mwenyewe nikiwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke sawa jambo hili kwamba Mkuu wa Mkoa wa Manyara hakutengua agizo nililolitoa, lakini alisema jambo hilo lisubiri mpaka Waziri wa Ardhi atakapoenda kwenye eneo la tukio. *(Makofi/ Kelele)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa msikilizeni, yeye ndio anayejua. Haya, sema Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Manyara alisema wananchi waondoe shaka, yeye, mimi na Waziri wa Ardhi tutakwenda kuweka mipaka na kushughulikia jambo hilo pamoja. Kabla hajatoa agizo hilo, alizungumza nami na nikamwelekeza kwamba tayari mimi na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi tumeshakubaliana kwenda kwenye eneo hilo na kwa sababu ziara hiyo ipo, basi tutafikia kwake, tutaambatana naye tutakwenda kuweka jambo hilo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imo ndani ya *framework* ya miezi tisa ambayo nilitoa kama kipindi cha maangalizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka umenilindia muda wangu, sasa hii siyo nafasi yako ya kujitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, sasa hivi kumekuwa na matamko mbalimbali na ya ajabu ya kuhatarisha usalama wa nchi. Yupo mtu mmoja anaitwa Cyprian Musiba, anaita mkutano na Vyombo vya Habari anaanza kushukutumu baadhi ya Viongozi na kutoa maagizo, kwamba ningekuwa mimi ningeua hata 200. Juzi Maaskofu wamezungumza, anaitisha Vyomb vya Habari, anasema ningeua hata 200. Hivi nchi hii si Usalama wa Taifa wapo, nchi hii si ina dola? Hivi huyu mtu mnamkalia kimya ina maana mnamtuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi watu wanapotea, sasa hivi watu wanauawa, mtu anasimama hadharani anasema ningekuwa ningeua 200, ningekuwa ningeua 300, halafu anaangaliwa tu hivi na anaandika kwenye gazeti lake. Wakati Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, shemeji yangu, unafungia magazeti kwa sababu mbalimbali, huyu anatoa matamko kwenye hilo gazeti lake kwamba ataua, atakamata, atafanya nini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho amenitaja mimi kwamba ni mmoja kati ya majasusi wa CHADEMA. Nataka niwaambie, kwa sababu watu wamepotea hapa watu wameuawa hapa, Serikali mnamsikia Ndugu Musiba mnakaa kimya, hamumchukulii hatua, mimi nataka nijenge hoja kwamba Serikali mnawajua wauaji, kwa sababu Musiba anawatamka hamchukui hatua, ni mtu wenu. Vinginevyo, njooni hapa mtuambie huyu Musiba ni nani na mchukue hatua dhidi yake. Vinginevyo, kujenga nyumba ni jambo gumu lakini kuibomoa ni kwa siku moja; *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili waasisi walilijenga kwa nguvu, kwa shida kubwa, lakini watu kama akina Musiba kwa sababu ya kutafuta *political mileage,* wanalivunja. Kwa sababu kama ataniua mimi, mimi nina

ukoo wangu, mimi nina ndugu zangu, nina rafiki zangu, hicho kisasi mtakibebea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Peter Msigwa baadaye Mheshimiwa Bobali ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote watatu wa TAMISEMI, pamoja na changamoto tulizonazo lakini unaiona ile *sense* ya utendaji kazi na kufika kwa haraka kwenye maeneo ambayo tunafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tutakuwa tunafanya makosa tusipowapongeza, hasa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo, amekuwa msikivu na anajitahidi, pamoja na kwamba vitendea kazi vinaweza visiwepo, lakini niwapongeze kwa ujumla wenu, pamoja na Mzee wangu, Mheshimiwa Kapteni Mkuchika katika eneo lake la mambo ya Utawala Bora ambalo mimi ndiyo nitajikita zaidi na nitakupa vidonge kidogo Mheshimiwa Kapteni Mkuchika kwenye eneo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu suala la utawala bora, ambalo kwenye hotuba yake Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, amegusagusa tu mambo mengine lakini mambo ya msingi hujayagusa. Ndugu zangu Taifa hili ni letu sote, kwa bahati mbaya kuna watu wengine wana *notion* kama Wapinzani ni *intruders* na kwamba kuwepo kwetu hapa ni kama fadhila fulani ambazo tunapewa na mtu fulani. Sisi hapa ni Watanzania halisi, hii ni nchi ya kwetu na tulifanya chaguzi, tumekuja hapa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunazo haki na Katiba yetu inaturuhusu kuwepo kwetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali iliyofikia kwa sasa hivi kwa mazingira ya utawala bora ni hali ya hovyohovyo sana katika nchi yetu. Tatizo kubwa katika Taifa letu tuna-*embrace*

*mind* ndogo na tunapuuza *big mind.* Taifa ambalo halitaki *big mind,* watu wenye uelewa mkubwa hawatakiwi, watu wanaohoji, wanaodadisi hawatakiwi katika Taifa letu. Tukitaka kujenga Taifa lenye nguvu, lenye uchumi mpana ni lazima tuwe na hoja zinazokinzana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na Bunge ambalo linapenda kushangilia vitu vya hovyohovyo na hii inatokana kwenye Taifa letu kunapofanyika *promotion* au *appointment* au *placement* kwenye eneo lolote, haitegemeani na *merit.* Unapomchagua Katibu Mkuu wa Wizara unamchagua kwa vigezo gani, unataka aka-*add value* gani? Unapomchagua Mkuu wa Mkoa unamchagua kwa kigezo gani, anaenda ku-*add value* gani kwenye ule Mkoa? Unapomchagua Mkuu wa Wilaya unamchagua kwa kigezo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulilalamika wakati Serikali hii inaingia madarakani kwamba mmewatoa ma-*DED* waliokuwa wazuri, wanafanya kazi, wana weledi kwenye ofisi zao, wakaletwa watu ambao kwa sababu tu walivaa *uniform* za CCM, leo tumeona jinsi ambavyo Halmashauri zetu zinavyoshindwa kufanya kazi. Kumekuwa na *nepotism* ya hali ya juu sana, kumekuwa na upendeleo wa hali ya juu sana kwa sababu hawa wote wanaochaguliwa hawaendani na kazi walizopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ofisi ya Katibu Mkuu ni ofisi *serious* kabisa, unamwona mtu kama Profesa Kitila Mkumbo, badala ya kushughulikia na namna ya kumtua mama ndoo kichwani yeye amekazana anaandika kuwajibu Maaskofu ambao wanashughulika na roho za watu mitaani, badala ya kukaa kwenye ofisi haya ndiyo ninayosema mtu hajui anaenda kuongeza *value* gani na nimezungumza mambo ya *placement* haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamchukua mtu kama Profesa Kitila anayezungumzia mambo ya elimu unampeleka kwenye mambo ya maji, anakaa ofisini badala ya kuzungumza mambo ya kumtua mama ndoo ambalo ni

wazo zuri, yeye anakazana anataka amjibu Askofu kwa sababu ya mawazo waliyotoa kwamba hakuna demokrasia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dola karibu milioni 500 za India zimerudi huko kwa sababu ya utendaji wa hovyo kabisa wa Serikali zetu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter tafadhali kaa. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 64(b), kwamba mzungumzaji, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala. Sasa Profesa Kitila Mkumbo hivi kweli yupo kwenye mjadala hapa kama siyo tunataka kufanya mambo yasiyostahili ni nini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mbunge tunza heshima yako kwa kuzungumzia mjadala, usiharibu hii agenda nzuri ya Mheshimiwa....

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mama, hangaika na viwanda.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba angejikita kwenye agenda tuliyonayo mezani ambayo ni hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Jafo, subiri basi hata kwenye Wizara ya Maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ninayozungumza. Dada yangu namheshimu sana na ni *Engineer* huyu, anashindwa kuelewa, yaani anashindwa kuunganisha utawala bora ninaouzungumza na natoa kwa mifano. Sasa hizi ndiyo *appointments* ambazo zinatolewa, haelewi kabisa hapa ninapozungumza. Nimezungumza kuanzia uteuzi wa Katibu Mkuu, ukienda kwenye Wakuu wa Mikoa...

**MBUNGE FULANI:** *DNA!*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu kama akina Mnyeti, anasimama kinyume kabisa na utaratibu wa sheria, Mkuu wa Mkoa kabisa anagawa kadi za Chama cha Mapinduzi barabarani. Mtumishi wa umma, tunazungumzia masuala ya utawala bora, anagawa kadi na anasema sitashirikiana na Wapinzani, halafu mtu kama huyu bado yuko kwenye ofisini, halafu mnakuja hapa mnasema kuna utawala bora. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, analipwa kodi ya nchi hii, halafu...

**TAARIFA**

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Mkuu wa Mkoa ni Mjumbe halali wa Kamati ya Siasa ya Mkoa. Kwa hiyo, anao wajibu wa kueneza itikadi ya Chama cha Mapinduzi kama Mjumbe halali wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena ndiyo haya niliyoyazungumza...

**MBUNGE FULANI:** *DNA!*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna-*embrace* vitu vidogovidogo; huyu kijana mdogo, msomi, anashindwa kutofautisha kazi ya Mkuu wa Mkoa na kwenye vikao ndani ya Chama cha Mapinduzi, *this is very sad,* hawezi kuelewa tofauti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu kama Mnyeti hapaswi kuwa kwenye ofisi ya Umma ya Serikali, mambo ya CCM akayafanye kwenye ofisi ya CCM huko. Unamchukua mtu kama Makonda, kila siku anaharibu, alianza madawa ya kulevya, leo...

**MBUNGE FULANI:** *DNA!*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tafadhali.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kupima *DNA.(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tafadhali naomba utulivu. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, malizia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unilinde.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *DNA* niko tayari na naweza kushughulika vizuri.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Amezaa na wewe.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa moja kwa wakati, Mheshimiwa Dokta Mollel.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kwani Mheshimiwa Mollel nawe unataka kupima mbegu? Mheshimiwa Mollel unataka kupima mbegu?

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba utawala bora ni pamoja na uongozi wa kujiongoza mwenyewe. Wabunge hawa waliokaa hapo wanalipishwa kwa mwezi mchango wa milioni 73 kwa kuchangia, lakini wameshindwa hata kuajiri watu wanne wa kuweza kuwasaidia kutengeza *speech* huku ndani waweze kusoma.

**MBUNGE FULANI:** Dokta Shika!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Acha ujinga, pumbavu kabisa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** ...Mimi siendi kwenye *DNA* kwa sababu ni mambo binafsi hayo, lakini kuna mambo mengi ambayo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** ...umesikia mazuzu eeh, misukule wananizomea. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Njaa!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tulieni azungumze, ama sivyo muda nitapunguza. Ongea Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimsaidie huyu bwana bidhaa anayenunuliwa kama karanga barabarani... *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwanaume mzima anauzwa barabarani kama karanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hotuba ya Serikali imeandaliwa si chini ya miezi sita na haijaandaliwa na Waziri, imeandaliwa na timu kubwa, leo mnataka sisi tuandae kwa dakika moja kwa sababu mnaamini tunafanya mchezo hapa, nakupuuza wewe, sijui Daktari wa wapi wewe. Sasa narudi kwenye hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, ama sivyo atakosa muda. Mheshimiwa Mchungaji Peter, endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa tukiishauri Serikali hii na tutaendelea kuishauri...

**MBUNGE FULANI:** Afute kauli.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwashauri juu ya makinikia ni aibu kubwa mkagonga ukuta kwa sababu ya utawala bora ambao hauendani. Tuliwashauri juu ya sukari, tuliwashauri juu ya Bombadia ni kwa sababu ya kuweka watu ambao hawaendani kwenye ofisi, hili ni suala la utawala bora ambalo nazungumiza. Leo mnakosa hoja hapa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter, naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapozungumzia utawala bora, wengi hapa tunapozungumza tumekuwa tukishauri na ndiyo wajibu wetu, tumetoa ushauri mkapiga kelele hapa kwamba tutapewa trilioni 490 ziko wapi leo? Leo kuna watu wanapitapita hapa kuwaambia Wabunge wa CCM msizungumze masuala ya makinikia kwa sababu ni aibu, hakuna hela hizo. Akaja Dokta yule akawaambia atawapa hela, bilioni 300, ziko wapi? Mheshimiwa Dokta Mpango atuambie ziko wapi kwenye bajeti kwenye vyanzo vyake, kwenye mpango wake ziko wapi hizo hela za *Acacia*? Mambo yote yamekuwa ni aibu kwa sababu hamtaki ushauri na unakosekana utawala bora. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kipaumbele cha nchi hii ni kipi katika masuala ya utawala bora?

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi tena?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline.

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, jirani yangu, kwamba kwenye suala la utawala bora analozungumzia ni jambo la msingi sana, lakini pia nadhani kwamba unapoanza kuonesha kidole kwenye jicho la mwenzako tazama kwanza vidole vingine vinne vinakutazama wewe. Nataka kusema tu kwa misingi hiyo ya utawala bora angeanza na yeye mwenyewe, yuko sawasawa? Kwenye suala la *DNA* ameshaenda Dar es Salaam kucheki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe hiyo taarifa; na yule inasemekana ni mke wa mtu.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter, endelea. Mheshimiwa Maryam, hakuna taarifa juu ya taarifa, muache Mheshimiwa Mchungaji Peter aendelee.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mbunge; mama nataka nikwambie niko vizuri sana, kama mnataka suala la *DNA* niko vizuri, labda kama mnahitaji vitu vingine, napo niko vizuri kabisa,

anayetaka kuja aje tu. Kama mnadhani hiyo ni kiki mnapoteza muda niko vizuri kabisa na nina watoto saba. Mawaziri wote tutawapima *DNA* humu ndani, si mnataka tupimane, haina shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza ndiyo haya, tunaacha kuzungumza mambo ya maana tunazungumza mambo ya kipuuzi kwa sababu tuna-*embrace* akili ya kijingajinga, tunaacha kuzungumza mambo ya uchumi wa nchi hii unahangaika na *DNA* yangu, ya nini? Au unanitaka? Hapa *we are talking about serious matters... (Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza masuala ya uchumi katika nchi hii...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnafanya vurugu mpaka muda unamalizika.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza masuala ya barabara mbovu katika nchi hii, tunazungumza masuala ya utawala bora, watu wanakufa, watu wanauawa, unahangaika na *DNA* ya kwangu, haya ndiyo mambo ninayoyazungumza... Bunge ambalo linatakiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa muda wako umekwisha, inatosha. Ahsante sana.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Aah! Wewe vipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii niweze

kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hizi mbili; Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Utumishi.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kazi kubwa anayoifanya. Kiukweli amethibitisha kwamba anaweza, ingawa Wizara hii ina changamoto nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wabunge wote hapa leo ukiwauliza kama kweli tunahudhuria kwenye vikao vyetu vile vya Halmashauri vya Madiwani, hakuna mtu ambaye halalamiki juu ya fedha kutoka Hazina kutopelekwa Halmashauri. Kama kuna Mbunge hapa leo anaweza akatuthibitishia kwamba fedha wanapelekewa kwa wakati na kadri zilivyopagwa basi labda hiyo ni Halmashauri ya nchi nyingine haipo Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo haliko kwingine, tatizo liko kwa Wizara ya Fedha, tatizo analo Mheshimiwa Dokta Mpango. Kwa nini fedha za miradi mikubwa yote, Mheshimiwa Dokta Mpango, anazo, kwa nini fedha za Halmashauri ambako ndiko waliko wananchi, ndiko wanakohudumiwa wananchi wa chini, fedha hana kwa nini? Tunapokwenda kwenye vikao vya Halmashauri, Wakurugenzi tukiwabana wanatuambia ninyi ndiyo mnatoka Bungeni na ninyi ndiyo mko na Waziri wa Fedha huko, muulizeni kwa nini haleti fedha. Kwa hiyo, mtu mmoja ambaye labda anaweza kukwamisha Wizara ya TAMISEMI isifanye kazi vizuri ni Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa sababu hapeleki fedha Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la watumishi, Ofisi ya Utumishi, Mwenyekiti wangu wa Kamati ameeleza hapa kwamba mwaka huu Wizara inayoongozwa na Mzee wangu, Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, bajeti yake imepungua kwa shilingi bilioni 152 kutoka kwenye bajeti ya

mwaka jana na hii ndiyo Wizara inayoajiri, hii ndiyo Wizara inayosimamia Utumishi wa Umma nchi hii. Sasa tunataka Mheshimiwa Waziri atueleze, hiki kiasi kilichopungua cha bilioni 152 maana yake ni nini? Kwamba shughuli za kuajiri hazitafanyika tena, kwamba hakuna ajira mpya, kwamba hakuna promosheni? Maana suala la kuongezwa mshahara nadhani Watumishi wa Umma sasa hivi wameshalisahau, limeshaondoka kwenye utamaduni wa kawaida. Hata hivyo, hata kuajiri hamtaajiri kama shilingi bilioni 152 mnaiondoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida nikisikiliza kwamba Rais anasema mwaka huu tutaajiri, napata shida ukisikia Viongozi wa Serikali wanasema tutaajiri watumishi wa afya, unapokuja kusoma vitabu vya bajeti unakutana na fedha zimepungua kwa bilioni 152, napata shida kuamini kwamba haya yanayosemwa kweli yatatekelezwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye TAMISEMI, nizungumzie suala la zahanati. Kwenye Halmashauri zetu tumejenga zahanati nyingi. Mheshimiwa Waziri, zahanati zimekamilika na nyingine zinabomoka, zimechakaa, zimekaa miaka minne, mitano, hazifunguliwi kwa sababu hazina watumishi. Sasa naomba kujua, nini mpango wake wa kutafuta watumishi wa idara za afya ili waende wakafungue zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu kuna zahanati tano zimekamilika, mbili Mheshimiwa Rais alipokuja mwaka jana mwezi wa Tatu alitoa agizo kwa Mkuu wa Mkoa kwamba hakikisha ndani ya miezi miwili ziwe zimefunguliwa, mpaka sasa zile zahanati hazijafunguliwa. Naomba Mheshimiwa Waziri amfikishie salamu Mheshimiwa Rais kwamba zile zahanati mbili zilizojengwa na mfadhili pale Mchinga na Ruvu ambazo Mheshimiwa Rais alitoa *order* zifunguliwe ndani ya miezi miwili, hazijafunguliwa, naomba ampelekee salamu hizo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI, nimesikitishwa sana kuona kwamba

Mawaziri wanatoa *order* kupeleka kwa Wakurugenzi na Wakurugenzi hawatekelezi, hili jambo linaumiza sana na wala siyo jambo la kushabikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi 2016 humu wakati tunachangia bajeti tulisema kitendo cha Wakurugenzi kuwa wateule wa Rais italeta *contradiction* kwenye Utumishi wa Umma, tulisema humu na mkichukua *Hansard* mtaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mkurugenzi hamuheshimu Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye aliyemteuwa ni Rais na Waziri kateuliwa na Rais na inawezekana ndani ya Chama yeye ni kada mkubwa anawadhifa mkubwa kuliko Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo anaona kwamba mimi ni kada mkubwa na mimi nimeteuliwa na Rais huyo huyo aliyemteua yeye inakuwaje katika mazingira ya kawaida Mkurugenzi anapelekewa *order* na Mheshimiwa Waziri na hatekelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa eti Mheshimiwa Waziri ambaye amedharauliwa kaka yangu Mheshimiwa Kigwangalla, sisi tunakutetea wewe ili ufanye kazi vizuri na wewe unakuja kutetea ulivyodharauliwa! Wabunge hatupendi kuona Waheshimiwa Mawaziri mnadhalilishwa hatupendi kuona mnatoa *order* ambazo Wakuu wa Mikoa ama Wakurugenzi hawataki kuzitii. *(Makofi)*

Najua kwamba najadili bajeti za Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Mpango hili nalielekeza moja kwa moja, Waislamu mwezi huu tunaita mwezi wa Rajab, tuko kwenye mwezi wa mfungo kumi, tunakaribia kabisa kuingia kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhan kufunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuulize Mheshimiwa Mpango, hivi Serikali hii itashindwa kuongoza, mtashindwa kukusanya kodi ikiwa tu mmeachia tende ziingie bure ikiwa tu tende peke yake mtaziruhusu ziingie bila kodi mtashindwa kuongoza Serikali? Kenya tende zinaingia *free*, Mozambique tende zinaingia *free*, Zanzibar wana mwaka wa saba tende *free,* huku Bara tende zinatozwa kodi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme inawezekana hamtuelewi tukisema kwamba, moja ya nguzo kubwa kabisa za Uislam ni kufunga na tunapofunga kuna sunna na kuna mambo ya faradhi. Jambo kubwa katika sunna katika funga ya Ramadhan ni Muislam kufungua kwa kutumia tende, leo tende mnaitoza kodi, hivi Kenya na wenyewe hawatozi kodi tende, Mozambique hawatozi kodi tende, Zanzibar hawatozi kodi tende na ninyi hapa jamani hamuoni aibu au ndiyo yale aliyosema bwege Waislamu hawana wa kuwasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali, tunaendelea na Mheshimiwa George Lubeleje na baadaye Mheshimiwa Angelina Malembeka ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hizi mbili. Kwanza niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, niwapongeze Watendaji wote wa Wizara hizi mbili kwa kazi nzuri. Nchi hii ina utawala bora, ndiyo maana tumetulia, ndiyo maana tuko hapa Bungeni tunafanya vikao bila wasiwasi nchi imetulia na *good governance* ni kwa sababu ya *political stability*. Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia kwamba ni Vyombo vya Usalama ndiyo vinafanya kazi nzuri, ndiyo maana tunatembea hata saa nane za usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni mapato ya Halmashauri. Sifa ya Halmashauri yoyote ile ni mapato, kukusanya mapato ya ndani, kama Halmashauri haikusanyi mapato ya ndani haina sifa ya kuitwa Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, wakati wa Kamati tuliwaeleza Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi Watendaji wajitahidi kukusanya mapato ya ndani wasitegemee zaidi ruzuku maana ipo siku moja Serikali ikisema kwamba ruzuku tunafuta, Halmashauri zitashindwa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niongelee suala la migogoro katika Halmashauri. Bahati nzuri mimi nimekuwa Diwani na Mwenyekiti wa Halmashauri miaka 15, kuna migogoro mingine inasababishwa na Wakurugenzi, Diwani ni haki yake kulipwa posho kila mwezi, lakini Madiwani wanakaa miezi miwili, mitatu, minne bila kulipwa posho hapo mgogoro lazima utakuwepo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mwingine ni kutokufahamu majukumu ya Madiwani. Tuliokuwa Madiwani zamani tulipelekwa Hombolo kwa ajili ya mafunzo ya mwezi mmoja, lakini hawa Madiwani wa siku hizi hawapelekwi na hivyo hawajui mipaka yao; mipaka ya Watendaji na mipaka ya Madiwani. Kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, muwapeleke mafunzo angalau wiki mbili hawa Madiwani waweze kujua mipaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni posho za Madiwani. Posho za Madiwani wanazolipwa, mwaka 2002 wakati Mheshimiwa Mizengo Pinda akiwa Waziri wa TAMISEMI aliunda Tume ya kushughulikia maslahi ya Madiwani na Tume ile iliongozwa na mimi mwenyewe na ikaitwa Tume ya Lubeleje. Kwa hiyo, mpaka leo wanapata kiwango kilekile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri majukumu ya Madiwani wa zamani na sasa ni tofauti. Zamani Madiwani ukiamka asubuhi unakwenda kwenye kikao ukitoka kwenye kikao unarudi nyumbani unapumuzika. Siku hizi mradi ukianza wa shule mradi wa zahanati lazima Diwani ushinde pale. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana angalau wawaangalie waongeze posho kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo lingine baada ya kuongezwa hii posho kidogo, Madiwani walikopa benki, wengi walikopa *CRDB*, walikopa *NMB,* sasa bahati mbaya sana kuna Wakurugenzi hawakati zile fedha na kupeleka kwenye haya mabenki. Kwa hiyo, mgogoro mkubwa sana, vyombo vya fedha *NMB* na *CRDB* wanaanza kuwafuata

Madiwani kwamba ninyi ndiyo mliokopa lakini mishahara yao imeshapelekwa Halmashauri, hawalipwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mishahara ya watumishi, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, wakati umefika ndugu zangu tuangalie watumishi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, maisha na gharama zinapanda kila kukicha. Sasa ufinyu wa bajeti sidhani na sitegemei kuna mwaka mmoja Serikali hii itasema sasa tuna fedha za kutosha, hakuna! Kwa hiyo, tuwafikirie Watumishi wanafanya kazi ngumu sana, sifa ya Tanzania wanaleta watumishi kwa kufanya kazi nzuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kucheleweshwa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Sasa Mheshimiwa mmoja amesema kwamba sisi ambao tunahudhuria vikao kwenye Halmashauri tusilalamike. Hii ni ruzuku ya Serikali Kuu na sheria inatamka kwamba Serikali Kuu ni lazima isaidie Halmashauri itoe ruzuku. Wabunge tunakaa hapa miezi mitatu kupitisha bajeti ya Serikali, lakini bahati mbaya sana fedha ambazo zinaidhinishwa hapa hazifiki zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati tunachambua bajeti ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa wengi mpaka hadi Februari, 2018 fedha ambazo wamepokea ni kati ya asilimia 51, 48, 60 lakini fedha nyingine hazifiki kwenye miradi. Kwa hiyo, ukitembelea Halmashauri nyingi kuna viporo vingi sana zahanati hazikamilishwi, vituo vya afya havikamilishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kuniletea shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Mima. Kazi inakwenda vizuri bado kuna Kituo cha Afya cha Mbori ambacho ujenzi wake bado kabisa na kile kituo kikishakamilika kitahudumia Kata Nne; Kata ya Kimagai, Kata ya Lupeta, Kata ya Matomondo na Kata ya Mlembule. Kwa hiyo, naomba milioni 500 zipelekwe tena Mbori kwa ajili ya kukamilisha kituo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nimalizie, ni suala la upungufu wa watumishi. Serikali inasema ombeni vibali, Wilaya ya Mpwapwa tuna upungufu wa Watumishi wa huduma Idala ya Afya zaidi ya 150, tumeleta juzi kuomba kibali watumishi 150, tumepewa watumishi sita tu. Kuna Kada zingine zile ambazo ni ndogondogo mziachie Halmashauri ziajiri badala ya kuomba kibali Utumishi ndiyo tuwaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Niwapongeze sana Mawaziri na Watendaji wao wanafanya kazi nzuri, ila wajitahidi sana kutembelea Majimbo yetu kwa sababu ukitembea kwenye Majimbo ndiyo unaona changamoto za kila Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Tunaendelea na Mheshimiwa Angelina Malembeka, baadaye Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Mboni Mhita wajiandae.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniapa nafasi na niungane na wenzangu wote kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Naibu Mawaziri wote wawili na Watendaji wao wote katika Wizara zao. Pamoja na pongezi zao hizo kipekee naomba niwapongeze madereva wao wote, wahudumu wao wote, na masekretari wao wote ambao wamefanya kazi hadi na wao wakaweza kuwakilisha hapa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu naomba nianze na Usalama wa Taifa. Mwaka jana wakati nachangia nilizungumzia suala la Usalama wa Taifa na hoja kuu ilikuwa suala la kutekwa nyara, nilisema hapa kutekwa nyara siyo mchezo, wengine wanajifungia ndani halafu wanapiga simu wametekwa nyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema naomba sehemu hii iongezewe pesa ili waweze kupata mafunzo zaidi na kununua vifaa zaidi vya kisasa, nafikiri kwa kufanya hivyo tutaweza kupunguza suala la kupekuliwa pekuliwa asubuhi, kuvuliwa nguo, kuvuliwa viatu na hata kufikia kwenye sehemu ya kwamba tunakuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni tumejionea jinsi watu wanavyojiteka nyara wenyewe na kufanya hii Idara ionekane kwamba haifanyi kazi wakati Idara hii inafanya kazi vizuri. Niombe Idara hii iendelee kuongezewa pesa ili wapate mafunzo zaidi na vitendea kazi ambavyo hata sisi vitatusaidia kutovuavua mikanda pale mlangoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, napenda nichangie kuhusiana na maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Viongozi wa Umma wanafanya kazi vizuri sana wamekuwa wepesi sana wa kutukumbusha kujaza fomu ni vizuri pia. Katika kutukumbusha kujaza fomu basi kama kuna kitu kinatakiwa basi wakiingize kabisa pale ili tunavyorudisha zile fomu twende nazo sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti hii iongezeke zaidi badala ya kuangalia tu zile fomu twende kwenye neno kamili Maadili ya Viongozi, kama watavuka kufikia huko nafikiri hakuna Kiongozi atakayeitwa na Mheshimiwa Makonda hapa, hakuna Kiongozi atakayepelekwa Ustawi wa Jamii, hakuna Kiongozi tutakayemwona huko mitaani anatangazwa kwenye magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wajitanue zaidi wapewe pesa wajitanue zaidi watufuatilie kweli Viongozi maadili ni kweli au ni fomu tu hizo za kuhakiki mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Idara hii imekuwa inafanya kazi vizuri, niipongeze Serikali kwa kuboresha majengo yao yote, wamefanya kazi vizuri sana, sasa hivi majengo yale matunzo yanaonekana, vifaa vinatunzwa kisasa na wafanyakazi wako kwenye amani. Hata hivyo,

hawana pesa za kutosha kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali na kuweza kupata kumbukumbu mpya na nyaraka mpya ambazo nyingine ziko mikononi mwa watu huko vijijini. Kuna watu wana historia ya nchi hi, kuna watu wana kumbukumbu nzuri lakini wanashindwa kuzileta. Ni vizuri basi wakaongezewa pesa ili wafanye utafiti wa kina na kwenda kwenye maeneo mbalimbali ili tuweze kupata kumbukumbu nyingine na kupata nyaraka nyingine ambazo bado ziko mikononi mwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusiana na suala la utawala bora. Kazi imefanyika vizuri niwapongeze sana, lakini kuna baadhi ya Halmashauri kazi haziendi. Vikao vya Halmashauri vya kikanuni haviendi vimekuwa vikikatizwa mara kwa mara na wengine wanaitwa tu kipindi cha kupitisha bajeti sasa hii imekuwa ni tatizo. Tatizo la posho liko palepale, Diwani anaidai Halmashauri, Diwani utaidaije Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona Halmashauri zijipange, tunategemea kwamba tuna Wakurugenzi wazuri ambao ni wabunifu, basi waendelee kubuni mbinu mbalimbali ya kujipatia pesa ili kuweza kuziendesha zile Halmashauri, pia kuondokana na migogoro ya madiwani. Posho ya Madiwani pia ni ndogo, tunazungumza mara nyingi jamani mishahara ya watumishi tuongeze lakini haijazungumziwa Madiwani. Madiwani ni muda mrefu wanafanya kazi na posho ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki miezi mitatu yote Wabunge tuko Bungeni, lakini Madiwani bado wako na wananchi, shida za wananchi wanazo Madiwani, lakini bado posho iko vilevile, nimwombe Mheshimiwa Waziri waliangalie hili kuhusu posho ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine tena ambalo limezungumziwa juu ya kujipanga kwa ajili ya chaguzi za Serikali za Mitaa 2019. Nimefurahi kwamba mmeliona mapema na mmejipanga. Hata hivyo, wakati tunalipanga hili tuangalie kuna Kata nyingine, Mitaa mingine na Majimbo

mengine ni makubwa kuliko tunavyofikiria. Kuna mitaa ambayo ina watu 10,000, nikitolea mfano katika Kata ya Msongola kuna mtaa wa Yangeyange una watu zadi ya 10,000, kuna mtaa wa Mbondole una zaidi ya watu 6000, sasa huo unakuwa mtaa au unakuwa kata. Ni vizuri basi wakati tunapanga uchaguzi huu wa mwaka 2019, basi waangalie jinsi gani ya kupunguza baadhi ya mitaa baadhi ya Kata na baadhi ya Majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusiana na uchelewaji wa fedha za maendeleo katika Halmashauri, kwa kweli hiki ni kikwazo kikubwa sana ambacho hata Wabunge tunapoenda kwenye miradi mbalimbali kukagua huwa tunashikwa na butwaa kwamba tumepitisha pesa, wale wako tayari kufanya kazi lakini pesa haziendi. Basi ni vizuri tunavyoidhinisha kwamba pesa fulani ziende basi ziende kwa wakati na ikiwezekana ziende zikiwa zimekamilika ili miradi ile iweze kukamilika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *TASAF* na MKURABITA;, *TASAF* na MKURABITA imesaidia sana wananchi, sasa hivi wako katika mazingira mazuri sana, tumeangalia katika awamu ya tatu ya *TASAF* uwezeshaji wa wananchi kiuchumu wananchi sasa hivi wengi wameweza kupeleka watoto shule, wameweza kupeleka watoto kwenye zahanati na wameweza kubuni miradi mbalimbali ambayo inawaongezea kipato na hivyo kuwanyanyua kiuchumi. Ni vizuri basi hii sehemu ya *TASAF* ziongezewe pesa na ziende kwa wakati ili waweze kufanya kazi vizuri wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika MKURABITA kazi imefanyika vizuri na akinamama wengi safari hii wameweza kunufaika na MKURABITA. MKURABITA vijana hawajanufaika, naomba utaratibu upangwe ili vijana nao waweze kunufaika katika mradi mzima wa MKURABITA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumzie kuhusu *TARURA* niipongeze kwanza *TANROADS* kwamba imefanya kazi nzuri katika barabara kuu, barabara ni nzuri

zinapitika, lakini huku kwenye *TARURA* bado pesa ni ndogo za kufanyia kazi barabara zile ni nyingi na fedha ni ndogo, kama ingewezekana tufanye mageuzi mazuri *TANROADS* wapewe asilimii 30, *TARURA* wapewe asimia 70 ili zile kazi za *TARURA* ziweze kuonekana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusiana na taulo za kike. Taulo za kike limekuwa gumzo, lakini wachache ambao wamekubali kuwa wawazi, wapo akinadada ambao ni wasichana wanashindwa kabisa kwenda shule wanapofikia katika siku zao kutokana na kukosa taulo za kike. Wengine wanaamua kujistiri hata kwa majani au matambala mabovu ilimradi tu aende shule, yule mwenye moyo mdogo akifikia hali ile anaamua kotokwenda shule kabisa na hivyo kufanya mtoto wa kike ashindwe kuhudhuria masomo na kupoteza mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yake azishauri Halmashauri, tunayo mikoa ambayo inalima pamba na kama inalima pamba na sasa hivi tuna Tanzania ya viwanda, kwa nini ile mikoa isitengeneze viwanda vidogovidogo vya kutengeneza hizo pamba angalau za kuwastiri akinadada halafu ziuzwe kwa bei nafuu au ikiwezekana zitolewe bure kwa wanafunzi ili waweze kushiriki vizuri masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitoe shukrani zangu na pongezi kwa Wenyeviti wangu wa Kamati wote wawili, wameonesha ushirikiano mzuri, kubwa zaidi kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, niseme kwamba Mawaziri wetu wanashaurika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Malembeka. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa, baadaye Mheshimiwa Mboni Mhita ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hotuba mbili za Mawaziri wawili wa TAMISEMI pamoja na Utawala Bora. Naomba uniruhusu niwashukuru sana Viongozi wangu wakiongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunipa salaam za pole baada ya kupata msiba wa marehemu mama yangu, nawashukuru sana kwa pole hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niruhusu niwapongeze sana Mawaziri hawa wawili kwa maana ya Mheshimiwa Selemani Jafo pamoja na Mheshimiwa Kapt. Mst. George Mkuchika ni Mawaziri wanaochapa kazi zao vizuri na hotuba zao kwa kweli zinajielekeza wazi. Mchango wangu nitajikita sana katika kushauri na kuomba, lakini namwomba Mwenyezi Mungu anijaalie ili niishauri vizuri Serikali nisiende kwenye mkumbo ule mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza, nivipongeze sana vyombo vya usalama, vyombo vyetu hivi vinafanya kazi nzuri sana Usalama wa Taifa, pia TAKUKURU wanafanyakazi nzuri sana na niwaombe viongozi wao wakuu tunapoambiwa kwa mfano, makusanyo kuanzia Julai mpaka Machi kupitia *TRA* tumeweza kukusanya shilingi trilioni 11.78, nina uhakika kwamba TAKUKURU, Usalama wa Taifa wao ni wadau wakubwa sana kwa sababu mianya mingi ambayo imekuwa ikijitokeza wao wamekuwa jicho la kwanza kuiona na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili twende mbele zaidi, nawaomba sana wenzetu hawa wa Vyombo vya Usalama na TAKUKURU, katika nchi yetu hii ninyi ni watu muhimu kweli hasa kwenye suala zima la uchumi wa nchi yetu na usalama wa nchi yetu. Kwa hiyo, ombi langu kwenu ni kwamba endeleeni kuwa wazalendo kwa nchi hii ili kuweza kuokoa rasilimali za nchi yetu. Mkiwa wazalendo hata haya tunayoyazungumza humu ya mapato, upungufu huu, nafikiri mtatusaidia kabla hatujaenda kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, narudia tena, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, *TIS*

nawashauri sana kwa sababu ninyi ni watalaam, mnajua mambo mengi, tunaweza tukakusanya pesa nyingi zaidi mkiamua kutusaidia, tunaweza tukazuia mambo mengi mkiweza kutusaidia kwa kutumia vizuri weledi wenu, nafahamu ni watalaam. Hebu ongezeni weledi wenu najua ni wazalendo sana sina shaka na hilo, lakini ongezeni jitihada ili kusudi nchi yetu iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *TARURA*. Chombo hiki tumekianzisha juzi ni chombo kizuri sana. Nina ushauri kwamba tulipoanzisha Mfuko wa Barabara tulikubaliana kwamba tuweke asilimia 70 kwa 30 ili asilimia 30 hii iende kwenye barabara za vijijini kwa maana ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwa sababu nia ni njema sana, tunaambiwa kuna kilometa zaidi ya laki moja, kwa pesa hii ya asilimia 30, naona kama vile haitoshi. Naomba kwa sababu tulianzisha Mfuko huu kwa Sheria ya Mfuko wa Barabara, niiombe Serikali ilete *amendments* ili tujaribu kubadilisha kwa jinsi tutakavyoona inafaa, kwa sababu hatuwezi tu kuamua hapa sasa hivi, ni lazima tulete mabadiliko ya sheria kwa sababu Mfuko huu tulianzisha kwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo napendekeza kwa kuanzia na Wabunge tunaweza tukaridhia, tutoke kwenye asilimia 70 twende kwenye asilimia 65, twende taratibu ili tusiathiri upande mwingine, tufanye 35 kwa 65. Nafikiri kwa kufanya hivyo tutakuwa tumesaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa sababu ya pesa hizi kidogo na makusanyo yetu hayajatengemaa vizuri na jambo hili nililisema huko nyuma wakati Waziri wa TAMISEMI akiwa marehemu Kingunge Ngombale Mwiru. Lazima tufike mahali tuzisaidie Halmashauri zetu, kwa sababu ya pesa hizi kidogo tukiamua kama ni mwakani au lini, tukiamua kila Halmashauri ikawa na *grader* lake kwa ajili ya kutengeneza barabara zinazoharibika, ni uamuzi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Halmashauri ikawa na *Grader* hizi pesa kidogo kidogo hizi tunazokusanya, barabara inapoharibika mara moja mnaweka mafuta, *grader* inakwenda kutengeneza barabara inapitika asubuhi na mchana lakini inapitika masika na kiangazi ni suala la uamuzi. Kwa zile Halmashauri ambazo zina *grader* nafikiri barabara zao huwa haziharibiki mara kwa mara. Huo ulikuwa ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la Jimbo. Naomba Mheshimiwa Jafo nilishakwenda kwake, Waziri wa Elimu anisaidie shule zangu mbili za sekondari na huwa napata tabu wanapogawa pesa wanasema shule kongwe, lakini kuna shule moja kongwe, shule ya wasichana, Sumve *Girls* ya *A-Level.* Inachukua wasichana kutoka nchi nzima wanachaguliwa wa Lindi wapo, kutoka Mtwara wapo, wanakwenda Sumve kusoma pale, ni shule ya siku nyingi. Shule hiyo amesoma Mama Maria Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali mahitaji yao wanayo, upanuzi wao wanahitaji mabweni mawili, madarasa manne, bwalo moja na jengo la utawala moja, kiasi cha shilingi kama zaidi ya milioni 400. Naomba sana Serikali shule hii ya wasichana waiangalie kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Pia kuna shule ya Taro. Kuna pesa zilitolewa mwanzo milioni 206 cha kushangaza Serikali kwa makusudi ikaja ikazibeba zile pesa zote, baadaye ikarudisha milioni 80. Nakuomba sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Jafo, nilishakwenda ofisini tukazungumza na watu wake, nikaenda kwa Mama Ndalichako, Waziri wa Elimu, nikazungumza naye, pesa hizo mpaka leo hazijarudi. Naomba ili tukamilishe mabweni mawili, madarasa manne, maabara mbili, tunahitaji milioni 168 ili kukamilisha kazi iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri pia hivi sasa kuna ongezeko kubwa la wanafunzi kuanzia ngazi ya chekechea, shule ya msingi mpaka sekondari, sina uhakika

tumejiandaa namna gani. Kwa ongezeko hili kufuatana na maelezo ya kitabu chako, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ni lazima tuangalie sasa miundombinu ya madarasa, vyumba vya Walimu, vyoo pamoja na Walimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ndassa muda wako umemalizika.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mboni Mhita na baadaye Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Neema Mgaya wajiandae.

**MHE. MBONI M. MHITA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kutumia fursa hii kwanza kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Jafo kwa kiasi cha shilingi milioni 400 ambacho wametuletea Handeni Vijijini kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata ya Kabuku. Pia ninashukuru sana maana nimeona tumetengewa bilioni moja na milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Mkata katika Jimbo la Handeni Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuna changamoro kubwa sana, naomba nikupe taarifa kwamba Wilaya ya Handeni kwa sasa ina Halmashauri mbili, Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Handeni Vijijini, kwa maelekezo ambayo tulikuwa tumepata ni kwamba Halmashauri ya Handeni Vijijini iondoke kwenda kuanza Ofisi mpya na zile Ofisi ambazo tulikuwa tukichangia na wenzetu wa Halmashauri ya Mji tuwaachie wenzetu wa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ni kwamba tulikuwa tunategemea pesa kutoka kwenye Serikali ili Handeni Vijijini tuweze kuhama na kuanzisha ofisi mpya. Kwa mshangao mkubwa zimeingia fedha kiasi cha bilioni 3.3 kwa maelekezo kwamba zile fedha ziende kwenye Halmashauri ya Mji ambao wao tayari wana ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na hili nilishaongea na kaka yangu Mheshimiwa Jafo na nikamweleza mshangao mkubwa ambao nimeupata, kwa sababu nilitegemea hizi fedha zioweze kuja kwenye Halmashauri ya Handeni Vijijini ili ambao hatuna ofisi tuweze kuhama, lakini kwa mshangao mkubwa ni kwamba hizi fedha sasa zimekwenda kwenye Halmashauri ya Mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ni kwamba hizi fedha za miradi ambazo zimekuwa zikija katika maeneo yetu ni fedha nyingi ambazo kwa namna moja ama nyingine zinahitaji uangalizi wa hali ya juu na ndiyo hapa sasa nitaingia upande wa baba yangu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na nitajikita zaidi kwa *Prevention and Combating of Corruption Bureau* (TAKUKURU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba rushwa inachangia umaskini kwa kasi ya juu sana. Ni dhahiri kwamba unapodhibiti upotevu wa fedha kwenye maeneo mbalimbali basi ni hakika kwamba unapunguza umaskini. Nayasema haya kwa sababu mimi ni mwanamke na nimeona ni jinsi gani ambavyo wanawake na akinamama wa Jimbo la Handeni Vijijini wamekuwa wakitembea umbali mrefu, wakihangaika kwenda kutafuta maji na siyo kosa lao na wala siyo kosa la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetuletea pesa kwa ajili ya miradi ya maji, lakini nasikitika kusema kwamba miradi yote ya maji ambayo ililetewa fedha katika Jimbo la Handeni Vijijini hakuna hata mradi mmoja ambao tumeona matokeo yake, kwa nini? Kwa sababu kumekuwa na ubadhirifu mkubwa sana wa fedha na kuna harufu ya rushwa katika miradi yote. Kuna mradi mmoja wa mabwawa ambao

uliingiziwa bilioni nne na zile fedha mpaka leo zimeingia kwenye huo mradi, lakini mradi ule mpaka leo hakuna ambacho tumekiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na mradi wa visima ambao mpaka leo wananchi wa Jimbo la Handeni Vijijini hakuna ambacho wamenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sasa kifanyike? Naomba Serikali iweze kwa namna moja ama nyingine kuwawezesha wenzetu wa *PCCB* ama TAKUKURU kwa namna zifuatazo:-

Kuna maeneo mengine ambayo tumejionea kabisa kwamba Ofisi za TAKUKURU haziko katika kiwango ambacho kinatakiwa ama zile *basic needs* za ofisi, pia wawezeshwe kwa vitendea kazi kama magari. Nasema haya kwa sababu wangekuwa na vitendea kazi ambavyo viko imara hakika wanaweza kufanya kazi zao kwa umahiri na kufika kwenye maeneo hayo na kuepusha upotevu mkubwa sana wa fedha ambazo kuna baadhi ya Watumishi wamekuwa siyo waaminifu sana, wamekuwa wakitumia zile fedha kwa manufaa yao wenyewe na matokeo yake wananchi wetu wameendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu, naomba nitoe *reference* kwa wenzetu wa Luxemburg, wenzetu wa Sweden ambao wao wana *National Anti-Corruption Unit,* wenzetu wa Finland ndiyo Mashirika makubwa ama taasisi kubwa za uzuiaji wa rushwa duniani zinazoongoza. Kigezo kikubwa ambacho kimefanya hizi taasisi katikan hizi za Sweden na Finland kuongoza ni kwa sababu ya *transparency* na *access to information* ama uwazi na upatikanaji wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ofisi zetu ziwe na ushirikiano na wenzetu hawa wa TAKUKURU ili taarifa ziweze kupatikana, kwa sababu kama tunavyoona hawa ni *prevention and combating,* lakini tumezoea kuona kwamba wao wanafanya *combating* zaidi siyo *prevention.* Kwa hiyo, naamini kwamba wakiwa na *access* ya kupata taarifa basi wataweza kuepusha matumizi mabaya ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niokoe muda wako, naomba nihitimishe kwa kusema tu:-

Moja; naomba sana Serikali itusaidie kuweza kuona nini ambacho kimetokea katika Wilaya ya Handeni hasa kwenye hizi bilioni tatu na milioni mia tatu. Mbili; Uwezeshwaji wa wenzetu wa TAKUKURU. Tatu; Waweze kupata ushirikiano hasa kwenye *access to information* na *transparency* ambayo ni uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mboni Mhita. Tunaendelea na Mheshimiwa Mendrad Kigola baadaye Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Ahmed Shabiby wajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara ya TAMISEMI na Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizi ni nyeti sana kwa sababu ni Wizara ambazo zinaleta maendeleo ndani ya nchi yetu. Kwanza kabisa nitoe pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Magufuli kwa kazi yake nzuri anayoifanya. Pia nitoe pongezi kwa Mawaziri wote kwa ujumla wake, sana kwa Mawaziri hawa wa Wizara ambazo tunazijadili leo hii. Mheshimiwa Waziri Jafo kwa kweli kazi unafanya vizuri na Naibu Mawaziri wote wawili kazi wanafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wakuu wa Mikoa nawapa pongezi sana kwa sababu nikitoa mfano, Mkuu wangu wa Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Amina Masenza anafanya kazi nzuri sana nampa pongezi. Vilevile *DC* wetu pamoja na Mkurugenzi wetu, wote wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema utawala bora lazima tuwe makini sana. Kwanza wewe unayejadili utawala bora lazima ujipime. Kwa mfano, hawa watu niliowataja ukiangalia *profile* yao imesimama iko vizuri na wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, kwenye utawala bora binafsi naona wamekaa vizuri na nchi hii inapiga hatua na tukisema uchumi unakua ni kwa sababu ya utawala bora, kama utawala bora haupo uchumi hauwezi kukua, lakini sasa hivi Tanzania uchumi unakua na sasa tunakwenda 6.8, tuko mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya niliyochangia kwenye utawala bora, naishukuru Serikali kwa upande wa afya kwa kweli wameenda vizuri sana. Nikichukua kwa ujumla wake katika Wilaya yangu ya Mufindi tunaenda vizuri. Serikali imeangalia sana vituo vya afya na wameangalia Tanzania nzima, lakini wamekuja mpaka Wilaya ya Mufindi. Kwenye Jimbo langu la Mufindi wameleta milioni 400 na mpaka sasa hivi kituo cha afya cha Malangali kinatengenezwa vizuri sana na wananchi wanaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunajenga hospitali ya Wilaya ya Mufindi ambayo sasa hivi Serikali imeshatutengea *1.5 billion* kwa ajili ya kujenga hospitali ya Wilaya. Tunawapa pongezi kubwa sana, naiomba Serikali tukimaliza ile hospitali ya Halmashauri, naomba ile hospitali ya Wilaya ambayo iko Mafinga basi tuifanye Hospitali ya Rufaa. Tukifanya hivi wananchi wanaweza wakatibiwa vizuri, tukiwa na hospitali ya rufaa tunajua huduma zitakuja zitakuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye mpango, kwamba mna mpango wa kuboresha vituo vya afya vyote Tanzania nzima vikiwepo na vile vya Mafinga vya Wilaya Mfindi. Jana wakati nauliza swali la msingi niliuliza Vituo vya Afya vya Mninga na Mtwango pale. Bahati nzuri Serikali imejibu vizuri imesema tayari vifaa wameshaandaa na wamesema kufikia mwezi wa Tano watakuwa wameshamaliza, hiyo ni juhudi nzuri sana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vizuri vinavyofanyika lazima tupongeze ukidharau na kile kizuri wewe tayari unafanya dhambi, binafsi naipongeza sana Serikali na Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo, nakuomba sana hivi vituo vya afya ambavyo tayari na fedha unayo na mipango imekaa vizuri, basi umalizie kama ulivyosema mwezi wa Tano utakuwa umemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kidogo kwenye suala la viwanda, bahati nzuri Wilaya ya Mufindi tuna viwanda vingi sana, lakini tuna kero moja ya ukusanyaji wa kodi *TRA* pale. Mfanyabiashara anatakiwa alipe kodi lakini asidharaulike, hivyo, wakusanyaji wanaokusanya kodi wasiwadharau wafanyabiashara. Kuna kitu kinaitwa lugha ni kitu kidogo sana, ukienda kukusanya kodi ukisema kwamba asipolipa kodi labda utamfungia biashara yake tayari unamkatisha tamaa. Naiomba Serikali watu wanaotoa lugha mbaya kwa wafanyabiashara wasifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunajua tuna viwanda vingi, bahati nzuri naipongeza Serikali na Mheshimiwa alikuwa anasema kule Mkuranga kuna viwanda karibu 80 na Mufindi tuna viwanda vingi tena ni viwanda vikubwa, tukitaja viwanda kuna viwanda vingine ni vikubwa. Kuna kiwanda kimoja mimi sijakipenda sana, kuna hiki kiwanda kinachochinja wanyama wanachinja sana punda, hiki kiwanda sijakipenda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wanyama ambao wanatumika kwa binadamu kwa kazi za binadamu za kila siku, punda anatumika kubeba mizigo, punda anatumika katika kulima, lakini kwa nini tena punda uanze kumla? Hiyo sijaipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka miaka ya nyuma Wahehe walikuwa wanachinja mbwa, lakini baada ya kugundua kwamba mbwa ni askari wa kulinda usiku wakaacha kumchinja. *(Makofi/Kicheko)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni wetu

hatujazoea kuchinja punda, naomba punda wasichinjwe waachwe, kile kiwanda cha punda tusifuate Wachina, kama kwao wanachinja basi wawe ni Wachina, lakini kwetu huku tuna viwanda vingi ambavyo vinaweza vikatuingizia hela nyingi, tuachane na viwanda vya punda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji, Waziri wa Maji nakupongeza sana alikuja kule Mufindi alifanya kazi moja nzuri sana. Ile kazi kwanza Wabunge na Madiwani alitupatia semina Waziri wa Maji ilikuwa nzuri sana. Bahati nzuri tukagawanya fedha tukasema kwamba ile Kata ya Nyororo sasa ipate maji ya *gravity* kwa sababu tulikuwa tunachimba tu visima na akasema tuachane na visima sasa maji ya bomba yatakuwepo, mlolongo ulikuwa mzuri sana pale Igowole tukafanya vilevile na mradi wa Sawala tukafanya vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji sasa kwa sababu fedha zipo, naomba usimamizi uende *speed* kwa vile tulisema kufikia mwezi wa Sita na Saba ile miradi itakuwa imekamilika. Sawala Mkandarasi yuko *site,* lakini bado *speed* ile ndogo sana, kwa sababu manunuzi tu yanachukua karibu miezi miwili. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa sababu *system* ya maji na vituo vya afya viko kwako tunaomba usimamizi wa maji ukae vizuri kama tulivyokuwa tumeahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya barabara hasa zile za vijijini. Barabara tumepeleka *TARURA* lakini usimamizi bado unalega sana kwa sababu zamani kwenye Halmashauri tulikuwa na mpango kila mwaka barabara zinatengenezwa, unaweza ukaona labda tumepanga barabara tano, kwa mfano pale Mafinga Wilaya ya Mufindi tuna Majimbo matatu kwa kila Jimbo kila mwaka kwa mfano kwa Mheshimiwa Mgimwa zilikuwa zinawezekana kutengenezwa hata barabara tano, kwenye Jimbo langu la Kusini zikatengenezwa barabara hata tano, lakini sasa hivi kwa mfano kwangu inatengenezwa barabara moja tu.

Naomba sasa kuna barabara ya Maguvani inakuja Mtambula mpaka Kilolo, imeharibika haipitiki kabisa na iko *TARURA* naomba ile barabara itengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna inatoka hapa Sawala inaenda Kata ya Luhunga mpaka kule Iyegelo, ni mbovu na maeneo yale kuna wakulima wa chai, wanashindwa kusafirisha chai, naomba ile barabara itengenezwe. Inaanzia Sawala inaenda kata ya Luhunga mpaka Iyegelo kuna wakulima wamekamilika, ni wafanyabiashara wazuri sana, sasa naomba TAMISEMI isimamie ile barabara iweze kutengenezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tuna ujenzi hospitali kubwa, bahati nzuri Serikali niipongeze mlishatutengea 1.5 bilioni, tunategemea mwaka huu tunaanza kujenga ile hospitali na niliomba ramani, mkitupatia mapema sana nategemea haiwezi kuchukua mwezi mzima kutafuta ramani tu, hiyo *just a week* labda wiki mbili, tatu ili tuanze ujenzi, wananchi kule wamelipokea vizuri sana, Wilaya ya Mufindi nzima wamewashangilia, wakati Waziri anajibu swali waliwashangilia sana wananchi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameshaleta *proposal* tayari kwa Wabunge, wamesema ile hospitali ikijengwa basi hospitali ya Mafinga itakuwa Hospitali ya Rufaa na Mheshimiwa Mgimwa Mbunge wa Jimbo la Kaskazini tulikuwa tumekaa tumejadili kwamba ile hospitali tukikamilisha itasaidia Wilaya nzima na hospitali ya Mafinga tutawapunguzia idadi ya wagonjwa kutibiwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi kila siku analalamika hapa anasema ile hospitali inazidiwa, lakini kama hospitali ya Mafinga kwa mfano wagonjwa wale wakatibiwa kwenye hospitali hii ambayo tunajenga na hospitali ya Mafinga ikawa Hospitali ya Rufaa na ikaongezewa huduma tukapata Madaktari, basi Majimbo haya yatakuwa yamekaa vizuri na Wilaya nzima itakuwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali imepanga vizuri sana kwamba watatuletea fedha, lakini fedha zije haraka, bahati nzuri wananchi wa Wilaya yetu ni waaminifu sana walitoa eneo bure bila *compensation,* walitoa bure wakasema kwa sababu tunajenga hospitali, basi ngoja tutoe eneo, tumepewa tayari kubwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwenye hilo kwamba itasimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee suala la umeme. Kwanza Serikali imefanya vizuri sana, watu wa *REA* wako *speed* na bahati nzuri wamezunguka katika Majimbo yote. Jimbo la Kaskazini wameenda kwa Mheshimiwa Mgimwa, kwangu Kusini kule wamekuja, katika vijiji vyote wanafanya vizuri, lakini kuna changamoto moja imejitokeza; wale wataalam wakifika pale kufanya *survey* walikuwa wanaishia sehemu; wanaonesha kwenye vitongoji vingine walikuwa hawendi, kwa hiyo kuna vitongoji bado havijafanyiwa *survey*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wabunge tutaandika vitongoji vyote ambavyo hawajafanya *survey* ili tukuletee Waziri wa Nishati aingize kwenye ule mpango wa *REA* ili viweze kupewa, bahati nzuri Waziri wa Nishati yuko vizuri, hotuba zake huwa nazifuatilia vizuri sana na anafanya ziara kila Jimbo hata kwangu alishakuja pamoja na Naibu wake, wote wawili wako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *speech* zao ukizisikiliza ziko vizuri, walisema kwamba siyo *issue* ya kuweka nguzo watu tukaangalie nyaya walisema ni *issue* ya kupeleka kwenye kaya, tuone nyumba *by* nyumba zina umeme na wananchi nimeshawaambia nitapita kila nyumba nione kuna umeme unawaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja kwa mikono miwili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Kigola tunaendelea na Mheshimiwa Neema Mgaya na baadaye Mheshimiwa Ahmed Shabiby wajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda niungane na Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Hamidu Bobali kumpongeza Mheshimiwa Selemani Jafo kwa kazi nzuri anayoifanya ndani ya Wizara yake. Hii inadhihirisha ni jinsi gani Waziri huyu kwa kushirikiana na Naibu Mawaziri wake wanavyoweza kuisimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyotakiwa. Pongezi sana kwa Waziri huyu na Manaibu wake Josephat Kandege na Mheshimiwa Joseph Kakunda, bila kumsahau Mheshimiwa George Mkuchika, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa maombi ya jumla ndani ya Mkoa wetu wa Njombe. Mara kwa mara nimekuwa nikisimama ndani ya Bunge hili Tukufu nikiuliza maswali, nikichangia Mheshimiwa Selemani Jafo watu wa Njombe shida yetu katika Wilaya zetu zote nne kwa maana ya Wanging'ombe, Ludewa, Makete na Njombe tuna uhaba wa Walimu wa Sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba watuongezee Walimu wa sayansi, tunaomba watuongezee Walimu wa shule za msingi, tunaomba watuongezee Wauguzi na wataalam wa afya. Mheshimiwa Jafo tunamtegemea sana katika hili ili tuendelee kumsifu kwa utendaji wake mzuri wa kazi na tuna imani na yeye, sisi watu wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo ukurasa wa 112, ameainisha mikakati mahsusi ambayo ataifanya mwaka huu mwaka wa fedha 2018/2019 na katika malengo hayo mahsusi ambayo ameainisha ni pamoja na ujenzi wa hospitali 67 katika Halmashauri 67 za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Jafo nimekuwa nikiomba mara kwa mara hospitali ya Wilaya ndani ya Halmashauri ya Wanging'ombe,

namwomba Mheshimiwa Jafo na watu wa Wanging'ombe tuwe wanufaika katika kuhakikisha kwamba mwaka huu tuanze kujengewa hospitali ya Wilaya ya Wanging'ombe ndani ya Halmashauri yetu ya Wanging'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wilaya ya Njombe katika Halmashauri ya Njombe Vijijini, wananchi wameshaandaa eneo *square meter* 52, wananchi wamejitolea ili kuiweza kujenga hospitali ya Wilaya. Tunaomba sasa kwa kuwa wananchi wameshajitolea eneo la *square meter* 52, Wizara sasa watusaidie tuingie katika malengo haya mahsusi ya kujengewa hospitali ya Wilaya ya Njombe ndani ya Halmashauri ya Njombe Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe. Tunaishukuru Serikali kwa kutupatia pesa na kushirikiana na wananchi pia katika kuhakikisha kwamba tumeweza kuboresha miundombinu ya shule ya Wanike Sekondari na miundombinu ya Makoga Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Katibu Mkuu alikuja pale Makoga na Wanike Sekondari akatoa maelekezo ya kufanya. Sisi watu wa Wanging'ombe tumefuata maelekezo yale, tumekamilisha, miundombinu iko vizuri, tunachokiomba kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba wanatupa kibali hivi sasa tuweze kuchukua wanafunzi wa kidato cha tano kuanzia mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vituo vya afya, Wanging'ombe tuna kituo cha afya cha miaka mingi sana cha Makoga. Kituo kile hatuna huduma ya upasuaji kwa sababu hatuna chumba cha upasuaji. Ikitokea mtu anahitaji huduma ya upasuaji, inabidi atembee kilomita zaidi ya hamsini (50) kwenda kufuata huduma ya upasuaji katika hospitali ya Kibena. Tunaiomba Serikali itujengee chumba cha upasuaji na vilevile tunaiomba Serikali itupatie ile *ambulance* na vitanda viwili ambavyo vilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kituo cha Afya cha Palangavano, tunaishukuru Serikali kutupatia milioni 100 kuweza kujenga kituo kile. Niitarifu tu Serikali kwamba zile milioni 100 tuna uwezo wa kujenga mpaka kufikia lenta, tunaiomba Serikali mtupatie pesa tuweze kumaliza kituo kile cha Palangavano kwa sababu kituo kile ni kituo cha kimkakati, kipo katikati ya Wilaya ya Wanging'ombe, wananchi kutoka Luduga, kutoka Malangali, Usuka, Ilembula, Igwachanya ni rahisi kutumia kituo kile cha afya, hivyo basi naiomba Serikali iweze kutupatia pesa kwa ajili ya kuweza kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Palangavano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara katika Halmashauri ya Wanging'ombe, tunaomba kilomita mbili tu Igwachanya na tunaomba kilomita mbili Ilembula, lakini vilevile tunaomba watujengee daraja letu la halali ambalo liko pale Kata ya Ilembula, kwani kipindi cha masika tunapata tabu kuvuka, tunaomba mtusaidie kwa sababu daraja lile ni muhimu, watu wanalitumia kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Wanging'ombe kwa sababu ile Tarafa nzima ya Wanging'ombe na baadhi ya Kata kutoka Tarafa ya Imalinyu wanatumia daraja lile kupita kwenda Igwachanya katika Makao Makuu ya Wilaya ya Wanging'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende Ludewa tuna shule yetu ya sekondari ya Manda, tunaiomba Serikali watusaidie tuweze kukamilisha kuboresha mabweni, hivi sasa tupo katika kuboresha miundombinu ya maji na umeme, watusaidie tuweze kukamilisha na baadaye watupe kibali cha kuweza kupandisha hadhi ya kuweza kuchukua watoto wa kidato cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la afya ndani ya Wilaya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. Wananchi wa Ludewa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wameweza kujenga vituo vya afya 17, tuko kwenye mchakato wa kujenga vituo vya afya 17. Uwezo wetu ni kujenga kuanzia ngazi ya *foundation* mpaka kuezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba kwa Serikali watusaidie katika suala zima la *finishing* kwa sababu wananchi wa Ludewa kwa kushirikiana na wadau tunaweza kujenga kuanzia msingi mpaka kuezeka. Hivyo ombi letu kubwa kwa Serikali ni kutusaidia katika *finishing* ya vituo hivi vya afya 17 ndani ya Halmashauri ya Ludewa ili viweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara za Halmashauri ndani ya Wilaya ya Ludewa, tunaomba watujengee barabara ya Lupingu kwenda Matema *beach.* Barabara hii ni muhimu katika suala zima la ulinzi na usalama kwa sababu barabara hii iko karibu na mpaka wa Malawi na Tanzania. Vilevile barabara hii itatusaidia katika masuala ya utalii na itasaidia kufungua uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendee kwenye Halmashauri ya Makete. Kama unavyojua jiografia ya Wilaya ya Makete iko vibaya sana siyo rafiki katika suala zima la kufikika. Hivyo basi, tunaomba ile Tarafa ya Ukwama ipatiwe kituo cha afya ili wananchi wale wa Tarafa ya Ukwama ambao wapo pembezoni sana Makete waweze kupata huduma ya afya kwa urahisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, malizia sentensi yako ya mwisho.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika suala zima la Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana, naomba Serikali ilete sheria ndani ya Bunge tuweze kupitisha ili tuweze kuwabana Wakurugenzi ambao hawatoi pesa zile za mikopo ya akinamama na vijana katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya. Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nianze kumpongeza Mheshimiwa Mawaziri wote wawili pamoja na Naibu Mawaziri wao na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kujikita kwenye Jimbo langu na hasa kwenye Kituo cha Afya cha Gairo kwa sababu Gairo ni Wilaya lakini bado haina hospitali ya Wilaya. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri baada ya kufika Gairo na kuona kwamba kile kituo cha afya kina umuhimu sana na kiko katikati ya barabara ya Morogoro Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kile kinapokea majeruhi wengi sana na wagonjwa wengi kutoka Wilaya ya Kongwa ambayo imepakana nayo, Wilaya ya Kilindi pamoja na Wilaya ya Kiteto. Kituo kile kimekuwa ndiyo sehemu yao ya hospitali yao ya rufaa pamoja na kuwa ni kituo cha afya. Namshukuru pia kwa kutupa pesa milioni 400 kwa ajili ya kujenga majengo ya operesheni na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja cha ajabu sijui huku TAMISEMI kwa hawa Wakurugenzi wa hizi Idara nini wanafikiria, nini wanafanya na wanaangalia kwa vigezo gani kugawa watumishi kwenye wilaya, bado sipati jibu, leo nimeheshimu tu, lakini siku nyingine kwa kweli hatutoelewana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri anajitahidi, lakini Wilaya ya Gairo kituo hicho cha afya na Wilaya nzima wametuletea mwezi wa Novemba mwaka jana Wauguzi Wasaidizi watatu, wakati upungufu ni zaidi ya Wauguzi 70. Wametuletea Matabibu wametuambia ni Matabibu baada ya kuwachunguza kumbe ni Matabibu Wasaidizi, tumewarudisha huko watubadilishie mpaka leo hakuna kibali cha kubadilisha ili waajiriwe. Kwa hiyo, ina maana hatukupata mtumishi yoyote kwenye kituo cha afya cha Gairo na Wilaya nzima ya Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kufungua

vituo vya afya vitano, lakini hatuna Matabibu wala hatuna Wauguzi. Ukija kwa wale Madaktari pale ni sehemu ya barabarani nimesema ile ndiyo 'Tumbi' ya Dodoma - Morogoro kwa sababu mtu yoyote akipata matatizo na ukiangalia hata idadi ukisoma ya *accident* nyingi zinazotokea katika maeneo yale, Madaktari wenyewe operesheni na Madaktari wengine tunahitaji zaidi ya wanne au watano lakini hatujapata hata mmoja. Sasa sielewi ni nini kinachofanyika hapa kwenye hizi Idara zenu za TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija hata watumishi katika Halmashauri ya Gairo; ukienda uhasibu hakuna watumishi wa daraja la pili, halafu leo tukipata hati chafu watatufungia hiyo Halmashauri kama alivyozungumza Waziri Mkuu? Haiwezekani kwa sababu watumishi Wahasibu hawapo! Utumishi kwenyewe hamna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru dada yangu hapa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu ametupatia gari la wagonjwa, Wilaya ile haina kabisa magari ya wagonjwa. Bahati mbaya ina Tarafa nyingine kutoka Gairo ni kilometa 100 inaitwa Tarafa ya Nongwe, hii Tarafa milima yake ni kuliko milima ya Lushoto, nako wanahitaji gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo gari lililoletwa na Wizara ya Afya nalo halina Madereva. Halmashauri imeomba kuajiri Madereva watano lakini kutoka Wizara ya Utumishi hakuna kibali mpaka leo. Kwa hiyo sasa mnataka hiyo gari aendeshe Mbunge? Matatizo tupu! Naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu shule za Msingi wale wengine wenye vyeti feki wameondoka wengi na mwaka huu wanastaafu Walimu 50 na sasa hivi pana upungufu wa Walimu zaidi ya 270. Kwa hiyo, shule za msingi utakuta kuna shule sasa hivi ina Walimu wawili ama Mwalimu mmoja. Sasa ndugu zangu wa TAMISEMI sielewi ni vigezo gani wanavyotumia kutafuta hawa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine, wakati

tunatoka Wilaya ya Kilosa kugawanya kuwa Wilaya mbili tuliangalia ukubwa wa eneo Wilaya ya Kilosa ilikuwa na Tarafa saba, tukakubaliana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwamba ianzishwe Wilaya ya Gairo kuwa na Tarafa tatu, Tarafa ya Nongwe, Tarafa ya Gairo na Tarafa ya Magole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikatokea baada ya ile Wilaya kuanzishwa uchaguzi wa 2010 ulishafanyika, kwa hiyo Mheshimiwa Rais aliyepita akasema sasa itabidi kwa sababu huku wamechagua Mbunge na huku nako wameshachagua Mbunge kwa hiyo *NEC* wametuambia baada ya zoezi hili likishapita wakati wa uchaguzi 2015, ile Tarafa ya Magole irudi Wilaya ya Gairo kama ilivyoamuliwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2015 ile Tarafa haijarudishwa, kwa hiyo utashangaa wa pale Gairo ukitoka kilometa sita unakuta tena kijiji kipo Wilaya ya Kilosa, Berega yote, Kiegeya yote hata pale wanakouza viazi kwa mbele pako Wilaya ya Kilosa, kwa hiyo wanawatesa wananchi bila sababu. Wale Wapinzani sasa wameingia na majungu wanasema kwamba Mbunge wa Gairo hawapendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine liko kwenye Utumishi; hili lazima tulizungumze wazi mimi ni Mbunge wa CCM na nimepitia kwenye ngazi nyingi nimekuwa Kamanda, nimekuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, nimekuwa Mbunge miaka mingi sana kwenye hiki Chama. Sasa hivi kuna watu kwenye ofisi za Serikali huku kwenye utumishi wanatafuta mbinu ya kujifanya watu wanafanya kazi zao lakini kuichafua Chama cha Mapinduzi na kuchafua Viongozi wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kijana yule Abdul Nondo ana umaarufu gani mpaka wamwite kwa kutumia vyombo vya habari, hawawezi kufanya *investigation,* wafanye *investigation,* wamwandikie barua anaitwa, lakini hapo ni kutaka kuichafua tu wanataka kuichafua Serikali ya CCM kwamba aambiwe yule kuna mbinu ya aina yoyote anatafutiwa, ana umaarufu gani mpaka yule mtu wa

*Immigration* aende akakae anaanza anataka cheti cha bibi, cheti cha mjomba, cheti cha babu mpaka aandike kwenye vyombo vya habari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapa watu umaarufu wakati kesi iko Mahakamani mtu anapatikana, kuna watu wengine watatumia ile kusema mmeona sasa, Serikali ya CCM ikimtaka mtu inaanza kumwambia siyo raia, wakati siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwenye utumishi waambieni watu wenu, televisheni kila mtu anaipenda, lakini uwe na mambo ya maana ndiyo uende ukajiangalie kwenye televisheni. Sasa itakuwa basi kila mtu akitaka kitu anatoa taarifa kwenye televisheni au kwenye mitandao siyo sawa! Wanachafua Serikali yetu wakati hakuna mtu mwenye habari na mtu mdogo kama yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye utumishi tuangalie haya masuala, mnayaona ya kawaida lakini kuwapa watu maneno na mambo mengine ya kuongea au watu kufikiria au kuwasababisha watu wajue kwamba Serikali inamtafuta yule kijana, wakati Serikali nina uhakika kabisa haina mpango na mtu mdogo kama yule kwa sababu hana madhara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yangu, ahsanteni sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jioni hii ya leo ndio tumemalizia hapo na muda wetu umemalizikia. Kabla sijaahirisha shughuli za Bunge naomba tu niwataje kabisa Wabunge ambao wataendelea kuchangia kwa siku ya kesho au wataanza kesho asubuhi.

Mheshimiwa Catherine Ruge, Mheshimiwa Zainabu

Mndolwa, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Musa Sima na Mheshimiwa Almasi Maige hao ndiyo watakuwa wachangiaji wetu wa mwanzo kwa siku ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninawapongeza kwa kazi nzuri tuliyoifanya kwa kutwa nzima ya leo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamis, Tarehe 12 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*